Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Kumi - Tarehe 18 Juni, 2010**

*(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:**

Randama za Makadirio ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 69

**Mafao kwa Mwenyekiti wa Serikali**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO (K.n.y. MHE. BALOZI ABDI MSHANGAMA)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kuwalipa mafao Wenyeviti wa Serikali za Vijiji ambao ni wadau muhimu katika kusimamia maendeleo ya wananchi vijijini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama Mbunge wa Lushoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Vijiji Na. 25 ya mwaka 1975 Mwenyekiti wa Kijiji ni Kiongozi wa Serikali ya Kijiji anachokiongoza. Kiongozi huyu ndiye chimbuko na chemchemi ya Uongozi kwa vile anaongoza ngazi ya kwanza na ya msingi ya uongozi mzima wa Taifa.

Katika Tanzania asilimia ipatayo 80 ya Watanzania wote wanaishi vijijini. Hivyo ni wazi kabisa kwamba viongozi hawa wanaongoza kundi kubwa na muhimu la wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wote ni mashahidi kwamba viongozi hawa wakisaidiana na Viongozi wenzao katika Serikali zao za vijiji wamefanya mambo makubwa kusukuma ajenda za maendeleo katika maeneo yao. Mafanikio tunayojivunia hasa katika ngazi za vijiji ukiwemo ujenzi wa shule za msingi na sekondari za kata, ujenzi wa zahanati na vituo vya afya, ujenzi wa barabara n.k. yote yametokana na usimamizi thabiti wa wenyeviti wa vijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kazi kubwa inayofanywa na viongozi hawa Serikali kupitia Bunge lako Tukufu ilikwishatoa maelekezo kwa Halmashauri zote nchini kutenga asilimia 20 ya mapato yatokanayo na fedha za fidia ya vyanzo vilivyofutwa zinatolewa na Serikali kama *General Purpose Grant* kuhudumia Ofisi za Kata, Vijiji na Mitaa.

Fedha hizi pamoja na kufanya kazi za kununulia nyenzo za kufanyia kazi kama vile shajala, kalamu, karatasi na kulipia bili za maji na umeme, kiasi kingine kisichopungua shilingi 20,000 kwa mwezi kitengwe kuwalipa posho Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa. Kwa Halmashauri zile ambazo zina uwezo hususan Halmashauri za Mjini hutenga fedha kutokana na vyanzo vyake vya ndani (*Own Sources*) kuwalipa posho Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa. Ni matumaini yangu kwamba maelekezo haya yanazingatiwa na Halmashauri zote.

Nawaomba Waheshimiwa Wabunge ninyi kama Madiwani katika Halmashauri zenu mhakikishe zinatengwa fedha za kutosha kulipa posho za Wenyeviti wa vijiji na Mitaa.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu na maelezo yake fasaha sasa kwa kuwa hata Waziri Mkuu naye ni Mbunge. Je, anaweza sasa kutusaidia kutoa tamko kwamba Bunge lijalo lihakikishe kwamba suala linatekelezwa kwa dhati?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shellukindo anataka nitoe tamko hapa, lakini jana hapa tulikuwa kwa hapa ndani hapa na Mheshimiwa Waziri Mkuu aliulizwa swali hili ambalo naulizwa hapa.

Mimi kwa kutoa jibu lile jibu ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu amelitoa jana hapa lile ndilo tamko la Serikali na hiki nachokisema mimi natamka hapa tamko la Serikali. Kwa hiyo, mimi siwezi kutengua torati hapa kazi yangu ni kuimarisha torati maneno aliyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu jana ndiyo hayo. Kwa hiyo hapa habari imekwisha tamko lilitolewa jana wakati alipokuwa anaulizwa Maswali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. MOHAMED ALI SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa hizi asilimia 20 katika Halmashauri nyingi hasa katika Halmashauri yetu ya Shinyanga Vijijini, jimbo la Solwa ni kidogo mno kutosheleza wenyeviti wa Serikali ya vijiji na vitongoji. Kwa nini Serikali isiichukue hii ikaipangia Bajeti kwa mwaka wa fedha ujao ikaongezewa fedha za kutosha kwa ajili ya kuwalipa hasa wenyeviti wa vijiji na vitongoji. Kutokana na kazi kubwa mno wanayoifanya kutangaza ilani ya Chama cha Mapinduzi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, hela zilizozungumzwa hapa elfu ishirini tumesema ndiyo kiwango cha chini ambacho Halmashauri inatakiwa itoe. Kama Halmashauri ina uwezo inaweza ikatoa zaidi ya hapo.

Lakini la pili la kwamba inakuja kwenye Bajeti inayokuja hapa, bajeti ni mpango ni wa Serikali unaotuonyesha jinsi hela ziatakavyopatikana na namna zitakavyotumika. Kama sisi tutaona kwamba kuna haja ya kuingiza hii katika Bajeti na kuweka kiwango kingine hapa suala hili linalozungumzwa hapa ni suala la kisera ni jambo ambalo linahitaji sasa maamuzi makubwa zaidi. Ninachoweza tu kusema hapa tamko la Serikali ni hilo kwamba unapolipa hakikisha kwamba hulipi chini ya shilingi 20,000.

Kama ilivyoelezwa katika jibu la msingi hela zile tunazozipeleka kwa ajili ya fidia ndiyo hizo tunataka uchukue pale. Yale mapato mengine ambayo yanatoka na mapato ya ndani ya Halmashuri yatumike kwa ajili ya kulipa hizi hela. Kwa hiyo, itategemeana na Halmashauri kwamba inataka kulipa zaidi ya hapo kwa kweli hapa haikuzuiliwa.

**MHE. DR. WILIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Kamati yako ya *LAAC*, ni juzi tu imerudi kutoka mikoa saba na kwa kuwa siku zote Kamati yako ilikuwa inatekeleza maamuzi ya Serikali kwamba asilimia 20 ya vianzio vya fidia inarudishwa vijijini kwa ajili ya shughuli za maendeleo na Kamati yako imesimamia hilo na imelazimisha Halmashauri zote kuhakikisha inarudi asilimia hiyo kwa ajili ya maendeleo.

Je, ni lini sasa Serikali ilibadilisha mpango huo na kuagiza kwamba iwe inawalipa wenyeviti wa vijiji ni kwanini Serikali inatoa kauli mbili tofauti bila maelekezo ya wazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, sasa mimi hapa sijui kama nimemwelewa vizuri natambua kwamba huyu anayezungumza vizuri ni Mwenyekiti wa

*The Local Authorities Accounts Committee.* Lakini tunachosema hapa hela zinazokwenda pale kwa ajili ya fidia kwa maana ya yale mapato ambayo yalikuwa yaingie katika Halmashauri tukasema kwamba hizi ni kodi ambazo zinaonekana kwamba zina kero kwa wananchi.

Kwa mfano ushuru wa vitumbua, ushuru wa samaki, ushuru wa binda, vilevile vitu vidogo vidogo mnavyomwezesha mwananchi kwenda kujikimu tukafuta, tulipofuta tukasema Serikali itaangalia kila Halmashauri ilikuwa inakusanya kiasi gani hicho kiasi ambacho kilikuwa kinakusanya, Serikali ikasema itarejesha kule kwenye Halmashauri, asilimia 20 ya hizo zinazorejeshwa zipelekwe moja kwa moja ziende mpaka kule kwenye kijiji pale ndiyo nachozungumza hapa.

Sasa kwamba kuna tofauti ya matamshi hapa sijaelewa vizuri labda nielezwe hapa, halafu ili niweze kujibu vizuri, lakini mimi navyofahamu kinachoelezwa ndiyo hicho ndicho alichosema hata Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa na ndicho ambacho nimekirudia hapa.

**SPIKA:** Tofauti inakuwa hivi, subiri basi Mheshimiwa Naibu Waziri, anavyouliza Mheshimiwa ni kwamba asilimia 20 kuna nyakati Serikali imetamka inarudi kwa ajili ya mipango ya maendeleo kijijini. Wakati mwingine sasa inasemekana inarudi ili kuwalipa wenyeviti. Sasa au inafanya yote mawili nadhani ndiyo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Mimi nadhani sasa nimekuelewa baada ya kufafanua hilo, tunachosema hapa ni ile hela inayorudi kam fidia, hela zinazokwenda kwenye maendeleo, ni hela zile zinazoitwa *Local Government Capital Development Grant* hizo ndizo zinazokwenda kama hela za maendeleo.

Sasa mimi *I say to be corrected* sasa kama kuna fact ambazo tumezichanganya hapa nitamuomba Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, tukae naye tuzungumze vizuri tuelewane katika hili. Lakini kinachozungumzwa hapa ni zile hela zinazokwenda kama fidia. (*Makofi)*

**SPIKA**: Nadhani tutapata faida mkikaa pamoja labda Mheshimiwa Ndugai, Mwenyekiti Ndugai anaweza kuwa na ufumbuzi fulani hapa.

**MHE. JOB Y. NDUGAI**: Mheshimiwa Spika, ahsante, swali moja dogo la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba uongozi wa Serikali za Mitaa unaanzia ngazi za vitongoji na vijiji kwenda juu lakini iko ngazi chini ya kitongoji inayoitwa balozi wa nyumba kumi.

Kwa miaka mingi katika uongozi wa nchi yetu, ngazi hii ndiyo ilikuwa chanzo cha uongozi kwenda juu. Sasa mara kwa mara Waheshimiwa mabalozi wilayani Kongwa na maeneo mengine nao wamependa sana watambuliwe katika uongozi rasmi wa Kiserikali.

Je, Serikali ina mpango wowote wa kuwatambua mabalozi ili waingie katika mfumo rasmi na baadaye na wao nao wapate chochote kitu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu naona kimeongezwa kigogo kingine tena.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nimeona hilo zito maana ngazi ya mabalozi ni mfumo ambao uko chini ya Chama cha Mapinduzi na unatumika kwa ajili yak u-*facilitate* shughuli ya chama kinachohusika.

Kwa hiyo, kusema kwamba sasa ile ngazi igeuke au tuigeuze sasa iwe ni mfumo wa Serikali mpaka ngazi ya chini, hiyo sasa inahitaji maamuzi mengine ya kisera na ya yakubalike ndipo tunaweza tukakubaliana juu ya jambo hilo. Ingawa najua litakuwa na ugumu kwa sababu Dr. Willibrod Slaa atapiga kelele tu anajua wale watabaki ni wale wale. *(Makofi)*

Lakini rai ni nzuri isipokuwa inahitaji kutazamwa tena upya, ili tuweze kama kuna mfumo mzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, nimeona tu nisimame kwa sababu naona hili suala la asilimia 20 bado linaleta kutokueleweka vizuri pengine nitakachomwomba tu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) nikitoa maelezo yale ambayo tumekuwa tukiyatoa muda wote kwamba katika ile asilimia 20 kile kinachopatikana kimegawanyika tena katika asilimia ndogo ndogo asilimia 3, asilimia 5 jambo fulani na ndani yake humo iko hata *component* ya fedha ambayo inabaki kwa ajili ya kusaidia shughuli za maendeleo katika kijiji kinachohusika.

Si kwamba hela yote kwa mgawanyiko ule ulivyo yote unasema inagawanywa kwa ajili ya shughuli tu za wenyeviti, iko mgawanyo na una *component* ya uendeshaji wa shughuli za ofisi na *component* kidogo kwa vitu vidogo vidogo kwa kusaidia ngazi ile ya kijiji kuweza kutumia kwa ajili ya shughuli kama hizo.

Kwa hiyo, nadhani ufafanuzi utakaotoka ni vizuri ukaweka hiyo baya ili watu waweze kujua ni kiasi gani na kwa hiyo kimegawanyika vipi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri sasa limekaa wazi, hatimaye tunahamia Wizara nyingine sasa.

Na. 70

**Maendeleo ya Benki ya Wanawake Tanzania**

**MHE. JANET B. KAHAMA** aliuliza:-

Kuzinduliwa kwa Benki ya Wanawake Tanzania mwezi Julai, 2009 kuliwapa matumaini mapya ya kasi ya maendeleo kwa wanawake wengi wa Tanzania hasa katika kupata mikopo kwa masharti nafuu:-

(a) Je, ni wanawake wangapi wamepewa mikopo hadi sasa na kwa masharti yapi na wangapi kati yao wanaishi vijijini?

(b) Je, ni Watanzania wangapi kwa mchanganuo wa wanawake na wanaume wamenunua hisa katika benki hiyo na zina thamani gani?

(c) Je, ile idara iliyoahidiwa siku ya uzinduzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo ya kuwapatia wajasiriamali wanawake mafunzo ya kibiashara na taaluma ya kufanya michanganuo ya Mradi ya Kiuchumi imekwisha tekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janet Bina Kahama, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu a, b, na c kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, idadi ya wateja waliokopeshwa hadi Juni, 2010 ni 3,200 wanawake wakiwa 2,665 na wanaume 535. Thamani ya mikopo hiyo yote ni Tsh. Milioni mia tisa (900 m.). Kati ya wateja hao waliopewa mikopo wateja 360 ni wanawake waishio vijijini katika maeneo ya Ukonga Kipunguni na Kibaha. Thamani ya Mikopo iliyotolewa kwa wanawake wa Vijijini ni Tsh. Milioni sitini na nne (64m.). Aidha, masharti ya mikopo ni kuanza kufungua akaunti yenye thamani ya asilimia 25 kama amana ya mkopo na kuwa kwenye kikundi ambacho ndicho dhamana ya mwanakikundi. Vilevile, hati ya makazi, hati miliki ya nyumba, kiwanja na kadi ya gari hutumika kwa dhamana ya kupewa mkopo ya kibiashara.

(b)Mheshimiwa Spika, idadi ya Watanzania ambao wamenunua hisa katika Benki ya Wanawake ni 134, wakiwemo wanawake 90 wenye hisa zenye thamani ya shilingi 79,450,000?= na wanaume 44 wenye hisa za thamani ya s hilingi 46,728,000/=.

(c)Mheshimiwa Spika, ahadi iliyotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Wanawake ya Tanzania siku ya uzinduzi wa benki hiyo kuhusu kuundwa kwa idara ya kutoa mafunzo kwa wajasiriamali imetekelezwa. Mafunzo ya biashara na taaluma ya kuandaa michanganuo ya miradi ya kiuchumi kwa wajasiriamali yanaendelea kutolewa.

Aidha, mafunzo hayo, ambayo ni ya lazima kwa ajili ya kuwaadaa wateja kabla ya kupewa mikopo hutolewa kwa muda wa wiki tano.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali la nyongeza tena, nina nyongeza kwa maeneo mawili. Pamoja na kazi nzuri ambayo benki imeanza kufanya nilitaka kujua kuwa kuna asasi nyingi ambazo tunazo zinazotoa mikopo midogo midogo na mikopo ya kati. Asasi hizo ni kama vile *FICA, PRIDE* na kadhalika. Je, Waziri haoni kuwa kunaweza kuwa na manufaa ya iwapo atazijumuisha asasi hizo pamoja na wajasirimali wanawake wakaweza ku-*form* kitu kama *consortium* au *forum* ya kuweza kuzungumza kutatua matatizo ya wanawake?

La pili, kuna *SACCOS* nyingi za wanawake zimeanzishwa *SACCOS* hizo zina malengo ambayo ni sawa na malengo ya benki ya wanawake, *well* benki inaweza kuwa na malengo zaidi lakini malengo mengi yanafanana.

Je, sasa kutokana na majibu haya ni kuwa wanawake wamekuwa wakikopa, ni *SACCOS* ngapi kama ziko zimekopa nijue maana yake nasikia wanawake ni watu binafsi. Je, kuna SACCOS zozote ambazo zimeingia kukopa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika nchi yetu tuna asasi nyingi ambazo zinatoa mikopo kwa Watanzania na sio wanawake tu, kwa sababu hata benki yetu haitoi mikopo kwa wanawake tu. Sasa benki hii imeanzishwa kama chombo kimajawapo ambacho kitakuwa na mfumo mkubwa jinsi siku zinavyokwenda kuweza kutoa mikopo mikubwa na kwa masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, hizi asasi kama *FICA, Pride, Self* na nyinginezo zinakuwa ni asasi ambazo pia nazo zinafanya biashara kwa sababu unakuta kwamba masharti yao kwa kweli ni makali sana pamoja na kwamba wanasaidia kuondoa umaskini mimi naomba niseme pia kwa njia nyingine inafanya wanawake wanabeba mzigo mkubwa. Unapewa mkopo leo baada ya wiki moja unatakiwa kuanza kuulipa tofauti na benki yetu.

Hivyo basi kwa sababu wale ni watu ambao wanajitegemea na hawako chini ya Mfumo wa Serikali sisi kama Serikali hatuwezi tukawaingilia.

Lakini ningependa kusema kwamba kama wao wangependa kutengeneza a *forum* ya kuweza kushirikiana katika kuondoa umaskini kwa Watanzania wote siyo wanawake tu. Mimi hilo litakuwa ni jambo zuri na sisi kama Serikali tutapenda kushirikiana nao lakini kushirikiana nao ni katika kuangalia sera na mfumo ambao utatumika katika kufanyakazi kwa pamoja ili tusije tukaona kwamba ile *forum* itakayotengenezwa itaongeza mzigo wa kulipa riba kubwa ili waweze kufidia sasa zile gharama za kuwa na mfumo ni wa kuunganisha asasi zote.

Mimi naomba niwapongeze kwa sababu wale ni washiriki na ni wasaidizi wa Serikali katika kupambana na tatizo la umaskini.

Swali la pili, ni kweli kwamba katika Benki yetu ya Wanawake tumetoa mikopo kwa *SACCOS* na vikundi vya wanawake. Lakini sisi kama mfumo kwa sababu *SACCOS* wanatakiwa kwanza wanunue hisa halafu wafunge akaunti ndio waweze kupata mikopo. Mpaka sasa hivi ninavyozungumza siyo *SACCOS* nyingi zimenunua hisa na kufungua akaunti kwenye benki yetu.

Sasa mimi ningeomba kwamba *SACCOS* zifungue akaunti. Lakini idadi kamili nitamweleza Mheshimiwa Mbunge, baadaye nitajaribu kufuatilia kwa sababu mpaka sasa hivi siyo asasi nyingi. Lakini najua kwamba tunaweza tukawa na idadi kamili kama nitalifuatilia.

Mheshimwia Spika, mimi ninaamini kwamba *SACCOS* kama *SACCOS* zina uwezo wa kufanyakazi lakini sisi tunalenga zaidi vikundi vya wanawake maskini pamoja na wanawake na Watanzania maskini ambao wataunganika kwenye kikundi. Nashukuru. (*Makofi*)

Na. 71

**Kuzuia Biashara ya Bidhaa Bandia**
**na Zisizo za Viwango**

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA (K.n.y. MHE. PINDI H. CHANA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na bidhaa bandia na zisizo na viwango katika nchi nyingi na kwamba madhara yake ni makubwa kwa wananchi:-

(a)Je, Serikali ina mpango gani wa kufunga maduka na kuzuia leseni za maduka yanayofanya biashara hiyo?

(b) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuzuia biashara ambazo zina madhara kwa wananchi ambayo yanaweza kusababisha vifo?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, pindi inapobainika kuwepo kwa bidhaa hafifu, Serikali kupitia Sheria mpya ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009, imelipa Shirika la Viwango Tanzania mamlaka ya kuondoa bidhaa hafifu zilizoko sokoni; kufuta leseni ya mfanyabiashara husika; kutoza faini; kuweka taratibu za kufanya marejesho na au fidia na kuweka taratibu za kuharibu bidhaa duni au kuzirudisha zilikoagizwa.

(b)Mheshimiwa Spika, ili kuzuia biashara ambazo zina madhara kwa wananchi yanayoweza kusababisha hata vifo, Serikali kupitia *TBS,* hufanya ukaguzi wa bidhaa toka nje ya nchi katika Bandari ya Dar es Salaam na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa bidhaa zilizo katika soko kwa kuchukua sampuli na kupimwa ili kuhakikisha kwamba bidhaa zinazotoka nje ya nchi ni zile zenye ubora unaotakiwa ili zisilete madhara kwa wananchi na hata kuweza kusababisha vifo.

Aidha, ili kuimarisha zaidi ukaguzi wa bidhaa zinazoingia nchini, Shirika liko mbioni kuanzisha mfumo wa ukaguzi wa bidhaa katika nchi zinakotoka kabla ya kusafirishwa kuja nchini yaani *Pre-shipment Verification of Conformity to Standards* mfumo ambao utatumika sambamba na mfumo uliopo *(Destination Inspection),* na cheti cha ubora yaani *Certification of Conformity to Standards* kitatolewa kwa bidhaa zinazokidhi matakwa ya ubora wa viwango vya taifa au kimataifa.

Vile vile ili kuimarisha udhibiti wa ubora wa bidhaa vikiwemo vyakula toka nje ya nchi, Shirika limefungua ofisi za ukaguzi katika Bandari ya Tanga, Horohoro (Tanga), Holili (Kilimanjaro) na Sirari (Mara) tangu Novemba 2007 ambapo ofisi ya ukaguzi katika mpaka wa Namanga imefunguliwa mwaka huu. Katika mwaka 2010/2011, *TBS* inategemea kufungua ofisi ya ukaguzi katika mpaka wa Tunduma.

Aidha, Shirika linaendelea kutoa elimu kwa wananchi kwa ujumla ili waelewe umuhimu wa kutumia bidhaa zenye viwango vya ubora kuendeleza biashara, kulinda afya ya watumiaji pamoja na mazingira.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Ushindani kwa upande wake, inafanya ukaguzi wa bidhaa mara kwa mara katika maeneo yote ambayo bidhaa huingia nchini hasa katika bandari zetu na inapobainika kuwepo kwa bidhaa bandia katika maeneo hayo, huzizuia bidhaa hizo na wahusika huchukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na bidhaa hizo kuharibiwa kwa gharama zao.

Aidha, kuna sheria nyingine ambazo zinasimamia masuala yanayohusu afya ya binadamu kwa mfano sheria inayounda Mamlaka ya Chakula na Dawa.

**MHE. FAIDA M. BAKAR:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mbali na bidhaa bandia kutoka nchi za nje. Je, Serikali inabaini bidhaa bandia zinazotengenezwa na viwanda hapa nchini na kama imeshabaini inachukua hatua gani kwa viwanda hivyo vya hapa nchini? (*Makofi*)

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Faida Bakar kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa hatuwezi kukubali nchi yetu kugeuka jalala na bidhaa hafifu ama zinazotoka nje, au zinazotengenezwa ndani ya nchi yetu.

Kwa hiyo, sheria siyo kwa bidhaa zinazotoka nje tusikubali bidhaa zote zilizo hafifu kwa manufaa ya afya zetu na kwa kulinda nchi yetu kwa sababu nchi ikiwa ni soko la bidhaa bandia au hafifu wawezekezaji wataogopa kuja na kwa hivyo lazima tulinde nchi yetu na iwe soko la bidhaa ambazo zinategemewa na zenye ubora unaotakiwa. (*Makofi*)

**MHE. KHALIFA S. KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hali halisi inaonyesha kuwa wimbi kubwa la bidhaa hizi hafifu ni kutoka China. Ukitazama katika hali ya kawaida unaweza kuona labda watu wanalalamikia bidhaa za chakula au vingine lakini tatizo kubwa sasa hivi ni masuala ya vipuri vya magari kwani mengi yanaharabika kwa kufungwa vipuri ambavyo vinatoka China ambavyo ni hafifu sana. Je, Serikali hili hamlioni na kama mnaliona mnachukua hatua gani? (*Makofi*)

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, namshukuru kwa swali lake ambalo linanifanya mimi nizidi kufafanua jambo hili ambalo ni muhimu kwa uchumi wetu na kwa afya ya watu wetu.

Mheshimiwa Spika, bidhaa zinazoangaliwa na *TBS* pamoja na shirika letu la *FCC* au *Fair Competition Commission* siyo za chakula peke yake bali nimetilia umuhimu kwenye chakula kwa sababu ni la hatari kwa afya ya binadamu lakini shirika la linaangalia bidhaa zote vikiwemo vipuri vya magari na mashine zingine.

Mheshimiwa Spika, bila kujali kwamba bidhaa inatoka China au nchi gani ikishakuwa hafifu sheria itachukua mkondo wake. Napenda kuutangazia umma na wafanyabiashara kwamba tutakuwa tunanyang'anya leseni za biashara na kwa kufanya hivyo tutakuwa tunafunga biashara ya wale ambao wanaleta bidhaa hafifu na ambao wanakubali bidhaa hafifu kuuzwa kwenye maduka yao. (*Makofi*)

Na. 72

**Ahadi ya Barabara ya Ngorongoro**

**MHE. KAIKA S. TELELE** aliuliza:-

Kwa kuwa moja kati ya vigezo vya kuhakikisha maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii ni pamoja na kuwa na miundombinu ya barabara na kwa kuwa tarehe 20 Machi, 2007 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliahidi barabara kupitia Mto wa Mbu – Engasero – Loliondo kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

(a) Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

(b) Je, Serikali haioni kwamba sasa ni muda muafaka wa kutekeleza ahadi zake hasa tunapoelekea kwenye kipindi cha Uchaguzi Mkuu 2010?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mbunge wa Ngorongoro, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza ahadi zake ikiwa ni pamoja na maandalizi ya kujenga barabara ya Mto wa Mbu – Engasero – Loliondo kwa kiwango cha lami. Mpango wa ujenzi wa barabara hiyo ulikwisha andaliwa na kazi ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami hivi sasa imekamilika. Vile vile mkataba wa usanifu wa kina ulitiwa saini tarehe 26 Agosti, 2009 na kazi za usanifu zinaendelea.

Mara baada ya kukamilika kwa usanifu wa kina na gharama ya mradi kujulikana, Serikali itatafuta fedha za kugharamia ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Je, kati ya upembezi yakinifu na upembezi wa kina katika maandalizi ya mradi wowote na hasa huu wa ujenzi wa barabara ni dhana ipi ya utekelezaji inachukua muda mrefu zaidi kuliko nyingine?

(b) Je, Serikali kama kweli imedhamiria kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami, katika kuharakisha utekelezaji wa barabara hii, isingekuwa busara kuweka wakandarasi wawili au watatu ili kuharakisha barabara hii ambayo inasubiriwa na wananchi wa Monduli, Ngorongoro na Longido?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, moja kuhusu tofauti ya muda kati ya upembuzi yakinifu na usanifu lipi linachukua muda mrefu. Hii inategemea sana na aina ya mradi wenyewe. Kuna miradi ambayo migumu zaidi katika upembuzi na kuna miradi ambayo ni migumu zaidi katika usanifu. Kwa hiyo, hakuna sheria maalum kwa muda kati ya kati hizo mbili.

Kwa ajili ya barabara hii kubwa na nyeti kazi zote mbili zitahitaji muda kwa bahati tumemaliza sasa hivi upembuzi yakinifu. Kwa hiyo, tunakwenda sasa kwenye *stage* ya pili ya usanifu ambayo tumeanza kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba tumeanza mwezi wa Agosti, 2009. Serikali itajitahidi kuhakikisha kwamba kazi hiyo tunaifanya kwa umakini na kwa haraka iwezekanavyo. Kwa swali la pili kama ingefaa tuweke wakandarasi wawili bila shaka itakapofikia hatua hiyo pendekezo la Mheshimiwa Mbunge tutalitilia maanani tumefanya hivyo katika miradi mingine ya barabara ndefu kwa sababu hii barabara ni ndefu sana kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge barabara hii inatoka Mto wa Mbu mpaka Loliondo mpaka *Clins Camp* mpaka Mugumu, Nata mpaka Makutano. Kwa hiyo, ni barabara ndefu karibu inazidi kilomita

400 ambayo bila shaka umakini wa ujenzi wake itabidi iwekwe wakandarasi zaidi ya mmoja.

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imetoa fedha kwenye Bajeti iliyopita kutengeneza barabara kutoka Longido – Kitumbini mpaka barabara hii anayoulizia Mheshimiwa Telele wametoa kilomita 10. Je, Serikali sasa wako tayari kumalizia sehemu iliyobaki kwa Bajeti hii?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ina nia sana kuhakikisha kwamba barabara hii inayounganisha Wilaya mbili Wilaya ya Longido na Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro kwa maana ya Loliondo kuiwekea fedha ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Tumeanza kufanya hivyo mchakato wa Bajeti ya mwaka mpya wa fedha 2011 unaendelea haujakamilika tutazingatia hoja ya Mheshimiwa Mbunge ikiwezekana tutatenga fedha ambazo zinakidhi mahitaji.

Na. 73

**Ujenzi wa Barabara ya Mtama – Newala**

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya km 5 kati ya Mtama – Newala eneo la Kinolombedo kwa kiwango cha lami:-

(a) Je, fedha hizo zimepatikana?

(b) Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza?

**WAZIRI WA MAENDELEO MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kuwa upo umuhimu wa kujenga sehemu ya barabara ya Mtama – Newala katika eneo la Kinolombedo lenye urefu wa kilomita 5 kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kutokana na ufinyu wa bajeti, Serikali haijatenga fedha kwa ajili ya kujenga sehemu ya barabara katika milima ya Kinolombedo kwa kiwango cha lami. Kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii kuanzia mwaka 2008 jumla ya shilingi 1,010,650,000/= (bilioni moja, milioni kumi na mia sita hamsini elfu) zilitengwa na Serikali na zilitumika kuzifanyia matengenezo barabara za Kitama – Mkwiti na Newala – Kinolombedo kwa kiwango cha changarawe ili ziweze kupitika kipindi chote cha mwaka. Serikali itaangalia uwezekano wa kutenga fedha katika Bajeti zijazo kwa ajili ya ujenzi wa eneo hilo la barabara kwa kiwango cha lami.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa eneo la Kinolombedo ni korofi na limekuwa likisababisha vifo na upotevu wa mali kwa wananchi wanaotumia barabara hii.

(a)Je, kwa nini vifo na upotevu wa mali unaotokea pale usionekana kuwa ni maafa na hivyo hatua za dharura zikachukuliwa?

(b)Je, Serikali yetu inashindwa kupata fedha angalau kwa awamu za kujenga kilomita 5 tu?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, moja kama nilivyokiri katika swali langu msingi kwamba tunatambua umuhimu wa kulifanyia matengenezo eneo hilo kwa kiwango cha lami ili kuondoa madhara ambayo wananchi yanawakumba wanapopita katika barabara hiyo. Ndiyo juhudi ambayo tumeiweka kupatengeneza kwa kiwango cha changarawe kwa sasa kufuatana na upatikanaji wa fedha.

Tutaendelea kuweka juhudi ya kuhakikisha kwamba tunafikia kiwango hicho cha lami mapema iwezekanavyo tutajitahidi katika mchakato ikiwezekana kwenye mchakato huu wa mwaka unaofuata wa fedha ikishindikana katika Bajeti nyingine ili tuhakikishe kwamba eneo hili linajengwa kwa kiwango cha lami kama vile ambavyo Mbunge kwa kipindi kirefu amekuwa akifuatilia kuhusu eneo hili. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba mwaka 2008 walitumia kama bilioni 1.2 kilomita tano zinahitaji bilioni 1.5.

Je, Waziri haoni kwamba mipango mibovu *otherwise* wangeweza kumaliza hii barabara kwa haraka sana?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kujibu swali la Mkuu wa Kambi ya Upinzani kama ifuatavyo:-

Kwa tathimini ya ujenzi wa barabara hivi sasa kilomita moja ya *double surface dressing* ni bilioni 5 ukiweka na tathimini za ulipaji wa fidia na mazingira mengine ni bajeti inayozidi bilioni 6 kwa ujenzi huo.

Kwa hiyo, bilioni moja haiwezi ikajenga kilomita tano lakini kama nilivyosema tunatambua umuhimu wa ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa sababu ni eneo hatarishi tutajitahidi kuhakikisha kwamba tunalijenga mapema iwezekanavyo.

Na. 74

**Nyumba zilizobomolewa Barabarar ya Tanga – Horohoro**

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA (K.n.y. MHE. NURU AWADHI BAFADHIL)** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Kata ya Mabokweni katika Jiji la Tanga walilazimishwa kubomoa nyumba zao ili kupisha ujenzi wa barabara ya Tanga – Horohoro – Mombasa, lakini barabara hiyo haitapitishwa maeneo hayo na badala yake itapitishwa sehemu nyingine ambayo hakuna nyumba.

Je, Serikali haioni kuwa haikuwatendea haki wananchi waliolazimishwa kubomoa nyumba zao?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika zoezi la kuainisha nyumba zilizotakiwa kubomolewa ili kupisha ujenzi wa barabara ya Tanga – Horohoro, ilionekana kuwa nyumba nyingi katika kijiji cha Mabokweni zingeathirika.

Kutokana na hali hii mfadhili wa mradi huu ambaye ni Serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa Changamoto ya Milenia *(MCC)* alishauri barabara mpya ipite nje ya kijiji ili kuzinusuru nyumba hizo. Ushauri huu ulizingatiwa na hivyo barabara inayojengwa itapita nje ya kijiji cha Mabokweni na hivyo kuzinusuru nyumba zote zilizotakiwa kuvunjwa.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

(a)Kwa kuwa, hawa watu wa Mabokweni tayari walikuwa wamelazimishwa kubomoa nyumba zao ili kupisha ujenzi wa barabara, pamoja na barabara hiyo kutopita Mabokweni hilo si suala la wananchi?

Je, Serikali haioni busara kuwalipa wananchi hawa fidia kwa sababu yenyewe ndiyo iliwaamuru kubomoa nyumba hizo?

(b) Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais wakati anafungua ujenzi wa barabara hii alitoa kauli kwamba wale waliotii amri ya kubomoa nyumba zao wenyewe kupisha eneo la barabara ni lazima walipwe fidia.

Je, Mheshimiwa Waziri unakinzana na usemi wa Rais? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mkiwa, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niseme kwamba Mabokweni hapakuwa na nyumba ambayo ilikuwa imevunjwa, kwa maana hiyo ni kwamba wakati maamuzi yalipofanywa kukwepa Kijiji hicho hakuna nyumba ya mwananchi ambayo imevunjwa na barabara imekwepa kijiji ili kuepusha madhara hayo ambayo nyumba nyingi zingekuwa zimeathirika.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, kuna eneo katika barabara hii ya Tanga hadi Horohoro ambapo notice zilitolewa mwaka 2003 na baadhi ya wananchi wakavunja nyumba zao, wale ambao walivunja nyumba zao kabla ya ujenzi hawakuwepo kwenye tathmini wakati taratibu za ujenzi zinaanza.

Mheshimiwa Rais alipofanya ziara Mkoani Tanga tarehe 28 Mwezi Mei na kulikuta tatizo hilo wakati anaweka jiwe la msingi kwenye barabara hii, akaagiza kwa eneo lile kwa wananchi wale ambao walikuwa wameshavunja nyumba na kuondoka, wananchi hao wafanyiwe utaratibu wa kufidiwa nyumba zao na Serikali sasa hivi inafanya taratibu hizo ili wananchi hao waweze kulipwa kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais.

Na. 75

**Tatizo la njaa nchini**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa muda mrefu kumekuwepo na kilio cha njaa sehemu nyingi nchini; na kwamba Serikali bado haijafikia lengo la kutumia mito isiyokauka na mabonde yenye rutuba kuleta mapinduzi ya kweliya kilimo:-

Je, Serikali imejifunza nini kutokana na tatizo hili linalojitokeza kila mwaka kutokana na mabadiliko ya hewa duniani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salum, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kutokana na tatizo la njaa linalojitokeza kwa baadhi ya maeneo hapa nchini, ambayo aidha husababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa duniani, Serikali imejifunza kwamba hatuwezi kutegemea mvua peke yake katika kilimo chetu ambacho ni chanzo kikuu cha chakula hapa nchini.

Kwa kutambua hilo, Serikali inatoa kipaumbele katika uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji ambacho hakitegemei msimu wa mvua.

Kwa mfano, kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*) takribani asilimia 75 ya fedha zinaelekezwa katika uendelezaji wa maeneo ya umwagiliaji. Aidha, ili kuhakikisha kuongezeka kwa uzalishaji na tija kwenye kilimo, katika maeneo ya umwagiliaji na maeneo yanayopata mvua za uhakika; Serikali inatekeleza mikakati ifuatayo:-

(i) Kuhakikisha wakulima wanapata pembejeo za uzalishaji hususan mbegu bora na mbolea kwa bei nafuu na kwa wakati muafaka kupitia utaratibu wa vocha. Tathmini ya awali inaonesha kwamba, kutokana na utekelezaji wa utaratibu wa ruzuku, tija katika uzalishaji wa mazao ya chakula imeongezeka.

(ii) Kuongeza idadi ya wataalam wa ugani kutoka 4,439 waliopo hivi sasa hadi kufikia wataalam 15,082 ifikapo mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Maji na Umwagiliaji zinaendelea kushirikiana kuhakikisha kuwa, Halmashauri za Wilaya zinashirikisha wananchi vijijini kuibua, kuandaa na kutekeleza miradi ya umwagiliaji kupitia *DADPS* ili kuongeza eneo linalotumia kilimo cha umwagiliaji.

**MHE MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru! Nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nini tatizo kwa Tanzania, Misri yenye mto mmoja tu imejitosheleza kwa chakula, Tanzania ambayo ina mito isiyokauka zaidi ya 300 tunaendelea kulia njaa na kuomba omba, kitu ambacho ni aibu na fedheha kwa Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, suala hapa siyo kuwa na mito tu, bali suala pia linatokana na uwezo wa kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji. Kwa hiyo, kama tulivyoeleza kwamba Serikali inashirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na wadau wengine, ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na miundombinu mingi ya umwagiliaji, hiyo itakuwa inatekelezwa mwaka hadi mwaka kutokana na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Salim kwamba, hilo tunalitambua lakini pia tuelewe kwamba uchumi unatofautiana nchi hadi nchi. Nchi ya Misri uwezo wake ni mkubwa kuliko wa kwetu kwa sababu pengine wenzetu wana mafuta ama wana mambo mengine. Lakini kwa suala la Tanzania na sisi tunajitahidi, hata ukiangalia mavuno ya miaka miwili iliyopita ni tofauti na sasa kutokana na hatua hizi hizi ambazo ni za kuendeleza kilimo kupitia kwenye umwagiliaji.

**MHE. ENG. MOHAMMED HABIB MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru! Kwa kuwa, mabadiliko ya tabianchi udhibiti wake ni mgumu na tutategemea yataendelea kwa muda mrefu, na kwa maana hiyo bado nchi yetu huenda pengine tutaendelea kupata ukame; na kwa kuwa, Mipango ya Kilimo cha Umwagiliaji ndiyo ipo kabambe lakini vile vile tunajua kuna nchi nyingi duniani ambazo hazina hata ardhi ya kilimo na hawalalamiki kilio cha njaa.

Je, mbali na mipango ya umwagiliaji na kwa kuwa, nchi yetu kuna miaka ambayo inakuwa na mazao mengi, Serikali yetu itakuwa na mpango gani wa kuhakikisha njaa haitusumbui kwa kuwa na mipango kabambe na tusisingizie ukame tu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimia Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnyaa kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mabadiliko haya ya tabianchi hatuwezi tukajua yataendelea mpaka lini kuathiri nchi yetu, lakini na sisi tuna mipango mbalimbali, nimezungumzia masuala ya umwagiliaji. Lakini pia ipo mipango ya kutoa ruzuku ili wakulima waweze kuzalisha zaidi kwa maeneo yale ambayo mvua zinanyesha vya kutosha. Lakini vile vile tunawashauri wananchi katika maeneo yao kutumia miradi hii ya *DADPS* waweze kuandaa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mipango tuliyonayo kusema kweli ni mingi. Ni kweli kabisa niliishawahi kuongea na wewe kwamba, kuna nchi kama Botswana ambazo hazilimi lakini wananchi wake hawafi njaa, lakini niseme tu kwamba wenzetu wana mipango mingine, nchi ile ina Almasi nyingi sana kiasi ambacho inaagiza chakula kutoka Afrika ya Kusini, wao hawalimi lakini wanaagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, sisi tuna ardhi, tuna mito. Kwa hiyo, tunaendeleza miundombinu iliyopo hatuwezi tukasema kwamba tutaagiza chakula kutoka nje, na nikuhakikishie kwamba katika miaka mitano au sita iliyopita hatujawahi kuagiza chakula kutoka nje na hatujawahi kupata msaada wa kutoka nje. Tunalima kwa kutumia nguvu zetu na wananchi wetu wenyewe. (*Makofi*)

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika kwa kuwa nchi yetu ina takribani heka milioni 29 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, na kwa kuwa maji ya kutosha kumwagilia maeneo hayo yapo, na kwa kuwa, hadi sasa ni asilimia moja tu ya eneo hilo ambayo iko chini ya umwagiliaji.

Je, Serikali haioni kuwa asilimia 75 ya fedha ambazo amezungumza Mheshimiwa Waziri za Programu ya *ASDP*, programu ambayo ina trilioni 2.5 na ambayo inafikia sasa, ambazo zimepelekwa kwenye Halmashauri kwa umwagiliaji.

Je, haoni kwamba fedha hizi hazijatumika kwa kazi ya umwagiliaji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Salim yeye ni Waziri Kivuli wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa hiyo, anayoyazungumza pia tunayazungumza kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba tuna eneo zuri la umwagiliaji lenye ukubwa wa hekta milioni 29 na mpaka sasa hivi tunamwagilia takribani hekta 300,000 tu ambazo ni sawa na asilimia moja.

Lakini niseme kwamba pamoja na kwamba fedha hizi asilimia 75 zinatumwa kule, lakini pia kiasi ambacho tulitegemea tukipate kwa muda wa miaka saba ya mwanzo ya trilioni 2.5 kusema kweli kiasi kinachokuja ni pungufu.

Kwa hiyo, kile kiasi kinavyokuja pungufu na kiasi ambacho kinatengwa ni pungufu basi tunaendelea kutekeleza kutokana na ukubwa wa fedha tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Salim H. Khamis, kwamba tutaendelea kuhakikisha kwamba tunatenga asilimia 75 ya fedha zote za *ASDP* kwa ajili ya umwagiliaji kadri fedha zitakapokuwa zinapatikana.

Na. 76

**Mpango wa Kuwasaidia Wakulima**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH** aliuliza**:-**

Kwa kuwa, zaidi ya asilimia 98 ya wakazi wa jimbo la Iramba Mashariki ni wakulima na wanategemea kilimo duni kwa kutumia zana zilizopitwa na wakati, na kwa kuwa fedha za wawekezaji zilishindwa kuwafikia wakulima kutokana vigezo vilivyotolewa na Benki za Biashara:-

(a ) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha benki ya wakulima ili wakulima wapate huduma ya mikopo?

(b) Je, Serikali imeandaa utaratibu gani wa Mapinduzi ya kweli ya kilimo ili Mtanzania atoke katika kilimo cha zamani cha kulima kisasa?

(c) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kutoa mbolea ya ruzuku kwa Mikoa ya kati kama vile Singida, Dodoma na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na ( c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini na hivi sasa Benki Kuu ya Tanzania ikishirikiana na Mtaalam Mwelekezi inaendelea na mchakato wa utaratibu wa uzalishaji wa Benki hiyo.

Aidha, Serikali kupitia Benki ya Raslimali Tanzania (*TIB*) imeanzisha Dirisha la Kilimo katika Benki hiyo na jumla ya shilingi bilioni 20/= zilitengwa katika bajeti ya Serikali ya mwaka 2009/2010 ili kutoa mikopo kwa wakulima kupitia dirisha la kilimo katika benki hiyo. Aidha, Serikali inaendelea kutoa huduma za mikopo kupitia Mfuko wa Taifa wa pembejeo za Kilimo.

(b) Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2006, Serikali ikishirikiana na wadau wa sekta ya kilimo, inatekeleza Programu ya Kuendeleza Kilimo *(ASDP).*

Aidha, tarehe 3 Agosti, 2009 Serikali ilitangaza azma ya Kilimo Kwanza ambayo inalenga katika kuleta Mapinduzi ya kijani nchini. Utekelezaji wa Kilimo Kwanza unafanyika kupitia *ASDP* na katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya ambapo asilimia 75 ya fedha zote za *ASDP* hupelekwa huko na wakulima wanaibua na kutekeleza miradi yao ya kilimo kupitia Mipango ya Wilaya ya Kuendeleza Kilimo. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2009/2010, Serikali ilitoa ruzuku ya mbolea na mbegu bora za Mahindi na Mpunga kwa wakulima 1,500,000 katika Mikoa 20 nchini ikiwemo Mikoa ya Dodoma na Singida chini ya utaratibu wa vocha.

Kwa mfano, katika Mkoa wa Singida Serikali ilitoa tani 260 za mbolea yenye ruzuku. Aidha, tani 26 za mbegu bora ya Mpunga ilitolewa katika maeneo ya Wilaya za Manyoni na Singida Vijijini. Wakulima wa Mkoa wa Dodoma walipata tani 270 za mbolea ya kupandia na kukuzia.

Aidha, tani 17 za mbegu bora za Mahindi na tani 19 za mbegu bora za Mpunga zenye ruzuku zilisambazwa katika Wilaya za Mpwapwa na Bahi katika Mkoa wa Dodoma. Hivyo basi, hata mikoa ya Kati hususani Dodoma na Singida walipata pembejeo za ruzuku.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na hasa hili alilozungumzia juu ya uanzishaji wa Benki ya Wakulima tunakubali baada ya kusikia Bajeti lakini naomba Mheshimiwa Naibu Waziri anieleze.

Kwa kuwa, kumekuwa na tabia benki nyingi zinapoanzishwa zinaanzishwa mijini hususani Dar es Salaam. Je, kwa hii Benki ya Wakulima ili wakulima waweze kupata huduma iliyo sahihi na kwa wakati, isianzishwe katika maeneo ambayo ni ya wakulima na wanaweza kuifikia kwa haraka na wakahudumiwa? *(Makofi)*

La pili, mwaka 2008/2009 kupitia mfuko wa Pembejeo Halmashauri ya Wilaya ya Iramba iliidhinisha mkopo wa Matrekta kwa wakulima watatu, Nikodemus na Pegwa huyo anaitwa Milimoduo anatoka Msigiri halafu yuko mwingine anaitwa John Tutu anatoka Ulemo na mwingine anaitwa George anatoka kijiji cha Mambata.

Lakini toka mwaka huo mpaka sasa wakulima hao toka wameidhinishiwa hawajapata huo mkopo pamoja na kuanzishwa kwa hili dirisha dogo. Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje ili hao watu waweze kukidhi Kilimo Kwanza?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Juma H. Killimbah, kama ifuatavyo.

Kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Killimbah kwa jinsi anavyowatetea watu wake wa Jimbo lake la Iramba Magharibi, anawatetea kwa kila sekta hususan sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza linahusu benki hii kwamba iweze kuwepo maeneo ambayo wananchi au wakulima wanaweza kuifikia kwa urahisi. Niseme kwamba wazo lake hili ni zuri lakini tusubiri kwanza benki ianzishwe halafu ndipo tutaona kwamba inakwekwa katika matawi yapi na tutatumia taratibu zipi ili kusudi wakulima wote Tanzania waweze kuwa na *access* na benki hiyo.

Pili, kuhusiana na wakulima wake watano ambao hawajapata mikopo ya pembejeo, niseme kwamba mikopo hii ina masharti yake kwamba kama mtu hajatimiza masharti yale kwa kweli hawezi kupata ule mkopo.

Kwa hiyo, ninapenda nionane na Mheshimiwa Killimbah hapo baadaye kusudi niweze kuona kwamba pengine kuna masharti ambayo hawakutimiza tuangalie ni jinsi gani yanaweza kutimizwa ama haiwezekani basi hawatapata. Lakini kusema kweli mikopo ile inatolewa kwa Watanzania wote ambao wamekidhi masharti ya mikopo.

Labda niseme kwamba masharti yale ni pamoja na kuwa na shamba ambalo halipungui hekta 50, kuwa na Hati Miliki ya vitu visivyohamishika yaani kwa maana ya shamba au nyumba, iwe Hati Miliki sawa na trekta ile unayotaka kununua, uwe na ankara kifani yaani *profoma invoice* ya trekta unalotaka kununua lakini pia uwe na andiko ambalo linaonyesha kwamba ni jinsi gani utarudisha mkopo ule. Sasa kama hujatimiza masharti hayo ni vigumu kusema kweli kupata huo mkopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa maelezo ya ziada!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa kwanza kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu makini aliyoyatoa kwa maswali haya yote.

Lakini nataka kuongeza kuhusu Benki ya Kilimo, Mheshimiwa Killimbah anataka kujua ile benki itakuwa na mtandao kiasi gani, kwa namna yoyote ile benki ikianza inachukua muda kuweza kuwa na mtandao wa kila mahali.

Kwa hiyo, ushauri wa Serikali ni kwamba tuwashauri wakulima waanzishe *SACCOS* ili baadaye *SACCOS* zile ziweze kutumika kama vyombo vinavyoweza kumfikishia mkulima mdogo mdogo mkopo kwa sababu hata ukiwa na benki moja Tanzania itakuwani vigumu sana kumfikia kila mkulima mahali alipo.

Ni lazima kuwe na vyombo vya fedha vilivyo karibu zaidi na wakulima ambavyo vinaweza vikatumika kumfikishia mkulima mikopo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali sasa umefika na maswali yamekwisha na muda umekwisha.

Matangazo nikianza na wageni kwanza wapo maafisa waandamizi wa Sektretariet ya Maadili ya Viongozi wa Umma wakiongozwa na Kamishna wa Maadili Mheshimiwa Jaji Stephen Ihema. Pamoja naye yupo Bwana Frederick Mandara Katibu Kitengo cha Viongozi wa Siasa. Naona kama wageni hawa pengine hawajafika, basi nisiendelee na wale wanaofuata.

Pia wako wageni 13 wa Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ambao ni wanafunzi katika Vyuo Vikuu vya Dodoma wanachama wa *CUF* wakiongozwa na Ndugu Edson Mulyowa, Mwenyekiti wa *CUF UDOM* na *Saint John's.* Naomba wasimame niwatambue, wale pale. Ahsante karibuni sana tunawatakia mema katika masomo yenu. (*Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri Dr. James Wanyancha, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi ni wawili ni Ndugu Lyoba Mrema, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Yule pale ahsante sana na Ndugu Lyimo Saimon Ndugu yake Mheshimiwa Dr. James Wanyancha.

Wageni wa Mheshimiwa Castor Ligallama ni kama ifuatavyo. Ndugu Neema Ligallama mwanawe, yule pale, ahsante sana karibu sana, Ndugu Mukabatunzi Derek, rafiki wa mtoto wake, ahsante sana na Ndugu Benito Mwandu mwanafunzi wa *UDOM* mwaka wa pili.

Wageni wa Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela ambao ni wanafunzi wanaosomea Shahada mbalimbali katika Chuo Kikuu cha Dodoma na wanatokea Wilaya ya Kyela wakiongozwa na viongozi wao ambao ni Ndugu Yohana Maziba, Ndugu Itika Godfrey na Mwamengo Amon. Looh!! Hii Kyela wanasoma sana wote hawa wanatoka Kyela. Haya tunawatakia mema katika mafunzo yenu. (*Makofi)*

Wapo wageni wanafunzi 35 na walimu watatu (3) kutoka Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma, haisemekani chuo hiki kiko wapi, lakini kama wapo naomba wasimame ili tuwatambue, aah wale pale. Ahsanteni sana. Pia tunawatakia mafanikio katika masomo mje muungane na Watanzania wengine kusukuma gurudumu la maendeleo ya Taifa.

Wapo pia washiriki saba (7) wa Miss Utalii Vyuo Vikuu Kanda ya Kati ambao wanashiriki mashindano hayo ya Kanda ya Kati leo usiku wakiambatana na Mkurufunzi wao Sarah John wale warembo wale. Ehee, mbunifu wao wa mavazi Diana Magesa na Mratibu wa Mashindano Fabian Njenga. Ahsante sana.

Nadhani nichukue fursa hii kuwa mwaliko Waheshimiwa Wabunge ambao watapenda kuona hatma ya mashindano haya na nani atakuwa mshindi kati ya hao washiriki wa Miss Utalii. Haisemwi ni wapi sijui. Itakuwa *Kilimani Club.* Kuna Mbunge mmoja mbunifu tayari anajua ni wapi.

Tunaye hapa ndani Balozi wa Malaria nchini na mshindi wa tuzo tatu (3) za muziki za *Kili Awards,* Ndugu Nasib Abdi Juma, yule pale. Jina la Kizanzibar hili naona Nasib Abdi Juma, maarufu kama *Diamond.* Bwana mbona unakaa upesi upesi tena , simama tu. Ehee!!!. Huyo ndio *Diamond* na mtunzi wa kibao kikali sana kinaitwa, "Kwetu Mbagala" *(Makofi)*

**Uamuzi wa Spika Kuhusu Malalamiko ya Mhe. John M. Cheyo Kuondolewa Wadhifa wa Uwaziri Kivuli Katika Kambi ya Upinzani**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hakuna matangazo yoyote ya Kamati. Ila sasa nitatoa uamuzi wangu kuhusu tukio lililotokea katika Kambi ya Upinzani.

Nilichonacho hapa ndiyo ushauri wa Watalaam wa Kisheria. Nimeusoma nimeongea na baadhi ya Viongozi. Nilimwita kwa mfano Naibu Kiongozi wa Upinzani, Mheshimiwa Dr. Wilibrod Slaa jana kujaribu kuelewa yaliyotokea. Nia ni kutenda haki ieleweke kwamba, si wajibu wa Spika kuingilia masuala ya "*caucus"* za vyama.

Lakini kama Mbunge amelalamika kama hivi ambavyo alilalamika Mheshimiwa John Cheyo, baada ya adhabu aliyopewa, ni wajibu wangu kuona kama Kanuni zimefuatwa na haki imetendeka. (*Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sitausoma ushauri wote kwani makala ni ndefu. Nitachukua tu sehemu muhimu. Kutambua uwepo wa Vyama vya Upinzani Bungeni na kuwezesha sauti za wachache kusikika kunazingatiwa katika Kanuni ya 15 (1) ambayo ni mahsusi kwa ajili ya kuwezesha uundwaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Imefuatiwa na Kanuni ya 15 (2) ambayo imempa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni mamlaka ya kuteua Wasemaji Wakuu wa Kambi hiyo kwa Wizara zilizopo kuwiana na zilizopo Serikalini.

Aidha fasili ya nne (4) ya Kanuni ya 16 imeelekeza kwamba vyama vyote vyenye uwakilishi Bungeni vinaweza kutunga Kanuni zao kwa ajili ya uendeshaji bora wa shughuli zao za "*caucus*". Hapa Kambi ya Upinzani katika Bunge letu ilifanya hivyo na inazo Kanuni zake ambazo ni nzuri wala haziathiri chochote katika Kanuni za Bunge.

Kwa hiyo, hapa swali lilikuwa ni kujiridhisha. Je, Kiongozi wa Upinzani kwa kuchukua hatua aliyochukua alifuata utaratibu uliopo katika Kanuni za "*Party Caucus*" ya Kambi ya Upinzani? Pili, kama Mamlaka hayo yalitumika kwa mujibu wa kinachoitwa hapa "*Best Parliamentary Practice".* Sasa wataalam wamesema na mimi naafikiana nao na ndio maana nasoma ushauri huu.

Katika kitabu kilichotungwa na watalaam watatu M. O. Kickerson, Thomas Flanagan na Brenda O. Neil waliochambua Bunge la Uingereza ambao mfumo wake na sisi tunaufuata yaani *Parliamentary System* kiitwacho *Best Parliamentary Practice* waandishi hao katika eneo hili walisema hivi nanukuu kwa kingereza "*Party Discipline in Parliament is normally maintained through a method known as "whip Line" whereby the party's caucus Parliamentary Leader is entrusted with the duty of maintaining discipline among members of his Party".*

Waheshimiwa Wabunge, isitoshe hao hao wanasema hivi, kwa kiingereza tena ninanukuu. *"The necessity of proper conduct of Party Politics in Parliament has led to the strengthening of Party discipline in all Parliamentary Systems. A member's loyalty to the Party caucus takes precedent over personal views or loyalty to constituency. A member who does not support the party caucus position on the floor of the House or in a committee can be punished in various ways". (Makofi)*

Sasa kwa kuzingatia maelezo hayo, kwa mujibu wa *Parliamentary Practice* na Kanuni tulizonazo. Jana nilitaka kujiridhisha kwamba, Mheshimiwa John Cheyo alishirikishwa katika maamuzi ya Kamati ya Upinzani kuniwezesha kuelewa uzito wa uamuzi wa Kambi ya Upinzani. Nilihakikishiwa kabisa alishirikishwa na isitoshe alisaidia hata kuwakusanya wenzie ili wahudhurie *party caucus. (Makofi)*

Kwa kuzingatia yote hayo sasa, kitendo cha Mheshimiwa John Cheyo, kuunga mkono Bajeti ya Serikali ili hali wana msimamo anaoujua wa Kambi ya Upinzani kwamba, wasiunge mkono, ni kitendo cha utovu wa nidhamu, hasa ukizingatia kwamba Bajeti ya Swerikali. Hata lingekuwa upande wa pili, Mbunge wa Chama Tawala (CCM) ambaye angepiga kura kuikataa Bajeti naye pia angeshughulikiwa ipasavyo. (*Makofi*)

Kwa kuzingatia ufafanuzi huo ni dhahiri basi kwamba kitendo alichokifanya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni cha kumchukulia hatua za kinidhamu Mheshimiwa John Cheyo kwa kosa la kwenda kinyume na msimamo wa kimsingi uliowekwa na Kambi yake ni halali kikanuni na kiutaratibu wa Kibunge. Basi hiyo ndiyo hali itakayotuongoza siku zijazo kwa pande zote mbili, upande wa Serikali na upande wa Upinzani. (*Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2010/2011 - Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hadi kufika jana nawashukuru sana Wenyeviti waliokuwa hapa mezani, mjadala ulifika pazuri tu.

Sasa niliona ni busara kwamba Waheshimiwa Wabunge wawili ambao ni walemavu wapate nafasi, halafu kuna masuala mahsusi yaliyoulizwa ambayo yanahusu sekta mbalimbali za Wizara kwa sababu hoja ni ya Waziri Mkuu basi walijaribu kuhoji baadhi ya mambo ambayo yapo katika sekta nyingine.

Kwa hiyo, nitawaita Waheshimiwa Mawaziri sita (6) ili waweze kutoa ufafanuzi baada ya hapo tutakuwa na dakika 60 za Waheshimiwa Naibu Waziri na Mawaziri wawili waliomo katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mawaziri wao wana dakika zisizozidi 60 yaani Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Phillip S. Marmo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mheshimiwa Cellina Kombani na Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Aggrey Mwanri. (*Makofi)*

Baada ya wachangiaji wengine ambao ni dakika kumi kumi wao wana dakika zisizozidi 60. Kwa mpangalio huo sasa namwita Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda. (*Makofi)*

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba nzuri iliyotolewa na Waziri Mkuu pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Awali ya yote kabla sijasahau maana yake kengele isije ikanigongea nasema naunga mkono asilimia mia moja. (*Makofi)*

Mimi nimeona Bajeti nyingi zinapitishwa hapa katika kipindi chote cha miaka mitano (5) lakini kipindi hiki nimeona tumefika mahali ambapo kweli hali yetu ya kiuchumi inakwenda sawasawa na ndiyo maana nasema kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ilikuwa ni nzuri sana. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Cellina Kombani, Mheshimiwa Phillip Marmo, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kusema kweli nawashukuru sana kwa kujikunja maana mmefanya kazi nzuri sana.

Nawatakieni wote kila la kheri haya maneno wanayosema wenzetu haya Mavuvuzela hao, hebu mngeziba masikio kidogo halafu ndiyo maana yake wamewekwa humu ndani kwa kazi hiyo hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, msiwajali sana wakawanyima usingizi. Endeleeni na kazi yenu sisi tupo pamoja na mimi nasema kwamba mwenendo huu wanaokwenda hao mavuvuzela nasema CCM ushindi ni lazima. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Mpanda, nadhani una maana Mavuvuzela ni Wabunge au?

**MHE. DR. SAMSON MPANDA:** Nina maana wanaonyemelea majimbo ya Uchaguzi. Nikiendelea naomba dakika zangu ziongezwe.

Nawashukuru tena wananchi wangu wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, kwa kunipa nguvu, kwa kunipa kila hali ya msaada wakati wote nilipokuwa naumwa na ninavyoumwa na kusema kweli sikupata matatizo yoyote. (*Makofi)*

Kwa kweli wamenisaidia sana na nawashukuru sana na nategemea kwamba sikuwaangusha na sintowaangusha endapo watanipa nafasi hii ya kuwaongoza tena, japokuwa ulemavu huu ni jambo la kawaida tu. Wote hapa sisi ni walemavu watarajiwa na hakuna mmojawapo hapa duniani ambaye anasema kwamba atakufa kama alivyozaliwa. *(Makofi)*

Wote sisi ni walemavu watarajiwa. Sisi tu walemavu ndiyo nakubali, lakini hakuna mtu yoyote ambaye ana stakabadhi au barua kutoka kwa Mwenyezi Mungu inayosema kwamba anaanza na hali hii na atamaliza na hali hii. Kama yupo basi nasema mpigieni kura, lakini nadhani kama hakuna mtu kama huyo hao ndio watu wa ajabu ajabu tunasema.

Jambo la pili nililotaka kusema ni kwamba niseme Waziri Mkuu amezungumzia masuala yote muhimu ambayo Serikali yetu inaikumba. Sasa hivi maendeleo kusema kweli yanaonekana na jimbo langu la Kilwa Kaskazini, kusema kweli linaonekana kwenye ramani ya Tanzania na kusema kweli sina haja ya kusema kwamba mambo yamekwenda vibaya, ila tu nina mambo mawili au matatu ambayo nataka niyazungumzie.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, barabara za kwetu kule jamani mziangalie maana hata Waziri Mkuu mwenyewe anapokuja kule kwetu Kilwa anapita pwani. Kilwa imegawanyika upande wa Mashariki na Magharibi upande wa Kipatimu, sasa hawezi kufika kwa sababu ya hali ya barabara ilivyo. Sisi tunaona kama tumetelekezwa kwa namna fulani, angalau hata Waziri wake, Mheshimiwa Mwanri au mwingine, sijamsikia amepita kuja kule kwetu; hakuna. Yote najua ni kwa sababu ya hali ya barabara ilivyo. Sasa naomba kwa kipindi kijacho au kwa kipindi cha hivi karibuni, mchukue nafasi kidogo na ninyi mje kuliona Jimbo la Kilwa Kaskazini upande wa Magharibi, mwone hali inavyokwenda na wananchi wanavyofanya shughuli zao na maendeleo wanayoyapata. Nitashukuru sana kama mtafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ufuta. Mheshimiwa mwenzangu hapa wa Kambi ya Upinzani alisema, watu wameuza ufuta kwa shilingi 700 lakini ninavyoona mimi si kweli kwa sababu ufuta kweli umepungua bei kwa sababu ya stakabadhi ghalani. Stakabadhi ghalani ni Sera ya Nchi yetu. Sasa yeye anasema kwamba, wanauza shilingi 700 ni wapi; Kilwa Masoko au wapi? Hapo mimi ndiyo sijaelewa. Kwa kwetu sisi tunauza shilingi 1000 na zingine tumeambiwa kwamba tutalipwa, isipokuwa hawa wenzetu wa Kilwa Kusini au wa Kilwa Masoko, labda pengine elimu ya mambo ya stakabadhi ghalani hawajaipata kikamilifu ndiyo maana wanalalamika sana. Kwa hiyo,

ninapendekeza kwamba, hawa watu wapewe elimu badala ya kukitukana Chama cha Mapinduzi; wanaandamana wanafanya nini, wanasema kwamba wanatuibia, nadhani huo si ustarabu wa kuishi. Halafu mambo ya kusema CCM wezi, basi kama ni wezi Mahakama zipo na Mahakama si CCM, Mahakama ni Serikali inayojitegemea, tena mimi namuunga mkono sana Mkuu wangu wa Mkoa, Bwana Sadiki Meki Sadiki, ambaye anajaribu sana kutuliza haya mambo. Hawa watani zetu wanakuja na maneno ya ajabu ajabu, mimi nazungumza sana ninapokuwa Jimboni lakini wananielewa, lakini upande wa pili huko sijui wenzangu kama wameacha au vipi. Yote kwa yote, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali usiwasikilize sana, mimi kwa upande wangu shuwari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kabisa; nilikuwa nimeomba kwa Mheshimiwa Celina Kombani, kuhusu Jimbo la Kilwa Kaskazini. Jimbo la Kilwa Kaskazini ni kubwa mno jamani; kutoka Malendego mpaka Zinga Kibaoni, Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe aliona; alishindwa kufika kule na kulala Masoko ikabidi atoke pale Masoko mpaka Zinga Kibaoni na Zinga Kibaoni kwenyewe alifika saa mbaya kabisa akaenda mpaka Liwale. Ni mbalimbali kweli, halafu ukitoka Ngarambi kuja Masoko ambako ndiko kwenye Makao Makuu ya Wilaya ndiyo usiseme.

Mheshimiwa Spika, naomba Jimbo langu ligawanywe. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilitamka kwamba, kutakuwa na Mawaziri idadi yao sita watakaoongea, sikuwataja na bahati mbaya naona baadhi yao hawamo humu Ukumbini. Kwa ajili ya maandalizi, Mawaziri waliopangwa kuongea ni Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe - Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi; Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa - Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii; Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa - Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu; Mheshimiwa Stephen Wasira naye alikuwepo na atarudi na wawili hawakuja kabisa; Mheshimiwa Mwandosya, nadhani yupo kwenye ziara na Mheshimiwa Rais, pamoja na Mheshimiwa William Ngeleja. Sasa kwa hao wawili sijui itakuwaje, lakini nitaanza na wale waliopo ili kuona kama pengine hata Naibu Waziri katika sekta hizo mbili, Sekta ya Nishati na Madini na Maji na Umwagiliaji. Kwa sasa tunaendelea na Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji.

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, sina budi kukushukuru kwa kunipatia nafasi asubuhi hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha asubuhi hii kusimama humu na mimi kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa muda wote huu wa miaka mitano kuingia katika Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nashukuru miaka mitano hii yote imekaa vizuri, nimejisikia vizuri, nimepata ndugu, baba, mama na kaka. Kwa Wabunge wote, natoa shukrani kwa mchango wao, kwa msaada wao, kwa maelekezo yao na hasa zaidi shukrani nyingi kwa Mzee Shellukindo, amenilea vizuri sana; kwa hiyo namshukuru, Mungu ambariki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Unasema amefanyaje amekulea? *(Kicheko)*

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Spika, amenipa maelekezo na kunisaidia. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Haya ahsante.

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Wasaidizi wake wote, kwa hotuba yao nzuri ya bajeti; imeeleweka, inafahamika na inasomeka na haina kasoro. Kuna usemi kwa sisi Waislam unasema *Kamilillahi taa'llah;* yaani aliyekamilika ni Mwenyezi Mungu tu. Kuna usemi kwenye Injili ya Yohana unasema Sote ni Wakosefu. Kwa hiyo, nasikitishwa na wale wote ambao hawayaoni mema, hawayaoni ya maana, hawayaoni yaliyotendeka. Wao yote wanaona ni upungufu na yote ni kasoro. Kwa hiyo, nasikitishwa sana na watu hao, warudi wakasome vitabu. *(Makofi)*

Mwenyezi Mungu katupa vidole vitano; hivi vyote vina tofauti. Kwa hiyo, tofauti hazikosekani; kuna chembamba na vinene. Huu ni mfano na kwa binadamu sote mfano hi huu vidole. Naipongeza sana Ofisi ya Waziri Mkuu, kutokana na kero za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano. Kwa hiyo, napongeza sana kwamba, baadhi ya kero hizo zimefanyiwa kazi na nina imani zilizobakia zitafanyiwa kazi na kukamilika.

Mheshimiwa Spika, nikizungumza kuhusu elimu nasikitishwa, tumejenga sekondari watu wanasema hazina maana. Waswahili wanasema; utanunuaje mbeleko na mwana hajazaliwa? Kwa hiyo, sisi tumejenga majengo; walimu, madawati na vingine vitakuja baadae. *(*Makofi*)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu afya tunashukuru pia huduma za afya zimeboreka mijini na vijijini, upungufu haukosekani sisi si malaika, tunasaidiwa na Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, mipango anatusaidia Mungu, hatuwezi kukamilisha mambo yote kwa pamoja, lakini hata hivyo kwa hatua iliyofikiwa tunashukuru. Ila hapa kuna tatizo kwa upande wa Wizara ya Afya, bado wazee wanasikitika wakienda hospitali kuhudumiwa kutokana na hali zao na Sera iliyowekwa kwamba, wasichangie lakini bado baadhi ya watendaji wetu wanatuharibia kazi. Hata ndugu zangu walemavu nao wamenilalamikia, wakienda na wao wakishashughulikiwa wanaambiwa dawa hakuna, inakuwa ni vigumu kupata pesa za kununua dawa. Kwa hiyo, wahusika wote naomba wayashughulikie masuala haya kwa kuelimishwa hawa watendaji wetu.

Mheshimiwa Spika, kuna hii habari nimeiuliza sana kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu kile Kituo cha Manyanya Kinondoni. Kituo kile hatima yake vipi? Kinafanyaje? Wale waliopo pale wanataka kujua hatima yake na itashughulikiwa vipi na Serikali. Naomba nipate jibu kutoka kwa Waziri wa Afya atakapokuja.

Suala lingine ni kuhusu hawa watendaji wetu ambao hawana uaminifu wala uadilifu kwenye shughuli zetu mbalimbali za kimaendeleo za kutumikia wananchi; washughulikiwe ipasavyo kwani wanataka kutuharibia maendeleo yetu na nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hao wote wanaosema kwamba, hakuna lililofanywa, Ilani wanatembea nayo na wao wala haijawahusu kwa nini na wao hawatengenezi Ilani zao? Hawakuzuiwa na wao watengeneze wasome na wananchi watambue. Kwa hiyo, kuhusu umaskini; umaskini si ajabu na umaskini upo maisha hautakwisha mpaka mwisho wa dunia. Mimi nilipata safari mwaka 1993 nilikwenda Indonesia kwa kozi fupi nikapita Bombay, Bombay ndiyo Mji wa India na India imeendelea na kila kitu. Nilishangaa pale *airport* nilikuta Wahindi tele wakaniambia bahashishi bahashishi, sasa wale nao ndiyo vipi na India tumeambiwa imeendelea? Nilishangaa ikabidi nivue miwani yangu nikawaambia kama ni bahashishi mnipe mimi. Kwa hiyo, kwenye kuendelea utajiri upo, umaskini upo na wakati upo. Tusikae tukilaumiana tu, hakuna ya kusaidiana wala mazuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mimi ninaushukuru Muungano, naishukuru UWT, kwa kutuwezesha watu wenye ulemavu wanawake kuingia katika Bunge hili na tunawashukuru tunasikia wametuongezea nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nautakia Uchaguzi wetu Mkuu mwezi wa kumi uwe uchaguzi wa kheri, uwe wa salama, uwe wa maendeleo mazuri, pia nahimiza kuhusu masuala ya watu wenye ulemavu ambapo Mkataba wa Kimataifa ulileltwa hapa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu na karibuni tumepitisha Muswada wa Sheria; kwa hiyo, ninaiomba Serikali iyafanyie kazi ili na sisi tule matunda na tufaidi nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, hawa wafanyakazi wanaodanganyana na kubabaishana, kuna Hotuba ile ya Hayati Mwalimu Nyerere inasema wao kila wakikaa wanadai tu, wanadai wanamdai nani na hii ni nchi yetu tushirikiane tulete maendeleo pamoja na tufanye kazi pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii na naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zuleikha kwa mchango wako, umejaa hekima na ni wa dhati kweli kweli. Waheshimiwa Wabunge, kuna Waheshimiwa Wabunge wawili ambao walirukwa katika mfululizo wa wachangiaji. Kwa hiyo, nitawaita sasa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Fuya Kimbita atafuatia.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Ni kweli jana ndiyo nilitakiwa nichangie na nilikuwa na udhulu Jimboni nikaondoka saa tano usiku nimerejea hapa alfajiri ya leo. Kwa hiyo, nilipofika niliikumbusha Ofisi yako kwamba, jana nilitajwa jina lakini bahati mbaya sana sikuweza kuwahi kuchangia na sasa nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu linakamilisha au linakaribia kukamilisha kuandika historia ya utumishi wake wa miaka mitano ya Awamu ya Nne ya Taifa letu mara baada ya Bunge hili kumaliza Mkutano huu. Hakuna mashaka kwamba, chini ya

Uongozi wako, Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, limekuwa Bunge la Viwango na Bunge ambalo limejitahidi sana kukidhi matarajio ya Watanzania kwa kiwango kikubwa. Tumelifikisha Bunge hili mahala ambapo Watanzania wana hamu ya kulisikiliza Bunge lakini si kusikiliza tu, wanalifurahia Bunge na Mabunge ya Nje yanakubali kabisa na watu makini wanakubali pia kwamba, Bunge lako ni la Viwango na linasimamia maslahi ya nchi kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa utumishi wake uliotukuka, lakini zaidi ninaipongeza kazi kubwa ambayo ameifanya kwa muda tangu ameteuliwa na Mheshimiwa Rais. Jimbo langu la Simanjiro haliwezi kumsahau na kusahau mchango wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kulitambua tatizo kubwa la maji ya Wilaya ya Simanjiro na kuwa Waziri Mkuu wa nchi yetu ndani ya Bunge hili kueleza kwamba, japo Watanzania wana matatizo makubwa ya maji, lakini Wilaya ya Simanjiro inaongoza. Najua hakupendelea na hana tabia ya kupendelea lakini alieleza hali halisi.

Mheshimiwa Spika, ninajua yote haya tumeyafanya na kulifikisha Bunge letu mahala stahiki kutokana na uongozi na ushirikiano wa mtu anayeheshimu mgawanyiko wa majukumu ya mihimili mitatu ya dola na huyu si mwingine ni Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete. Unaweza kusema lolote unaloweza kusema, lakini Mheshimiwa Kikwete, kwa miaka yake mitano ya uongozi wa taifa letu, amejitahidi sana kutembea kwenye maneno yake. Hakuna mashaka kwamba, kwa mwaka huu wa uchaguzi, watanzania wakifanya tathmini ya kweli, watakuwa hawana sababu yoyote ya kutomrejesha madarakani Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete na kwa wale wote wenye nia ya kugombea na Mheshimiwa Kikwete ni haki yao wanakaribishwa ila wafahamu Waswahili wanasema mbuyu hauangushwi kwa kisu cha kukatia nyanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri pia kwamba, taifa hili linatarajia mara baada ya uchaguzi ujao wa mwezi wa kumi, liendelee kuwa na Rais makini na liendelee kuwa Bunge litakaloendelea kutetea maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa Wananchi wa Urambo wakikuchagua wewe na nina hakika watakuchagua, sioni ni kwa namna gani Wabunge walioko leo na watakaokuja wasikuchague kwa mara nyingine kuliongoza Bunge hili la Viwango na kuendelea kuiweka nchi yetu katika rekodi ya Dunia na kuweka mahali ambapo sisi tutaendelea kuheshimiwa katika Mabunge ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, najua kwa kutimiza wajibu huu wa Mbunge yeyote makini, upo uwezekano wa kukanyaga vidole vya watu na ninajua kwa miaka mitano tumekanyaga vidole vya watu hasa pale tunapogusa maslahi ya watu wachache. Watanzania walio wengi wameridhika na ndiyo maana nina imani watakuchagua wale wa Urambo, Watanzania watamchagua Kikwete na Bunge lijalo *Inshallah* linaweza kuendelea kukuchagua wewe kuwa Spika wa Bunge hili ukisharudi hapa na ninaona afya yako ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wanaweza kusema Ilani ya Uchaguzi tumeahidi lakini hatukutimiza. Ninachukua nafasi hii, kuwahakikishia Watanzania, tuliyoyaahidi tumeyatekeleza na ni imani yangu kuwa, Watanzania hawana sababu kwa nini wasiturejeshe tena tuendelee kutekeleza yale ambayo yako mbele. Wanasimanjiro wanajua kwamba, wakati tulipochaguliwa, Wilaya ya Simanjiro kwa kiwango cha elimu ilikuwa nyuma. Mtihani wa Darasa la Saba, Wilaya ya Simanjiro ilikuwa ya mwisho kwa Mkoa wa Manyara, kwa miaka mitatu mfululizo Wilaya ya Simanjiro imekuwa Wilaya ya kwanza kwa Mkoa wa Manyara na kwa mwaka huu mtihani uliopita sisi ni Wilaya ya pili Kitaifa kwa kufaulisha na kufanya vizuri kwenye Mtihani wa Darasa la Saba bila kujali mazingira ya umbali wanakotoka watoto wa wafugaji kwenda shule.

Mheshimiwa Spika, hatua hii ni ya kujivunia na ninapenda kuchukua nafasi hii, kuwapongeza walimu wote wa shule za msingi katika Wilaya Simanjiro, kwa kuijengea Wilaya yetu heshima ya kuwa Wilaya ya pili kwa Mtihani wa Darasa la Saba kwa mwaka uliopita. Ninajua siyo muhimu sana kutoa pongezi, lakini wakati mwingine siyo vyema kuwa mwizi wa fadhila. Nichuke nafasi hii kumwomba sana Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wanaomsaidia, kuendelea kutambua tatizo letu la maji, tumechimba visima kadhaa pale Orkesumet, tumechimba kisima kimoja Lormorijoi, tumechimba kisima kimoja Narosoito**,** tumechimba kingine eneo la sekondari, kingine tumechimba Lekayanga na pia tumechimba kisima kingine Loonderkes; hivi ni visima ambavyo tumefanikiwa kupata maji.

Mheshimiwa Spika, tumechimba vingine Namalulu, Loswaki, Engonongoi, Mbuko na vyote hivyo na vingine zaidi ya kumi ambavyo naogopa muda wa Bunge unaweza kuwa ni mfupi, lakini hatujakamilisha miundombinu yake ikiwemo matanki ya kuhifadhia maji kwa maana ya maeneo ambayo mifugo inakunywa maji na maeneo ya binadamu kuchota maji. Imani yangu ni kwamba, Serikali hii ya Awamu ya Nne iliyo sikivu itaendelea kututazama Wananchi wa Simanjiro kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kama unavyofahamu, mara baada ya Kikao hiki cha Bunge, tutakuwa na likizo ya kutoka mwezi wa saba tutakapovunja Bunge na kurudi mwezi wa kumi. Mimi ninaita ni likizo kwa sababu ninajua Wananchi wa Simanjiro wamenieleza kwamba ni likizo na kwamba, mwezi wa kumi ninarudi kutafuta moja ya viti vilivyoko hapa. Sina tabu na Kiti nilichokikalia hapa, lakini nichukue nafasi hii kumwomba Waziri Mkuu kwamba, kwa muda huu ambao tutakuwa likizo, aangalie mambo makubwa mawili:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara katika Wilaya ya Simanjiro, kulikuwa na eneo ambalo lilikuwa linadaiwa kuwa ni Ranchi ya Olmoti inayogusa Vijiji vya Terrat, Nadonjukin, Sukuro, Kitiengare, Naberera na Okulu. Eneo hili bado linanyemelewa na wawekezaji bila kufuata utaratibu uliowaelekeza; uliwaelekeza kwamba, waende kuwabembeleza Wananchi wa Vijiji vile ili wapate ridhaa ya Mikutano Mikuu ya Vijiji katika eneo hilo ambalo wanalitegemea kwa malisho, bado kuna baadhi ya watu ambao wameamua kufanya kazi ya udalali ambao ni Viongozi na Watendaji katika Serikali unayoiongoza, ambao wameamua kubeba bango kuzunguka na kuondoka maofisini kwa kushawishi Wananchi watoe maeneo hayo ambayo

wanayategemea kwa malisho yatolewe kwa mwekezaji huyo na kusahau maslahi ya walio wengi (wafugaji).

Mheshimiwa Spika, inawezekana hiki ndicho chanzo na ninataka niwahakikishieni ndiyo chanzo cha baadhi ya migogoro yetu na baadhi ya Viongozi wengine kwenye runinga na kwenye maeneo mengine. Nilipoomba Ubunge, niliwahakikishia Wananchi wa Simanjiro mambo kadhaa; moja niliwaambia kwamba, nitatimiza wajibu wa mwakilishi makini na sitamwomba radhi mtu yeyote katika mambo yenye maslahi kwa wananchi lakini sitavunja Sheria. Nilichokuwa ninafanya ni kutetea maslahi ya wananchi wangu na ninaomba kwa muda wa likizo yangu, mhakikishe kuwa, wananchi wale hawanyang'anywi eneo lao. Nimwombe pia Waziri Mkuu na Waziri Ngeleja, wahakikishe Wananchi wa Mererani waliokuwa wanapitishwa kwenye *scanner* na Kampuni ya *Tanzanite One* ambao sasa hivi wanaendelea kufanya *lobbying* ili *scanner* zile ziendelee kurejeshwa, taarifa ya watu wa mionzi zinasema kuna vijana walioathirika na mionzi ile ambayo inatumika kukagua mizigo pale uwanja wa ndege, kama mnayoona kuna *scanner* au kuna eneo lingine ambalo binadamu anapita na kama una chochote pale itasema lakini mzigo unapitishwa kwenye *scanner* maalumu.

Mheshimiwa Spika, *scanner* hiyo ya kupitisha mizigo ndiyo hiyo inayofanana na *scanner* wanayopitishwa Watanzania katika maeneo ya Mererani na hasa katika Mgodi wa *Tanzanite One*. Mgodi pekee unaotumia *scanner* ambayo hakuna mahali pengine katika Nchi za Afrika ya Mashariki na Kati, inayotumia *scanner* za aina hiyo. Serikali yetu ikilinyamazia hili, itakuwa inahujumu roho za Wananchi. Ninamwomba Waziri Mkuu, asikubali hilo lifanyike. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, anayetujalia wingi wa rehema. Nami naitumia nafasi hii pia, kuipongeza Serikali yetu; ni Serikali makini inayoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda pamoja na Mawaziri wote na Watendaji wengine wote Serikalini. Pia nisiwe mchoyo wa fadhila kuishukuru Serikali hii ya Awamu ya Nne, kwa mambo makubwa na mazuri iliyotufanyia katika Wilaya yetu ya Hai. Kwa niaba ya Wananchi wa Hai, naomba niishukuru sana kwa kutaja machache tu nianzie na kile kitu kibaya ambacho kinajulikana kama njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuja kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikamlilia kilio cha uhaba wa chakula kule Wilayani Hai. Kwa kuanzia, maeneo ya tambarare tukapata chakula lakini hata milimani kulikuwa kuna upungufu nako tuliweza kupata chakula cha msaada. Nami kwa niaba ya Wananchi wenzangu wa Wilaya ya Hai, napenda niishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Hatukuishia hapo, Serikali ya Awamu ya Nne imeendelea kutufanyia mambo makubwa katika masuala yote ya kijamii; huduma za afya, elimu ambapo kwa upande wa elimu, Wananchi wa Wilaya ya Hai ndiyo wanaofahamu idadi kamili ya sekondari ambazo zimejengwa katika kipindi hiki na kuondoa uhaba uliokuwepo hapo siku za nyuma. Upande wa maji safi na salama, Wananchi wa Wilaya ya Hai wanatambua vizuri

kwamba, tutafikia asilimia ngapi tukimaliza ule mradi mkubwa unaoanzia Machame Kaskazini hadi maeneo ya tambarare ya kule Mkalama.

Mheshimiwa Spika, lakini upande wa miundombinu, Serikali imeendelea kushirikiana na sisi kama Halmashauri ya Wilaya ya Hai kwa kuimarisha miundombinu yetu. Barabara kutoka Boma Ng'ombe - Longoi hadi kule Kikavu Chini - TPC inapitika vizuri sana. Barabara kutoka kwenye Jiwe hadi upande wa Masama nako inapitika na hivi sasa tunavyozungumza, Mkandarasi yuko kule anaendelea kuikarabati ile barabara. Haikuishia hapo, ipo barabara kutoka Lukani kuzunguka hadi maeneo ya Losaa kwa Mzee wetu Elinewinga, nako inaendelea kutengenezwa pamoja na barabara nyingine lakini zaidi ya yote, Serikali yetu imetupatia zile Kata mpya nne za Kiserikali ambazo tuliziomba miaka mingi sana.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Kia, Weruweru, Narumu na ile ya Masama Kati, ninazidi kuishukuru Serikali sana kwa msaada huo. Kilikuwepo kilio kikubwa kwa ile Tarafa ambayo ni kubwa kuliko Tarafa tatu tulizonazo katika Wilaya yetu ya Hai, maana tunazo Tarafa za Lyamungo, Machame na Masama cha hitajio kubwa sana la barabara ya Kwasadala kwenda Masama kujengwa kwa kiwango cha lami. Mimi nilipomwomba Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete wakati wa kampeni pale Boma Ng'ombe mwaka 2005, aliitikia na hivi sasa tunavyozungumza ile ahadi inaendelea kutekelezwa. Mkandarasi yuko barabarani anasubiri tu mvua zisimame ili kazi iweze kuanza. Ninaishukuru sana Serikali na kuipongeza.

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni nzuri kama wazungumzaji wengine walivyotangulia kusema na mimi naomba niiunge mkono. Kwa sisi tuliosoma hesabu hasa *pure mathematics,* nikisema naunga asilimia mia kwa mia ina maana naunga kwa asilimia moja; mimi naunga kwa 100%. Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ambayo tunatarajia itawasilishwa katika Bunge hili, mimi ninaikubali kabisa, ninaomba ije haraka na tuweze kuipitisha kwani Mataifa mengi yaliyoendelea yanaweza kuwa yanashirikiana baina ya Sekta Binafsi na ile ya Serikali. Nizidi kuishukuru Serikali kwa sababu imezidi kusemea kilimo, kwa maana ya ruzuku katika pembejeo, mbegu na madawa; ni hatua kubwa mno na ya mapinduzi katika kilimo chetu.

Mheshimiwa Spika, pale Wilayani Hai sasa hivi tunazidi kumwomba Mwenyezi Mungu, mvua zimalizike vizuri na tunatarajia kuvuna vizuri. Kwa kiwango kikubwa, hayo mavuno makubwa na mazuri tunayotarajia hivi sasa, yanatokana na msaada mkubwa unaotoka Serikalini na kupata ruzuku kwenye mbegu na mbolea. Ninazidi kuishukuru Serikali na kuipongeza na kuiomba iendelee kufanya hivyo hivyo ili wananchi wetu waondokane na baa la njaa. Kilimo hiki hakitakuwa kizuri au endelevu kama tutaendelea na utaratibu tulionao wa jembe la mkono. Nazidi kuiunga mkono Serikali izidi kuhimiza Watanzania wenzetu kuwa kilimo chetu kiendelee kufanywa kiwe cha *mechanization* zaidi kwa kutumia *machine* au vyombo vya ziada katika kukiwezesha kiwe kizuri.

Mheshimiwa Spika, ningeomba tusiendelee kutegemea zaidi mvua, tunayo mito ya kutosha hapa nchini mwetu ambayo tukiitumia vizuri, tutaondokana na baa la njaa na

tutalisha nchi zinazotuzunguka. Kuthibitisha yote haya, kwa upande wa umwagiliaji, Wilayani Hai tumedhihirisha hivyo. Nilileta kilio kuhusu Banio la Mijongweni pale na ile mifereji mingine ya kwa Musa Mwijanga na sehemu nyingine za tambarare. Ninaishukuru Serikali kwamba, lile banio limekamilika na juzi katika Mbio za Mwenge tumelizindua. Kwa hiyo, kilimo cha umwagiliaji ni kizuri, kitatusaidia sana. Kwa upande wa mifugo ni kwamba, mwaka juzi niliuliza swali kuhusu mizani kwenye maeneo yetu ya minada na ni wazo au jambo ambalo linawezekana kabisa badala ya kuuza mifugo yetu kwa kuiangalia kwa macho tu, ningeomba mifugo yetu tuiuze kwa kupima kwenye mizani.

Mheshimiwa Spika, kwa mtindo huo, inawezekana mfugaji wetu na mkulima watafaidika zaidi. Suala la Ushirika; nizidi kusisitiza kwamba ni muhimu lakini pia tuvisisitize Vyama vyetu vya Msingi vielewe kwamba, vinalo jukumu au wajibu wa kutimiza uwajibikaji wao kwa wanachama wao. Viongozi wa Vyama vya Msingi siyo kwamba, wao ndiyo wenye vile vyama bali vyama vile ni vya wanachama wote. Natumaini wanaohusika watakuwa wananielewa, kwa sababu kuna baadhi ya maeneo magawio yanayopatikana kutokana na mapango mbalimbali wanayopangisha, sehemu kubwa ya yale mapato yanayopatikana badala ya kwenda kwa wananchi, yanatumika na Uongozi; siyo sahihi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Uendelezaji wa Mifumo ya Masoko ni jambo muhimu na sisi kule Hai tunashukuru kwamba, Soko la Kwasadala linafanya kazi vizuri. Juzi tu katika Mbio za Mwenge, tumeweza kuzindua soko la walaji pale Boma Ng'ombe, ambalo litakuwa linafanya kazi siku saba za wiki. Tunaishukuru Serikali kwa kuungana na sisi.

Utaratibu wa fedha vijijini, kuna mipango midogo midogo kabla hatujafikia SACCOS labda vikoba na watu wengine, lakini tutaziimarisha SACCOS zetu ili tuweze kuanzisha Benki za Wananchi kule vijijini.

Mheshimiwa Spika, upande wa ardhi ni kweli ni lazima tupime ardhi yetu ili kuondoa migogoro mbalimbali inayotukabili na hatimaye tuweze kuwa na makazi bora ambayo kila mmoja angependa aishi. Upande huo wa makazi, niruhusu pia niweze kuishauri Serikali katika lile eneo la Sheria ya Majengo; ni muhimu sana na nilichangia katika Bunge lililopita. Baada ya kuwa na Sheria nzuri kabisa katika hii *Construction Industry,* tunalazimika tuwe na Sheria ya Majengo. Tukiendelea kuzembea katika eneo hili, muda siyo mrefu tutakuwa na kilio kikubwa sana hapa Nchini Tanzania. Tunayo majengo mengi yanayojengwa chini ya viwango vinavyotakiwa, Bodi ya Wakandarasi, *Board of Architects and Quantity Surveyors* ilishapiga kelele sana katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, nami nipende kusema jambo hili na kwa msisitizo wa hali ya juu, nilizungumza na Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, Waziri wa Miundombinu, naye aliniahidi kuwa, Sheria ile iko mbioni kuja. Mimi nilikuwa naomba ile Sheria ni muhimu ije, tusije tukachelewa tukajikuta mwana si wetu kwa sababu tutaishia kwenye kilio kikubwa.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa viwanda, ninazidi kuikumbusha Serikali, tunalo eneo la *Machine Tools,* ambalo tulishafanya mazungumzo na NDC, tunachosubiri sasa hivi ni utekelezaji ili tuweze kuona vile viwanda vikianza kufanya kazi. Kwa maana ya kujengwa pia eneo la EPZ pale eneo la KIA, kwa sababu ya kuutumia vizuri Uwanja wetu wa KIA.

Mheshimiwa Spika, ningeomba pia kukumbusha kwamba; ni muhimu sana tuzalishe bidhaa za kutosha na tuweze kupeleka nje ya nchi, kwa maana ya kuisaidia pesa yetu iwe ya uhakika.

Nizungumzie upande wa fedha. Tanzania inasikitisha kuwa ni nchi pekee ambayo ukifika dukani mtu atakuuliza kuwa unataka kulipa kwa shilingi au kwa dola! Ningeomba Serikali iliangalie jambo hili, linazidi kudidimiza shilingi yetu. Tuheshimu sana shilingi yetu iweze kuwa *stable* kama inavyotakiwa, siyo kama sasa hivi mtu unafika dukani unaulizwa unapendelea ulipe kwa shilingi au kwa dola.

Mheshimiwa Spika, upande wa reli; naishukuru Serikali kwa hatua iliyochukua kuhusu *RITES,* lakini tunaiomba ifanye haraka kumpata mbia kuondoa kilio kilichopo katika nchi yetu cha usafiri wa reli.

Nashukuru sana kwa nafasi hii, ninazidi kuunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, utakapowadia muda, naona kama tuna muda kidogo wa ziada, nitawaita Waheshimiwa Mawaziri kwa mpangilio ufuatao; Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe - Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi; atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa - Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii; Mheshimiwa Stephen Wasira - Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika; na Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa - Waziri wa Miundombinu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa kulingana na muda, bado tuna muda kidogo na nimeona siyo vibaya kwa hawa walioniandikia na kwa wale waliokuwa na subira ya kubaki humuhumu kama hawapo basi, lakini nadhani Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu yupo, angeweza kufuatiwa na Mheshimiwa Tatu Ntimizi na Mheshimiwa Martha Mlata naona amekata tamaa, lakini amesikia basi nafasi ipo kwa dakika kumi.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha binadamu sisi kuwa humu ndani na wengine wako nje wanachacharika na maisha. Vilevile namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi kubwa aliyoifanya na kwa Hotuba yake nzuri, ambayo ameiwasilisha akiambatana na timu yake ya Mawaziri waliokuwa chini ya Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda nichukue nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kutupendelea au kutufanyia kazi nzuri Watanzania hususan kwa Serikali kuweza kutimiza ahadi zake kwa Mkoa wetu wa Pwani; ninawashukuru sana. Pia

ninapenda nitoe shukrani na pongezi kwa Mkuu wetu wa Mkoa, akishirikiana na RAC wake na Wakuu wote wa Wilaya; Kisarawe, Bagamoyo, Rufiji, Mafia na Mkuranga. Hawa wameweza kuwa timu mahiri kwa kuweza kuangalia Ilani ya Chama cha Mapinduzi inatekelezwa na inatimizwa. Ninapenda pia kuwashukuru Wanawake wa Mkoa wa Pwani na Wananchi kwa ujumla. Ninazidi kuomba ushirikiano wao na ninazidi kusema kwamba, Wanawake wa Mkoa wa Pwani, tumesimama kidete kuhakikisha Chama cha Mapinduzi kitachukua nafasi yake kubwa ya ushindi hususan kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete; tuna hakika ushindi wake utakuwa wa kishindo na sisi akina mama jukumu letu liko palepale la kuhimizana na kuhakikisha kura zinapigwa kwa kishindo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia jambo lingine, naomba niwaase na niwasihi wenzangu wa Vyama vya Upinzani; ninawaita wenzangu kwa sababu sote tumo humu ndani na tulisimama kwa wananchi kuomba kura ili tuchaguliwe na tutimize yale ambayo tumeahidi na tumetaka yafanyike kwa wananchi wetu. Tahadhari ninayowapa ni kuwa wao wasiwe wanapinga kila kitu; macho wanayo wanaona kazi za Chama cha Mapinduzi na Ilani ilivyotekelezwa, wamekazana kusema hiki hakijafanywa, hiki hakijafanywa; je, wao wanaweza wakatuonesha japo kimoja walichokifanya?

Mheshimiwa Spika, mwisho wake, kauli yao hii itawaponza hata pale watakapokuwa wanafanya kitu fulani, kwa sababu wameshazowea kusema Chama cha Mapinduzi hakijafanya na wao wataonekana hawajafanya. Wanapokaa kwenye majukwaa wasifie na wahimize, ikiwezekana na wao wafanye yao tuyaone, wanayo majimbo yao wamo humu ndani wameomba uwakilishi kwa Wananchi; je, wanawafanyia nini? Wanategemea sisi tuwafanyie mpaka wao? Tumewapa nafasi wengine wameingia humu kwa mgongo wa Chama cha Mapinduzi, wanatarajia sisi tuwasimamie tuwape mpaka kijiko cha kulia chakula!

Mheshimiwa Spika, haifai, tunaomba msimame na mjue mnachokiongea ni kitu gani na mnachotakiwa kukifanya kwa wananchi wenu ni kitu gani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme machache katika hotuba ya Waziri Mkuu. Mkoani tumeweza kupata gati, tumepata kiwanja cha ndege kwa Mafia, tumepata mitumbwi Rufiji, tumepata barabara na kadhalika, tunashukuru sana na bado tunaomba tufanyiwe yale ambayo hayajakamilika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunapozungumzia maendeleo ya Tanzania na tunahimiza Kilimo Kwanza, sisi Watanzania tunategemea Kilimo na Kilimo Kwanza kimehimizwa lakini kilimo hiki hakitakuwa na maana kama miundombinu haitaboreka.

Mheshimiwa Spika, nikisema miundombinu hapa nina maana ya barabara. Kabla sijalichambua suala la barabara, nataka nichukue nafasi hii nitoe pongezi kwa mashirika ya taasisi za hifadhi ya jamii kwa maana ya *PSPF, NSSF, PPF, LPF* na mengineyo, kazi kubwa wanayoifanya kwa nchi hii tumeiona.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwenye suala la barabara, nchi nyingi zilizoendelea na nyingine ambazo zinazidi kuendelea zinahakikisha zinajenga barabara ambazo hazina matatizo, sisi bajeti yetu ya barabara ni mara moja kwa mwaka, kila Mkoa unatazama Wizara hiyo inapotoa bajeti yake, lakini mwisho wa siku mwaka ule ukipita ile barabara imekwisha au haikwisha ni tatizo, barabara imeharibika hakuna kifungu cha kusaidia kuendeleza ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba ni kwamba, tunayo mashirika haya ya hifadhi za jamii ambayo yameonesha mfano na kazi kubwa sana imefanywa, ushahidi tunao, *UDOM* iko pale, nyumba za askari na kadhalika. Kuna nchi ambazo zimewaingiza washirika hawa kuwa wajenzi wazuri wa barabara na barabara hizo zinaleta manufaa kubwa sana. Tuurudishe ule utaratibu wa *Road Toll*, tuyaambie haya mashirika ya hifadhi ya jamii, yana uwezo mkubwa sana na nina hakika wakiambiwa hawataacha kufanya kazi hiyo. Wapewe kazi hiyo watujengee barabara, kama ikiwezekana ianzie Dar es Salaam kwa kuanzia tu tuwape majaribio iishie Chalinze na hata tatizo lililokuwepo la foleni kubwa Dar es Salaam, Ubungo, Magomeni, makutano ya barabara wanaita *red cross* basi wao wapewe wajenge barabara za kisasa *fly overs* ambazo zitatusaidia sisi.

Mheshimiwa Spika, vile vile *squaters* nyingi sana Mjini Dar es Salaam, hata kule Mwanza wale wazee wangu na watoto wangu wanaokaa vilimani kule, mashirika haya wapewe nafasi wajenge nyumba za kisasa ambazo watazipangisha na kujirudishia wao pesa. Hili linawezekana kwa sababu ni kitu ambacho kinafanyika siku zote kwa mtindo wa lugha ya Kizaramo wanasema *Build, operate and then transfer*.

Mheshimiwa Spika, hili linawezekana tuwape hayo mashirika yafanye hizo kazi. Naomba Waziri Mkuu alichukue hili, nina hakika mtoto wa mkulima ana uwezo, tuachane na urasimu wa kwenye Wizara, tumeona urasimu uliofanyika kwenye daraja la Kinondoni mpaka leo, sijui ni bilioni ngapi ambazo tumepoteza, tumepoteza hata wafadhili ambao walikuwa tayari kutaka kutusaidia kujenga daraja lile.

Mheshimiwa Spika, nakuomba unifikishie salamu zangu kwa Waziri Mkuu, naomba ninong’one, atumie rungu lake, atumie meza yake, uwezo huo anao, ayaite haya mashirika, aziite Kamati zinazohusika za kudumu za Bunge waweze kukaa chini, uamuzi wa haraka utolewe ili tulete maendeleo ya nchi yetu badala ya kila siku kusifia wenzetu kwamba ukienda Japan, ukienda Harare, ukienda sijui wapi, hapana na sisi Watanzania tunataka. Mfano mzuri Nigeria, walikuja kuangalia Mji wa Dodoma, wamekwenda wamejenga Abuja, sasa hivi tunaisifia Abuja sisi na Dodoma yetu tumebaki pale pale.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo si vizuri kugongewa kengele, naomba tuhakikishe haya niliyoyasema Waziri Mkuu na timu yake wanayachukua na kuyafanyia kazi haraka na nitaomba nipate majibu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi)*

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nakushukuru kwa huruma.

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza hotuba ya Waziri Mkuu na naiunga mkono. Nawashukuru kwa utendaji wao wa kazi kuanzia Waziri Mkuu na watendaji wake wote kwa kazi ambayo wameifanya kutokana na hotuba hii, tunajua kwamba kwa kweli wana haki ya kupongezwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimkumbushe Waziri Mkuu kuhusu jambo lililofanyika kwenye Jimbo langu la kutaka Halmashauri, Waziri Mkuu alipokuja Jimboni kwangu wananchi walimweleza katika kijiji cha Kigwa, kwamba ana furaha sana kazi zote zimefanyika, utaratibu kuanzia Vijiji, Kata mpaka Wilaya tayari maelekezo yote yamefanyika kisheria na sasa wanangojea hatma ya kupata Halmashauri yao. Chonde chonde Makao Makuu ya Wilaya ya Uyui yako mbali, wananchi wangu watapata tabu sana kama hawakupata Halmashauri, naomba Halmashauri hii kwa sababu ya manufaa ya wananchi wetu na jambo hili lipo katika ofisi yako tafadhali iliangalie kwa macho ya huruma ili Jimbo la Igalula lipate Halmashauri yake liweze kujitegemea katika kupata huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, Rais alipokuja mwaka jana wananchi waliomba umeme katika maeneo muhimu, hasa Kigwa ambayo ni *center* kubwa sana na barabara ya Itigi ndipo inapopita na hapo pia kuna sekondari ya Kisanji, hapo ilikuwa makao makuu ya wakimbizi, kuna miundombinu mingi sana. Rais akasema kwamba Wizara hii ifanye utaratibu wa kuviwezesha vijiji hivi kupata umeme kwa sababu umeme umeingia Uyui ambako ni Makao Makuu Isikizya lakini kuna kijiji kinaitwa Mayombo, Mayombo mpaka Kigwa ni kilomita ambazo hazizidi tano, ni rahisi kuteremsha umeme pale kutoka Kigwa kuja Igalula na Igalula kuja Igoweko angalau *center* kubwa kama hizi zipate umeme. Lakini watalaam kila mara wamekuja kutazama wanapita katika Jimbo zima uwezekano wa kuanza kuteremsha umeme lakini imekuwa ni safari za utalii wanaingia na kutoka kila mwaka si chini ya miaka mitatu, je ni nini hatma ya kupata umeme?

Mheshimiwa Spika, Jimbo hili ni kubwa, umaskini tunao lakini bila kuwa na umeme kwa kweli itatuletea matatizo, nitashukuru sana kama suala hili la umeme bado liko katika maandalizi yao angalau tuone hatua gani inafanyika.

Mheshimiwa Spika, lingine mwaka juzi na mwaka jana nilizungumzia kuhusu majengo yaliyojengwa ya zahanati, wananchi wamejitolea, Serikali imetusaidia, niliendelea kuzungumza katika Bunge lako, kwa hiyo majengo haya yamekamilika mpaka nyumba za wauguzi zimekamilika na wananchi wamejitolea sana kufanya kazi hii, lakini kwa kweli miaka mitatu hospitali ya Itundaukulu, Nzigala, Kalangasi ni maeneo ambayo sasa hivi mwisho tunaweka wafanyakazi wengine, wananchi wanapata taabu. Maeneo ambapo zahanati zipo ni mbali kutoka katika maeneo yao, ndiyo maana Serikali ikahimiza kwamba kila kijiji kuwe na zahanati angalau wananchi wapate huduma hizi, lakini kwa masikitiko kila mara Waziri akisema kwamba tunajitahidi kupeleka wahudumu lakini kila mwaka inakuwa ni ahadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ionee huruma watu wangu katika Jimbo hili, ni Jimbo ambalo lina matatizo, ni Jimbo ambalo halifikiki kwa haraka kutokana na misitu iliyopo, sasa hizi hospitali hazijaanza kufanya kazi, wananchi wangu bado watapata matatizo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana sasa angalau nipewe taarifa wanaanza lini na je, ni nani atakarabati majengo hayo kwa sababu majengo hayo wananchi wamefanya kazi sana katika kujenga lakini sasa yanahitaji ukarabati ambao ni mkubwa, naomba Serikali iendelee kusaidia kukarabati wakati huo tupate watalaam wa kufanya kazi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwashukuru wapiga kura wangu katika Jimbo langu la Igalula, bado nina hakika wananihitaji kwa kazi nilizozifanya, inataka mwendelezo, ikipata Halmashauri na naishukuru Serikali imenipa Kata tano za ziada, wamefurahi sana bila *transistion* ya mimi Mbunge wao, nina hakika kutakuwa na matatizo ya utekelezaji, wapo vipeperushi wanakuja lakini wanajua ni nani mfanyakazi hodari na ni mwenye uchungu na uwezo, kusoma peke yake si kuelimika.

Kuna tangazo la kusema mimi nimesoma ni nani asiyesoma, ni Mbunge gani asiyesoma hapa, watu tumesoma na tumeelimika na ndiyo maana tunafanya kazi, nina imani kabisa wana Igalula bado wananipenda, wananiheshimu na kuthamini kazi ninazozifanya. Nina imani watanipa miaka mitano ili niweze kukamilisha mambo ambayo yamekwishaanza na wameyaona kwa vitendo wala si kwa nadharia.

Mheshimiwa Spika, vipeperushi vya kuungana na Rais, mimi ndiye ninayependeka na Rais, hivi utamtumia Rais kwa namna hiyo? Rais ni wa wote si wa mtu mmoja, leo watu wanachukua kompyuta wanaweka sura zao wanashikana mkono na Rais, ni nani hajashikana mkono na Rais, mbona Wabunge wote anatupenda na hasa Wabunge wa CCM, sisi ndiyo tulimfanyia kampeni ili Chama chetu kishike madaraka, leo ndiyo imekuwa tija kupita na kusema mimi ndiyo mgombea, mimi ndiyo mwenye elimu, nani asiyekuwa na elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba tugombee lakini tusigombane, mambo ya kusanifu watu wengine wasifanye, mimi ndiyo mtu mzima, mtu mzima dawa. Unaweza kuwa kijana na bado usiwe na uwezo na unaweza ukawa mtu mzima kweli ukawa ovyo, lakini nina uhakika kabisa utu uzima wangu umeendeleza Jimbo la Igalula na bado nina nguvu za kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, msibabaike wana Igalula ninakuja tena na mtaniunga mkono kwa baraka zake, Mwenyezi Mungu na Mtume wetu Muhammad *Swalla llah Alaih Wasalaam* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana Jimbo la Igalula, mwanzo wa kupata Halmashauri ndiyo mwanzo wa kufuatilia kupata Wilaya. Imesemekana kwamba Jimbo hili halina watu wengine, nafikiri sensa haikufanya kazi nzuri. Jimbo lina watu wa kutosha na ndiyo maana tumepata Kata za ziada na bado nasubiri Tarafa kwa sababu tuliahidiwa na Rais Benjamin Mkapa, wakati wake kwamba ni kweli amepata taarifa za kutosha kwamba hili Jimbo la Igalula ni kubwa lazima liongezewe Tarafa na Kata.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kupata hizo Kata lakini bado naisubiri Tarafa kwa hamu sana, kwa sababu kuwa na utawala wa karibu ndiyo kuwasaidia wananchi. Kwa hiyo, naomba sana Tarafa hii isisahauliwe na kama nilivyosema kupata kwangu Halmashauri ndiyo upatikanaji wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kweli mtu anayetoka mpakani mwa Tabora na Singida, kilomita 176 anafika Tabora Mjini, asafiri kilomita nyingine 50 kwenda kuitafuta Wilaya, ni jambo ambalo kwa kweli tulipiga kura kisiasa lakini siyo kwa maslahi ya wananchi. Ndiyo maana nimehangaika na Serikali ikanisaidia kupata Halmashauri ya Jimbo la Igalula na ni dhahiri mambo yote yamekamilika bado TAMISEMI kutoa kauli yake kwani nina imani hata Wilaya iko katika Mfuko wa Halmashauri hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana haya ninayoyazungumza, mimi ndiye natembea katika Jimbo lile. Hakuna Kitongoji wala Kijiji nisichokifahamu katika Jimbo langu. Hakuna mwananchi asiyenifahamu, mpaka watoto wadogo wananifahamu, nikifika tu wanasema 'Tatu Washika' Kwa hiyo, nina hakika kabisa wana imani na kazi ninayoifanya na wananiheshimu na kunipenda, kwa hiyo hawa wote mnaokuja jamani muone kazi iliyofanyika katika Jimbo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sio kuja kula mayai na kuku hapa Dodoma, ni kufanya kazi na ukirudi Jimboni ni kufanya kazi, lakini siyo kuonyesha suti wala vitenge. Hapo ni kuonesha kazi na upendo kwa wananchi. Nina imani kabisa wananchi wangu wanaamini na wanafahamu kazi ninayoifanya, naendelea kufanya na uzoefu nilionao, utanifanya niweze kumalizia kazi ambayo nimeanzisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hayo ndiyo yalikuwa maelezo yangu, lakini nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Igalula, jinsi wanavyoniunga mkono kila siku. Kila nikimaliza Bunge niko Jimboni kwao na kusikiliza shida zao, kuwasaidia mtu mmoja mmoja na hata kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naendelea kuunga mkono hoja na kuwashukuru wananchi wangu na kuwaomba waendelee kuniunga mkono.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Tatu Ntimizi. Sasa namwita Mheshimiwa Martha Mlata, baada ya hapo nawaomba radhi wale ambao wameendelea kuniandikia hapa, kila kitu kinakwenda kwa muda. Baada ya hapo itakuwa ni zamu ya Waheshimiwa Mawaziri.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii, japokuwa dakika ni chache lakini nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ambayo imejitosheleza. Lakini napenda nichukue nafasi hii kwanza kabisa, kuwashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Singida hasa wanawake kwa kuweza kunipa ridhaa yao ili niweze kuwawakilisha hapa Bungeni. Lakini pia niwapongeze sana wanawake hawa wa Mkoa wa Singida kwa sababu wamekuwa mstari wa mbele sana katika kushiriki utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nawapongeza sana na Mungu awabariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na pongezi hizo kwa wananchi wa Mkoa wa Singida na wanawake, napenda pia niipongeze Serikali kwa jinsi ambavyo imeweza kutekeleza Ilani yake ya Chama cha Mapinduzi, hususan katika Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ninavyoongea nikitoka hapa baada ya masaa mawili nikikupigia simu kwamba niko Singida usishangae kwa sababu barabara ni nzuri kabisa ambayo inapitika kwa haraka sana. kile kipande kilichobaki tunajua kitakwisha baada ya muda mfupi kwa sababu hata nyumbani kwako au kwa mtu mwingine huwezi ukakamilisha vitu vyote kwa wakati mmoja, lakini mafanikio yanapoonekana, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza sana Serikali kwa upande wa zahanati pamoja na elimu. Watoto wetu sasa hivi hasa katika Mkoa wa Singida wengi wako madarasani wanasoma. Ukija Mkoa wa Singida huwezi kupata msichana au mvulana wa kazi. Ahsante na naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hata kwa upande wa ajira zile milioni moja ambazo tulikuwa tunazisema, zimetimizwa kwa sababu hata ukichukua wale waendesha pikipiki peke yao au uchukue wale wa Bajaji bado inaonesha ni namna gani kasi ya ahadi na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi inavyokwenda kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kushukuru Serikali kwa kufuta ushuru wa mafuta ya alizeti. Mkoa wa Singida ni Mkoa ambao umekuwa ukilima sana alizeti. Serikali imefuta ushuru pamoja na mashudu yake, sasa naamini kabisa wananchi wa Mkoa wa Singida wataweza kufaidika zaidi kwa zao hili lakini bado hapa nilikuwa na ombi tu kwamba, ile mikopo inayotolewa ya pembejeo za kilimo, hivi juzi nilikuwa nazungumza na wanawake, wanasema sisi tumeungana lakini bado tunapotaka kwenda kuchukua mikopo kwa ajili labda ya trekta au *power tiller* unakuta masharti yake ni magumu sana.

Mheshimiwa Spika, wanasema lazima uwe na ekari 50, lakini akina mama unakuta wameungana wao kila mmoja na kuwa na ekari tano lakini haziko pamoja. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliangalie hili kwamba kama wameungana wamefikisha ekari 50 hata kama haziko pamoja waweze kupatiwa mkopo huo.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 48 kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, kichwa cha habari kinasema 'Habari na Utamaduni'. Pale amezungumzia tu suala la habari, lakini suala la utamaduni hakuweza kulizungumzia. Sasa namuuliza Mheshimiwa

Waziri Mkuu, je, ni kwanini sasa Wizara hii isitenganishwe kwamba kuwe na Wizara ya Habari peke yake na Wizara ya Utamaduni? Kwa sababu kama utamaduni inamezwa ndani ya Wizara ya Habari ina maana Utamaduni haishughulikiwi, sanaa inakuwa haishughulikiwi.

Mheshimiwa Spika, Wasanii wanapata matatizo makubwa sana. Nilikwishawahi kuzungumza hapa ndani ya Bunge na ukanikataza nisilie kwa ajili ya Wasanii, sasa bado tunaona kwamba hata kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, Wasanii bado hawajatajwa. Kwa hiyo, naomba sana ili Wizara hii iweze kutenganishwa ifanye kazi sambamba na matakwa ya sanaa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, labda Mheshimiwa Waziri Mkuu anijibu, je, ni kwa nini mpaka sasa hakuna bodi ya *COSOTA* kwa ajili ya kushughulikia masuala ya wasanii?

Mheshimiwa Spika, nampongeza kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba matumizi ya magari yaweze kupunguzwa na tumeona kwenye bajeti kwamba, hakuna ununuzi wa magari. Sasa niulize je! ni kiasi gani Serikali imeweza ku-*save* kutokana na kubana matumizi ya ununuzi wa magari na hizo pesa, je, zimetumika kwa kitu gani?

Lakini pia nataka kushauri kwamba, basi fedha hizo zielekezwe katika kununua vitendea kazi hasa kwenye upande wa Jeshi la Polisi. Wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu sana ukizingatia kwamba hawana usafiri, basi wanavyobana kwenye sekta zingine naomba Jeshi la Polisi liangaliwe kwa undani zaidi. Hasa katika Mkoa wa Singida tuna gari moja tu. Nampongeza sana Kamanda wa Polisi wa Mkoa ule Mama Kaluba tunasema, tunaweza na tunaweza kweli amekuwa akifanya kazi sambamba, amekuwa akishirikiana sana na vijana wake. Nawapongeza sana. Lakini ninaomba waangaliwe kwa jicho la huruma, waongezewe magari. Maana kuna gari moja tu.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu alipofanya ziara katika Mkoa wa Singida, gari la *escort* kama inaweza ikabaki nyuma hiyo haiwezi kuitwa *escort*. Lakini bado hata tulipopokelewa na maafisa wa hapa Dodoma gari ikaanza kufuka moshi ilibidi ikae pembeni. Kwa hiyo, naomba sana suala la usafiri kwenye upande wa polisi waangaliwe zaidi kwa jicho la huruma upande wa Singida.

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda kuzungumzia suala la afya. Tunaomba sana zile pikipiki za miguu mitatu za kuwasaidia akinamama wakati wa kujifungua wanashindwa kufika katika maeneo ambayo wanaweza wakapata huduma kwenye vituo vya afya haya magari yamekuwa yakiimbwa sasa huu ni mwaka wa tatu au wa nne. Nilikuwa naomba sana mwaka huu haya magari, hizi pikipiki za miguu mitatu ziweze kununuliwa kwa ajili ya kuwasaidia akinamama.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya yote napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, naomba bajeti hii kwa sababu inaishia mwaka 2011 basi iangalie yale maeneo ambayo Serikali haijakamilisha, naamini imeshakamilisha kwa kiasi kikubwa sana kilichobakia ni kidogo tu. Lakini iangalie kwa jicho la huruma sana ile barabara inayotoka Singida kwenda Babati isije ikasuasua kama hii ambayo tunaisifia sasa hivi,

maana yake mikataba inayowekwa wakati mwingine inavunjwa. Tulikuwa tunaomba sana, tunaitegemea sana ile barabara kwa ajili ya kuinua na kukuza uchumi wa Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana na Mungu abariki bajeti hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Martha Mlata.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa hotuba ya kina na uchambuzi mkubwa hata hivyo naomba kwa muhtasari kutoa ushauri au mapendekezo yafuatayo:-

1. Tunaomba mji mdogo wa MAKAMBAKO upewe hadhi ya mji kamIli ili kupunguza kero (matatizo) mengi yaliyopo. Ni mji unaokuwa kwa kasi kubwa kuliko miji mingine yote katika Nyanda za juu. Mji una sifa zote zinazohitajika. Pia wataalam toka TAMISEMI wamefika na kuona hali ya Makambako, taratibu zote zimefuatwa, maombi haya yalikuwa pamoja na yale ya Njombe zaidi ya miaka mitano (5) iliyopita.Mji huu sasa una watu zaidi ya 75,000 na una Kata tano (5).

2. Serikali ifikirie kuunda Wizara ya Maendeleo Vijijini ili kusimamia vizuri kukua kwa vijiji-minyororo na vijiji-mji. Leo Wilaya ya Njombe peke yake ina vijiji vikubwa kama Mji Mdogo wa Kibaigwa 48. Mwaka 2040 vitakuwa kama Makambako vipi serikali isirudishe Idara ya maendeleo Vijijini na Kamishna wa Maendeleo Vijijini.

3. Kuna haja ya Serikalli kudhibiti ongezeko kubwa la idadi ya watu ili kuongeza kasi ya maendeleo na mapato. *Excessive population growth is big stumbling block to Economic Development*. Elimu itolewe kwa wananchi.

4. Serikali ipanie kuondoa tatizo la uhaba wa nyumba za walimu na vyumba vya madarasa kwa mwaka mmoja. Majukumu yagawanywe kati ya Serikali Kuu na Halmashauri za wilaya na miji. Viwanja vya michezo mikoani vilijengwa katika mikoa (1980s) kwa njia ya harambee. Vipi leo nyumba za walimu zisijengwe kwa njia ya harambee wilayani? Serikali itoe mchoro na igharamie bati. Mradi huu uwe chini ya Wakuu wa wilaya na mikoa?

5. Serikali ipunguze gharama za kuendesha serikali yake hasa kwa kupunguza:-

- Sherehe tafirja mapokezi makubwa.
- Kutumia magari ya gharama kubwa na samani za gharama lakini hafifu.
- Kugeuza ofisi kuwa mahali pa starehe kunywa na kula, samani, frigi, makochi, viti vya mzunguko na kadhalika.
- Kutokuwa na *inventory* rasmi ya vyombo ofisini na majumbani .
- Watumishi kutunza wakati *(punctuality).*
- Kuwa na muda rasmi wa kusikiliza wageni ofisini , (kwa kutumua ziadi ya ½ saa kwa mgeni mmoja ni muda mrefu mno).

- Kuna haja ya kupunguza maneno na maandishi *(Actions speak launder than words).*

- Kuna haja ya kufufua siasa ya Ujamaa na Kujitegemea (Moyo huu unapunguza).

- Haja ya kufufua haraka Elimu ya Kujitegemea Mashuleni. Leo mashamba ya shule ya Elimu ya Kujitegemea yamegeuka mashamba ya walimu na kuzifanya shule kushindwa kupata hata fedha ya kununua chaki au karatasi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAVERINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, Muda umekuwa mfupi sana michango ni mingi sana naomba niongezee kwenye mchango wangu kwa kuzungumzia Kamatai ya Hesabu za Serikali *(P.A.C.)*. Tumetembelea Kilimanjaro - Moshi, mpakani mwa Kenya na Tanzania. Tumeona *Customs* zetu na za Kenya za kwetu ni aibu inatia aibu sana majengo yalivyo sehemu za kupaki magari yanayofikia pale pamoja na kazi nzuri ya *TRA* inayofanya ya ukusanyaji wa mapato majengo yenyewe yalivyo aibu Serikali yetu inaonekana haijali watumishi wake ndio maana Wasomalia hupitia kwa urahisi kutokana na mazingira yalivyo pamoja na barabara kutoka mwanga hadi Usangi. Serikali iwe inaangalia sehemu hizo wananchi wa huko Usangi wana mazao mengi hawana pakuyapeleka kwa sababu ya miundombinu.

Pensheni imeboreshwa na iwe inawafikia kwa wakarti muafaka. Shida nyingi kwa wastaafu, wanategemea hapo hapo mpango wa kuuza bidhaa zetu nje kwa kuuza uchumi swala hili likifanyika tutashukuru hata kahawa zetu turuhusiwe kuuza nje kuuza viwanda vyetu pamoja na matunda yetu tunayalima hapa nchini. Kero ya wakandarasi wamekuwa ni kero. Naomba Serikali ifanye uchunguzi mkubwa pamoja na *TANROAD* ndio wanawapa viburi watengeneze vibaya barabara kusudi wasimamishwe ili serikali iwalipe. Je, kiburi ni cha *TANROAD* au ni wizara au ni serikali. Hizo pesa zinazolipwa ikipigwa hesabu zinaweza kutengeneza barabara nyingine.

Narudia tena kusema kuwa Bajeti iwe inalenga sehemu ambazo ni muhimu sana.Wanatoa misaada kwa watoto yatima na walemavu kwenye vituo mbalimbali kishule Mgeza mseto na mgeza shule ya msingi. Zaidi sana nilitembelea kwa mara ya kwanza Kagera. Hata kuwatembelea unawapa moyo watu wa Bukoba Mjini, Kata ya Kahororo. Chonde chonde zaidi ya watoto wana matatizo makubwa wanakolala. Vitendea kazi serikali iboreshe kituo cha Afya zamzam kiweze kutusaidia kama wilaya kupunguza msongamano wa hospitali ya mkoa, sindano madawa kliniki shughuli zote zirudi hapa na vurugu malalamiko yatapungua kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua kuchangia huduma ya Afya kwenye hospitali ya Bukoba wananchi wengi wanalalamika. Mwananchi kukata cheti na kuona Daktari 5000, wanaandikiwa dawa wanaambiwa hakuna dawa ukanunue na pesa hawakurudishiwi pesa ni kero kama tunavyo jua kipato cha wananchi. *(Makofi)*

Mwisho natoa rai kwa Watendaji wote Wakuu wa Wilaya wanaopelekwa Mkoani Kagera na kuamua kupiga walimu viboko basi hivyo viboko wapigwe kwa mishahara watu walipelekwa shule wakasoma kwa nguvu za wazazi leo hii unawadhalilisha mbele ya wanafunzi heshima iko wapi. Malezi yako wapi?

Naomba kujua Polisi kipindi cha Uchaguzi Mkuu wanalinda tume au nani? Naomba kuunganisha mchango wangu huu na mchango wangu wa kusema hapa Bungeni nitashukuru nikitendewa haki.

Lini Serikali yetu itajipanga kuacha mambo ya kuparamia mambo au kutokuwa na mkakati madhubuti. Tuache kulalamika nchi yetu ni maskini hatuna umaskini wowote. Sisi ni matajiri tusidanganyane, kelele za kila siku uchumi umeshuka unashuka kwa walio wachache kama wananchi wetu walio mskini unapanda kwa mafisadi kwa nini? Tusiwe watu wa kuangalia nchi jirani wanakuzaje uchumi wao. Je, ni lini serikali itaacha kuwa vipofu na viziwi. Tunatembea kila nchi hatuoni wivu kwa wenzetu?

Mheshimiwa Spika, tumeshindwa miundombinu ya kutosha na ndiyo kitu muhimu hata na Kilimo Kwanza bila miundombinu ni bure. Pamoja na hayo tunaingia soko la pamoja. Je, sisi Watanzania tutalifaidi taifa letu au wenzetu ndio wanafaidi kuwaandaa wananchi wetu wakaelewa na kua na bidhaa za kupeleka kwenye soko tutakuwa watumwa.

Niliomba gari la kubebea wagonjwa kagera wagonjwa wanateseka niliuliza swali kwenye Mkutano wa Kumi na Nane(18) na naibu waziri akanijibu kwamba tayari magari yameshafika. Je, magari haya yalikkuwa ya hospitali au yalikuwa ni magari ya kuombea kura. Alipeleka Kata ya Kashai pamoja na Rwamishenye mpaka sasa bado nadai gari la kubebea wagonjwa la Mkoa wa Kagera kama hamna naomba majibu? Je, Serikali ina mpango upi wa kufufua viwanda vyote kuliko kutegemea wawekezaji?

Je, vijana wengi wanatafuta ajira hasa machinga ambao wanatumia nguvu zao wenyewe na ni ajira tosha. Je, jengo lao litafunguliwa lini wapate ajira waache kutangatana na kupigwa viboko na mgambo wa Jiji?

Tatizo la kubambikiza kesi linalosababisha msongamano wa wafungwa magerezani liangaliwe kwa umakini mkubwa kwani sio tu inagharimu serikali kwa namna mbalimbali inawanyanyasa wananchi wasio na uelewa wa mambo yanayohusiana na utoaji haki.

Kuibuka kwa tatizo la wananchi kujichukulia sheria mikononi kwa kuvunja majengo ya polisi na magereza wakiwatafuta wahalifu liangaliwe kwa umakini kwani kinachoonekana hapa wananchi wanaona wanaofanya uhalifu wanaachiwa ovyo na wanaendelea kutesa jamii vijijini.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nachukua nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe na kumshukuru mwenyezi mungu kwa kutuwezesha kufika kipindi hiki na kwa kutunusuru katika matatizo mbalimbali hasa tuwepo safarini.

Nichukue nafasi ya pekee kukupongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu , Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, na wakuu wote wa taasisi zilizopo chini ya Waziri Mkuu.

Naipongeza kazi zote zilizofanyika pamoja na ufinyu wa Bajeti yetu, hususani katika suala zima la mbolea katika Mkoa wa Ruvuma. Hali ya ruzuku ya mbolea ni nzuri na imechangia kuleta mapato mazuri.

Hata hivyo ninayo maoni ya wananchi wa Litembo wilayani Mbinga ambao nilifanya nao mkutano kuwa ikiwezekana utaratibu uliopo uboreshwe katika kuhakikisha kuwa bei ya mbole katika wilaya badala ya kuwa tofauti kati ya Kata na Kata, hali hiyo inaleta manung'uniko kwa Kata jirani hivyo basi ni vema kuona uwezekano wa kujumuisha gharama hizo na kupata *average price.*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Ruvuma tunayo furaha kwa jinsi ambavyo suala la kupandisha Makumbusho ya Majimaji kuwa ya Taifa. Kituo hicho kimekuwa kivutio kikubwa kwa wageni wetu, hasa katika suala zima la kuheshimu Mila na Desturi zetu. Tunashauri serikali inapoandaa ratiba ya viongozi wake kutembelea Mkoa wa Ruvuma basi Makumbusho Maji Maji iwe ni sehemu ya ziara hasa inapohitaji kukutana na wazee na watu maarufu Mkoani Ruvuma. Kwa kufanya hivyo itasaidia kukuza utalii wa Makumbusho hususani katika Mkoa wa Ruvuma na Kanda ya Kusini kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, suala la Mimba. Pamoja na kuweka mikakati ya kujenga mabweni ni vema kuwa na kampeni maalum ya kuelimisha wazazi na wanafunzi wenyewe na pia kupanga mikakati ya pamoja ya kuondoa tatizo hilo. Mfano Ruvuma watoto 400 walipata mimba. Dawa za uzazi wa mpango hazipatikani kiasi kwamba hazikidhi lengo lillilokusudiwa la kudhibiti idadi ya watu.

Naipongeza serikali kwa kuwa na vipaumbele vichache mwaka huu ili kutumia vizuri pesa zilizopo. Lakini vilevile kutenga pesa za kutosha kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu, hivyo itasaidia kuona kuwa vituo vya kupigia kura vinakuwa karibu na watu, usimamizi mzuri, pamoja na vifaa vya Uchaguzi Mkuu ambao ndio mtaji wa Demokrasi na Amani.

Nimeshtushwa na mchango mkubwa wa sekta ya uvuvi kufikia bilioni 780.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, CCM ushindi ni lazma pamoja nasi, naunga mkono hoja.

**MHE. BALOZI DR. GERTUDE I. MONGELLA**: Mheshimiwa Spika, Uvuvi endelevu utafanikiwa tu kama yafuatayo yatazingatiwa.

Taifa kutambua sekta ya uvuvi na kukubali kuwekeza na kuimarisha technologia masoko uhifadhi na usindikaji wa mazao ya samaki. Kama inavyofanya kwa kilimo na mifugo.

Kuanzisha mfuko wa wavuvi kama ilivyokubalika kwenye semina ya kilimo kwanza huko Mwanza. Usalama wa wavuvi na zana zao .

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Kilimo Kwanza ni pamoja na Uvuvi.

**MHE. SAMUEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza Waziri Mkuu na Baraza zima la mawaziri kwa kuandaa hotuba nzuri na yenye manufaa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mimi sina jambo jipya bali naishukuru serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza ahadi karibu asilimia tisini na tano (95%).

Awali ya yote barabara za jimbo la Buchosa zilikuwa hazipitiki kwa urahisi. Kwa mfano mtu kutoka wilayani Sengerema hadi Kahunda aliweza kutumia muda

usiopungua saa 8 hadi kufika mahali hapo kwa siku mbili. Hivi leo watu wanasafiri kwa muda wa saa moja au saa moja na nusu. Hivyo zote hizi ni juhudi za serikali hii.

Ni wazo jema kabisa kukumbuka kuimarisha viwanja vya ndege vya Tabora na Kigoma hadi kujengwa kwa Lami. Pia ni jambo jema Mpanda kupata uwanja wa Ndege mzuri sehemu hii au eneo hili liko mbali sana hasa kwa mtu atokaye Arusha, Dar es salaam au Mwanza ambaye anapedna kwenda Mpanda kutokana na umbali watu wengi huchoka either hukata tama ya kwenda maeneo hayo kutokana na kutokuwa na usafiri mbadala kama wa ndege. Kujenga viwanja hivi kutakuza uchumi wa nchi katika sekta mbalimbali. Napongeza, ni jambo jema kabisa.

Jimbo langu kwa muda wote hakuna Umeme lakini kwa bahai nzuri una neema ya pekee serikali kupitia mradi wa *MCC* tayari mkandarasi yupo hatua za mwisho hivyo wakati wowote kazi ya kuweka nguzo za umeme itanendelea kwa maana hiyo sina cha kuilaumu serikali na sina malalamiko badala yake naipongeza serikali kwa kazi nzuri iliyoifanya kwa wananchi wangu wa Buchosa.

Kivuko kiitwacho *MV-KOME II*. Kivuko hiki ni kipya. Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alipotembelea Buchosa miaka kadhaa aliyopita aliahidia kuleta kivuko kipya badala ya kivuko cha zamani kilichokuwa kimeharibika. Alitimiza ahadi hiyo kwa kuleta kivuko kipya na cha kisasa kabisa MV – *Kome II.* Mie naona kwa haya na menginwe serikali yangu imenitendea haki na hii inanithibitishia kuwa nitarudi Bungeni kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga hoja hii mkono kwa 100%. Ninaomba Waziri mkuu atembelee Buchosa.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, napedna kumshukuru na kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, kwa umahiri wake katika utendaji wa majukumu yake kwa Taifa, uharaka katika kusaidia kutatua kero na migogoro ya jamii na uwezo mkubwa katika kujibu maswali ya papo kwa papo hapa Bungeni. Pia ushirikiano wake kwa watendaji wote katika ofisi zake na kwa waheshimiwa wabunge.

Mheshimiwa Spika napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jitihada binafsi alizofanya kuwezesha wilaya ya Muheza kupata Kata mpya kumi na vijiji vya awamu ya pili. Watendaji wa wilaya ya Muheza hawakufika Dodoma ili kukamilisha takwimu na uhakiki wa Kata na vijiji. Kwa hali hiyo orodha ilifungwa bila ya kuingizwa katika mpango kwa ushirikino mkubwa na TAMISEMI.

Hivyo wilaya ya Muheza ikaweza kupewa, nawashukuru sana waheshimiwa mawaziri wa TAMISEMI na watendaji wote waliowezesha Muheza kufanikiwa kuongezeka kwa vijiji na Kata mpya. Kuongezeka huko kunasaidia kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi zikiwemo huduma za kilimo Afya na Elimu. Kata zilizoongezwa kwa eneo la mji mdogo wa Muheza zitaongeza kufikiwa kwa vigezo vya kuwezesha Muheza kupata mji kamili na hivyo kuwa na Halmashauri ya mji wa muheza.

Mheshimiwa Spika, Fedha nyingi kutoka Serikali Kuu sasa zinaelekezwa katika Halmashauri za wilaya bado usimamizi ni dhaifu na hujuma kubwa zinaendelea

kuzifanyia ubadhilifu fedha hizo. Waheshimiwa Wabunge ni madiwani katika Halmashauri za wilaya, lakini licha ya malalamiko ya wabunge kwamba vikao muhimu vya maamuzi ndani ya Halmashauri vinafanyika kwa wakati wabunge wakiwa Bungeni! Wakati mwingine vikao vinaahirishwa hadi wabunge waondoke majimboni, lengo ni kuondoa mchango wa mbunge hasa katika uwezo wake wa kuchambua mipango na taarifa za utekelezaji zinazotolewa katika vikao.

Mheshimiwa Spika, bado mbunge ni kiongozi wa Kata zote katika Jimbo lakini Diwani mmoja kwa Kata moja tu anapewa nafasi ya kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri au Meya na kujijengea mazingira ya kuwa na madaraka makubwa zaidi hata kuliko Mbunge wa Jimbo. Baadhi ya wenyeviti hao elimu na uwezo wao wa kiutendaji ni mdogo sana na kwa hali hiyo watendaji waovu hutumia nafasi hiyo kufanya wanavyotaka na hata kudiriki kuandika Taarifa za uongozi za utekelezaji wa miradi na kuziwasilisha hata mbele ya kamati za Bunge akiwepo mwenyekiti wa Halmashauri wilaya.

Mfumo huu kama ambavyo nimeueleza katika Bajeti za 2008/2009, 2009/2010 na sasa 2010/2011, unahitaji kufanyiwa marekebisho ikiwa ni pamoja na kuona jinsi ya kupunguza wingi wa akaunti za fedha katika Halmashauri zetu za wilaya.

Kwa matarajio makubwa ya uchambuzi wa mapungufu kwa lengo la kuimarisha ufanisi katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa WaziriMkuu, amegusia hatua mbalimbali ambazo zimeanza kuchukuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi *(NEC)* katika kufanikisha maandalizi ya Uchaguzi huo. Miongoni mwa hatua ambazo zinachukuliwa ni pamoja na kuboresha Daftari la kudumu la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu shughuli za uandikishaji wa wapiga kura kwa upande wa Tanzania Zanzibar unasimamiwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar *(ZEC).* Daftari hili ndilo ambalo pia linatumiwa na *NEC* katika Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na Wabunge. Lakini kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwamba maandalizi ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa upande wa Zanzibar umegubikwa na matatizo mengi sana, ikiwa ni pamoja na baadhi ya wananchi kunyimwa haki hiyo kwa visingizio mbalimbali. Aidha kuna baadhi ya wananchi wanaandikishwa zaidi ya mara moja ama kwa kutumia majina tofauti na katika vituo tofauti vya kujiandikisha.

Kadhalika kuna baadhi ya wapiga kura majina yao kuachwa kwa makusudi au kuhamishwa na kupelekwa vituo vingine vya mbali na wanapoishi.

Mheshimiwa Spika, matatizo haya pamoja na mengine ambayo sikuyataja hapa lengo lake kubwa ni kuwanyima baadhi ya wananchi haki yao ya kikatiba ya kuchagua viongozi wanaowataka. Aidha baadhi ya wananchi wanapewa fursa zaidi ya moja ya kuchagua viongozi ili viongozi Fulani wachaguliwe kwa kura za kishindo kinyume na taratibu zinazokubalika. Kuna baadhi ya watu hasa mipakani na raia wa Msumbiji

waliopo Zanzibar huwa wanapiga kura katika nchi mbili tofauti. Hali hii ni ukiukwaji wa misingi ya Demokrasi na kuwanyima watu wengine haki yao ya kikatiba.

Mheshimiwa Spika, ili kuepukana na matatizo haya ninaishauri serikali kupitia Tume ya Uchaguzi ya Taifa *(NEC)* kulihakiki kwa kina Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambalo wamelipokea kutoka kwa *ZEC,* kwa kufanya hivyo wakazi ambao si raia wa Tanzania wananchi waliojiandikisha zaidi ya mara moja wanaondolewa katika Daftari hilo na hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi ya watu hao.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Uchaguzi *NEC* isimamie ipasavyo Uchaguzi wa Rais wa Muungano na Wabunge katika upande wa Tanzania Zanzibar *(ZEC)* wameonyesha udhaifu mkubwa katika kusimamia suala zima la Uchaguzi zilizopita. *NEC* izibe ufa kuepuka kuja kujenga ukuta.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake amegusia pia maaandalizi ya kufanya sensa ya watu na makazi ambayo kwa kawaida hufanywa kila baada ya miaka kumi. Sensa ya mwisho ilifanyika mwaka 2002 hapa nchini na sensa ijayo imepangwa kufanyika mwaka 2012 hatua mballi mbali zimeanza kuchukuliwa kuhakikisha sensa hiyo kwamba ifanyike kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Sote tunafahamu umuhimu wa takwimu za watu na makazi zinavyotumika katika shughuli za kimaendeleo. Vivyo hivo takwimu za idadi ya mifugo na mtawanyiko wake ni muhimu sana katika kupanga maendeleo ya sekta ya mifugo nchini, kwa bahati mbaya ni zaidi ya miaka 20 sasa imeshapita sense ya mifugo *(Head Count)* hapa nchini haijafanyika.

Mheshimiwa Spika, kumetokea maafa kadha ambayo yamesababisha vifo vingi vya mifugo yakiwemo mafuriko, Ukame na Wizi wa mipakani nchini inahitaji kujua kwa yakini idadi ya mifugo iliyopo hapa nchini kwa madhumuni mbali mbali kwa hiyo ninashauri serikali sambamba na kufanya Sensa ya watu na makazi pia ifanye Sensa ya mifugo nchi nzima.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kufika hapa Bungeni bila ya kushikwa mkono. Pia nikupongeze wewe binafsi kwa umahiri wako katika kutuogoza vyema hapa Bungeni. Kwa kuzingatia hotuba ya Waziri Mkuu ni wazi isiofichika kujua nia ya serikali katika kukuza nchi. Hotuba ya Waziri Mkuu imesomwa leo siku ambayo nchi yetu inaadhimishia HAKI YA MTOTO WA AFRIKA, naipongeza serikali kwa kufunga mkataba wa kimataifa juu ya mtoto wa Afrika na kuwa na Wizara maalum ambayo inasimamia maendeleoya jinsia na watoto.

Mheshimiwa Spika, Mtoto ana haki nyingi ikiwemo kuishi kuendelezwa na pia kumlinda kwa kuzingatia hali hii kuna baadhi ya maeneo katika nchi yetu watoto wanaishi katika mazingira magumu hasa kule vijijini ambako kazi kubwa ni kilimo na mifugo. Je Serikali inashughulikiaje watoto hao kwa kuwapatia huduma zao za kimsingi? Pia mtoto katika nchi yetu huwemo katika mazingira ya kazi, mazingira ya michezo pia kwa wakati mwingine maharusini katika mazingira haya baadhi ni makosa kwa jamii kuwashirikisha watoto. Je serikali imechukua hatua gani ndani ya jamii kusimamia haki hizi za mtoto?

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Waziri Mkuu kuwa ni mtoto wa mkulima naomba nizungumzie kilimo, pamoja na serikali kupunguza kodi ya baadhi ya zana za kilimo ila iko hoja ya serikali kutekeleza kwa vitendo nia yake ya KILIMO KWANZA. Mara nyingi serikali utekelezaji wake hubaki katika andiko jambo ambalo huambulia umasikini kuwepo kwa mabwana shamba, mbolea mbegu bora za kisasa pia kuwepo utaratibu maalum wa mikoa yote kuhakikisha kuwepo kwa huduma zote kwa wakulima kwa wakati. Nchi yetu itaweza kujigomboa katika dimbwi la umaskini kwa kufanikisha azma hii ya serikali juu ya kung'oa mkulima katika umasikini ni kuwepo kwa miundombinu ya uhakika masoko pamoja na bei nzuri kwa mazao yao. Haya yatawezekana pale serikali itapokuwa na viwanda vya kutosha .

Mheshimiwa Spika, kuhusu Elimu, serikali haina upanuzi kwa Nyanja za elimu. Elimu ina mambo mengi sana ikiwemo walimu wa kutosha mashuleni, vitabu nakadhalika. Changamoto zinazoikumba wizara ni uhaba wa walimu mashuleni. Vitabu jambo ambalo hupelekea wanafunzi kufeli. Serikali inapaswa kukidhi mahitaji ya walimu wenye uwezo mashuleni.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo sina budi kumpongeza Waziri Mkuu kwa umahiri wake wakati akiwasilisha hotuba ya Bajeti yake Bungeni. Ahsante sana.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba nzuri uliyoitoa kuna mambo muhimu kadhaa ambayo hujagusia, nayo ni kama ifuatavyo:-

1. Maendeleo ya Kigamboni, tumesikia fununu kwamba inauzwa kwa kmwekezaji. Je, jambo hilo lina ukweli gani ? Naomba utufafanulie?

2. Umeme vijijini na hasa kule Kilwa ambapo bomba la gesi halijapita liko mbali na hilo linaturudisha nyuma kimaendeleo.

3. Katika utawala bora ni vema walemavu wakapewa nafasi mbali mbali hasa nafasi za mawaziri, ukurugenzi na kadhalika. Kwani tuna walemavu wengi na ni wasomi na wenye uchungu na nchi hii kama illivyo kwa Watanzania wengine.

4. Serikali yetu inawachukulia hatua gani wale wanaoghushi vyeti vya shule, vyeti vya kuzaliwa na kadhalika ambao hao wanasababisha kuleta mdondoko katika jamii na nchi yetu ambayo ina sifa nzuri mpaka hivi sasa.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri aliyotoa leo tarehe 16 Juni, 2010.

Mheshimiwa Spika, nimeona nami nichangie hotuba hii kwa kina. Kuhusu jambo ambalo limeibuka hivi karibuni nchini kwetu la uchanganyaji wa mafuta ya taa na *diesel* na *petrol* maarufu kwa jina la *(Chakachua).*

Mheshimiwa Spika, kwa vile mimi ni mfanyabiashara ya mafuta tena mzoefu na nimekuwa nikiliongelea jambo hili kwa mda mrefu sasa hapa Bungeni wakati wa

kuchangia hotuba ya Wizara ya fedha mwaka 2007, na nikarudia tena katika hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, hata neno wanalotumia la *chakachua* ni mimi ambaye nilileta Bungeni ambalo hutumika na waharibifu hawa.

Mheshimiwa Spika, pamoja katika hotuba ya waziri wa fedha Wabunge wengi hulizungumzia hili kwa huzuni na majibu aliyotoa waziri wa fedha akijibu hoja za Wabunge naona bado haitasaidia pale aliposema kutakuwa na magari ya maabara.

Mheshimiwa Spika, Ikumbukwe kama nilivyochangia mwaka 2009, hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini kwamba sio mchezo huu unafanywa na wenye vituo tu wengi wanofanya mchezo huo ni madereva na nilizitaja sehemu hizo ni Mdaula- Kibaha wao huweka vituo vya mafurta vidogovidogo na kujenga magereji nyuma ya vituo vyao kazi yao ni kuongea na madereva wanaoenda mikoani na nje ya nchi na kuingiza magari yao ndani na kota mafuta mazuri kwa kutumia *Dram* na kuwarudishia mafuta ya taa na kuwalipa madereva kila *Dram* la mafurta mazuri aliyotoa shs 50,000.

Mheshimiwa Spika, *EWURA* kwenda kupima vituo vya mafuta na kupiga faini au kuwafungia wenye vituo sio suluhisho wakati wanaharibu mafuta ya nchi nzima yanaharibiwa.

Mheshimiwa Spika, Suluhisho la uhakika la mchezo huu ni kupandisha kidogo kodi ya mafuta ya taa si lazima ifanane na *Diesel* angalau kodi ikipandishwa kwa shs. 200 tu itatosha kukomesha biashara hii. Kwa vile kodi itafika 254 na ukichanganya na kodi ya sasa ya shs. 54 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, hapo biashara hii itakoma kwa vile faida itakuwa ndogo, hawatoweza kugawana dereva na mnunuzi wa la sivyo mafuta ya taa yataendelea kutumika kama malighafi na Serikali itaendlea kukosa mapato.

Mheshimiwa Spika, vile vile hawa wanunuzi wana mitandao mingi na hata kwenye vyombo vya habari kwa mfano gazeti la uhuru la tarehe 15 Juni, 2010 kwenye habari inayoeleza uchafuaji wa mafuta lilimnukuu mtu anaejiita mwananchi, kwa jina la Niresh akitoa mawazo yake mafuta ya taa yasipande bei yatampa mzigo mwananchi wa chini, wakati yeye ndiye mwenye gereji pale Mdaula ya mchezo huo.

Mheshimiwa Spika, nategemea haya niliyoyaeleza yatatoa mwanga mzuri kama kuna nia dhabiti. Ahsante sana.

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja. Pili kwa niaba ya wananchi wa Handeni tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Celina Kombani na Naibu Waziri, Mheshimiwa Aggrey Mwanri kwa kutuwezesha kupata hadhi ya Halmashauri ya Mji kwa mji mdogo wa Handeni, wilaya ya Handeni ni moja ya wilaya zilizoanzishwa zamani. Hatua hii itaendeleza maboresho ya wilaya ya Handeni, tunawashukuru sana .

Dhana ya matumizi ya rasilimali kushabihiana na *value for money* ifuatiliwe kwa karibu misingi iwe ni kufikia *economic* na *allocative efficeiencies.*

*Committment* ya kuwaendeleza wa ngazi za chini kwenye Halmashauri itaimarika kupitia utendaji bora na wa makini wa wafanyakazi wa halmashauri zote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wangu wa karatasi nyingine naomba pia nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi kubwa na nzuri hasa katika kushughulikia uhuru wa Watanzania katika kutoa mawazo yao na suala la ujambazi ambalo kwa muda wa miaka minne lilikuwa shwari.

Lakini hali ya sasa katika baadhi ya maeneo imeanza kurudi tena. Mfano Kinondoni na katika maziwa makubwa kama vile Visiwa vya Ukerewe. Pia nalaani mauaji ya kina mama na watoto kama yale yaliyotokea Mkoani Ruvuma. Hali ya ugomvi katika familia pia inaonekana kuwa ndiyo chanzo cha mambo haya.

Je, serikali ina mpango gani wa kurekebisha hali hiyo ikiwemo mauaji ya *Albino* ambayo bado ni tishio?

Suala la mpaka wa Malawi na Tanzania (Ziwa Nyasa) limefikia wapi? Ni vema suala hilo lishughulikiwe mapema ili kuondoa kero ya usalama na kuishi kwa wasiwasi na pia kuwezesha uwekezaji.

Mwisho, tunakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu endapo mungu ataturejesha kwenye nafasi uliyo nayo na hakika mungu ni mwaminifu atafanya hivyo tunakuomba Makumbusho ya Majimaji ya tarehe 27 Februari, 2010 ambayo ni kichocheo chetu cha uchumi. Tunaomba pia wizara ya Maliasili na utalii itupatie gari kwa ajili ya kuendeleza utafiti. Pia kwa kushirikiana na wizara ya mambo ya nje kutoa mwalilko kwa Balozi mbalimbali ili kutembelea Makumbusho hiyo, pamoja na vivutio vingine kama kona za milima ya Lukumburu ambayo ilileta hamasa kubwa kwa Balozi wa Sweden Mheshimiwa Staffan Harrison.

Kituo kinakabiliwa na tatizo la uzio na pia ipo haja ya :-

1. Kupima na kuhifadhi maeneo mengine ya Utalii ya Makumbusho hayo kama eneo la Chief Mputa na mkewe Nasere.

2. Kuyatambua maeneo mengine.

3. Kuboresha barabara iendao mlima Matogoro mpaka Chanzo cha Mto Ruvuma kama walivyofanya wenzetu wa Zimbabwe na *Victoria Falls.*

Mimi ni mdau katika suala la taka mjini, suala hilo halipewi uzito wa kutosha, makandarasi hawalipwi kwa wakati na badala ya kusonga mbele tunarudi nyuma.

Serikali ilibuni jambo jema tena kwa kuwatumia wazalendo lakini nadhani huu ni utamaduni wetu kazi za Wazalendo hazipewi kipaumbele labda kwa kuwa ni wenzetu tuliangalie eneo hili.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja aliyoitoa Waziri Mkuu kwa 100%. Hotuba yake ni *well balanced* na imetoa malezo sahihi kwa kila Wizara na vitengo vyote vya Serikali. Mambo yote aliyosisitiza katika HITIMISHO yanatelelezeka kinachohitajika kwa sisi viongozi wote ni kuunga mkono hoja hii na kuhakikisha kila mmoja anasimamaia na kutekeleza wajibu wake.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Misamaha ya kodi kwenye vyombo vya usafiri kwa madiwani vipi mbona hakieleweki?

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri Mkuu, Mawaziri wake na Naibu Waziri kwa hotuba nzuri ya Bajeti. Aidha pongezi ziwafikie watendaji wa ngazi zote katika ofisi hii.

Naipongeza Serikali ya awamu ya nne kwa maendeleo makubwa iliyoleta katika Nyanja zote hasa:-

Elimu ya Sekondari katika nchi nzima lakini hasa kwenye Wilaya ya Dodoma Mjini, ambayo ilikuwa ni kati ya wilaya zenye idadi ndogo sana ya shule za sekondari.

Elimu ya juu katika nchi nzimna na hasa Dodoma hivi sasa vipo vyuo vikuu 2 ikilinganishwa na sifuri mwaka 2005. Aidha udahili kwenye vyuo vya *CBE,* Mipango na Madini umeongezeka zaidi ya maradufu.

Ujenzi wa barabara za lami nchi nzima na hasa ndani ya mji wa Dodoma. Aidha matayarisho yamekamilika ya kuweka lami kwenye barabara maarufu ya *THE GREAT NORTH ROAD* kutoka Iringa kupitia Dodoma hadi Babati.

Kuwezesha uwekezaji wa Rasilimali *(Investment)* kwa kiwango kikubwa wilayani Dodoma ambacho hakijapata kutokea kwa kipindi kifupi cha miaka minne iliyopita ujenzi wa *U-DOM* na miundombinu yake umeingiza rasilimali nyingi sana Dodoma na umeuchangamshwa uchumi wa Mkoa wa Dodoma.

Hatua muhimu za kuchukua ili kusaidia ujenzi wa mji wa Dodoma chini ya uongozi wa *CDA:*-

Serikali itenge fungu la kutosha ili viwanja vya ujenzi wa makazi vipimwe kwa wingi vinginenvyo *CDA* itaendelea kuelemewa na ujenzi holela. Dawa pekee ni kukidhi mahitaji ya viwanja ambavyo yameongezeka sana.

Serikali ichukue jukumu la kujenga barabara zote za Dodoma Mjini ili viwango vyake viendane na matarajio ya mji mkuu mtarajiwa. Hivi sasa mafungu yanayotengwa hayatoshi kujenga barabara zinazokidhi viwango. Aidha utaalamu na weledi bado haupo ndani ya manispaa ya Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Spika, masuala ya kero zinazohusu Muungano wetu yanayochukuwa muda mrefu kupatiwa ufumbuzi ni chanzo cha kudhoofisha Muungano huu. Hivyo ni vyema kero hizo zikapatiwa ufumbuzi haraka. Aidha wananchi ni vyema wakaeleweshwa jinsi Muungano wetu unavyoimarika siku hadi siku.

Maendeleo ya wanawake na watoto ni jambo jema na inafaa kuendelezwa. Tunaipongeza serikali kwa hilo, lakini bado kuna changamoto nyingi zinazowakabili wanawake na watoto hivyo ni vyema wizara, Asasi, Halmashauri, *NGO's* na makundi tofauti kama TAMWA na kadhalika. Kuandaa mkakati maalum unaowiana kwa maendeleo ya wanawake watoto na kuingiza katika mipango na malengo ya makundi maalum yaangaliwe kwa unyeti wake na uchambuzi wa kina wa matatizo yanayowakumba hasa wanawake na watoto.

Mfano - Halmashauri inalo fungu la kusaidia familia maskini ili kuwezeha watoto wapate Elimu lakini tumeshuhudia makundi hayo yakishindwa kupatiwa Elimu ya Sekondari, kukosa Ada na kadhalika.

Suala la unyanyasaji wa kijinsia nalo linasumbua sana makundi haya na imani kwa baadhi ya ndugu zetu wananume imetoweka hivyo tatizo hili ni vyema serikali na jamii kuliondolea huruma na kukabiliana nalo kikamilifu.

Vijana ndio nguvu kazi ya Taifa katika kuleta maendeleo vivutio na fursa zilizopo zielekezwe kwenye kundi hilo mjini na vijijini ili misongamano mjini iweze kupungua.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, Pongezi kwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, (Mb) kwa hotuba mzuri ambayo ina mwelekeo mzuri na Uchaguzi wa Ilani ya uchaguzi 2005. Pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Celina Kombani (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Mwanri (Mb) Katibu Mkuu Maimuna Tarishi na wataalamu wote wa Wizara zote zilizo chini ya uongozi wa Waziri Mkuu. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Ruzuku ya Kilimo ninatoa ushauri kwamba Tabora Manispaa inazo kata nane (8) ambazo hushughulika na kilimo ambazo ziko pembezone nazo ni MISHA, NDEVELWA, TUMBI, TONJANDA, KALUNDE, UYUI, ITETEMIA, MALOLO, ambazo hulima bila kupewa Ruzuku na kwa kuwa kuna mazao ya biashara kama vile Tumbaku, Mahindi, na kadhalika ningeomba serikali ielekeze sasa kilimo kwanza kwa kupewa Ruzuku ya Pembejeo .

Kuhusu Mifugo katika Mkoa wa Tabora, unayo mifugo mingi sana ambayo inahitaji Ruzuku ya madawa ya ng'ombe ili angalau wafugaji waweze kuwa na mifugo bora. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Manispaa ya Tabora alijionea Josho ambalo wananchi kwa nguvu zao wameweza kujenga. Tunaomba wasaidiwe nayo ni Kata ya ya Uyui,(Imalomikeyo)

Kuhusu Kilimo cha Umwagiliaji, Mkoa wa Tabora una maeneo ambayo yana mabonde makubwa ambayo yanafaa sana kwa kilimo cha umwagiliaji kama vile wilaya ya Nzega ina Bonde kubwa sana la NATA/LUSU ambalo hulima Mpunga na mboga mboga.

Wilaya ya Igunga, Chuma cha Nkolo, Sigili na mabonde mengine makubwa yako. Hivyo niombe sana kilimo cha umwagiliaji kipewe kipaumbele ili kuondokana na umasikini.

Kuhusu Elimu na Mafunzo kunakuwa na ruhusa za kwenda masomoni kuwa walimu mashule za msingi /sekondari kwenda kwa wingi au kwa pamoja zaidi ya nusu ya walimu na kusababisha shule nyingi kukosa walimu, kuwepo na mkataba wa walimu kurejea kwenye shule husika baada ya masomo kwani wengi wao baada ya kumaliza masomo hawarudi tena serikalini au Halmashauri husika na kusababisha hasara.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kuhusu upungufu wa nyumba za walimu. Kukamilisha ujenzi wa nyumba za walimu madarasa ambayo yako chini ya TASAF. Ni vema kusiwepo na miradi mipya kwa mwaka huu wa fedha 2010/2011 ili wakamilishe iliopo kwani imekuwa ni kero kwa wananchi ambao huchangia nguvu zao.

TAMISEMI itoe mwongozo kwa Wakurugenzi ukamilishaji wa wa miradi yote ya MMES ambayo ilikuwa chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo kwa miaka 2006/2007. Upungufa wa walimu katika shule za sekondari za *Tabora Boys, Tabora Girls, Mirambo* ambako mpaka sasa hakuna *Geography.* Naomba serikali itoe kipaumbele kwa shule hizo. Maalum

Sasa ni posho kwa Madiwani. Wizara ya TAMISEMI naomba iangalie upya posho za madiwani kwani naona hufanya kazi ngumu sana kwa kutumikia wananchi. Waongezewe *Gratuity* ili wapate moyo na kutekeleza ilani ya Uchaguzi kwa kina, wakopeshwe vitendea kazi kama vile Pikipiki, ili watembelee miradi yote kwani maeneo ni mapana sana. Hata hiyo Kata ni kubwa sana.

Kuongeza vituo vya kupigia kura ili kutoa fursa ya kupiga kura kwa wananchi ambao hushindwa kutembea umbali mrefu hasa wazee na wanawake waja wazito.

Serikali iangalie maambukizi katika wilaya ya Igunga na Nzega kutokana na kuwa kwenye Barabara kuu ya Magari makubwa yanayokwenda Rwanda / Burundi watengewe fedha ya kutosha ili kukabiliana na hali hiyo kwa kupewa Elimu, Dawa na Chakula kwa waathirika. Itengwe fedha za kusomeshsa watoto yatima.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja 100%.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kupongeza kwa dhati hotuba nzuri ya Waziri Mkuu, ambayo imegusa kila sekta ikiwa ni pamoja na mchango mkubwa wa Mawasiliano katika pato la Taifa. Aidha ninakupongeza kwa hotuba yako nzuri kuhusu maelezo ya kiutendaji na mapitio na mwelekeo wa kazi wa mwaka 2010/2011. Hata hivyo serikali imejipanga kutekeleza mradi wa Anuani za Makazi na Simu za Posta nchi nzima; mradi ambao kwa sehemu kubwa utatekelezwa na Halmashauri za Wilaya. Je, TAMISEMI imejipanga vipi katika kutekeleza mradi huu muhimu wa Kitaifa?

Nawapongezeni sana kwa mipango mizuri.

**MHE. MOSSY SULEIMANI MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimwa Waziri Mkuu, pamoja na watendaji wote katika ofisi yake kwa kusimamaia kutekeleza yale yote ambayo yanaelekezwa kutoka ngazi za juu kwani ofisi hii ndiyo mtekelezaji wa mipango yote ya serikali hii.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana ofisi ya Waziri Mkuu itoe kipaumbele sana katika maamuzi ya kilimo kwanza kwa sababu mchango wa azma hii itakuwa mkombozi kwa asilimia 80% ya watu wetu ambao ndio wamiliki wa ardhi kijijini, sana hii ya kilimo kwanza kisipokwenda sambamba na viwanda vidogo vidogo ambavyo vitasindika vilivyo limwa vilivyovuliwa hatimaye kusafirishwa nje kwa kuuza hapa lengo litakuwa limekamilika ipasavyo na mchango wa kuingiza fedha za kigeni, hivyo kuongeza pato ambalo litangeza hata kufidia pengo la Bajeti zetu ambazo kwa kiasi fulani tunanyanyasika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa mkombozi katika hili katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Elimu ni msingi wa yote hivyo naiomba ofisi ya Waziri Mkuu itilie maanani sana kuboresha kiwango cha ufanisi kwa walimu pamoja na kuboresha nyumba zao, madawati na mafao yao naamini tutapata wananchi wenye elimu ambao watajua namna ya kuichangia serikali yao katika kujikwamua na umasikini.

Mheshimiwa Spika, Suala la uwajibikaji ni muhimu sana katika majukumu ambayo tumegawana naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu hili aliangalie sana kwani ufanisi katika asasi za Serikali unapungua siku hadi siku hivyo namshauri ziara zisizo rasmi aziandae kwa maslahi ya Watanzania hasa katika taasisi za Afya, Bandari na hata Mashule hii itasaidia kuchochea uwajibikaji kwani bado Watanzania baadhi wanaamini kusimamiwa zaidi kuliko kujituma.

Mheshimiwa Spika, bado naamini kama Watanzania kama tutajituma tunaweza kukidhi Bajeti zetu. Naomba misamaha isiwe katika vileo tu kuhamasisha kodi lazima vivutio katika viwanda vidogo vidogo kuwepo kama mwananchi ananunua kiwanda nje kwa fedha zake yaani nini tena kuomba dhamana ya nyumba badala ya kumhamasisha vipi ajikite katika uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania napendekeza Mheshimwa Waziri Mkuu awe na ofisi zake Zanzibar hii itasaidia sana katika kuboresha Muungano wetu.

Mwisho naomba ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu akusanye nguvu za wataalam kuondoa kero za foleni Dar es salaam zinashusha uchumi wa nchi yetu ili nalo lipatiwe ufumbuzi sambamba na hili kutumia mbinu za kumwaga maji baharini lizingatiwe. Naipongeza Serikali kuiunga mkono suala la *P.P.P.* hili ni mkombozo kwa kupiga hatua kwa kasi maendeleo katika Serikali yetu.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, Maendeleo na Usimamizi wa Matumizi ya Halmashauri za Wilaya *Vs* Posho/Mishahara ya Madiwani.

Maendeleo na fedha zinazopelekwa Halmashauri na Serikali katika dhana ya kupeleka madaraka Serikali za mitaa imekuwa inapeleka fedha nyingi zaidi ya asilimia 70% ya *Budget* ya Taifa zinakwenda kwenye Halmashauri.

Mfano, tumeshuhudia baadhi ya Halmashauri zikipewa hadi bilioni 13 au zaidi. Fedha hizi ili zilete matokeo mazuri ni lazima.

i. Halmashauri ziwezeshwe kuwa na wataalamu.

ii. Halmashauri ziwe na *Automomy* ya kushirikiana na wananchi na kufanya maamuzi yake katika kupanga na kutekeleza majukumu yake.

iii. Usimamizi madhubuti ili fedha zote ziende kwenye kufanya kazi za maendeleo.

Lakini kutokana na mapungufu yanayotokana na mambo niliyoyataja hapa juu tunashuhudia waziwazi kwamba fedha hizi nyingi zinapotelea mikononi mwa wabadhilifu wa mali za Umma na hivyo maendeleo kutopatikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mishahara au posho za Madiwani;Madiwani ndio wenye Halmashauri ndio wasimamizi wa shughuli za maendeleo na fedha zote zinazokwenda Halmashauri. Yaani madiwani hawa ndio wasimamizi wa mabilioni yanayokwenda Halmashauri, cha kushangaza hawa wenye dhamana na jukumu hili kubwa wanalipwa kiwango kidogo sana cha posho. Mfano baadhi ya Halmashauri wanapata sh.30,000/=, 60,000/=, 120,000/= na kadhalika. Hii ni sawa na mfabiashara mwenye duka lenye mali za mabilioni kuweka mlinzi anayelinda kwa Kirungu na hivyo kusababisha duka kuibiwa wakati wowote na majambazi wenye silaha za kisasa.

Mheshimiwa Spika, sasa napendekeza kuwa:-

a) Serikali bila kusita iboreshwe maslahi ya madiwani ili:-

- Kuongeza motisha kwa madiwani ya kulinda mali na kusimamia maendeleo katika Halmashauri zao (Mishahara na Posho).

- Viwango vya posho view vizuri vinavyoweza kusaidia kuleta ushindani kwenye nafasi za madiwani na kuweza kupata nafasi za madiwani na kuweza kupata madiwani wenye sifa nzuri.

b) Izipe Halmashauri *FULL AUTONOMY* ili kuharakisha maendeleo katika halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, sasa ni posho za Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa. Wnyeviti wa vijiji na mitaa ndio wanafanya kazi zao karibu sana na wananchi. Ndio wanaohamasisha wananchi katika shughuli mbalimbali za maendeleo wakishirikishwa na watendaji wa vijiji na Kata.

Ninapendekeza kuwa Serikali ifanye maamuzi ya kuanza kuwapa posho wenyeviti hawa, viongozi hawa ambao ndio kiungo kikubwa cha shughuli za maendeleo. Wanalalamika sana shughuli za mtendaji wa kijiji zinategemea sana mwenyekiti wa kijiji/ Mtaa.

Sasa ni kuhusu taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG). Ninapendekeza kwamba zile taarifa zinazohusu baadhi ya Halmashauri kutumia vibaya fedha za Halmashauri zitolewazo na CAG – mkaguzi mkuu hizo Halmashauri zihojiwe na Bunge kuhusu sababu za mapungufu hayo.Hii itasaidia sana viongozi wa Halmashauri kuwajibika zaidi katika majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho nampongeza sana mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri. Naunga hoja mkono.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuisifu serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa jinsi ilivyojitahidi kuleta maendeleo ya dhati kwa Watanzania. Nchi imepiga hatua sana kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, Same Mashariki ina matatizo mengi sana sasa hivi yanayosababishwa na uvamizi wa msitu wa Shengena.

Mheshimiwa Spika, msitu wa Shengena ndicho chanzo cha mvua na mito yote inayowezesha uwepo wa kilima ndani ya Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, kuna uharibidu mkubwa sana wa mazingira ndani ya msitu wa Shengena. Uharibifu uliopo ndani ya msitu wa Shengena kulingana na report ninazopewa na wapiga kura wangu ni kama ifuatavyo:-

(1) Uchimbaji batili wa dhahabu;

(2) Ukataji wa miti hovyo kwa sababu yale madini yanakaa chini ya mizizi ya miti;

(3) Upasuaji wa mbao kwa kutumia mashine kwa jina la *SHENSO 4;*

(4) Kuharibu mazingira na maji ya Mto Saseni kwani watu wote hawa hawana vyoo na ni mamia ya wastu waliovamia msitu huo;

(5) Maji ya mito yote ya Same Mashariki ikiwepo Mto Saseni yamebadilika rangi yake na hivyo tuna wasi wasi wa kutofaa kwa matumizi ya nyumbani; na

(6) Mbao zote hizo zinazovunwa kiharamu zinapitishwa njia ya TAE kwenda Makanya.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa Wilaya analifahamu hili lakini nafikiri uharamia huu sasa unahitaji mkono wa serikali kuu tena ni vyema serikali ichukue hatua ya haraka.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana wananchi wangu wa Same Mashariki milimani kwa jinsi walivyoshirikiana na mimi Mbunge wao na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same na kuanza ujenzi wa Kiwanda Kidogo cha Kusindika Tangawizi ili kuongeza thamani ya zao hili na kuwafanya wananchi wauze tangawizi iliyosindikwa kwa bei ya juu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyekuja Same Mashariki na kutuwekea jiwe la msingi. Tulijitahidi mimi na wananchi wangu tukakamilisha jengo letu kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kukubali kwake kuwa mgeni rasmi kwenye Harambee ya kununua mtambo wa kusindika tangawizi. Harambee ilifanikiwa na tukapata zaidi ya Shilingi milion 300.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumeingia mkataba na *SIDO*. naambatanisha kivuli cha mkataba huu kwa ajili ya *recond* kwa Waziri Mkuu. Mkataba huu ni wa kuweka mtambo wa kukausha na kusindika tangawizi katika kiwanda hiki cha Umoja wa Walima Tangawizi. Mkataba huu ni makubaliano ya kuweka mitambo hii kwa muda wa miezi minne (4) kuanzia tarehe 4 Juni, 2010 na kutukabidhi kiwanda hiki kidogo tarehe 4 Oktoba, 2010. Uwezo wa kulipa gharama hii tunao. Tunatakiwa tulipe Shs. 88,895,000/=. Fedha hizi ziko ndani ya uwezo wetu. Tumeshalipa awamu ya kwanza ya Shilingi 69,421,250.00 na kazi imeanza.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mwenyezi Mungu tulipoanza tuliona tunakokwenda ni mbali lakini sasa tutafika.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ituunge mkono kifedha na kielimu ili tuweze kutoa bidhaa zenye hadhi ya Kimataifa na tuuze nje ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali Kuu ijuhusishe kwa kiasi kikubwa kutupa elimu na utaalamu wa kukiendesha kiwanda hicho cha aina yake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Timu yake yote ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI).

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mawazo au mchango wangu kama ifuatavyo:-

Pamoja na hatua kubwa iliyopigwa na Serikali yetu ya Awamu ya Nne, Serikali hii hii ielewe kuwa bado kuna Watanzania wanaoishi kwenye dhiki kubwa. Hawana hakika na kupata mlo wa siku. Hii ni hakika na kweli. Serikali yetu ipange mipango ya maendeleo kwa kulenga jamii zinazoishi maisha duni. Bajeti ilenge jamii duni.

Mheshimiwa Spika, mimi naipongeza sana Serikali; lakini nawalaumu Watendaji Wakuu. Kuna baadhi ya Watumishi wa Serikali hawatimizi majukumu yao katika maeneo yao. Ukilinganisha Watumishi wa Serikali na *NGOs* utaona *NGOs* wana-*deliver* kwa kuwa kuna ufuatiliaji wa karibu.

Mheshimiwa Spika, Watanzania walio wengi Maofisini (Serikalini) ni wavivu. Kuna tatizo kubwa la kutowajibika na hivyo kutaka kusimamiwe. Kwa mfano; kule Arusha kuna hoteli nyingi za watalii. Cha kushangaza, utakuta watumishi wengi wa hoteli ni wageni (siyo Watanzania). Ukiuliza kulikoni, mbona mpaka wahudumu ni Wakenya? Meneja anasema Watanzania ni wavivu na wanadharau kazi ya kufanya usafi. Kazi nyingine wanaona aibu kufanya, wakati wenzao Wakenya wanaomba kwa kujitolea bure miezi miwili.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tuache tabia ya uvivu na uzembe na huku tunalalamikia Serikali kuwa hakuna ajira. Wenzetu wageni wanapata ajira nchini kwetu na vijana wetu wanabaki majumbani bila ajira.

Mheshimiwa Spika, pili, naiomba Serikali iangalie upya posho za mafuta kwa Wabunge wa Viti Maalum. Kwa mfano, Jimbo moja la Uchaguzi la Simanjiro au Kiteto Mkoani Manyara, lina ukubwa wa *square kilometers* zaidi ya Mkoa wa Kilimanjaro au Mtwara. Sasa utakuta Mbunge wa Viti Maalum kutoka Manyara anayepaswa kuzungukia Wilaya sita za Mkoa, anapewa posho ya mafuta sawa na wa mikoa niliyoitaja. Hili si haki, naomba posho hizi ziangaliwe upya. Hii ni sambamba na muda unaopewa posho za kuzungukia mkoa. Hii irekebishwe ili kwa watakaobarikiwa 2010 – 2015, wapate ahueni ya kuzungukia maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba mpango wa Serikali kupeleka *power tillers* kwa wakulima wa maeneo mbalimbali uangaliwe upya. Maeneo mengine *power tillers* hazifai, kwa kuwa hata wakulima hawanunui. Maeneo/mashamba makubwa yanahitaji matrekta na wananchi wako radhi kukopeshwa matrekta badala ya kutumia *power tillers.*

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali wafanye utafiti kabla ya kusambaza zana hizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kutumia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wa Nchi, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Wataalamu wote waliohusika katika maandalizi ya bajeti. Nakiri kwamba, bajeti ni nzuri; hata hivyo, napenda kuchangia kwenye maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninavyoelewa mimi ni kwamba, mji wowote unapokuwa na hadhi ya Mji Mdogo kama ilivyo Mji Mdogo Vwawa, Wilayani Mbozi, unakuwa upo kwenye mapito *(transition).* Sasa nataka nielezwe ni miaka mingapi unatakiwa Mji Mdogo utoke hapo kwenda kuwa Mji Kamili na hivyo kuwa na *vote* yake? Nasema hivyo kwa sababu Mji wa Vwawa ulipata hadhi ya kuwa Mji Mdogo zaidi ya miaka

minne iliyopita, hadi leo bado ni Mji Mdogo. Mji hauwezi kujiendesha vizuri kwa sababu shughuli zake zinapanuka, lakini kiwango cha fedha za kuendeshea mji, bado ni kidogo sana. Je, ni vigezo vipi ambavyo tunatakiwa Mji wa Vwawa tuvikamilishe ili tupate hadhi ya Mji Kamili?

Mheshimiwa Spika, miji midogo inaendeshwa na Halmashuri ya Mji, ikiwa chini ya Mwenyekiti anaechaguliwa kutoka miongoni mwa Wenyeviti wa Vitongoji. Mtendaji wa Mji *(Town Executive Officer),* ndiye Katibu wa Baraza. Sasa nataka kujua nini wajibu wa Diwani katika Mji Mdogo kama Vwawa ambako tayari kuna Serikali Kamili?

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bunge, imejenga Ofisi nzuri sana ya Bunge kule Tunguu – Zanzibar. Hilo ni jambo zuri sana la kupongeza. Hata hivyo, tatizo langu lipo kwenye matumizi ya jengo lenyewe. Kimsingi, jengo hili halitumiki ipasavyo, matumizi yeke ni madogo sana, nachelea kusema jengo litaoza!

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri kwamba, badala ya Kamati zote za Bunge kukutana Dar es Salaam, ambako kumekuwa na msongamano mkubwa sana wa magari barabarani na hata sehemu ya kupaki magari ni tabu, basi baadhi ya Kamati ziwe zinakutana Zanzibar. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tunaimarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, napongeza uamuzi wa Serikali yetu na zaidi Bunge, kwa uamuzi wa kuanza kujenga Ofisi za Wabunge Majimboni. Hata hivyo, kiasi cha shilingi bilioni moja kinachotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi hizo ni kidogo sana. Kama hali hiyo itaendelea hivyo, basi itachukua muda mrefu sana kukamilisha ujenzi wa Ofisi hizo. Nashauri kwamba, kiasi kinachotengwa kiongezwe bajeti ijayo kufikia shilingi bilioni mbili. Aidha, zoezi hilo liende sanjali na uwekaji samani na kompyuta kwenye ofisi za zamani na mpya zinazojengwa sasa. Naomba pia huduma nyingine kama vile sukari na *stationary* zitolewe kwenye Ofisi za Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nazipongeza juhudi zinazofanywa na Serikali, kuongeza idadi ya vocha za mbolea na mbegu za ruzuku. Pamoja na jitihada hizo, bado kiwango kinachotolewa ni kidogo sana; kwa mfano, Wilaya ya Mbozi ambayo ina kaya karibu 120,000 ni kaya 80,000 zinapata vocha hizo. Hii ina maana kaya 40,000 zinakosa vocha hizo. Je, tuna dhamira ya kweli ya kwenda na dhana ya Kilimo Kwanza? Vocha hizo ni kwa ekari moja tu! Nashauri kiasi cha vocha kiongezwe.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine kubwa tulilonalo hapa ni wizi/upotevu wa vocha za mbolea na mbegu za mahindi. Wapo Viongozi ambao walituhumiwa kwa upotevu wa vocha hizo. Wapo waliokamatwa na kupelekwa Mahakamani, lakini waliachiwa kwa kile kinachoitwa ukosefu wa ushahidi, pamoja na ushahidi wa kimazingira unaonesha kwamba, maofisa hao walihusika katika upotevu/wizi wa vocha hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri kwamba, maofisa wote waliotuhumiwa na wizi/upotevu huo, pamoja na kuachiwa na Mahakama na wale wote ambao hawakufikishwa Mahakamani, lakini walituhumiwa, basi Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe, awachukulie hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kuwastaafisha kwa manufaa ya umma, kushushwa vyeo na kadhalika. Watendaji kama hao hawana uzalendo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuleta Bungeni Sheria Na.17 ya Mwaka 2008 *(The Mortgage Finance Act No.17 of 2008)* na hatimaye kupitishwa na

Bunge. Nataka kujua, je, Sheria hiyo nzuri, yenye nia ya kuwapunguzia kama si kuwaondolea kabisa Watanzania wengi tatizo la makazi, utekelezaji wake umefikia wapi na Watanzania wa Vijijini watafaidikaje na mikopo hiyo? Nashauri mikopo hiyo iwakumbuke Watanzania wengi ambao wanaishi vijijini.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb) – Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile ya Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani (Mb) – Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako, maoni ya Wanafunzi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, ambayo naiomba Serikali iYAfanyie kazi.

Kwanza, wanaomba Siku ya Kumbukumbu ya Msiba wa Mwalimu Nyerere, Rais wa Kwanza wa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kitaifa ni vyema ukawekwa utaratibu wa kuingiza katika ratiba na kuwawezesha kushiriki katika kumbukumbu hizo kwa nia ya kuenzi jina lake linalotumiwa na Chuo hicho.

Pili, wanaiomba Serikali pia izishawishi Benki zilizopo Dar es Salaam hasa Benki ya CRDB, NMB na NBC, zifungue huduma za ATM katika Chuo hicho. Hivi sasa wanafunzi wanapata tabu sana na kuhangaika kufuata huduma hizo mjini.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wa Chuo hicho cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, wanakabiliwa na kutokubalika katika taasisi nyingine kwenda kufanya mafunzo ya vitendo *(Fieldwork),* kwa wale wanafunzi ambao wanachukua masomo yanayohusu elimu ya siasa. Taasisi zielimishwe kwamba, chuo hicho hakifundishi siasa bali kinafundisha taaluma.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kujibiwa hapa Bungeni kwamba, Mpango wa Uboreshaji Miji/Makazi Duni Awamu ya Tatu kwa Mkoa wa Dar es Salaam utahusisha Kata za Mbagala, Mbagala Kuu na Charambe Jimbo la Kigamboni. Wananchi wa Kata hizo tuliwafikishia kauli hiyo ya Serikali kupitia majibu Bungeni ni hivi sasa wanausubiri Mpango kwa umuhimu mkubwa. Je, maandalizi yake yamefikia wapi na utagharimu kiasi gani cha Fedha za Tanzania?

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam ni sehemu ya utawala na mitaa kwa Jiji zima/lote lakini kuna maeneo ambayo yalikuwa ni vitongoji au vijiji, bado ni mapori na yanaendelea kwa shughuli za kilimo na wananchi wa maeneo hayo maisha yao yanategemea kilimo hicho, ufugaji na uvuvi mpaka sasa. Naiomba Serikali iwasaidie tena wakulima hao katika mipango yake ya wakulima na kuondokana na dhana ya Dar es Salaam ni eneo la Serikali za Mitaa na kuona kutokuwa na haja ya kuweka mipango ya kilimo.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Kwa niaba ya Wananchi wa Rombo, natoa shukrani nyingi na za dhati kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kunusuru walioathirika na ukame uliokuwa mkali sana, tangu mwaka 1948 haujaonekana. Mifugo, ilikufa, kahawa na migomba ilikauka na iliyonusurika haiwezi kuzaa. Vyakula vya njaa vilivyofika kwa wakati na ugawaji kusimamiwa vizuri, vilifanya binadamu wasife.

Mheshimiwa Spika, pili, tunashukuru sana kwa kupatiwa mbolea kwa utaratibu wa vocha kwa kiasi kikubwa ingawa haikuweza kuwafikia wakulima wote. Tatu, tunashukuru kwa ruzuku kufidia ujenzi wa shule za sekondari zilizosimama kwa wananchi kushindwa kuchangia kutokana na ukame huo wa kihistoria.

Mheshimiwa Spika, narudia tena niliyosema nilipochangia Hotuba ya Bajeti kwamba ili tuondokane na umaskini uliokithiri ni lazima tulenge ngazi ya kaya katika uwekezaji. Mfano ni mbolea tunayotoa sasa kwa vocha kwa mkulima mmoja mmoja, madawa kwa mfugaji mmoja mmoja na kadhalika. Yaani tuzisaidie kaya moja moja kuinua uchumi wao kwa njia za uzalishaji mali, biashara na viwanda vidogo. Aidha, tutoe misaada kwa kaya fukara ili kila mtoto apate elimu bure hadi chuo kikuu. Kama wazo hili lingefanyiwa kazi inawezekana. Elimu ni lango kuu la kukimbizia umaskini. Mtoto mwenye elimu ni tofauti na wazazi na watoto wake hali kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pia tusogeze huduma ya maji nyumbani au karibu sana na kila kaya. Uvunaji wa maji ya mvua ngazi ya kaya (mapaa) au ya mito na mifereji ya muda wakati wa mvua ni lazima. Kwa kuwa maskini hana uwezo huo kifedha, inawezekana kubuni mbinu za kufanikisha wazo hili, kwa kutegemea mahali. Hili lisiwe la hiari, liwekewe sheria ndogo na adhabu kwa wasiojishughulisha. Mwenye maji anaweza kuyatumia kwa njia mbalimbali za kujikwamua; mfano, umwagiliaji wa matone, ufugaji wa kisasa (ng'ombe) na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, tuwe na programu za kuinua hali ya kiafya katika kaya, hasa kwa njia ya kinga kwa wote siyo tu watoto kama ilivyo sasa. Mambo ya kufanya ni madogo lakini muhimu. Mfano, kila mtu kuwa na choo, kuchemsha maji, kuwa msafi wa mwili na mazingira ya kaya. Mengine yanahitaji fedha; mfano, kutokomeza minyoo, dawa za virutubisho na kadhalika. La muhimu pia ni kutoa elimu ya Lishe bora kwa kila kaya. Watu wengi hawali kisayansi *(balanced diet)*, wala hawana mchanganyiko mzuri wa milo (wanga, proteni, mboga, matunda na kadhalika). Lishe na kinga ni silaha muhimu za kupambana na umaskini kwa kuboresha afya ya kaya na kukwepa magonjwa mengi.

Mheshimiwa Spika, kama tungefanikisha hayo kwa Mpango wa MKUKUTA II tutakuwa tumepata maisha bora kwa wote. Hasa kama papo hapo tutakuwa tumewekeza vilivyo katika nyanja zinazomsaidia mwanakaya kama barabara kuu na za vijijini zinazopitika kila wakati, kuwa na mpango mzuri zaidi wa ajira na kujiajiri, kuwa na dawa hospitalini, usafiri wa kuaminika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa nyakati mbili tofauti, Rais ameisifu Wilaya ya Rombo hadharani, kwa juhudi zake za ujenzi wa Shule za Kata na ametuunga mkono kwa vitendo, hata katika bajeti hii kama nilivyoeleza hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Rombo ina Shule za Kata 48 na za Taasisi; Kanisa Katoliki na Wazazi. Kila Kata ina shule mbili isipokuwa tatu ambazo zina moja na nyingine zina tatu. Mwaka jana shule hizo zilipeleka watoto 651 Kidato cha Tano *(Form V)* na mwaka huu ni watoto 788 wasichana wakizidi wavulana kwa zaidi ya 100. wanaobeza Shule za Kata ni wavivu wa ubunifu. Sisi Rombo tumechukua hatua kujaza upungufu uliopo; mfano kutafuta vitabu hasa vya sayansi, kuajiri walimu wasiolipwa na Serikali na kadhalika. Nimefarijika kusikia kuwa mwaka huu kila shule itapatiwa walimu watano, ingawa mahitaji ni makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, wakulima wa kahawa Rombo na pia Wilaya nyingine zinazounganishwa na Chama cha Ushirika cha *KNCU,* wanalo tatizo la kutoweza kulipa wakulima mwaka huu. Tatizo ni fedha zao kushikiliwa na CRDB kutokana na kutofaidika na fidia iliyotolewa kwa wanunuzi wa mazao walioathirika na mdororo wa uchumi duniani. Naomba uingilie kati kwani iko hatari kahawa kutonunuliwa msimu huu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru, naunga mkono tena.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwa Hotuba yake nzuri. Aidha, niwapongeze Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Wataalam, kwa maandalizi mazuri ya Hotuba na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nasema ninaiunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, napenda nichangie katika maeneo machache. La kwanza, Kilimo Kwanza, tukitaka mkakati huu ufanikiwe lazima tuhakikishe tunakifanya kuwa endelevu kwa kuangalia uwezekano wa kufungamanisha Kilimo Kwanza na mafunzo katika shule zetu za sekondari ili baadhi ya wanafunzi hao wasioendelea na masomo waweze kushiriki katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, Progamu ya Serikali ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo pamoja na *components* zake, yaani ruzuku ya mbolea, mbegu bora, madawa na kadhalika, ni Programu nzuri. Hata hivyo, kwa upande wa ruzuku wa mbolea, nashauri tuangalie uwezekano wa kuongeza kiwango cha mbolea inayotolewa angalau itosheleze ekari tatu au nne. Naelewa pendekezo hili litakuwa na gharama kubwa lakini faida itakayopatikana ni kubwa. Kama hilo haliwezekani kwa kuwa lina gharama kubwa, basi Serikali ifungamanishe utaratibu wa sasa wa utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa eka moja pamoja na utoaji wa mikopo ya mbolea kwa wakulima ya masharti nafuu. Hatua hii itaongeza uzalishaji wa mazao na hivyo kuleta Mapinduzi ya Kijani, uhakika wa chakula na kipato ili kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Kuboresha Mfumo wa Serikali za Mitaa inayotekelezwa na Serikali nchini kote imekuwa na mafanikio, hasa katika kujenga uwezo wa Serikali za Mitaa pamoja na kuwawezesha wananchi kushiriki katika upangaji wa mipango yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio ambayo yameanza kuonekana, bado Programu hiyo inakabiliwa na changamoto nyingi hasa uwezo mdogo wa wananchi wa kubuni maendeleo. Ili kuleta maendeleo ya ndani ya Wilaya moja na Wilaya ndani ya Mkoa mmoja, nashauri Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha katika kila Halmashauri ya Wilaya, kitengo cha kutoa ushauri wa kiufundi *(technical advice)* kwa wananchi vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali Kuu inatoa rasilimali fedha nyingi sana kwa mamlaka za mitaa kwa lengo la kuchochea maendeleo. Naipongea Serikali kwa dhati kwa hilo. Hata hivyo, katika baadhi ya Halmashauri kama pale Bariadi, upo usimamizi hafifu na rasilimali zinazotolewa kutokana na baadhi ya watumishi kutokuwa waaminifu wanaochumia matumbo yao. Tusaidiwe kwa kuwahamisha watumishi waliokaa kwa kipindi kirefu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niiombe Serikali ichukue uamuzi wa haraka wa kufufua Reli ya Kati na kuifanya ya kisasa *(standard gauge).* Serikali isake misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka kwa nchi rafiki kama China na India. Tujifunze haraka namna ya ku-*access* mikopo ya masharti nafuu inayotolewa na nchi hizo, tusipofanya hivyo fedha hizo zitachukuliwa na nchi nyingine katika Bara hili la Afrika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nimalize kwa kusema naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia.

**MHE. ARCH. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hotuba hii nzuri, yenye mwelekeo kwa Taifa letu na inayotupa matumaini zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wanaomsaidia pamoja na Watendaji wengine wote waliohusika kutuletea hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Serikali yetu kwa kutuletea maendeleo mengi na makubwa kule Wilayani Hai katika sekta zote, yaani afya, elimu, utawala bora, kilimo na zaidi ya yote, miradi ya umwagiliaji na kujengewa Barabara ya Kwasadala – Masama kwa kiwango cha lami. Kwa niaba ya Wananchi wa Hai, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, ninaanza kuiunga mkono Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, itakayowasilishwa hapo baadaye kwani itakuwa ni kichocheo kikubwa sana kwenye maendeleo yetu, kwani mataifa mengi duniani yamepiga hatua kubwa za kimaendeleo kupitia utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kutupatia ruzuku ya mbolea, mbegu bora, miche ya kahawa na madawa ambapo pia tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia mvua nzuri kwani tunayo matarajio makubwa sana ya mavuno mengi na mazuri. Kwanza, niseme hiki Kilimo Kwanza kitafanikiwa tu ambapo tutabadilisha kilimo chetu kutoka kwenye jembe la mkono na kutumia mashine *(mechanization).*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo, pamoja na ruzuku ya chanjo na madawa, ninazidi kusisitiza upande wa soko ili huyu mkulima mfugaji asipunjike tuweke mizani kwenye minada yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna haja kubwa sana ya kuviimarisha Vyama vyetu vya Msingi ili kuzaa ushirika mkubwa wenye manufaa lakini msisitizo ukiwa ni Wanachama ndiyo wenye ushirika na wala siyo Viongozi waliowachagua. Pia mapato yanayopatikana kutokana na pango la mashamba ya ushirika yatumike kwa manufaa ya wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, nashauri tuzidi kuwaelimisha wananchi wetu kuhusu Programu ya Huduma za Kifedha Vijijini, ikiwa ni pamoja na kuanzisha vimifuko vidogo vidogo na hatimaye kuunda SACCOS na mwishowe kuanzisha Benki za Wananchi.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa migogoro ya ardhi ni lazima tufanye bidii sana kupima vijiji vyetu ili tuweze kupata ramani za kudumu na zenye kuainisha mipaka yetu. Pamoja na Sheria mpya ya *Unit Titles,* Sheria ya Mikopo ya Nyumba na Kurasimisha Makazi ili tuweze kupata makazi na maisha bora ni lazima tuwe na Sheria ya Majengo ili kuepuka madhara makubwa yanayoweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda na biashara, ninaomba nielezwe ni nini kinachoendelea kule Wilayani Hai katika eneo la Machine Tools na KIA? *Something has to be done please.*

Mheshimiowa Spika, ili tuweze kuimarisha shilingi yetu ni lazima kuongeza mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana Serikali yetu kwa kuongeza pesa katika ujenzi wa barabara zetu za vijijini na mijini na hii itatusaidia sana kuimarisha uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, ninashauri Serikali yetu iharakishe kuutengeneza Uwanja wa Ndege wa KIA baada ya KADCO kushindwa, lakini niulize kulikoni reli yetu kutoka Dar es Salaam hadi Arusha kufa? Ni lini itafufuliwa?

Mheshimiwa Spika, hivi ni kwa nini tumeshindwa kuzitumia vizuri bandari zetu zote za maziwa na bahari? Mlima Kilimanjaro ni kivutio kimojawapo cha utalii na kinachotuingizia mapato mengi sana. Halmashauri tano zinazouzunguka mlima huu hazipati gawio lolote rasmi ili kuendelea kuchochea maendeleo ya hizi Halmashauri. Tuzidi kuvitambua na kuvitangaza vivutio vipya vya utalii na vile vya zamani, kwani uwekezaji katika utalii ni wa gharama ndogo zaidi lakini mapato yapatikanayo ni makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, ni nini kinachoendelea katika ufufuaji wa Kituo cha Kuzalishia Umeme cha Kikuletwa kule Hai? Maji yapo ya kutosha.

Tuendelee kuwasaidia wachimbaji wetu wadogo wa madini na hasa tusimamie vizuri madini yetu ya vito, kwa maana ya kuyakachua hapa hapa nchini kwa mfano *Tanzanite.*

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Serikali kwa kutuunga mkono katika Sekta ya Maji Safi na Salama. Ninashauri elimu yetu sasa ya lazima iwe ni kiwango cha Kidato cha Nne badala ya Darasa la saba. Tusisahau elimu ya ufundi kote nchini. Pongezi sana kwa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mheshimiwa Spika, tuongeze bidii katika vita dhidi ya malaria, tuendelee kuwahimiza walemavu na kuwaendeleza, pia kuwatunza wazee. Tuisimamie sana Sera Mpya ya Maendeleo ya Mtoto kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa msisitizo wake katika matumizi ya Lugha yetu ya Kiswahili pia kwa kurudisha utaratibu wa Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusisitiza usimamizi mzuri wa pesa tunazozipeleka katika Halmashauri zetu pamoja na kuangalia thamani ya pesa zilizotumika.

Mheshimiwa Spika, kwa nini wananchi wetu wanalazimika kwenda Nairobi kupata *visa* za kwenda Uingereza? Angalizo, tuwe makini katika ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uzima ili na mimi niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Waziri wa Nchi (TAMISEMI), Mheshimiwa Celina Kombani; Naibu Waziri, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, pamoja na Wataalam wote kwa Hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nielekeze mchango wangu kwenye suala la miundombinu, afya na elimu. Naomba niikumbushe Serikali kuhusu ahadi za Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu na Rais wa Awamu ya Nne kuhusu ujenzi wa Barabara ya JIA – Mirerani. Naishukuru Serikali kwamba, tayari imepandishwa hadhi na kuwa Barabara ya Mkoa. Ahadi ya Rais itekelezwe, siyo kawaida Rais kutoa ahadi hewa; tutashangaa.

Mheshimiwa Spika, naleta kilio changu leo kwa kuwa muathirika mkubwa wa barabaa hii ni mimi. Mwaka 1998 niliwapoteza watoto watatu, wakati binti yangu akijifungua mapacha. Wakati tukijaribu kumpeleka Hospitali ya Rufaa KCMC baraba iligeuka kuwa mto na baada ya kupoteza damu nyingi tukiwa njiani alipoteza maisha pamoja na watoto mapacha. Toka mwaka 2005 hadi 2009 tumekuwa tukipewa ahadi na Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa tunamalizia kipindi cha miaka mitano Awamu ya Nne. Wapiga kura wetu wanataka kusikia kwamba, Ahadi za Rais wetu zinatekelezwa pamoja na Barabara za Vijijini. Tunaomba gari la kuhudumia watoto chanjo.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Mirerani una wakazi wapatao 52,000, kuna kituo kimoja cha afya, lakini tuna tatizo la watoto kutokupatiwa chanjo kwa wakati. Hakuna gari maalum kwa ajili ya kuhudumia chanjo mpaka wangojee gari linalotoka Wilayani ambapo ni kilomita 145. Je, gari moja tu inaweza kuhudumia chanjo Wilaya nzima? Tunaomba gari maalum kwa ajili ya Kituo cha Afya Mirerani ili liweze kuhudumia chanjo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niipongeze Serikali kwa kuimarisha miundombinu ya elimu katika shule za awali, msingi, sekondari, vyuo vya ufundi stadi na kadhalika. Pia Serikali imepiga hatua kubwa katika kupanua elimu ya juu pamoja na kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Dodoma, lakini kuna tatizo la wanafunzi kurundikana madarasani kutokana na uhaba wa shule za msingi. Maeneo mengine watoto ni wengi madarasa ni machache hivyo kupelekea wanafunzi kurundikana madarasani. Ningeomba Wizara ya Elimu ijaribu kuongeza fedha za MMEM kwa sababu zinazotolewa ni kidogo sana ili ziweze kuongeza madarasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imetenga eneo la Mji Mdogo wa Mirerani kuwa Maalum kwa Uwekezaji wa Viwanda *(Export Processing Zone - EPZ Centre);* na kwa kuwa Serikali imepiga marufuku uuzwaji wa madini ghafi nje ya nchi badala yake madini yakatwe, yasanifiwe na kuyahifadhi vizuri kwa ajili ya kuyauza nchi za nje: Je, tangu Serikali ilipotangaza Mji huu kuwa Maalum kwa ajili ya Uwekezaji wa Viwanda (EPZ), eneo limetengwa karibu hekta elfu mbili; je, ni sababu zipi zilizopelekea hadi leo hatimiliki haijapatikana? Kwa nini Wizara husika isianze kutengeneza miundombinu ya barabara, umeme, maji ili kuwavutia wawekezaji? Je, ni kweli Serikali inakusudia kufanya utekelezaji katika eneo hilo? Je, ni kwa nini Halmashuri ya Wilaya ya Simanjiro isishughulikie hati miliki ya eneo hilo kwa haraka ili tuweze kuwakaribisha wawekezaji?

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atakapohitimisha hotuba hii, anieleze sababu za kutokupatikana kwa hati miliki ya EPZ Mji Mdogo wa Mirerani.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Spika, mwaka huu wa 2010 ni Mwaka wa Uchaguzi wa kuchagua Viongozi wa kuiongoza nchi yetu; hivyo ni wajibu wa Serikali na Tume ya Uchaguzi kuuendesha Uchaguzi kwa uhuru, haki na uadilifu mkubwa, kwa kuwa kila mtu anayo haki ya kuchagua kiongozi anayempenda kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Uchaguzi kumekuwepo baadhi ya Vyombo vya Serikali vinavyojishughulisha na mambo ya uchaguzi, ambavyo kisheria hawatakiwi kufanya hivyo. Baadhi ya vyombo vimekuwa vikijishirikisha kuwatesa wapiga kura na baadhi ya watu hao hawawatendei haki wapiga kura na kuwabambikia kesi ambazo hazina msingi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Uchaguzi ndiyo chombo pekee ambacho kinatakiwa kutoa elimu ya wapiga kura jinsi ya kupiga kura, na ni wajibu wa Tume kuangalia orodha za wapiga kura, kuwaondoa wale ambao wamefariki na kuwaorodhesha wapiga kura wapya ambao wamefikisha umri wa kupiga kura. Vile vile Tume ijitayarishe vya kutosha ili kuondoa dosari wakati wa Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Muungano ndiyo chombo chetu kilichotuunganisha Watanzania, hivyo pamoja na vikao vinavyofanyika vya kutatua kero za Muungano, wakati umefika na hizo kero saba zilizobakia zipatiwe ufumbuzi wa kufaa ili kuondoa kero hizo tuendelee kuishi na kudumisha Muungano.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukua kwa hali ya uchumi lakini ukuaji huo hauwanufaishi wananchi walio wengi kutokana na mfumko wa bei, kupanda kwa mafuta ya petrol na dizeli kumechangia mfumko mkubwa hivyo mwananchi hajanufaika na ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Mtanzania. Asilimia 80 wamejiajiri katika shughuli za kilimo lakini bado kilimo tunachokwenda nacho ni kilimo cha jembe la mkono na bado upatikanaji wa pembejeo za kilimo hazipatikani ipasavyo; hivyo kuna haja ya kubadilika kama kweli tunataka Mapinduzi ya Kijani na Sera ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, uvuvi katika Bahari Kuu bado haujapatiwa muafaka, tunao samaki wengi lakini hawatunufaishi katika maendeleo ya nchi yetu. Uvuvi ambao unatazamwa zaidi ni uvuvi katika maziwa ndiyo kidogo unasaidia, kwani viwanda vya samaki vimejengwa tu. Ipo haja sasa kutazama Uvuvi wa Bahari Kuu.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mizengo Pinda (Mb), Waziri Mkuu, maarufu kama mtoto wa mkulima, kwa kazi nzuri ya usimamiaji wa shughuli zote za Serikali. Nampongeza Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani (Mb), nampongeza pia Naibu Waziri, Mheshimiwa Aggrey Mwanri (Mb), Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu na Watendaji wote. Pia nawapongeza Katibu Mkuu (TAMISEMI) na Manaibu wake, kwa ushirikiano wa pamoja katika kuandaa Bajeti hii muhimu ya kuhitimisha miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waziri Mkuu ndiye mratibu wa shughuli zote za Serikali, napenda kuchukua nafasi hii ili nitoe mchango kwa masuala kadhaa kama uboreshaji ili kufanya vizuri zaidi kwa hatua zijazo.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe kipaumbele kwa mikoa yenye hali duni kiuchumi, kipaumbele hiki ni kwa ongezeko la kutunisha bajeti (kuipandisha) ili kuhakikisha kwamba, nyongeza ya fedha itasukuma masuala mbalimbali ya kimaendeleo katika mikoa iliyo nyuma kimaendeleo. Kuendelea kuipa fedha kidogo mikoa iliyo nyuma kimaendeleo ni hatua ya kuifukarisha zaidi. Mkoa wa Singida tunahitaji nyongeza zaidi ya fedha ili kupiga hatua zaidi kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kwa hali ya mgawo wa fedha tuliyoipata Mkoa wa Singida ni ongezeko dogo sana kutokana na bajeti ya mwaka jana, ukilinganisha na mikoa mingine. Namwomba Waziri Mkuu kama Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali kuendelea kuujengea uwezo Mkoa wa Singida kifedha ili kukamilisha miradi mbalimbali ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa maeneo ya kiutawala; nafurahi hatua za Serikali kufanya mgawanyo kwa Kata mbalimbali zikiwemo Kata tatu mpya za Jimbo la Iramba Magharibi ambazo ni Mgongo, Ndulungu na Mang'ole. Pamoja na vijiji vyote vile vipya vya Iramba Magharibi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hiyo nzuri ya Serikali, naomba Serikali ione umuhimu wa kuigawa Wilaya ya Iramba ambayo sasa eneo lake la utawala ni kubwa sana; sasa baada ya ongezeko la Kata mpya zinafanya Wilaya ya Iramba kuwa na Kata 32. Kwa kuwa ilikuwepo ahadi ya Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliyoitoa wakati wa Kampeni 2005, juu ya kuigawa Wilaya ya Iramba; naomba sasa ahadi hiyo itekelezwe kwani ukubwa wa eneo unaleta ugumu katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa kuwaletea maendeleo wananchi.

Mheshimiwa Spika, juhudi za Serikali ya Mkoa wa Singida za kuanzisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Singida, bado ukamilishaji unashindikana kutokana na kukosekana kwa fedha. Naiomba Serikali itusaidie kuikamilisha Hospitali hii, kwani ni muhimu sana kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kilimo Kwanza; Mkoa wa Singida unategemea kilimo kwa asilimia 95. Ukulima wa Singida ni wa kutumia jembe la mkono na wanyama kazi, matumizi ya matrekta ni kidogo sana. Mvua za mm 500 – 700 ambazo hupatikana bila mpangilio maalumu bado zinafanya mkulima kutokuwa na uhakika wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri Mkuu achukue hatua juu ya Miradi ya Umwagiliaji ya Mlandala wa Mwaka 2007 uliotumia takriban shilingi milioni mia mbili na ishirini. Mradi huu kutokamilika hadi sasa, Mradi wa Masimba na Tyeme/Masagi kupoteza fedha za umma bila miradi hiyo kufanya kazi ni usaliti na wizi usiotakiwa. Bado nasisitiza zana za kilimo kupitia Mfuko wa Pembejeo usifanye upendeleo na pia kuwapatia mkopo mara moja kwa wale waliotimiza sifa.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa Watendaji wabovu wa Halmashauri za Wilaya, wale wabadhirifu, naomba Waziri Mkuu aendelee na fagio ili wabaki watendaji wanaozingatia maadili.

Mheshimiwa Spika, juhudi na elimu zielekezwe vijijini ili kupambana na Gonjwa Hatari la UKIMWI. Aidha, uratibu uendelee katika kubaini matatizo mbalimbali yanayokwamisha juhudi za kupambana na ugonjwa huu hatari.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba nzuri na inayoeleweka na inayoelezea fika mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nne na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mheshimiwa Spika, napenda nikubaliane na mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Nne. Kwanza kabisa, kitu muhimu cha maendeleo ni elimu na Serikali hii imejenga Chuo Kikuu cha Dodoma, ambacho kitakapokamilika kitachukua wanafunzi 40,000. Pia siyo Chuo hiki tu, bali kuanzishwa Vyuo Vikuu vingi ambavyo vinaongeza changamoto kubwa ya maendeleo nchini.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mipango ni kitu kigumu sana. Hata hivyo, maendeleo yaliyopatikana katika Mkoa wa Morogoro na hasa Wilaya ya Morogoro Vijijini na Mnono Jimboni kwangu, Ilani imetekelezwa hasa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya mwaka 1995, mtu asingethubutu kuzungumzia maendeleo katika Jimbo hili. Safari ya kutoka Kisaki hadi Morogoro ilichukua siku nne hadi wiki moja, sasa hivi Wananchi wa Kisaki Station wanaweza kusafiri kutoka Kisaki hadi Morogoro na kurudi siku hiyo hiyo. Barabara zinapitika wakati wote.

Mheshimiwa Spika, maendeleo yaliyopatikana siyo barabara tu, Jimbo sasa lina mawasiliano ya simu za viganjani za mitandao mitatu.

Mheshimiwa Spika, kielimu, Jimbo lilikuwa lina sekondari moja tu ya Matombo. Sasa hivi Jimbo lina sekondari 19. Ni kweli kwamba, Jimbo lina matatizo hasa katika eneo la walimu wa shule za sekondari na shule za msingi. Hili ni tatizo la Taifa zima.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Morogoro Vijijini bado ina tatizo la Makao Makuu yake. Hadi hivi sasa Makao Makuu ya Morogoro Vijijini bado yapo Morogoro Mjini. Hili ni tatizo kubwa sana na kizuizi kikubwa cha maendeleo. Hii ni kwa sababu ya hali halisi ya usafiri wa kutoka kona zote za Morogoro Vijijini, lazima waje Morogoro kwa mikutano yote na shughuli zingine zozote za kiserikali lazima wapite Morogoro na walale Morogoro Mjini kabla ya kurudi kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Halmashauri ya Morogoro Vijijini, limeamua kuhamishia Makao Makuu yao kwenye Kijiji cha Mvuha, ambacho kipo katikati ya Wilaya ya Morogoro Vijijini. Pamoja na ukweli kwamba, nia tunayo na sababu lakini uwezo hatuna. Katika Bajeti hii, Baraza la Halmashauri limeomba ombi rasmi la shilingi bilioni moja ili tuweze kuhama haraka. Ofisi ya Mbunge tumeamua kuijenga Mvuha. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hapa tunaomba msaada wako.

Mheshimiwa Spika, ninasikitika sana kwa kitendo cha TANESCO kumwongopea Rais kwamba, Tarafa ya Matombo ingepata umeme mnamo mwezi Aprili, 2010. Mheshimiwa Rais, aliwauliza kama itawezekana walijibu ndiyo lakini hadi sasa hakuna dalili za utekelezaji huu.

Mheshimiwa Spika, sina budi kuwapongeza TANROADS kwa kutimiza ahadi zao juu ya kumaliza Daraja la Mto Ruvu pale kwenye Kijiji cha Kijamila; na hali kadhalika wameihudumia Barabara ya Mkoa ya Morogoro hadi Kisaki Station na ile ya Msalabani hadi Tawa. Walimuahidi Rais na wametekeleza.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Morogoro Kusini wana masikitiko juu ya Ziara za Viongozi Wakubwa wa Taifa kutotembelea Jimboni kwao. Ni kweli kwamba, Jimbo la Morogoro Kusini linaanza kilomita sabini baada ya kutoka Morogoro. Ili kufika Kisaki Station ni umbali wa kilomita 144. Pamoja na umbali huo, Rais Jakaya Kikwete alifika wakati wa kampeni, lakini baada ya hapo hakuna Kiongozi Mkubwa aliyefika Jimboni zaidi ya Kijiji cha Mtamba, Matombo.

Mheshimiwa Spika, sitakuwa mwenye shukrani kama sitamshukuru na kumpongeza Mkuu wa Mkoa, kwa kutembelea huko mara kwa mara. Hali kadhalika, Mkuu wa Wilaya ambaye hachoki kutembelea Morogoro Vijijini. Ninawashukuru sana Viongozi hawa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa uongozi wake thabiti na mahiri. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na Watendaji wengine wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake, kwa hotuba nzuri na kazi nzuri. Naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kusimamia kwa ufanisi mkubwa sana utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya 2005. Ningependa kuchukua fursa hii, kuchangia kwa ujumla na hatimaye kuhusu Jimbo la Mkinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji, ipo haja kubwa ya kupambana na urasimu hasi na kuzidi kuhimiza Utawala Bora. Wilaya ya Mkinga imefaidika na Programu ya Huduma za Kifedha Vijijini kwa kiasi cha awali. Bado Wilaya hii mpya ina nafasi kubwa ya kufaidika na Programu hii.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mkinga imefaidika sana na maboresho ya mawasiliano, lakini napenda kurudia maombi ya kuboreshewa mawasiliano ya simu kwa maeneo ya pembezoni kama vile Mwakijembe, Jasini, Manza, Kwale, Mazola, Bamba, Boma na Kinyatu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda na biashara; Wilaya ya Mkinga inatarajia kufaidika sana na Mpango wa Maendeleo wa Kanda ya Kaskazini *(Northern Corridor)* hasa kuhusiana na Mradi wa Magadi Soda, Soko la Kimataifa la Matunda na Mboga Mboga la Segera pamoja na Miradi Midogo ya Usindikaji chini ya SIDO.

Mheshimiwa Spika, ingawa nchi imefaidika kwa kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa nje kama inavyoonekana katika ibara ya 44, nchi ingeweza kufaidika zaidi kwa kuongezea thamani bidhaa kuliko kuuza bidhaa ghafi kama ilivyo sehemu kubwa ya mauzo yetu mpaka sasa.

Mheshsimiwa Spika, Wilaya ya Mkinga inatoa shukrani nyingi sana kwa maboresho ya takriban barabara zote wilayani humo. Shukrani maalumu ni kwa ujenzi kwa kiwango cha lami Barabara ya Tanga - Horohoro, ambayo uzinduzi wa ujenzi wake ulifanywa na Mheshimiwa Rais hivi karibuni. Wakati kazi kubwa ya uboreshaji wa barabara ukiendelea Wilayani kote, mkazo wa pekee unahitajika kwa ujenzi wa barabara inayounganisha Makao Makuu ya Wilaya, Kasera na Maramba kupitia Magodi, Mwanyumba na Mbambakofi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mkinga ina nafasi nzuri ya kuendeleza Utalii wa Mwambao wa Pwani ikiunganishwa na maeneo mengine ya Tanga, Zanzibar na Mombasa. Pia Wilaya hii ina nafasi nzuri ya Utalii wa Milimani na Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mkinga inashukuru sana kuwekewa umeme katika Makao Makuu yake na vijiji vya jirani vya Mkinga Leo, Karoyo, Menjamwenye, Golasingo na Mwakiponda. Tuna matumaini makubwa kwamba, maombi yetu ya kuwekewa umeme Vijiji vya Daluni, Gombero, Kwale, Vuga na Boma, yatatekelezwa katika mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mkinga imefaidika sana kwa Miradi mbalimbali ya Maji, lakini maji safi na salama bado ni kero kubwa sana kwa Wilaya ya Mkinga. Bado Makao Makuu Kasera ina shida kubwa ya maji. Maombi kwa Mradi huu na Miradi mingine yamefikishwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Yapo matumaini makubwa ya kutekeleza baadhi ya Miradi hii katika mwaka huu wa fedha.

Hata hivyo, changamoto kubwa inatukabili katika Miradi ya Maji ya Vijiji 10 chini ya Ufadhili wa Benki ya Dunia. Gharama za Wananchi kuchangia zimekuwa kubwa mno kiasi cha wananchi kushindwa kuchangia. Kero hii inaikabili Wilaya nyingine vile vile na ipo haja ya Serikali kubuni uvumbuzi ufaao kwa changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, kwa Sekta ya Elimu, Wilaya ya Mkinga imepata mafanikio makubwa sana. Mpaka mwaka 2005, Wilaya ya Mkinga ilikuwa na shule za sekondari 46, ambazo hazikuwa zimekamilika sawa sawa. Hivi sasa Wilaya hiyo yenye Kata 12 ina jumla ya shule za sekondari 16, zaidi ya lengo la shule ya sekondari moja kwa kila Kata. Hata hivyo, bado tunakabiliwa na changamoto za upungufu wa walimu, nyumba za walimu, mabweni, maabara, maktaba, umeme na mifumo ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya, tumejenga zahanati kwa Kata zote na vijiji vingi. Hivi sasa shughuli kubwa ni ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na Vituo vya Afya kwa Kata.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa inayoikabili Wilaya ya Mkinga hivi sasa ni kupata fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Makao Makuu ya Jengo la Halmashuri ya Wilaya ya Mkinga.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia 100.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda (Mb),

kwa Hotuba yake nzuri sana, iliyoandaliwa vizuri na kuisoma kwa ufasaha. Naunga mkono hoja yake kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwapongeza Wasaidizi wake; Mheshimiwa P. Marmo (Mb), Waziri wa Nchi; Mheshimiwa Celina Kombani (Mb), Waziri wa Nchi (TAMISEMI); Mheshimiwa Aggrey Mwanri (Mb), Naibu Waziri (TAMISEMI); Mheshimiwa P. Lyimo, Katibu Mkuu (PMO); Bibi Tarishi, Katibu Mkuu (TAMISEMI); na Watendaji wote chini yao kwa kumsaidia Waziri Mkuu kwa bidii, uadilifu na kumpa ushirikiano wa dhati hadi kufanikisha uandaaji wa hotuba yake aliyoisoma leo hapa Bungeni. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote, napenda kukumbusha suala la Mradi wa Baraba katika Kata ya Milingano itokayo Kijiji cha Mashewa Wilaya ya Korogwe kwenda Kijiji cha Bumba ambacho kiko eneo la Milimani. Barabara hiyo ni mpya, hivyo haipewi fedha maana haimo kwenye orodha ya urefu wa barabara za Lushoto.

Mheshimiwa Spika, Barabara hii imeletwa kwenye Ofisi yako ili ipewe fungu maalum lakini ni muda mrefu sasa hakuna mafanikio. Barbara ina urefu wa kilomita tano. Gharama za awali zilikuwa shilingi milioni 200 lakini sasa inafikia shilingi milioni 300. Mheshimiwa Waziri Mkuu, bila shaka anaikumbuka Barabara hii kwa sababu alikwishaitolea maelekezo tangu alipokuwa Naibu Waziri (TAMISEMI).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jitihada zake katika kuleta maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, amekuwa ni mfano mkubwa na mzuri kwa Viongozi wote wa Tanzania, kwa kuonesha njia ya Uongozi Bora na uliotukuka kwa ushirikiano wake katika kufanya kazi kwa bidii na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru na kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Nne na kufikia kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2005 – 2010.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Pemba, napenda kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wakishirikiana na Wafadhili wetu wakubwa, Serikali ya Norway, kwa upelekaji wa umeme wa uhakika katika Kisiwa cha Pemba. Umeme huo ulianzia Tanga – Pemba kwa kutumia nyaya zilizopitishwa baharini kwa utaalamu mkubwa sana. Umeme wa uhakika katika Kisiwa cha Pemba ni kitendo cha kihistoria.

Mheshimiwa Spika, naitakia heri Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na tuweze kushinda Uchaguzi Mkuu ili tuendeleze maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja na kuipongeza sana Hotuba na Bajeti.

Mheshimiwa Spika, ninashauri Wabunge wa Viti Maalum waruhusiwe kuingia kwenye Kamati za Fedha, kwani Wabunge wengi ni RCs na Mawaziri hawaingii; hivyo, wananchi kukosa mwakilishi wa hoja zao Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ushauri; kwa mfano, Halmashauri ya Kinondoni ina Wabunge wa Viti Maalum wengi, waingie kwa *rotation* kila mwaka wawili kwa kubadilishana. Aidha, Wabunge wa Viti Maalum kutoingia kwenye *Full Council (Finance Committee),* wanaoathirika ni wananchi.

**MHE. DR. IBRAHIM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Naipongeza Serikali kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi. Naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Kilimo Kwanza; changamoto kubwa iliyopo ni kuhakikisha kuwa zana za kisasa za kilimo na hasa matrekta na *power tillers* zinapatikana. Tatizo lililopo ni uhaba wa zana hizi na ukosefu wa *spares* hasa za *power tillers.* Nashauri, msukumo mkubwa uwekwe kwenye upatikanaji wa zana za kisasa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni mbegu. Msimu uliopita, Kibaha hapakuwa na mbegu kabisa na matokeo yake ilibidi tutumie mahindi yaliyovunwa wakati wa vuli. Suala la mbegu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke wazi mkakati wa kutekeleza azma ya kuwa na Kituo cha Afya kila Kata na Zahanati kila Kijiji. Hadi sasa, katika Jimbo la Kibaha Vijijini, mpango huu haujaanza.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kituo cha Afya cha Mlandizi kimeelemewa na idadi kubwa ya wagonjwa. Hata hivyo, Kituo hiki bado kinapewa mgao wa dawa wa Kituo cha Afya cha Kawaida. Je, Serikali haioni kuwa wakati sasa umefika kuongeza dawa kwa Kituo hiki cha Mlandizi ambacho kipo kando ya Barabara Kuu ya Morogoro?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Kibaha haina Hospitali ya Wilaya; na Mkoa wa Pwani hauna Hospitali ya Mkoa; Serikali ina mpango gani wa kuisaidia Wilaya ya Kibaha iwe na Hospitali ya Wilaya kwa kukiboresha na kukipandisha hadhi Kituo cha Afya cha Mlandizi au kujenga nyingine na pahali pengine kabisa ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha?

Mheshimiwa Spika, nawatakia kazi njema na naunga mkono hoja.

**MHE. NURU A. BAFADHIL:** Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi Usalama Barabarani, linafanya kazi nzuri sana lakini kuna tatizo linalojitokeza barabarani.

Mheshimiwa Spika, askari huwa wana mtindo wa kusimamisha magari. Magari hayo yanaposimama, kondakta hushuka na kusimama nyuma ya gari na askari huyo, baada ya mazungumzo tendo la rushwa linachukua nafasi.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine ajali za barabarani husababishwa na mwendo kasi wa madereva wakiwa wamelewa. Serikali iwe macho kwa madereva hawa walevi ambao huchangia ajali za barabarani.

Mheshimiwa Spika, adhabu anayopewa aidha dereva au kondakta ni sahihi lakini na abiria wakati mwingine wanachangia katika kusababisha ajali; wakati mwingine gari huwa uwezo wake ni kubeba abiria sitini, lakini utakuta gari hilo linabeba watu themanini hadi tisini.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ingetoa adhabu kwa abiria yeyote atakayekutwa amesimama hakupata kiti cha kukalia kwenye basi. Hii itasaidia kila abiria kuwa makini kwa kuhofia kutozwa faini kwa kusimama kwenye basi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu walinzi wa sungusungu kujichukulia madaraka mikononi, kwa kweli kuna baadhi ya vijiji au vitongoji wanakuwa na walinzi wa sungusungu. Hawa wanajifanya ndiyo mahakimu katika sehemu zao za makazi, wanawadhalilisha sana wananchi kwa kuwapiga. Serikali iwakemee sungusungu wote wenye tabia hii, wanavuruga amani na utulivu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wauguzi wetu kwenye hospitali kwa kweli wauguzi hasa wanaofanya kazi kwenye wodi ya wazazi, hawa ni wakunga ambao wanawazalisha akina mama, wanawapa lugha zenye maneno machafu na wakati mwingine hawampokei mama mjamzito. Hii ilitokea Mwanza hivi karibuni, mama aliyekataliwa kujifungua katika Kituo cha Afya na hatimaye akajifungulia barabarani. Huu ni unyanyasaji mbaya sana.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuanza mchango wangu kwa kutamka kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia 100; ni hotuba nzuri, inayojitosheleza, lakini pia inaleta matumaini kwa wananchi.

Ninampongeza Waziri Mkuu, Waisaidizi wake; Waziri Kombani na Mheshimiwa Marmo, kwa kazi nzuri waliyofanya na ambayo inadhihirika kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu.

Ninaipongeza sana Serikali kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kahama, kwa hatua yake ya kusikia kilio cha Wananchi wa Mji wa Kahama cha kutaka Mji wa Kahama upandishwe hadhi na kuwa Halmashauri ya Mji wa Kahama. Ninaipongeza sana Serikali kwa uamuzi huu kwa vile utaongeza kasi ya maendeleo katika mji huo.

Sambamba na hili la Mji wa Kahama kuwa Halmashauri ya Mji, ninaipongeza pia Serikali kwa kuiingiza Wilaya ya Kahama katika mfumo wa wakulima wa zao la mahindi wa kupatiwa ruzuku ya pembejeo ya mfumo wa vocha. Hatua hii ambayo ilianza katika msimu wa kilimo wa mwaka uliopita, kwa hakika uzalishaji umeongezeka maradufu. Tatizo ni kwamba, wakulima hawa wa zao la mahindi hawana soko maalum wanapoweza kuuza mazao yao kwa bei inayostahili, badala ya sasa ambapo wanauza mahindi yao kwa walanguzi, wengine wakiwa wa kutoka nchi jirani.

Kama nilivyosema hapo awali, Bajeti ya mwaka huu ni nzuri, kinachotakiwa ni Serikali kuweka mazingira yatakayohakikisha pesa iliyotengwa kwa kila sekta inatumika ipasavyo. Mathalani, Serikali ihakikishe pesa iliyotengwa kwa ajili ya barabara vijijini, kwanza, imegawanywa kwa uwiano stahili kulingana na mahitaji, lakini inafanya kazi inayolingana na thamani ya fedha iliyotengwa.

Sekta ya Utawala Bora pia ni muhimu ikapewa kipaumbele hasa katika ngazi za vijiji na vitongoji, ambako zipo kero kama za watendaji wabovu, rushwa, watendaji kutokujua majukumu yao na kadhalika.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, tunaipongeza TRA katika mkakati wake wa kukusanya mapato, lakini ni vyema utaratibu huo usiathiri haki za binadamu. Imedhihirika tarehe 9 Juni, 2010, Tunduru Mjini karibu na Mgahawa wa

Mgesa, watu wawili walipigwa risasi wakiwa wamekaa pembezoni mwa Mgahawa wakati wa zoezi la kukusanya mapato kwa wenye pikipiki (bodaboda) na Ndugu Cavin na Ndugu Adamba wako Hospital ya Ndanda kule Masasi.

Mheshimiwa Spika, kitendo hiki ni cha aibu cha kutumia nguvu zisizo za lazima huku taarifa za kupotosha na kadhalika. Kulikuwa na mapigano kati ya raia, TRA pamoja na Polisi. Kitendo cha kupiga risasi raia si jambo la kawaida, Serikali ni lazima iwe makini kukomesha matukio haya.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa ardhi kwa mwekezaji anayejulikana kwa jina la ECO huko CHUBI, Kata ya Bumbuta, umeathiri wananchi wa ATA, Kata ya Kisese, ambao ardhi yoa imechukuliwa isivyo halali na mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, hivi Serikali ya Kijiji ina uwezo wa kummilikisha ardhi ekari elfu nne kwa Sheria ya Ardhi ya 1999 na tatizo hili Serikali italipatia ufumbuzi lini kuondoa mgogoro wa ardhi ambao pia unaathiri wananchi wenyewe wa Chabi kuimarisha alizeti fupi *(Cuttum).*

Mheshimiwa Spika, tatizo la meli za kigeni kuvuna rasilimali za samaki wetu katika Bahari ya Hindi huku maeneo ya Mwambao wa Bahari ya Visiwa vya Unguja na Pemba meli hizo zinaharibu zana za wavuvi wetu; mfano, Shehia ya Kengeja, Wavuvi wa Chole na Likoni, Shehia ya Kangani na Kukuu, wavuvi nao wameathirika na uvunaji samaki wa meli za kigeni. Je, Serikali inasema nini juu ya kero hii?

**MHE. RAJABU HAMAD JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na ni hotuba ya kazi ambayo imetuonesha tunapotoka tulipo sasa na tunapokwenda ndani ya miaka mitano ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapongeza wasaidizi wake Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni Mheshimwa Marmo na Mheshimiwa Celina na Mheshimiwa Mwanri kwa kazi nzuri wanayoifanya ndani ya majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzuri wa taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na wasaidizi wake nawashauri mambo yafuatayo:-

1. Wizara kuweka timu ya ufuatiliaji (*Monitoring team*) na kama ipo kuimarisha ili iweze kuziba mapungufu yaliyopo ya kuibuliwa matatizo na Kamati za kudumu za Bunge.

2. Tume ya kudhibiti madawa ya kulevya iunganishwe na Tume ya UKIMWI. Hii ni kwa sababu majukumu yao Tume mbili hizi yanafanana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuleta hotuba nzuri na jinsi ambavyo amekuwa akijibu kwa ufasaha maswali ya papo kwa papo hapa Bungeni. Pia nampongeza Mheshimiwa

Celina Kombani, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikaliza Mitaa na Naibu wake Mheshimiwa Aggrey Mwanri kwa kazi nzuri wanazozifanya Mheshimiwa Aggrey Mwanri amekuwa mahiri sana kwa kujibu maswali Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ninayo machache ya kuongelea nayo ni masuala ya umeme na barabara ya Kyaka – Bugene (Kilomita 59.1).

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2006, Serikaliimekuwa ikiahidi kupeleka umeme katika Tarafa ya Nyakiyonza kupitia Ihanda, Rwabwere, Kamagambo, Nyakagoyagoye, hadi Nyakaiga. Mwaka huu 2010, Bunge la April, akijibu swali la umeme kuhusu maeneo haya, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Adam Malima alikiri kuwa ahadi ya Serikalini ya muda mrefu tangu 2006 na hivyo Serikaliitatenga fedha hizo katika bajeti ya 2010/2011. Naomba na kuisihi Serikaliitimize ahadi yake kama ambavyo imekuwa ikiahidi.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna umeme unaokusudiwa kupelekwa Kijiji cha Ndama, Rukaka, Nyabwegira nguzo tayari zimeshasimikwa karibu miaka miwili iliyopita wananchi wanasubiri kwa hamu kuona umeme unawaka. Sambamba na hili kuna nguzo zimeanza kusambazwa kutoka Kayanga kuelekea Kituntu hadi Rwambaizi ingawa nguzo hizi zimekwisha eneo la Kakilo, Kijiji cha Runyaga tu na hazijapelekwa hadi Rwambaizi. Naibu Waziri alikiri kuwa fedha zipo, je, ni kwa nini umeme huo haupelekwi maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Serikaliya 2009/2010, ilipitisha fedha za kupeleka umeme eneo la Bisheshe, Nyakayanja, Nyaishozi hadi Ihembe, Serikaliiliahidi kuwa kazi hiyo ingeanza rasmi mwezi Mei, 2010. Leo hii tupo katikati ya mwezi Juni, 2010 na kazi hiyo bado haijaanza, je, Serikaliinasemaje kuhusu kuanza kwa mradi huu. Naomba jibu la uhakika kwani tayari wananchi wangu nimeshawahabarisha juu ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, barabara ya lami Kyaka - Bugene Kilomita 59.1 ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Napongeza juhudi za Serikalizilizokwishafanyika. Hadi sasa zabuni ya barabara hiyo ilifunguliwa tarehe 25/5/2010, wakandarasi watatu walijitokeza. Gharama ya chini ya ujenzi wa barabara hii ni karibu shilingi billioni sabini na sita.

Mheshimiwa Spika, taratibu za ujenzi wa barabara zinaitaka Serikaliilipe asilimia 15 za gharama yote ya mradi ambayo kwa mradi huu inaweza kufikia billioni kumi. Pia kabla ujenzi wa barabara haujafanyika ni lazima fidia ilipwe. Kwa barabara hii ni karibu bilioni tano zinahitajika. Jumla ya fedha inayotakiwa ili barabara hii ianze ni karibu billioni kumi na tano.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha bajeti inaonyesha barabara hii imetengewa shilingi 4.3 bilioni. Fedha hizi ni kidogo sana na hazitoshi hata fidia ya Shilingi bilioni tano na wala hazitoshi kulipa malipo ya awali ya mkandarasi Shilingi bilioni 10.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hii nina wasiwasi mkubwa kuwa kama fedha ya kutosha haitatengwa bajeti hii ni vigumu ahadi ya Mheshsimiwa Rais kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikaliifanye kila linalowezekana fedha ipatikane na barabara hii ianze kujengwa kabla ya Bunge hili kuvunjwa.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naiomba Serikaliifikirie maombi ya muda mrefu ya wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi la kupatiwa Wilaya ama kwa kuanzia Halmashauri, kutokana na ukweli kwamba Jimbo hili ni pana sana. Sensa ya 2002 haikufanywa vizuri katika eneo hilo na baadaye kuonesha idadi ndogo ya watu. Hata hivyo, zipo Wilaya ambazo ilitokea hivyo kwa sababu mbalimbali na hasa upana wa maeneo hayo.

Takwimu zifuatazo zinajieleza katika kuhalalisha hoja ya wananchi wa Manyoni Magharibi:-

(a) Wilaya ya Manyoni ni zaidi ya nusu ya Mkoa wa Singida. Wilaya ni zaidi ya $Km^2$ 28,000 kutokana na $Km^2$ 49,000 za Mkoa. Mkuu wa Wilaya (DC) na watendaji wanapata shida sana katika kuhudumia kwani Wilaya ni pana.

(b)

| **Wilaya** | **Ukubwa wa eneo** | **Idadi** |
|---|---|---|
| Longido | 7,929 | 86,801 |
| Liwale | 37,412 | 83,192 |
| Pangani | 1,784 | 50,410 |
| Mafia | 631 | 44,233 |
| Siha | 1,316 | 109,779 |
| Ruangwa | 2,835 | 139,168 |
| Nanyamba | 4,938 | 117,927 |
| Jimbo la Manyoni Magharibi | 18,957 | 80,184 |

Mheshimiwa Spika, miaka ya 70 na 80, Wilaya moja ya Masai iliweza kutoa Wilaya tano kwa sababu ya upana wa maeneo ya Wilaya hiyo Kilomita za mraba 64,755 lakini idadi ndogo ya wananchi. Leo hii jumla ya watu katika Wilaya zote tano ni watu 695,076:-

| **Eneo** | **Kilomita za Mraba** | **Idadi ya watu** |
|---|---|---|
| Monduli | 7,827 | 126,608 |

| | | |
|---|---|---|
| Ngorongoro | 15,8875 | 145,875 |
| Kiteto | 13,519 | 170,140 |
| Simanjiro | 19,593 | 165,752 |
| Longido | 7,929 | 86,801 |
| | **64,755** | **695,076** |

Mheshimiwa Spika, watu 695,076 wamesambaa sana katika maeneo ya Wilaya tano,lakini wangelikuwa karibu karibu kama Bukombe ama Kinondoni wangeweza kuwa na Wilaya moja tu. *Definitely* kigezo cha idadi ya watu tu si lazima sana pale ambapo watu wanahangaika kutokana na ukubwa wa maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wilaya mpya ya Manyoni au Halmashauri. Lengo ni kusogeza huduma kwa wananachi. Wakoloni walitumia kigezo cha idadi ya watu kutugawa ili iwe rahisi kututawala (*divide and rule*) ndiyo maana wakaweka *priority* kwenye kigezo hicho.

Mheshimiwa Spika, pili, naiomba Serikaliiingilie kati suala la wanafunzi wa shule ya msingi za Itigi Reli, Furaha na Sanjaranda, ambao wamefutiwa matokeo ya 2009 na Baraza la Mitihani, kwa madai ya kuibia mtihani. Watoto hao waliundiwa Tume na kuhojiwa ambako inadaiwa walikiri kuibia. Lakini ni kosa la nani hasa, kama siyo walimu na wasimamizi wa mtihani, kuwashawishi watoto hao kuibia ili wao wapate umaarufu na pia rushwa. Watoto hao hawana makosa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Baraza la Mitihani, Cap.107 ya 2002, inampa Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani kufuta matokeo ya mtihani, anapima kuna *irregularities* zilizojitokeza, lakini sera ya Wizara hairuhusu watoto kutungiwa mtihani mwingine. Watoto hawa takriban 200 sasa wako nje ya mfumo mzima wa elimu nchini, wanashauriwa wasome kama watu wazima.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikaliione uwezekano wa kuwasaidia wanafunzi hawa waendelee na masomo ya mfumo mzuri, wazazi wamepoteza gharama kubwa kuwafikisha hapo.

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikaliiongeze kiwango cha fedha zizotolewa kwa ujenzi wa hospitali ya Singida kutoka Shilingi bilioni mbili hadi angalau bilioni l.5 mpaka bilioni saba kwa mwaka huu ili kuchagiza kasi ya ujenzi wa hospitali hiyo.

Mheshimiwa Spika, nne, nawapongeza na naunga hoja mkono.

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kupongeza hotuba nzuri ya Waziri Mkuu pamoja na waandaji wote wa hotuba hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

(1) Kutokana na uhaba wa uchakavu wa majengo ya Mahakama, hususan Mahakama za Mwanzo na za Wilaya, nashauri ofisi ya Waziri Mkuu, iagize Halmashauri zote, hasa zile ambazo hazina Mahakama, zijenge Mahakama moja na nyumba ya Hakimu moja katika Tarafa husika kwa mwaka na waendelee hivyo mpaka watakapokamilisha mahitaji ya Wilaya zao.

(2) Uteuzi wa Wakuu wa Wilaya ni lazima uzingatie uwezo wa kiutendaji wa wateule. Orodha ya Ma-*DC* waliopo kwa hakika imejaa watu ambao hawana uwezo na wanaiabisha Serikaliyetu kwa tabia zao za ulevi na ukosefu wa maadili. Serikaliiwe makini sana katika kufanya uteuzi wa Ma-*DC* wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja ya Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi uliyonipa. Nianze kwa kumpongeza Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Naibu Waziri, Wakuu wote wa Mikoa, Makatibu Tawala wanaoshirikiana na Waziri Mkuu katika kazi za Serikalikwa ujumla wao, nawapongeza kwa ushiriki wao wakiwa wanashirikiana na umma.

Mheshimiwa Spika, yapo mengi yaliyotekelezwa na Serikaliya CCM katika Ilani yake. Maji: pamekuwepo na tatizo la maji Wilayani Misungwi kwa muda mrefu kutokana na hoja nilizopewa na wananchi nilizifikisha hapa na Serikaliimezifanyia kazi mfano, ni mradi wa maji wa Nyaluti hadi Misungwi Mjini, tayari mradi huo uko katika hatua za uzinduzi. Pongezi zimfikie Waziri wa Maji Profesa Mark Mwandosya kwa kusimamia mradi huu, atakumbukwa daima na wananchi wa Misungwi ambao wamekuwa na kero ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, pongezi zingine ni kwa Mhandisi Dr. Lwetabula Mkurugenzi wa MWAUSA na timu yake kwa kushughulikia mradi huo akisaidiana na Mhandisi Kiyenze na timu yake ya Wilaya ilikuwa chini ya Mkurugenzi Selekwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara: utekelezaji katika kuboresha mawasiliano ya barabara hasa zile za mkoa *(TANROAD)*, lakini bado kuna tatizo kubwa katika barabara za Halmashauri ambazo zipo barabara hazipitiki hasa wakati wa masika mfano halisi, ni barabara ya Misungwi – Mondo eneo la Nguge. Naiomba Serikali ilishughulikie tatizo hilo ili wananchi wa Vijiji vya Kata hiyo ya Mwaniko waondokane na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, juhudi za ujenzi wa shule za sekondari unaendelea vizuri, shule tatu zimejengwa Wilayani Misungwi, ziko katika Vijiji vya Bujingwa (Nyabumhanda Sekondari), Mamaye (Mamaye Sekondari) na Iteja (Iteja Sekondari).

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba, tumeomba na tumekamilisha mahitaji yote kwa sekondari ya Nyabumhanda, tayari wanafunzi waliokuwa

wamechaguliwa na kujishikisha katika Shule za Sanjo Sekondari, Kanyerere Sekondari, Idetemya Sekondari wapo na wanazidi kuumia kutokana na safari ndefu kwenda katika shule hizo.

Mheshimiwa Spika, nazidi kuiomba Serikali itoe kibali kwa shule hiyo kuanza kwani taratibu zote zimefanyika, mashaka yalikuwa wanafunzi wangepatikanaje, tayari jibu tumelitoa kwa idara husika kuwa wanafunzi wapo na walichaguliwa na kupangwa kwa muda katika shule nilizozitaja naomba shule ifunguliwe.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha pamba na bei za mazao (pamba), bado tunaendelea kuwasemea wakulima wa zao la pamba kwamba, bei inayotolewa haiendani na bei ya soko hivyo Serikali isimamie bei hasa za zao la pamba mfano, mwaka huu bei iliyopo ni kati ya *cent* 75 kama mkulima atalipwa vizuri basi anapaswa alipwe Shilingi 800 kwa kila kilo ya pamba mbegu yaani pamba toka kwa mkulima.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu ongezeko la Kata. Jambo hili litapunguza adha kubwa ya kufuata huduma za Serikali mbali. Ombi kwa Serikalini, ni vema ikaelekeza bajeti maalum ili kuzijengea uwezo Kata hizo vinginevyo wananchi watakaokuwa katika Kata hizo watakuwa na mzigo mkubwa kwani watahitaji kujenga sekondari za Kata zao, vituo vya afya vya Kata zao na vingine vingi hivyo Serikali iwe na mpango maalum.

Sambamba na hilo bado ombi langu Serikali ifuatilie posho za Wenyeviti wa Shule, Vijiji na Vitongoji, maana huwa hawapati na badala yake huishia pasipohusika. Kazi za watumishi hawa ni ngumu na muhimu katika kuleta maendeleo. Idara za Ukaguzi za Halmashauri zifuatilie ili kasoro hizo zisiendelee kujitokeza. Inashangaza kuona uongozi wa CCM Matawi, Kata, unapata posho kutoka chama lakini Serikali haipati ukilinganisha Serikali ndiyo yenye vyanzo vya mapato vingi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Misungwi inayo matatizo ambayo iliona ni vema tulete maombi maalum ili kuweza kufanikisha utekelezaji wa bajeti tuliyoleta Serikalini.

Mheshimiwa Spika, maombi hayo maalum ni:-

(i) Ujenzi wa ofisi kuu ya Halmashuri ya Wilaya ili watumishi wapate sehemu ya kufanyia kazi T.Shs.500,000,000/=.

(ii) Nyumba kumi ili kupunguza kero kwa watendaji wa Halmashauri TShs.500,000,000/=.

(iii) Ujenzi wa barabara ya Misungwi – Mondo T.Shs.283,280,000/=.

(iv) Suala la Maji katika kambi ya watoto Albino TShs.25,590,000/=.

(v) Barabara ya Buhingo – Isesa – Ihelele Tshs.441,400,000/=. Muhimu sana vinginevyo huduma ya mradi wa maji utashindwa kufikisha huduma ya madawa na spea katika eneo husika.

(vi) Hospitali ya Wilaya ya Misungwi Tshs.1,735,272,000/=.
(vii) Pesa kwa ajili ya usimamizi wa mitihani ya shule za sekondari pamoja na chakula ni Tshs.260,574,000/=.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali ilione hilo, jumla ya Bilioni 5.1 zinahitajika ili kutoa huduma kwa wananchi vizuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote wa Nchi katika ofisi yake, Makatibu Wakuu wote wanaokusaidia, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi, Mungu awajalie muweze kutekeleza majukumu yenu vizuri.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri za kutukuka anazofanya toka aingie madarakani. Pia nawapongeza Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Marmo na Mheshimiwa Kombani na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwanri, Katibu Mkuu, Ndugu Lyimo na Ndugu Tarishi, pia Manaibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa ofisi yako. Nampongeza pia kwa hotuba yake nzuri aliyoisoma jana, pia naipongeza hotuba ya Mheshimiwa Kombani.

Mheshimiwa Spika, kazi nzuri zinafanywa na wasaidizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kasoro nyingi bado zipo kwenye baadhi ya Halmashauri zetu za Wilaya, kuna Wakurugenzi wachache na Wakuu wao wa idara hawatekelezi majukumu yao sawasawa, hawasimamii miradi ya maendeleo, wanaandika taarifa za uongo kwamba miradi imekamilika lakini wakaguzi wanapokwenda kutembelea miradi hiyo haionekani na kama ipo basi inakuwa haikukamilika.

Mheshimiwa Spika, naomba sana ofisi ya Waziri Mkuu ifuatilie miradi yote ya *TASAF* iliyofanyika Mkoa wa Tanga hasa Wilaya za Muheza na Mkinga, kama haikutekelezwa wahusika wote wachukuliwe hatua haraka sana.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya 2009/10, Serikaliilitenga Shilingi milioni 500,000,000 kwenye *scheme* ya umwagiliaji Mwangeza na pia milioni 600,000,000 kwenye sehemu ya umwagiliaji kwenye Kijiji cha Msingi. Vijiji vyote hivi viko Iramba Mashariki, cha kusikitisha hadi laeo fedha hizo hazijatolewa na wala wananchi wa maeneo hayo kwa kupitia kwa Mbunge wao hawajaambiwa kasoro gani ilitokea juu ya miradi hii. Naomba kupitia ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nipate majibu niwapelekee wapiga kura wangu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa ari yake kubwa akiongozwa na Mheshimiwa Dr. Jakaya Rais wa Tanzania kuanzisha kilimo kwanza. Nawomba sana ahakikishe Serikali hairudi nyuma kwenye jambo hili. Serikali itafute nyenzo zote zinazotakiwa kuendeleza kilimo (matrekta na vifaa vyake, *power tillers*, majembe yanayokokotwa na wanyama kazi na kadhalika), mbolea, mbegu za kisasa na kadhalika, pia kubwa zaidi Watendaji wa Halmashauri wabanwe ili wawe karibu na wakulima katika maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wa 17 sisi wananchi wa Iramba Mashariki tunaomba tupewe Wilaya. Sababu kubwa tunayofanya tuombe Wilaya ni jiografia ya eneo letu na pia toka mwaka 1983 ilipendekezwa Iramba Mashariki, Mbulu wakati huo zimegwe itengenezwe Wilaya kwa ajili ya kukomesha wizi wa mifugo. Hata hivyo Rais wa wakati huo aliamua kwamba wakati huo ianzishwe Wilaya ya Hanang na hatimaye sisi tungefuata. Bado tunaomba endapo kutakuwa na mgawanyo wa wilaya na sisi tukumbukwe.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima wa afya na kuniwezesha kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru wapiga kura na wananchi wa Jimbo la Fuoni kwa ushirikiano wanaonipa nikiwepo Jimboni na pale ninapokuwa sipo na nawaambia wasishtuke na wanaopitapita kwani hakuna masika yasiyokuwa na mbu na dawa yao kujifunika kwenye chandarua kilichotiwa dawa, hao ni malaria na malaria haikubaliki.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waziri Kombani kwa kuwasilisha hotuba nzuri yenye kuonesha utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Mapinduzi kimefanya kazi kubwa na ya kupigiwa mfano na haifai kuibeza na wale watakaoibeza ndio wale wenye macho lakini hawaoni na wana masikio lakini hawasikii.

Mheshimiwa Spika, kweli kuna matatizo madogo madogo ambayo husababishwa na watu wasioitakia mema nchi hii ambao tunahisi ni wenzetu kumbe ni mchwa wanatula kidogo kidogo. Watu hawa ni hatari na wakati umefika sasa Serikali kuwashughulikia.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii Ukurasa wa 33 na 34 Serikali imeonyesha dhamira nzuri ya kuimarisha bandari zetu, kwa kutambua kuwa bandari ni chombo kinachoingizia mapato mengi Serikali. Kwa hivyo, naiomba Serikali uimarishaji huo usiwe wa ujenzi na vifaa bali hata wafanyakazi (watendaji) wazuri, kwa sababu kuna watendaji wameweka mbele ubinafsi na kuwasumbua watumiaji wa bandari kwa lengo la kupata kitu kidogo pia kuvujisha mapato kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, watu hawa pia hushirikiana na wafanyabiashara haramu wanaoingiza madawa ya kulevya na wale wakwepa kodi na baadaye hukutana mitaani.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya elimu Serikali ya Awamu ya Nne inayoongozwa na Mheshimiwa Kikwete imejitahidi kujenga madarasa nchi nzima na kupunguza ukosefu wa wanafunzi kukosa nafasi. Kwa hivyo, naiomba Serikali ichukue hatua hizo hizo kwa kujenga nyumba za walimu ambapo tutakapofanikiwa hili na ile shida ya walimu itakwisha, kwa sababu sio kama nchi yetu haina walimu na sio kweli kama wasomi wetu hawataki kazi za ualimu lakini kinachogomba ni mazingira ya shule zetu, hakuna nyumba za walimu na ndio wanakimbia na kusababisha ukosefu mkubwa wa walimu hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, sekta ya uvuvi inachangia ajira kubwa kwa wananchi wadogo wadogo na wakubwa lakini mara nyingi kunatokea migogoro na mivutano na Serikali. Suala hili hutokea pale wananchi wanapotumia umri haramu na Serikali kwa kulinda mazao ya bahari.

Mheshimiwa Spika, suala hili ni kero sasa, kwa hivyo, naomba Serikali pamoja na elimu kuweka maduka makusudi ya kuuzia vifaa vya uvuvi hasa nyavu pamoja na ulinzi katika bandari zetu kwa kuzizuia dhana hizo zisiingie nchini katika utaratibu wa sasa wa kuwanyang'anya wavuvi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba nilipata nafasi ya kulisemea kwa kuzungumza, sikupata muda wa kutosha kuhitimisha hoja yangu kwa muda wa dakika 10. Napenda kuihitimisha kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuhusu mafuriko Mjini Babati ni wazi kuwa kitengo cha maafa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu haijachukua hatua za kutosha kuzuia mafuriko kufuatia Sheria ya Kudhibiti Maafa ya 1990 na Mwongozo wake 2003.

Mheshimiwa Spika, inaonesha kuwa hakuna mahusiano baina ya matokeo ya ukaguzi na utekelezaji, kielelezo Na. 6.3 cha ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu hadi Machi 2010, Ukurasa wa 95.

Mheshimiwa Spika, ushauri ni kwamba, naomba kufahamu sasa ni hatua gani zinachukuliwa hasa katika ujengaji wa tuta la Kigongoni ambalo linachimbika kurudi nyuma na ni hatua chache tu kama 50 korongo litafikia daraja na itakapotokea hivyo ziwa litakuwa juu na hivyo itakuwa balaa na litahama lote na litasababisha maafa makubwa sana. Ushauri zaidi ni muhimu wakati wa kujenga barabara ya Babati – Dodoma kwa kiwango cha lami, kazi ambayo imeanza ifikiriwe kwa kina kujenga tuta kubwa na sakafu

yake iwe ya mawe na simenti hadi karibu kilomita moja kuelekea Mtoni na maeneo ya Tindiga. Hii itazuia mmomonyoko wa uchimbikaji kurudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafuriko maeneo ya Bonga, kumekuwa na athari kubwa ya korongo kutoka Kata ya Gidao na Ayasanda na Kijiji cha Endanachan ambalo limeharibu sana mashamba mengi na makazi na zaidi kujaza tope Ziwa la Babati. Maeneo haya hayawezi kudhibitiwa kwa bajeti ya Halmashauri ya Babati na Mji. Ni muhimu sana kitengo cha maafa kiende kufanya tathmini ya mafuriko yanatokea kila mara na hatimaye itafutwe njia ya kudhibiti mafuriko kwa kuainisha ni nini kila ngazi ifanye na nini Taifa lifanye. Korongo hili eneo la Bonga ndilo litakalohamisha ziwa na kuongeza mafuriko kutokana na tope linalojazwa ziwani. Naomba maelezo ya namna ya kutekeleza ili kuzuia korongo hili kuendelea kuleta maafa.

Mheshmiwa Spika, kuhusiana na uwezo wa kitengo cha maafa. Kufuatia ukaguzi wa mafuriko Babati ni wazi kitengo hiki hakijapewa uwezo wa kutosha kukabiliana na mafuriko na ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuwa na *Register* ya mafuriko ni muhimu sana. Taifa lazima libadili utaratibu huu wa kushughulikia mafuriko katika hali ya dharura. Tutatumia rasilimali nyingi kujenga upya badala ya kuzuia.

Mheshimiwa Spika, namtakia Waziri Mkuu na watendaji wote wa ofisi yake kila la kheri katika kazi hii nzito ya kuokoa maisha na mali za raia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kabisa, nina heshima kukupongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yako nzuri iliojaa hekima, busara na mwongozo mzuri hasa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imejaza maendeleo katika maeneo yote katika nchi yetu, Mheshimiwa Waziri Mkuu nakupongeza na natanguliza kauli yangu kwa kusema naiunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia maeneo machache yafuatayo:-

Uchumi wetu, Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa ya kuimarisha uchumi wetu ambao kweli umepiga hatua kubwa lakini naomba tuangalie sana eneo la uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana tutafute meli zaidi za uvuvi wa bahari kuu ambapo kuna utajiri mkubwa sana wa rasilimali ya baharini, ambapo kwa sasa unaporwa ovyo na nchi mbalimbali za kigeni.

Mheshimiwa Spika, uimarishaji wa bandari zetu, bandari zinachangia sana pato la nchi yetu. Naomba tuziimarishe bandari zetu na tujenge bandari nyingine kubwa kama kule Tanga, Zanzibar, Mtwara na kule kwenye maziwa yetu makuu kama Victoria, Lake

Tanganyika na kadhalika. Bandari ni moja wapo ya eneo kubwa la kuingiza fedha nyingi za kigeni na hata za ndani.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kilimo kwanza. Katika kutekeleza agizo la kilimo kwanza, basi ni vyema suala la elimu juu ya kilimo iwe pia ni ya mwanzo, shule zetu za sekondari na vyuo vikuu lazima zitumike ipasavyo, aidha, wataalam wetu watumike ipasavyo mashambani, teknolojia ya kilimo itumike, zana za kisasa zipatikane, mbegu safi na mbolea ya uhakika itumike ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, lazima utafiti mzuri ufanyike kwa kuangalia hali ya ardhi, hali ya hewa ya maeneo ya kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama wa barabarani, pamoja na juhudi kubwa inayochukuliwa ya usalama wa barabarani, lakini bado ajali zipo na zinapoteza wananchi wengi kwa vifo na ulemavu mkubwa. Naomba kushauri utaratibu wa utolewaji wa leseni za udereva ubadilishwe.

(1) Dereva lazima apimwe afya yake kikamilifu;

(2) Umri wa dereva huyo lazima uwe umefikia kisheria;

(3) Kuundwe Kamati au Bodi ndogo ya utoaji wa leseni;

(4) Matrafiki yaani (Polisi) waongezewe zana za usalama wa kuzichunguza gari ziendazo mwendo wa kasi na kumkagua dereva kama hakunywa pombe na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, katika kuchangia kwa kuzungumza katika hotuba ya bajeti ya Serikali nilieleza suala zima namna gani Serikali isivyo makini katika kadhia nzima ya msamaha wa kodi. Nilithibitisha kwa vipindi tofauti kauli ya Serikali juu ya ahadi ya kuondoa mianya ya misamaha ya kodi. Kauli hizo zimethibitika katika hotuba za bajeti kuanzia mwaka 2006 mpaka hata hii ya 2010/11.

Mheshimiwa Spika, ahadi za Serikali zinatoka mwaka 2006, msamaha wa kodi uliofanyika ulikuwa ni Shs.15,970,913,769. Lakini jambo la kushangaza licha ya ahadi hizo za Serikali kwa miaka tofauti ya kuondoa mianya ili kupunguza misamaha ya kodi. Mpaka 30 Juni, 2009 kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali fedha iliyosamehewa kama kodi ni Shs.752,398,800,000.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri, si kweli kuwa Serikali imejipanga au imekusudia kuondoa mianya ya msamaha wa kodi. Nilitaka maelezo kutoka kwa Wizara ya Fedha

lakini sikuyapata, sasa nauliza tena, kutoka Shs.15,970,913,769 kwa mwaka 2006 ndio kodi iliyosamehewa na mwaka 2009 ikafikia Shs.752,398,800,00, je, Serikali haioni kuwa kauli zake za kupunguza mianya ya kodi katika kusamehe hazikuwa za ukweli?

Mheshimiwa Spika, maelezo mengi yametolewa kuhusiana na suala la kuanzishwa Mahakama ya Kadhi hapa nchini ambapo kuwepo kwake pia kumetolewa na Ilani ya CCM ya mwaka 2005. Je, mpaka sasa kwa kufuatia utaratibu wowote ule suala hili limefikiwa wapi kwani katika bajeti ya Waziri Mkuu hakuna maelezo yoyote.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu ni wa uchaguzi lakini bado kuna tatizo kubwa la kisheria juu ya wapiga kura wanaomchagua Mbunge Zanzibar. Mbunge katika uchaguzi wake anatawaliwa na Sheria za Uchaguzi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi na sio Tume ya Uchaguzi Zanzibar (*ZEC*).

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya suala la uandikishaji la wapiga kura Zanzibar linatawaliwa na sheria ya uchaguzi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar ambapo huandikishwi mpaka uwe na kitambulisho cha Uzanzibar ukaazi. Je, haionekani kuwa ni tatizo kubwa hilo Wabunge wa Zanzibar wanaowachagua wanatawaliwa na sheria mbili ? Ahsante.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, mara zote fedha za matumizi ya kawaida huwa ni nyingi ukilinganisha na fedha za matumizi ya maendeleo. Pamoja na fedha za maendeleo kuwa ni kidogo lakini nyingi ya pesa hizo huwa zinatoka nje, (yaani toka kwa wafadhili) jambo ambalo linapunguza kasi ya maendeleo yetu. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiye kiongozi wa shughuli za Serikali basi Mheshimiwa alione hili na awe wa mwanzo kuhakikisha kwamba yale matumizi yasiyo ya lazima kama vile ununuzi wa samani wa kila mwaka, ununuzi wa sare na kadhalika unaondolewa ili fedha nyingi za ndani zitumike katika miradi ya maendeleo. Hii ni kwa sababu fedha za maendeleo zinachelewa kufika kwa wakati na hivyo kuchelewesha malengo yaliyokusudiwa na kupelekea fedha hizo kufanyiwa ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba Serikali imejitahidi kujenga shule nyingi kupitia mpango wa MEM, lakini lazima tukubali kwamba wingi wa shule sio ubora wa elimu, naomba sana tukijenga shule twende sambamba na kuboresha mazingira yote ya elimu kama vile kuhakikisha upatikanaji wa walimu wa kutosha ili tuondokane na adha ya mwalimu mmoja kufundisha shule nzima, jambo ambalo ni gumu na linapelekea kushusha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa nyumba za walimu ni muhimu ili mwalimu aweze kuwa na mazingira ya kuipenda kazi yake. Sambamba na hilo ujenzi wa maabara ni muhimu sana ili kunyanyua kipaji cha wanafunzi katika masomo ya sayansi, kwani somo hili linaonekana kuchukuliwa na wanafunzi walio wengi pamoja na umuhimu mkubwa wa somo hili hasa katika ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia, hivyo Serikali itilie maanani sana ujenzi wa maabara mashuleni.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha

kwa ufasaha mkubwa. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake wa kupigiwa mfano na uelewa wake wa masuala ya Kitaifa usiokuwa na shaka. Namtakia mafanikio mema katika uongozi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza Mawaziri wa Nchi wote wawili katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Naibu Waziri na watendaji wote katika ofisi hiyo, Mikoa na Wilaya kwa utendaji wao na ushirikiano wanaotupa. Nawatakia mafanikio mema katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, katika kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, maeneo mapya ya utawala. Kwa niaba ya viongozi wa wananchi wa Wilaya ya Ileje napenda kutoa shukrani nyingi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kukubali ombi letu la kuanzisha kwa Kata mpya mbili za Kalembo na Mlale, shukurani maalum zimwendee Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Naibu Waziri ambaye niliwasiliana naye na akashughulikia ombi letu kwa ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maombi ya Kata mpya, tulikuwa tumewasilisha maombi ya Vijiji vipya. Nilipokuwa naondoka Jimboni kwangu, tulikuwa hatujapata majibu ya ombi hili, naomba kufahamishwa kama ombi letu limekubaliwa.

Mheshimiwa Spika, pili, maeneo yenye mazingira magumu. Wilaya ya Ileje ni miongoni mwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizoainishwa na kuonekana ziko katika mazingira magumu zaidi. Kama ilivyokuwa kwa mwaka 2009/2010, tunaomba Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ipokee na kutoa msaada wa kibajeti kwa maombi maalum ambayo yamekwisha wasilishwa kwa taratibu za kawaida. Halmashauri ya Ileje bado haijawa na uwezo mkubwa wa mapato ya ndani na inahitaji watendaji wabunifu wa kuimarisha vyanzo vya mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, tatu, watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa kuwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara za kisekta ndiyo zenye wajibu wa kuhakikisha kwamba Halmashauri zinakuwa na watumishi wenye sifa zinazotakiwa na historia nzuri ya utendaji, tunaomba msaada maalum wa kuangalia na kuchambua timu ya watendaji iliyopo Halmashauri ya Ileje ili tuwe na watumishi watakaotekeleza majukumu yao kwa ufanisi na uadilifu.

Mheshimiwa Spika, nne, ujenzi wa Ofisi za Wabunge. Jimbo la Ileje, ni kati ya Majimbo ambayo hayana Ofisi za Wabunge wala hakuna fungu la fedha la uendeshaji ofisi, inalopewa, kama fungu hilo lipo kupitia ofisi ya *RAS* au *DAS*, ingefaa Mbunge afahamishwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo mfupi, naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi kuipongeza hotuba ya Waziri Mkuu na maelezo ya kiutendaji yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambayo kwa sehemu kubwa yamezingatia kuondoa kero mbalimbali za wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wetu wa Mtwara ulikuwa na kero ya muda mrefu juu ya mgawanyo wa Vijiji, Kata, Tarafa na Miji. Katika maelezo ya kiutendaji imeonyesha ni jinsi gani Serikali imelifanyia kazi jambo hili kwa kutangaza mamlaka za Miji midogo ya Handeni, Nzega na Masasi. Kwa niaba ya wananchi wa Masasi, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri mkuu, Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa kusimamia upatikanaji wa miji hii kwani tunaamini hii ni hatua ya maendeleo kwa nchi yetu na maeneo husika, sambamba na hili napongeza pia kwa mgawanyo uliofanyika wa Kata na vijiji kwa Wilaya ya Masasi kwa kweli mmetuondolea kero kubwa sana ambayo huenda ingesababisha kukwamisha uchaguzi mkuu ujao.

Mheshimiwa Spika, kero kubwa iliyopo hivi sasa kwa Wilaya ya Masasi ni majengo ambayo yalikuwa Chuo cha Wasioona yaliyopo Kata ya Mwenge Mtapika, kwa miaka mingi majengo haya yamekaa bila matumizi ya aina yoyote kwa kukosa wanafunzi ambao hivi sasa katika chuo hicho. Halmashauri ya Wilaya ya Masasi iliomba majengo haya kwa Wizara husika ili kubadili matumizi na yaweze kutumika kwa Sekondari ambayo ipo katika eneo hilo na Halmashauri ilikuwa tayari kukarabati majengo hayo hata Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa alipotembelea Masasi alipelekwa kuona majengo hayo ambayo hivi sasa ni magofu na aliombwa kufuatilia na kuishauri Serikali ili kufanyia mabadiliko ya matumizi.

Mheshimiwa Spika, pia Halmashauri iliomba kwa maandishi jambo ambalo Wizara husika haikuridhia kukabidhi majengo hayo bali walisema wametenga milioni thelathini na nne kwa ajili ya ukarabati, jambo ambalo hadi hivi sasa ukarabati huo haujafanyika na majengo yanaendelea kuharibika, ni kwa nini Serikali inaacha majengo haya yakiharibika bila matumizi yoyote, ni kwa nini Serikali isikubali ombi la Halmashauri ya Masasi ikaridhia kukabidhi majengo haya ili yaweze kutumika kwa faida ya wananchi na Taifa letu kwa ujumla? Je, hatuoni haya ni matumizi mabaya ya rasilimali tulizonazo?

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aone umuhimu wa ombi hili na aweze kulifanyia kazi ili rasilimali hii iweze kutumika badala ya kuacha uharibifu ukiendelea. Naomba sana nipate majibu na ufafanuzi wa suala hili.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo naiomba Serikali ni umuhimu wa kuongeza maslahi ya madiwani ambayo kwa hivi sasa Serikali imejitahidi sana kuboresha na kufikia sh.120,000 kwa mwezi lakini bado haikidhi haja kwani Madiwani ni kiungo kikubwa kwa Serikali na ndiyo wasimamizi wakubwa wa maendeleo katika ngazi za Vijiji, Kata na Wilaya, Kata zao ni kubwa, usafiri hawana, wananchi wanawategemea hata kwa shida zao binafsi. Hivyo, ningeomba Serikali kwa kipindi cha 2010/2011,

posho za Madiwani zingeongezeka kufikia shilingi laki mbili ili Madiwani hawa waweze kufanya kazi na kusimamia maendeleo kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wangu wa jana kuhusu Serikali kushindwa kutekeleza ahadi kuu ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa mwaka 2005 ya kupambana na kuondoa umasikini katika kipindi cha miaka mitano (2005/2010) na kujenga uchumi wa kisasa usio na utegemezi, naomba pia ofisi ya Waziri Mkuu itupe maelezo ni kwa nini imeshindwa kufikia malengo ya ilani hiyo yaliyomo kwenye Ukurasa wa 23, ambapo CCM iliahidi kukuza kwa asilimia 20. Takwimu za Waziri wa Fedha na Uchumi alizotoa hapa Bungeni zinaonyesha kuwa uchumi umekua kwa asilimia 6.9 tu na kilimo kimekua kwa asilimia 3.2 tu. Je, huku si kushindwa?

Mheshimiwa Spika, pili, tunaposhindwa kuwa na uchumi unaojitegemea na kuendelea kuwa tegemezi kama inavyoonekana katika bajeti zetu ikiwemo ya mwaka huu ambapo kati ya shs.11.1 trilioni, Serikali itaweza kukusanya shilingi trilioni sita peke yake, ni jitahidi gani zinachukuliwa kuondokana na hali hii? Tayari washirika wa maendeleo kama Marekani, Uingereza, Umoja wa Ulaya (*EU*) na *Switzerland* kupitia Mabalozi wao hapa nchini, wote katika kipindi cha karibuni wametoa kauli za hadharani zinazoonyesha kutushangaa, ni vipi Tanzania yenye utajiri mkubwa wa rasilimali inaendelea kutegemea ufadhili na misaada?

Katika hali kama hiyo kuna dalili za wazi za kuanza kuchoka kutusaidia na hata kusitisha au kupunguza misaada yao ya bajeti kama walivyofanya hivi karibuni ambapo walipunguza au kukata kiasi cha dola za Kimarekani 220 milioni. Serikali imejiandaaje pindi hatua takriban bajeti yote ya shughuli za maendeleo inawategemea wao?

Mheshimiwa Spika, tatu, Ilani hiyo ya CCM pia katika kifungu hicho kinachozungumzia ujenzi wa uchumi wa kisasa imeelekeza mambo matatu kuwa ndiyo msingi wake ambayo ni:-

(1) Kuleta Mapinduzi ya kilimo;

(2) Kuimarisha Elimu; na

(3) Kujenga na kuimarisha Viwanda na Miundombinu ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, hali halisi ya miaka mitano imejidhihirisha katika mipango ya Serikali kupitia bajeti yake ambapo tumeelezwa kuwa mwaka uliopita wa fedha kilimo kimekuwa kwa asilimia 3.2 tu, badala ya asilimia 20 iliyoahidiwa katika ilani. Elimu tunazungumzia ujenzi wa shule za sekondari za Kata lakini hatuelezwi kuwa uko ukosefu

mkubwa sana wa walimu kiasi cha shule nyingi kuwa na mwalimu mmoja tu. Ahadi ya Serikali ya kujenga nyumba za walimu 22,000 hadi sasa imetekelezwa kwa asilimia moja tu. Haya yamefanyiwa utafiti na kuthibitishwa na HAKIELIMU.

Mheshimiwa Spika, mwisho, tukija kwenye sekta ya viwanda na miundombinu ya kisasa hapa hapa Bungeni tumeshuhudia Serikali ikikataa mapendekezo yote ambayo yangelinda viwanda vyetu vya ndani. Mfano ni kukataa kuongeza kodi kwa usafirishaji wa mali ghafi au bidhaa zisizoendeshwa *(unprocessed product)* ili kutoa motisha kwa kujengwa viwanda vya ku-*process* mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, pia kuongeza kodi kwa bidhaa kama saruji inayoagizwa kutoka nje ili kulinda viwanda vya ndani posa Serikali imekataa. Hakuonekani katika miaka mitano iliyopita ujenzi wowote wa Viwanda vya maana hapa nchini. Tutafikiaje ujenzi wa uchumi wa kisiasa na hali ya hivyo hivyo kwa miundombinu. Njia zote kuu za usafiri znaporomoka *ATC* kwa mara ya kwanza imekuwa *grounded* kabisa. Reli imekwama mpaka unashangaa kwamba ilifanya kazi vyema mwaka 1914 lakini 2010 haifanyi kazi badala ya kwenda mbele tunaserereka na hata Bandari inayotegemewa ya Dar es Salaam utoaji wa huduma unaporomoka kiasi cha kulalamikiwa kila siku.

Mheshimiwa Spika, nne, ujenzi wa uchumi wa kisasa pia hauwezi kufikiwa bila ya nchi kuwa na umeme wa uhakika, leo Tanzania ina watu milioni 43 lakini uwezo wake wa kuzalisha umeme ni *megawatt* 600 tu; Afrika Kusini inazalisha megawatt 300,000; Norway yenye watu milioni nne inazalisha megawati 25,000; Singapore yenye watu milioni tano, inazalisha *megawatt* 25,000. Serikali iliahidi katika ilani ya CCM, kuongeza kiwango cha uzalishaji umeme na kuanzisha vyanzo mbadala.

Hilo halijatekelezwa kabisa na zaidi tunaingiza siasa hata katika uendeshaji wa Shirika la *TANESCO*. Tumefika mahali pa kuilaizimisha *TANESCO* kulipa *IPTL* shilingi bilioni 20 kila mwezi kwa kupata megawati 100 na hivyo kutumia shilingi bilioni 240 kwa mwaka ambazo zingeweza kununua mitambo mipya kama ile ya *Dowans* mara tatu, nini mipango ya Serikali kumaliza tatizo hili la ukosefu wa umeme wa uhakika?

Tano, hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu na hata ya kufungua kikao kilichopita cha bajeti ilizungumzia kuporomoka kwa nafasi ya Tanzania katika *ranking* ya kuwa na mazingira mazuri ya ushindani wa kibiashara kwa kushika nafasi ya 131 kati ya nchi 183 mwaka 2010. Tumeachwa nyuma na Rwanda ikiwa na nafasi ya 67, Kenya (75) Zambia (90) na Uganda (112). Ni zipi sababu zilizotufikisha hapa kwa tathmini ya Serikali? Je, huku kuingiza siasa katika mambo muhimu ya uchumi na uwekezaji hakuwakatishi tamaa wawekezaji na kuangusha *ranking* ya Tanzania Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, wakati akijibu hoja za Wabunge waliochangia Muswada wa Sheria ya kufanya marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi tarehe 12 Februari, mwaka huu na akijibu mchango nilioutoa mimi siku ya kwanza nilipoingia Bungeni, Waziri wa Nchi

Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) Mheshimiwa Phillip Marmo alikubaliana na hoja yangu kuwa muundo wa Tume ya Uchaguzi ya Taifa unahitaji marekebisho kulingana na mahitaji ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi ambao sasa umetimiza miaka 18 hapa nchini tokea mwaka 1992 ulipoanzishwa.

Mheshimiwa Spika, akilizungumzia suala hilo, alisema na naomba nimnukuu kutoka kwenye *Hansard;* ”Muundo wa Tume; hili limeelezwa vizuri sana na Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu. Niseme tu kwamba hoja hii imejitokeza mara nyingi ni hoja nzito na siyo hoja ya kupuuzwa hata kidogo isipokuwa hoja hii inagusa Katiba na sisi sote tunafahamu mchakato wa namna ya kubadilisha Katiba, kwa hiyo, pendekezo na ombi langu kwa Wabunge wote na wadau wote ni kwamba kwa vile muda uliobaki kati ya leo na Uchaguzi Mkuu siyo mrefu ni muda mdogo sana uliobaki na haitawezekana mchakato huu kukamilika basi jambo hili lishughulikiwe baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 kwa utaratibu wa kawaida wa mchakato wa kubadilisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.”

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kukubaliana na hoja yangu wakati ule na pia nakubaliana naye kwamba muda uliobaki kati ya sasa na Uchaguzi Mkuu ni mdogo sasa basi naomba ahadi yake aliyoitoa kwa niaba ya Serikali ifanyiwe kazi ili mara baadaya Uchaguzi Mkuu tuanze *process* hiyo, isije ikawa tena tunasubiri hadi mwaka 2014 na 2015 hoja hii ije ijibiwe tena hivi hivi kwamba muda uliobaki ni mfupi.

Mheshimiwa Spika, Watanzania kupitia taasisi mbalimbali zikiwepo vyama vya siasa jumuiya na taasisi za kiraia, jumuiya na taasisi za kidini na jumuiya zisizo za KiSerikali na Mashirika ya kutetea demokrasia na haki za binadamu, wamekuwa wakitoa na kusisitiza madai na haja ya kuwa na Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakayokidhi matakwa ya demokrasia ya vyama vingi na pia inayokwenda na wakati na utashi na matarajio yaani *hopes and aspirations* ya Watanzania wa leo.

Mheshimiwa Spika, *modernisation* ni muhimu sana hasa ikizingatiwa kuwa Tanzania ni Taifa la vijana. Takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 70 ya Watanzania ni vijana wa umri wa miaka 30 nanchini ya hapo, hawa wanahitaji Katiba mpya inayokwenda sambamba na mahitaji yao ya leo na ya wakati unaokuja.

Mheshimiwa Spika, nimuombe basi Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja kufanya majumuisho ya mjadala hapa atueleze ni vipi Serikali imejipanga baada ya uchaguzi kuhakikisha inakuja na mpango madhubuti utakaoanzisha mchakato wa kuandika Katiba mpya kama ilivyoahidi kupitia kauli ya Waziri wa Nchi ya tarehe 12 Februari, nasema hivi nikitambua kuwa Serikali ni endelevu kwa hivyo wowote watakaokuwa madarkani watapaswa kutekeleza ahadi hii ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge ya mwaka 2010/2011. Pamoja na kuiunga mkono hoja ya Waziri Mkuu,

napenda nigusie masuala machache tu yanayohitaji ufafanuzi na pale inapowezekana hatua mahsusi.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu tumekuwa tukijiuliza na hata kuiuliza Ofisi ya Waziri Mkuu bila mafanikio kuhusu hatma ya nafasi ya Diwani pale ambapo Kata yake inamezwa na Mamlaka ya Mji mdogo na kusababisha mabadiliko makubwa yafuatayo:-

(a) Chombo cha maamuzi cha Kata (*WDC*) ambacho Diwani alikuwa akikiongoza kama Mwenyekiti kinaondoka na badala yake kinakuwepo chombo kipya, Baraza la Mamlaka ya Mji mdogo ambacho kinaongozwa na mtu mwingine kabisa (mbali na Diwani) yaani Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo.

(b) Wajumbe wa chombo hicho kipya cha maamuzi si Wenyeviti wa Vijiji tena bali Wenyeviti wa Vitongoji ambao mmoja wao anachaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji mdogo.

(c) Afisa Mtendaji wa Kata aliyekuwa Msaidizi Mkuu wa Diwani katika utekelezaji wa maamuzi mbalimbali ya *WDC* hayupo tena. Badala yake yuko Mtendaji wa Mamlaka ya Mji mdogo (*TEO*) ambaye hawajibiki kwa Diwani bali kwa Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji mdogo na Baraza lake.

(d) Sheria Na. 7 ya Halmashauri za Wilaya haielekezi kuwa Diwani aliyekuwepo eneo hilo la mamlaka ya Mji mdogo awe sehemu ya mamlaka hiyo, bali inatoa fursa kwa Madiwani watatu wa Halmashauri ya Wilaya husika kuingia kwenye Baraza la Mamlaka ya Mji mdogo kama wajumbe na hivyo kuwa daraja muhimu kati ya Halmashauri na Mamlaka ya Mji mdogo na sheria haielekezi kuwa Diwani wa eneo hilo awe mmoja wa Madiwani hao watatu! Maana yake nini? Hakuna maana nyingine mbali na kwamba sheria haitarajii Diwani huyo kuendelea na wadhifa huo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo niliyoielezea, Diwani ambaye Kata yake imemezwa na Mamlaka ya Mji Mdogo anabaki kuelea hana mamlaka wala chombo cha kuzipokea, kuzichambua na kuzitolea maamuzi kero za wananchi wake na changamoto za eneo lake. Tofauti na Madiwani wenzake wenye Kata ambazo hazijakumbwa na mabadiliko hayo. Swali bayana linalojitokeza hapa ni huyu Diwani asiye na *WDC,* asiye na Afisa Mtendaji wake, asiye na mamlaka katika eneo lake la uongozi, ana mchango upi, “kiuongozi” na “kimaendeleo” kama si mzigo tu usio na tija?

Mheshimiwa Spika, hakuna anayeweza kubisha kuwa pale ambapo Mamlaka ya Mji Mdogo inaanzishwa kabla ya uongozi wa Mheshimwa Diwani kwisha muda wake kisheria basi Diwani huyo (pamoja na kuelea kwake) aendelee mpaka kipindi chake cha miaka mitano kiishe. Lakini baada ya kipindi chake kwisha hakuna sababu ya msingi kwa Udiwani kuendelea kugombewa kwenye Mamlaka ya Mji Mdogo, kuachia hali hiyo kuendelea ni kukaribisha migongano isiyo ya lazima kati ya Mwenyekiti wa Mamlaka na huyo, Diwani asiye na Kazi Maalum.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alitolee ufafanuzi au tamko suala hili maana tayari kwenye mamlaka zetu za Mji Midogo (Kyela, Makongorosi, Viwawa, Tunduma na kadhalika) harakati za kuwania Udiwani hewa huo zimeanza ni kheri zisitishwe mapema kabla ya kutuzalishia mitafaruku isiyo ya lazima. Ikumbukwe kwamba Kata ni eneo la utawala, unapoanzisha mamlaka lengo ni kuondokana na Kata huwezi kuwa na Kata na Mamlaka *at the same time*.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ninalotaka lizingatiwe ni kushindwa kwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kufanya maamuzi katika muda uliowekwa na sheria hivyo husababisha shauku ya muda mrefu inayoishia kuchochea migongano isiyo na sababu za msingi kwenye Halmashauri zetu. Nitatoa mfano wa suala lililotokea kyela tarehe 23 Novemba, 2009 la kumvua Mwenyekti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela wadhifa wake bila kufuata taratibu na misingi ya sheria. Kilichosababisha yote haya ni maslahi finyu ya kisiasa na ushawishi wa fedha.

Mheshimiwa Spika, siku nne baada ya uamuzi huo, yaani tarehe 27 Novemba, 2009, Mwenyekiti aliyeondolewa madarakani akakata rufani kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mujibu wa sheria akielezea (kwa muhtasari tu) kuwa:-

(a) Madiwani waliokuwa na hoja ya kumuengua walimtaka Mkurugenzi aitishe mkutano wa dharura ndani ya siku nne badala ya siku saba zilizowekwa na sheria, hivyo kumnyima muda wa kutosha siyo tu kuelewa msingi wa hoja dhidi yake bali vilevile kujiandaa vizuri kujibu tuhuma dhidi yake. Aidha, uharaka huo ulipelekea mjumbe ambaye lazima awepo kisheria yaani Mkuu wa Mkoa au mwakilishi wake ashindwe kuhudhuria, Mbunge wa Jimbo naye hakuweza kupata taarifa ya mkutano kutokana na ufinyu wa muda uliowekwa na Madiwani.

(b) Hoja iliyotumika kumwondoa kwenye wadhifa wake iliibuliwa tu kwenye mkutano na ilikuwa tofauti na hoja ya awali aliyoandikiwa Mkurugenzi na yeye kupewa taarifa.

(c) Hoja mpya iliyoibuliwa wakati wa mkutano haikumpa fursa ya kutosha kuelewa maudhui yake na kuweza kuijibu kwa utetezi papo kwa papo.

Mheshimiwa Spika, sheria iko wazi kuhusu muda ambao Waziri anapaswa kujibu rufani hiyo lakini mpaka leo, hii miezi saba baada ya kukata rufani hiyo, mrufani hajui kinachoendelea, kilichomtibua sana Mwenyekiti huyo aliyeondolewa madarakani ni hatua za baadaye zilizochukuliwa na Halmashauri za kumwita Mkuu wa Mkoa baada ya rufani kukatwa na *RC* kutangaza kuwa amebariki kilichotokea suala hilo likatangazwa sana na vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti aliyeondolewa kwenye wadhifa wake ni hakimu mstaafu wa siku nyingi anayefuatilia kila tukio kwa umakini. Kwa kuwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iko kimya (taarifa za mwisho nilizopata zilisema suala liko mezani kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, inaaminika siyo tu na mrufani bali vile vile watu

wengi wa Kyela (wakiwemo wapiga kura wake kwenye Kata) kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu imeafiki *RC* kubariki mchakato uliokuwa na makosa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu mwenyewe nikiwa Mwanasheria naona hii si sahihi hata kidogo. Tuna *set precedent* mbaya ya Wakuu wa Mkoa kubariki makosa nje kabisa ya taratibu za kisheria sasa rufani kwa mheshimiwa Waziri inabeba maana ipi kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, natambua sana kuwa Wakuu wa Mikoa ni watu wakubwa sana ambao siku hizi imefikia mahali wanaitwa "Maraisi wa Mkoa" ingawa kwa tafsiri yoyote ile ya Kikatiba na Sheria si sahihi hata kidogo. Tujikumbushe ibara ya 8(1)(a) na (c) ya Katiba kwamba wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na kwamba Serikali itawajibika kwa wananchi. Kimya cha Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwenye suala hili kimechangia sana kuivuruga kuliko kuijenga Halmashauri ya Wilaya ya Kyela. Mzigo wote huu nimetupiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, nimalizie mchango wangu kwa kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu matokeo ya uchunguzi uliokuwa unaendeshwa na vyombo vyetu vya usalama kwa kushirikiana na vyombo husika vya nje juu ya viongozi waandamizi wa Serikali waliojiuzulu kutokana na suala la *Richmond*. Serikali iliahidi kuwasilisha matokeo ya uchunguzi huo pindi ukikamilika kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Ni muhimu matokeo ya uchunguzi huo yakajulikana ili kujiridhisha kama uamuzi wa viongozi hao kujiuzulu ulikuwa sahihi au la.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba Serikali pamoja na kukiri kwamba kulifanyika makosa katika mchakato wa zabuni hiyo, iliweza kulishawishi Bunge baada ya kuridhishwa na *findings* za mamlaka zao za nidhamu kwamba, watendaji wote waliohusika na zoezi la zabuni ya *Richmond* hawakuwa na makosa. Hivyo, matokeo ya uchunguzi huo wa nje ni muhimu kujulikana, maana haiwezekani kuwa na makosa bila wakosaji! Uchunguzi huo utaisaidia kujua makosa hayo yalikuwa ya bahati mbaya tu au ya kudhamiria ili kujiridhisha na uamuzi wa kujiuzulu uliochukuliwa na viongozi hao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. MAUA ABDEID DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nakupongeza Waziri Mkuu kwa ufuatiliaji wa karibu wa shughuli za Serikali. Napenda kutoa maoni yafuatayo:-

Kwanza, ni kuhusu Kilimo Kwanza:-

- Kilimo huboreka pale maji yanapopatikana. Yapo maeneo hadi hii leo wanakunywa maji ya tope kama vile Kiluvya, Mkuranga. Hali ya ardhi ni kavu kama jangwa, maji wanayotumia wanakijiji ni mabwawa ambayo yanapatikana pale maji ya mvua inaponyesha.

- Serikali ya kijiji bado haijaamka kulisimamia suala hili ipasavyo. Aidha, kijiji hiki kiko mbali na Wilaya ya Kisarawe ambapo ndiko wanakowajibika, ni karibu na Kibaha vema basi kwa umuhimu wa huduma zake Wilaya ya Kibaha iwe karibu nao.

- Hawana barabara na madaraja na mvua ikiwa kubwa watoto wanabaki majumbani na mifugo pia, si hivyo tu wanasombwa na maji.

Mheshimiwa Spika, pili, huduma ya matibabu kwa mifugo ni tatizo kwa wafugaji wa Mkoa wa Pwani, Madaktari wanawatoza wenye mifugo fedha nyingi sana na *extension workers* hawaonekani kabisa, wengine wameajiriwa na watu binafsi, wananchi wa kawaida hawawaoni.

Mheshimiwa Spika, tatu, upatikanaji wa mbegu bora na elimu kwa wakulima ni ndoto. Hivyo ni vema maeneo hayo yatupiwe macho.

Mheshimiwa Spika, nne, mimi ni mkulima lakini sijawahi kuona trekta hata la mtu binafsi ili kukodisha, kwanza kutokana na barabara si rahisi kufika huko.

Mheshimiwa Spika, tano, naomba kwa makusudi kabisa wataalam husika kwa umoja wao wanapitia wananchi wa Kiluvya, Makurunge waone ni namna gani watawasaidia ili ardhi yao iweze kutumika kwa tija (upatikanaji wa maji, elimu ya kilimo bora uvunaji maji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sita, Viongozi wote wawezeshwe, washirikishwe kuwa mfano bora katika kilimo kwanza ili wao wawe ndio mfano kwa wale wanaowaongoza.

Mheshimiwa Spika, saba, huduma za uvuvi. Bado eneo hili linahitaji kupewa uzito na kusimamiwa. Mvuvi anakuwa masikini na dhoofu katika maisha yake tofauti na mfanyabiashara. Kazi yao ni *risking* na kama vile haina mwenyewe. Wengine wanapata majanga, uokoaji uko mbali, zana zao ni ghali na hakuna *subsidy* za kutosha. Endapo watapata msukumo misamaha fulani fulani kusimamiwa kwa karibu basi hali itabadilika. Tunashukuru miradi ya *MACEMP* ila wanufaika ni wachache mno.

Mheshimiwa Spika, nane, uwekezaji katika madini, nashauri wawekezaji wa nje ni lazima waingie ubia na Watanzania sio wawe wako peke yao tu. Usimamizi wa madini yetu sasa upewe uzito, ndege zinatua na kuondoka katika migodi bila kuonekana, hilo lifanyiwe kazi kwani hata ukipiga picha haitoki. Utafiti wa madini uwe na kiwango cha muda na tusitoe nafasi ya kunyonywa.

Mheshimiwa Spika, tisa, kuhusu wafanyakazi wageni, wakati umefika sasa kuona biashara zinazoweza kufanywa na Watanzania basi zifanywe na Watanzania, maeneo mengi Dar es Salaam hasa Kariakoo, Wachina wamehamia na wanafanya kazi ambazo zinapaswa kufanywa na Watanzania. Wameanza ku-*establish* viwanda ndani ya majumba wanayokodisha.

Mheshimiwa Spika, kumi, Jeshi kupiga raia na kuua. Hivi kuna nini kinachoendelea kila leo tunasoma mambo haya na huko nyuma askari wetu walikuwa waadilifu kweli, nini kimeharibu mambo. Polisi kujichukulia sheria mikononi mwao kulikoni . Nawapongeza wale wote wanaofuata maadili ya kazi zao. Tafadhali sasa ajira ya vijana katika Jeshi la Polisi iwe *serious*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. FATMA ABDALLA TAMIM:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mungu, kwa kuniwezesha kuchangia mchango wangu huu nikiwa katika hali ya uzima na usalama. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais, kwa utendaji mahiri. Mungu ndiye mlipaji. Pia nawapongeza watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, mimi kilio changu, ni kwa Jeshi la Polisi Zanzibar. Tunashukuru kwa upande wa makazi, Serikali imejitahidi kuwajengea makazi ya kuishi na nina imani mtapopata uwezo, mtaendelea kuwajengea ili kila mtu apate makazi mazuri ya kuishi.

Mheshimiwa Spika, naomba Jeshi letu la Polisi, wapatiwe vifaa vya kutendea kazi. Nimesikia katika hotuba kuwa iko mbioni kuwapatia vitendea kazi. Nashukuru lakini nasisitiza sana fedha zitakapopatikana, waangalie kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, linguine ni vituo vya kufanyia kazi, viko katika hali mbaya sana. Kwa hiyo, naomba fedha zitakapopatikana na vituo hivi vishughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa utendaji mzuri na utekelezaji wa Ilani ya CCM 2005, kwa Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri kwa kushirikiana na *SIDO* ziweke utaratibu wa pamoja kwa kuvitambua vikundi vya uzalishaji mali kwa kila Kata na kuvipatia ujuzi/mafunzo na mikopo ya vifaa (mashine za aina mbalimbali) kulingana na mahitaji ya maeneo husika, kwa kuzingatia matunzo waliojifunza. Hii itasaidia kuwakusanya pamoja na kusaidia Serikali kutambua kuwa na takwimu sahihi za vikundi vya akina mama na vijana.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye uamuzi wa makusudi na utashi wa kisiasa, kwa kuzipatia fedha za kutosha Taasisi zake ambazo zinagusa wananchi walio wengi, wenye hali za chini ambazo zikiwezeshwa zitaleta mabadiliko kwa kipindi kifupi na wananchi wataweza kujiari wenyewe na kuondoa umaskini. Taasisi kama *TIRDO, SIDO, VETA* na zinginezo zikiongezewa uwezo, jamii yetu itabadilisha fikra za watu wasiokuwa na mwelekeo wa maisha yao kwa kuendekeza biashara za mkononi (Machinga) na kwenda kwenye biashara za uzalishaji mali kama viwanda vidogo vidogo vya usindikaji wa matunda, ukaushaji wa mboga mboga, usindikaji wa mafuta ya Alizeti, Asali,

utengenezaji wa chaki, utengenezaji wa vifaa vya mapambo, sanaa, ufinyanzi, upishi, utengenezaji vikoi na aina mbalimbali ya mafunzo na stadi ambazo vijana wengi wataweza kujifunza na kisha Serikali iwakopeshe vifaa, kwa kufanya hivyo ajira kwa vijana itaongezeka.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Ushirika na Chakula, iboreshe Idara ya Ushirika, kwa kuweka utaratibu wa kuwapatia mafunzo vikundi vya Ushirika au Bodi katika Vyama vya Ushirika na *SACCOS* ili Vyama hivi viweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuleta tija katika eneo hili la mafunzo. Maofisa ushirika wawe na utaratibu wa kuzitembelea *SACCOS* na ushirika mara kwa mara ili kujua na kubaini matatizo yaliyoko katika SACCOS zetu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kupitia Mfuko wa Uwezeshaji kuziangalia *SACCOS* zifuatazo ambazo ni za wanawake, zipatiwe fedha mara mbili ya awamu ya kwanza, kwa kuzingatia idadi kubwa ya wanachama wake. *SACCOS* hizo ni *TEWO SACCOS (TEMEKE WOMEN SACCOS); ILALA WOMEN SACCOS; KINONDONI WOMEN SACCOS (KIDIWOSA); KITUNDA SACCOS (KISACCOS) na UKONGA SACCOS (USACA).*

Mheshimiwa Spika, *SACCOS* hizi zimekuwa Mkombozi Mkubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam na Mikoa jirani, kwa kuwakopesha wananchi walio wengi wenye vipato vya chini.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Nishati na Madini itoe huduma ya kuweka umeme eneo la Chanika Videte kuelekea Mvuti (Msongola) mpaka Charambe ambako kuna ongezeko kubwa la watu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ijenge kituo kikubwa cha Polisi eneo la Chanika, ikizingatiwa ni eneo lenye watu wengi waliohamia kwa kipindi kifupi. Lakini pia kuna umbali mkubwa wa kilomita 35 toka *Airport* au Kipawa kupata huduma ya masaa 24 na wahalifu wengi wanakimbilia kujificha huko.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kutoa Shs.680 milioni kama mgao wa Ludewa iliyo kwenye mazingira magumu. Hata hivyo, Shs.60 milioni za Boti bado hatujakabidhiwa. Nashukuru kuwa TAMISEMI wamekubali kutoa fedha hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuna utendaji na usimamizi mbovu/hafifu wa miradi inayotekelezwa au kusimamiwa na Ofisi za Kanda, mfano, ni mradi wa umwagiliaji maji – Lifua (Ludewa) ulioshindikana kukamilika kwa wakati na kwa tija. Nashauri fedha hizi ziwe zinapelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya moja kwa moja ili zisimamiwe vizuri na kwa ukaribu zaidi kuliko ilivyo sasa ambapo Halmashuri hazihusishwi katika miradi hiyo lakini hubeba lawama miradi hii inapopata matatizo.

Mheshimiwa Spika, napongeza dhamira nzuri ya Serikali kwa kutoa kipaumbele katika kutekeleza mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi katika Wilaya na Vijiji.

Nashauri mpango huu utoe kipaumbele Wilaya ya Ludewa ambako miradi mikubwa ya Chuma cha Liganga na Makaa ya Mawe Mchuchuma imeanza. Hii ni kuepuka migogoro ya ardhi na uharibifu wa mazingira unaoweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa mpango wa ujenzi wa magati maeneo mbalimbali nchini. Nikumbushe ahadi ya Serikali (kupitia barua ya Waziri wa Miundombinu na Bajeti ya 2009/2010) kujenga gati katika bandari ya Manda (Ludewa), ambapo Serikali iliahidi kutenga Shs.200 milioni.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuanza miradi mikubwa ya Liganga na Mchuchuma (Ludewa) pamoja na mpango wa kutenga matumizi bora ya ardhi. Naomba iandaliwe ramani ya madini Wilayani Ludewa na tutimiziwe ahadi ya kujengewa Ofisi ya Afisa Madini ya Wilaya ya Ludewa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Serikali ya kutekeleza Sera ya Taifa ya Mazingira na kusimamia Sheria ya Mazingira katika sekta zote, inaleta maswali mengi zaidi kuliko majibu kwa vile Serikali haikutenga fedha yoyote ya ndani katika bajeti ya 2010/2011, bali kutegemea fedha ya wahisani kwa asilimia 100. Hii inaonyesha kuwa, Serikali haina nia ya kutekeleza Sera na Sheria za Mazingira kwa dhati na lolote linalofanyika kwa misaada haliwezi kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo ya kina kuhusu hali hii.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, kwa kusema naiomba Wizara ya TAMISEMI kuangalia upya suala la Wenyeviti wa Mitaa, hasa katika Jiji la Mwanza ambalo nalifahamu vizuri.

Mheshimiwa Spika, ni kitu cha kusononesha sana tena sana, ambapo Wenyeviti wa Mitaa ambao wanafanya kazi kubwa tena sana ya kuhudumia wananchi, hawana muda maalumu au ukomo wa muda wa kazi, lakini Wenyeviti hawa hawana ruhusa ya kutumia Mihuri na Mihuri hiyo hukaa na Watendaji wa Mitaa. Lakini Watendaji hao huanza kazi saa mbili na nusu asubuhi na kumaliza saa tisa mchana na Ijumaa kumaliza kazi saa tisa mchana, Jumamosi hawaji kazini, Jumapili hawaji kazini mpaka Jumatatu.

Kitu cha kusikitisha ni kuwa, mtu akifiwa Ijumaa jioni, hataweza kutoa maiti mpaka Jumatatu mchana, hii ni hatari kwa uongozi na kama mtu amekamatwa, hatakuwa na barua ya dhamana, hata kama mtu anahitaji barua ya masuala yake ya haraka, hawezi kupata, kwani barua atapata lakini haina muhuri na sio rahisi kupata huduma bila muhuri kwenye barua hiyo. Haya ni matatizo kwa wananchi ambao wanategemea huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia Watendaji hawa hawana vitendea kazi, mbali na Ofisi hata karatasi hawana, panchi na hata mifuko imara na ya uhakika ya kubebea hata hiyo mihuri, kwani wengi wao hawana Ofisi za Mitaa na huchukua vifaa vichache walivyonavyo, kwenye mifuko ya Rambo. Hii ni aibu. Tunaiomba Serikali kabla ya kutenda na kuchukua hatua, utafiti wa kina ufanyike na kazi hii ifuatiliwe na viongozi na

sio Watendaji kwani wengi huwa sio makini au kwa kuwaamini Watendaji wa chini yao, ambao hawatekelezi kazi zao kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, pia naomba Wakuu wa Mikoa wapunguziwe madaraka waliyopewa, kwani baadhi ya Wakuu wa Mikoa ni Wanasiasa na huegemea zaidi katika itikadi za vyama vyao. Mfano kuwa ndiyo Wenyeviti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoani. Pia kuweza kumuweka mtu ndani kwa masaa 48 na n.k. Serikali ijue Watanzania wanaliona hili na wanashuhudia, huwezi kuwa mtenda haki wakati ni kada wa Chama. Hapo ndipo Chama cha Upinzani kama kina nguvu eneo fulani baadhi ya Wakuu hawa ambao ni Makada au Wanasiasa hutumia rungu lao kudhoofisha Chama hicho kwa kuwatia ndani viongozi wao. Ahsante.

**MHE. JOYCE M. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri. Aidha, nimpongeze Waziri wa TAMISEMI, kwa hotuba nzuri. Nasema Mama Kombani anatuwakilisha vizuri wanawake. Binafsi nampenda, Mungu aendelee kumjalia.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wanawake wa Shinyanga, naishukuru Serikali ya Awamu ya Nne, kwa juhudi kubwa ya kutuletea barabara nzuri Shinyanga, maji ya kutosha na madaraja mawili ya Kata ya Ndala na Kata ya Ngokolo. Nasema ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, ombi kwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji ni kwamba kuna baadhi ya Kata kama Mwawaza, Mwanalili, Kizumbi, Kitangili katika kijiji cha Lwelyangula hakuna maji kabisa. Tunaomba maji haya tufaidike wa Kata za Mjini na Vijijini.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuanzishwa tena JKT, kwani huko watafundishwa Kilimo Kwanza, ujasiri, adabu na heshima n.k. Uzuri wa JKT, mara wamalizapo watafanya kazi kwa adabu na migomo ya hovyo hovyo haitakuwepo. Naomba mara wamalizapo *Form VI* waende JKT kwanza halafu ndiyo waende Chuo Kikuu. Hapo tutapunguza migomo.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru Serikali kwa kukarabati Hospitali yetu ya Wilaya Shinyanga. Sasa inapendeza.

Mheshimiwa Spika, Polisi wana hali mbaya sana ya mahali pa kuishi. Nyumba ni mbovu sana. Tunaomba muwajengee ma-*flat* ili waishi vizuri na wapate moyo wa kufanya kazi kwa bidii.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara ya Ulinzi, JWTZ, Uongozi uende Shinyanga Kata ya Kizumbi kuna uonevu mkubwa kati ya JWTZ na wananchi. Wananchi wananyang'anywa ardhi na mifugo. Kuna chuki kubwa kati ya wananchi na JWTZ.

Mheshimiwa Spika, wanaobeza Shule za Sekondari na Shule za Msingi zilizojengwa na wananchi, hawawatendei haki wananchi kwani wanafunzi hao wanaosoma Sekondari ni vema zaidi kuliko wangekuwa majambzi, malaya au kitu kingine chochote.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Wizara ya Elimu ni kwamba nyumba za Walimu zijengwe za kutosha; maabara; Hostel kwa ajili ya wasichana kuepuka kudanganywa na MAFATAKI na upataji wa mimba za utotoni; Wenyeviti wa Vijiji wawe ndiyo walezi wa Walimu pale kijijini na awaelimishe wanakijiji kuwa Walimu hawa ni watoto wao na wakiumwa wao ndio wawajibike, (waangalie wasilogwe) maana Walimu wengi wanakimbia vijijini kwa ajili ya ushirikina.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kunipa nafasi ya kuchangia hoja hiyo hapo juu kwa kuongea, kutokana na ufinyu wa muda, naomba kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, bado naunga mkono kwa dhati hoja hiyo hapo juu na kutoa shukrani nyingi za Wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi, kwa Serikali ya Awamu ya Nne, kwa utekelezaji wake wa Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya 2005 nchini na katika Jimbo letu. Kwa kifupi nilielezea jinsi ambavyo Serikali inajikita katika utekelezaji wa mambo yafuatayo Jimboni humo; elimu; miundombinu ya barabara; afya; maji; kilimo na miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongeza kwa kusema Jimbo langu pia ni kati ya Majimbo 30 yaliyopata fursa ya kujengewa Ofisi ya Bunge katika kijiji cha Msangano, Kata ya Msangano, Tarafa ya Msangano. Jengo hili lilifunguliwa tarehe 14/10/2010 na Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI. Aidha, Jimbo hili limepatiwa mgao wa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo *(CDCF).*

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu wa kuongea nilielezea, pamoja na mafanikio hayo, matatizo yaliyopo Jimboni ikiwa ni pamoja na upungufu mkubwa wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari. Tatizo hili ni kubwa kiasi cha kuathiri mahudhurio na hata matokeo ya Mitihani ya Darasa la Saba (VII), Kidato cha Pili (II) na Kidato cha nne (IV). Kwa mfano tu mwaka 2009, wanafunzi wapatao 18,000 walifanya Mtihani wa Darasa la VII lakini kati yao wasichana walikuwa 2,500 tu (Jedwali Na. 18 Uk. 47 la Hotuba ya Waziri Mkuu 2010/2011).

Pia kwa hivi sasa shule kadhaa ikiwemo Shule ya Sekondari ya Kata ya Msangano yenye wanafunzi kuanzia Kidato cha I – IV kuwa na Mwalimu mmoja tu mbali ya Mkuu wa Shule ambaye muda mwingi hayupo pale shuleni. Naomba suala hili lishughulikiwe, kwani Walimu wamekuwa wakipangiwa kuja kule lakini hawafiki.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni kutokamilika kwa barabara. Jimbo langu, lina matatizo makubwa ya miundombinu ya barabara kutokana na ugumu wa jiografia yake kwamba nusu iko kwenye Bonde la Ufa lenye kina kirefu na mtandao wa mito hali ambayo inafanya mawasiliano na nusu ya pili iliyoko ukanda wa juu kuwa magumu. Barabara zilizopo, kutokana na kutengenezwa kwa tope tu, mara mvua zinyeshapo huharibika kiasi cha kutopitika kati ya Novemba na Mei kila mwaka.

Ombi la wana Mbozi Magharibi, hususani wale wa Kata za Kamsamba, Iruma, Mkulwe, Chilulumo, Chitete, Msangano, Nkangano, Chiwezi, Ndalambo, Myunga na Kapele, ni kwa Serikali kuwatengenezea barabara hizo ili waweze kusafiri na kusafirisha bidhaa zao kwa mwaka mzima. Barabara hizo ni pamoja na:-

(a) Tunduma - Sumbawanga kwa kiwango cha Lami;

(b) Mlowo – Kamsamba (Kipande cha Kilomita 25 kati ya Itumbula na Kamsamba pamoja na daraja la Mto Momba);

(c) Igamba – Msangano – Utambalila (Vipande kati ya Isalalo na Msangano na kipande kati ya Msangano – Tindinzoma chenye umbali wa km 30 pamoja na maboksi caravate manne ambayo kati yake moja tayari limejengwa);

(d) Chapwa – Chindi – Msangano (km 46). Barabara hii ikikamilika itaungana na barabara tajwa hapo juu (Na.3) na kuendelezwa kupitia Chilulomo, Mkulwe hadi Kamsamba. Barabara hii itaunganisha sehemu ya Jimbo hili iliyoko bonde la ufa yenye Kata za Chiwezi, Msangano, Chitete, Chilulumo, Ivuna na Kamsamba;

(e) Kakozi (Ndalambo) – Kapele – Ilonga. Barabara hii ni kiungo muhimu kati ya Mji wa Tunduma, Mkoani Mbeya na Bandari ya Kasanga, Ziwa Tanganyika; na

(f) Ikana – Mkumba. Barabara hii ni kiungo muhimu kati ya sehemu ya Jimbo ya Uwanda wa Juu na sehemu ya Bonde la Ufa la Rukwa kwenye barabara ya Tunduma – Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni la maji safi na salama. Serikali imetekeleza kwa dhati azma yake ya kuwafikishia wananchi maji safi na salama kwa kuchimba visima na kutandaza mabonde au kuweka pampu kwenye visima vya zamani katika vijiji vya Jimbo langu. Tatizo lililojitokeza ni Makandarasi kutofanya kazi hiyo kwa ufanisi, ama kwa kukosa waledi au kwa nia ya kupata faida kubwa kwa kazi duni. Matokeo yake ni visima hivyo kutotoa maji hasa katika Kata za Chilulumo, Ivuna, Kamsamba, Msangano na Myunga. Serikali ifuatilie kuona nini kilifanyika ili kudumisha imani waliyonayo wananchi kwake.

Mheshimiwa Spika, huduma za afya, tatizo hili ni kubwa kutokana na ukubwa wa Jimbo, hivyo pamoja na kuwa na Vituo vya Afya vitatu na Zahanati zipatazo 20 bado kuna mahitaji ya takribani 70 ili kuwa na angalau Zahanati moja kwa kila kijiji. Mbali ya uchache wa Zahanati, kuna tatizo la upungufu mkubwa wa watumishi wa vituo hivyo.

Namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutoa gari la kubebea wagonjwa kwa kituo cha Afya cha Kamsamba ambako litawezesha wagonjwa wa rufaa kupelekwa hospitali ya Wilaya ya Mbozi, umbali wa Kilomita 130.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mbunge, Jimbo la Mbozi Magharibi, Ofisi hii ambayo kinadharia ilifunguliwa tarehe 14/10/2010, pamoja na kuwa na miundo ya msingi, miundombinu ya umeme na maji, waya za umeme, taa, mabomba, masinki, vyoo vya kuvuta maji lakini hakuna umeme na maji kutokana na kutokuwepo jenereta la umeme na pia kutokuwepo kisima na pampu ya maji. Pia Ofisi hiyo haijawekewa samani ya aina yoyote na kutokana na hali hiyo hadi leo Ofisi hiyo haitumiki. Taarifa hii baada ya kufikishwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, alitoa maelekezo ya kumwona Katibu Tawala wa Mkoa (RAS), Mbeya, lakini yeye alidai fedha hizi ziko Wilayani; Wilayani *DED* akasema hana labda *DAS*, lakini *DAS* akasema hahusiki kabisa. Kwa hali hiyo, napenda kujua hatima ya Ofisi ya Mbunge, Jimbo la Mbozi Magharibi. Wananchi wanashinda nje ya Ofisi ambayo haitoi huduma yoyote hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, mgao wa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo. Jimbo la Mbozi Magharibi lenye ukubwa wa kilomita za mraba 6,275 kati ya jumla ya kilomita za mraba 9,679 za eneo la Wilaya ya Mbozi, Jimbo la Mbozi Mashariki likiwa na eneo la kilomita za mraba 3,404.

Mheshimiwa Spika, eneo la Jimbo likiwa moja kati ya vigezo vya mgao wa fedha za *CDCF,* nilitegemea kupatiwa fedha hizo kwa uwiano huo lakini cha kusikitisha fedha kwa kigezo hiki iligawanywa sawasawa kwa Majimbo yote mawili na kibaya zaidi ni suala la ukubwa wa maeneo hayo kuandikwa kuwa ni sawa yaani kilomita za mraba 4,793 kitu ambacho si kweli. Naomba kwa mgawo wa baadaye wa fedha, kigezo hiki kirekebishwa ili kiendane na ukubwa wa hali ya Jimbo ambalo ni $km^2$ 6,275 na si $km^2$ 4,793).

Mheshimiwa Spika, kigezo cha idadi ya watu pia hakikuzingatiwa kwa usahihi. Jimbo langu limepewa mgao pungufu. Kwa matokeo ya kitakwimu, ni mategemeo yangu kuwa Jimbo la Mbozi Magharibi sasa hivi lina Jumla ya wakazi 212,227 kwa ongezeko la wastani wa 3.2% kwa mwaka kulingana na sensa ya watu ya 2002. Hesabu iliyotumika kugawa fedha hizi ilikuwa ya miaka mitatu iliyopita ya watu 193,188. Naomba takwimu hizi ziwekwe sahihi pia kuanza mgao wa 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia bajeti hii ya Waziri Mkuu kwa mambo yafuatayo. Kwanza, ujenzi wa ofisi za Wabunge Zanzibar. Katika bajeti ya mwaka jana, 2009/2010, Jimbo la Mkanyageni lilipangiwa kujenga Ofisi ya Mbunge na mimi nikiwa Mbunge wa Jimbo hilo, nikaonana na Mkuu wa Wilaya kwa majadiliano na kupata eneo muafaka. Kutokana na barua ya Mkuu wa Wilaya, kwa Idara ya Upimaji ambapo gharama za upimaji nilitoa mfukoni mwangu, pamoja na hayo kwa nini mwaka mmoja umepita

kutoka bajeti ya mwaka jana hadi bajeti hii ya 2010/2011 kiwanja hicho hakijafanyiwa lolote? Mbunge sijui hadi leo kama fedha imepelekwa Zanzibar, wajenzi wa Ofisi hiyo ni nani, kwa nini hata msingi bado haupo na nini kinaendelea? Ofisi ya Bunge iliyopo Zanzibar inafanya nini? Utaratibu wa fedha hii ya Muungano kupitia SMZ sio tatizo, lakini tatizo linakuja fedha hii inatolewa bila ya ushirikishwaji wa Ofisi ya Bunge iliyopo Zanzibar ambapo Mbunge anaweza kupata taarifa zote.

Mheshimiwa Spika, naomba nipate taarifa kamili ziko wapi fedha za Ofisi ya Mbunge Mkanyageni na ni vyema utaratibu ubadilishwe vinginevyo fedha zitapotea na Ofisi hazitajengwa.

Mheshimiwa Spika, upotevu wa fedha za Halmashauri na uhamisho wanaopewa baada ya kuharibu sehemu fulani. Kutokana na ripoti mbalimbali za *CAG* zinazohusiana na upotevu wa fedha nyingi za Serikali, mimi nina shauri mambo mawili kwa Serikali:-

(a) Wote waliobainika wapelekwe Mahakamani mara moja, vitendo vya kuoneana haya, vitendo vya kulindana, vinatia aibu Taifa letu lakini hata Chama Tawala hakitakwepa kuitwa Chama cha Mafisadi, kwa tabia hii, watakiharibia sana Chama cha Mapinduzi; na

(b) Sasa Serikali haina budi kuanzisha utaratibu wa ajira za mkataba kwa vyeo vya Mkurugenzi, Waweka Hazina (DT's), Afisa Kilimo wa Wilaya na *DMO (District Medical Officer)*

Mheshimiwa Spika, watu hawa watakapopewa ajira za mkataba wa miaka mitatu mitatu na baadaye *performance* zao ziangaliwe, ndio njia pekee ya kupunguza ubadhirifu huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ukiukwaji wa uendeshaji wa shughuli za Serikali. Katika mada hii napenda kuwasilisha kwako malalamiko ya wananchi wa Wilaya ya Geita hasa Kata ya Nkome ambao wamewasilisha malalamiko yao kama mlezi wa Jimbo la Geita.

Mheshimiwa Spika, naomba malalamiko hayo yachunguzwe mara moja na hatua za kisheria zichukuliwe, tukiendelea kufumbia macho vitendo vya namna hii, basi Taifa hili maendeleo litayasikia tu. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alitolee ufafanuzi swali hili hapa Bungeni ili liwe fundisho kwa Watendaji wengine wa namna hiyo katika Kata na Halmashauri nyingine hapa Tanzania.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali yake, kwa utekelezaji mzuri wa Ilani na vilevile kwa hotuba nzuri ya Bajeti ambayo ameiwasilisha kwa umahiri mkubwa sana. Pongezi hizi pia ziwafikie Mawaziri, Naibu Waziri wa Wizara zote zilizopo chini ya Ofisi yake, Makatibu Wakuu na Manaibu wao pamoja na Watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuweza kufanikisha miradi mbalimbali iliyoanzishwa kupitia ahadi zake katika Ilani ya 2005. Huu ni ukombozi

mkubwa sana kwa wananchi wa Mkoa wa Pwani, kwani ujenzi wa Gati Mafia, Uwanja wa Ndege Mafia barabara ya Kilwa, Shule za Msingi na Sekondari, yote ni mafanikio kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ili kuzidi kupata hamasa na pia kulisaidia Jeshi la Polisi kwa Mkoa wa Pwani ili waweze kulinda Wananchi na mali zao, naomba Wizara yako iliangalie Jeshi hili kwa kuwapatia magari yatakayowasaidia kutekeleza kazi zao kwa ufanisi na ukizingatia kwamba Mkoa wa Pwani ni kiungo cha Mikoa yote ya hapa nchini. Naomba suala hili lipatiwe majibu wakati wa kujibu hoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifikirie na kutoa uamuzi wa haraka juu ya Mkandarasi wa Daraja la Kigamboni, hili ni tatizo na kero kubwa kwa wakazi wa Dar es Salaam na Pwani. Naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. KIUMBWA M. MBARAKA:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uhai na uzima ili niweze kuchangia kwa kifupi Hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri Mkuu na timu yake pia nimpongeze Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa CCM, Mheshimiwa Dr. Jakaya Kikwete, kwa kusimamia vyema Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa Sera mpya ya Maendeleo ya Mtoto Tanzania ya mwaka 2008 inayotoa Mwongozo wa Haki za Mtoto. Vile vile Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, imetungwa kutilia mkazo sheria zilizopo kwa kumlinda mtoto na haki za mtoto. Lakini bado kuna vitendo vya ukatili dhidi ya watoto, ni vitendo vya aibu kabisa na hakuna adhabu yoyote imechukuliwa kwa wahusika wa vitendo hivyo ambavyo havifai kufanywa na binadamu mwenye akili timamu. Unaambiwa, hakuna ushahidi, je, wale watoto wanaouza biashara barabarani, pia kunatakiwa ushahidi? Mimi naamini atakayekamatwa, atamtaja nani kampa biashara hiyo. Naiomba sana Serikali kuzifanyia kazi sheria zetu tunazozitunga ili kuondosha matatizo. Waswahili wanasema, ukitaka kuondosha tatizo basi uongeze tatizo. Tuache huruma, kwani huruma hailei mtoto lazima wahalifu wakamatwe na hatua zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuimarisha lugha ya Kiswahili kama kielelezo cha utamaduni wetu pamoja na kusisitiza umuhimu wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli rasmi za Serikali. Suala hili ni zuri na naamini litatekelezwa kwa vitendo na ninashauri kuwa hata Miswada yetu katika Bunge lijalo italetwa kwa lugha ya Kiswahili, lugha ambayo Watanzania wengi wanaielewa zaidi kuliko ilivyo sasa. Pengine ndio sababu ya wananchi wetu kutokuelewa kwa haraka sheria zinazotungwa katika Bunge lako Tukufu. Naunga mkono hoja.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kunijalia kuwa mzima na kuweza kuchangia kuhusu mada iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kukua kwa uchumi, ni kitu kimoja na kuutumia uchumi huu kwa ajili ya wananchi, ni kitu kingine. Mara nyingi sana, Serikali imekuwa inapiga kelele kuwa uchumi wa nchi yetu unakua tena kwa kasi kubwa lakini athari ya kukua huku, bado haijaonekana maana bado hali ya Watanzania walio wengi, ni duni sana, wengine kufikia hatua ya kula mizizi kutokana na ukosefu na sio tu wa pesa lakini na chakula.

Mheshimiwa Spika, inaelekea kukua kwa uchumi ni maneno tu ya vitabuni lakini kiutendaji hamna lolote. Wananchi wanataka waone kama kweli uchumi umekua basi uchumi huo uwasaidie katika kunyanyua hali zao za maisha. Sasa hivi kila kitu kinapanda bei hususani vyakula ambavyo si jambo la anasa. Wananchi wanajiuliza vipi kukua kwa uchumi kutatupunguzia ukali wa maisha, ikiwemo kushuka bei kwa vyakula, upatikanaji wa umeme ambao mtu anaweza kuingiza nyumbani mwake kwa bei muafaka, kuondokana na barabara za vumbi na kuepukana na kilimo cha kutumia jembe la mkono.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ukurasa wa 33, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameelezea kuhusu kuimarisha bandari na hasa ile ya Dar es Salaam kwa kuweka vituo nane vya kuhifadhi makasha nje ya bandari. Lakini tujiulize, je, hatua hiyo itatosha kuimarisha bandari na kuweza kuvutia wawekezaji nchini hasa wale wa usafirishaji?

Mheshimiwa Spika, pale bandarini Dar es Salaam, pamekuwa na uzoroteshaji mkubwa wa kupakuwa na kutoa mizigo na hata usalama wa mizigo inayopita pale. Wapo Wafanyabiashara wengi sasa wameamua kushusha mizigo ya kupitia bandari ya Mombasa. Je, Serikali haioni kwamba, kwa hatua hiyo wanayoichukua baadhi ya wafanyabiashara kutumia bandari ya Mombasa badala ya ile ya Dar es Salaam, inaikosesha Serikali mapato makubwa na hivyo kushuka kwa uchumi?

Mheshimiwa Spika, hivi ni lini hii Serikali chini ya Chama cha Mapinduzi, itaweka mazingira ya uchaguzi japo sio sawa lakini angalau safi? Hivi kweli demokrasia ndani ya uchaguzi wa Vyama vingi Tanzania itafikiwa angalau kwa asilimia 15 (15%)? Uchaguzi unatawaliwa na hila nyingi. Kwa mfano, uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika mwaka jana 2009, vyama vilishirikishwa kuandaa Kanuni lakini Kanuni zile katika dakika za mwisho hazikutumika na badala yake yakatumika maagizo na maelezo kwa Watendaji ili yatumike katika uchaguzi ule, jamani, hivi tutafika kweli? Ahsante sana.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba nzuri ambayo imeonesha asilimia 99% imetekeleza Ilani ya CCM ya 2005.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri Mkuu apuuze kejeli za Wapinzani, kila kitu kwao ni kibaya, chao kizuri hakuna, makelele kila siku, hawana mchango wowote katika maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali, ikisimamiwa na Waziri Mkuu, fedha za *D by D* zinazopelekwa katika Halmashauri, ukaguzi wa *CAG* uwe wa karibu sana. Mfano, hapa Dodoma kuna fedha zimetumika vibaya kutengeneza barabara inayoelekea katika bustani ya *CDA,* katika barabara ya Arusha, mfereji si mfereji, daraja si daraja, ni kero. Fedha nyingi zimetumika pale, *Engineer* hajakagua kazi hiyo, naomba barabara hii, Waziri mhusika atume Mkaguzi aende akaone, ni kero.

Mheshimiwa Spika, naomba kusisitiza, hapa Tanzania hatuna watoto wa mitaani, kwa nini watoto wa mitaani wanazidi kuongezeka? Sheria bado haijaanza kufanya kazi kwa kusimamia watoto. Namwoamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, wazazi wote wanaoshindwa kusimamia watoto wao, wakamatwe na walazimishwe kulea watoto wao hawa ili wapate elimu maana ni haki yao.

Mheshimiwa Spika, namtakia kheri Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, achaguliwe tena, Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Celina Kombani, watu wa Ulanga wamchague tena na mwisho Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwanri achaguliwe tena.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono asilimia mia.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri ambayo imeangalia maeneo mengi ya vipaumbele kwa manufaa ya wnananchi. Pia nampongeza Mheshimiwa Celina Kombani, Mheshimiwa Marmo, pia Naibu Waziri na watendaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa ushirikiano na utendaji mzuri hadi kufikia kuleta bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimwa Waziri Mkuu imeangalia kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 – 2010.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba nianze na kipengele cha Sheria ya Mtoto. Tutakumbuka kuwa, mwaka 2009 hapa Bungeni tulipitisha Sheria ya Mtoto na kwa muda huu tayari imeanza kutumika. Naipongeza Serikali kwa kuweza kuandaa Sera ya Maendeleo ya Mtoto. Je, katika kipindi cha kupitisha Sheria hiyo hadi kufikia leo hivi, ni wazazi wangapi waliowajibishwa kwa kukiuka Sheria hiyo? Kwani bado wapo wazazi ambao wanaendelea na unyanyasaji wa watoto pia watoto wa mitaani wanaendelea kuombaomba barabarani katika Jiji la Dar es Salaam, wakiulizwa wanasema wametumwa na wazazi.

Naiomba Serikali kuiona kwa jicho la kipekee Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kuitengea bajeti angalau ya kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi kwani hilo ni jukumu la Wizara hiyo. Pia Serikali iangalie nmna ya kufanya udhibiti na usimamizi ulio wa wazi ili kunusuru kuendelea kuathirika kisaikolojia watoto walio wengi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kumuendeleza mkulima kwa kumpatia kilimo chenye tija na kumnyanyua kimapato. Suala la uanzishwaji wa Benki ya Wakulima, utiliwa mkazo na kuangalia namna ya kuwapatia wakulima wakubwa na

wadogo mikopo bila kujali jinsia. Masharti nafuu ndio dira itakayowaendeleza wakulima walio wengi. Mikopo ni haki ya wakulima wote, wawe wakubwa na wadogo.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa ruzuku ya mbolea, dawa pamoja na zana nyingine za kilimo, Serikali ifuatilie kwa makini na usimamizi ulio wazi kwa maslahi ya wakuliwa uwepo ili kuondoa kero zinazojitokeza katika ugawaji wa ruzuku hizo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwamba katika kipindi hiki Serikali imetenga fedha kwa ajili ya utafiti.

Mheshimiwa Spika, MKUKUTA, napenda niipongeze Serikali kwa kuweka vipengele mbalimbali vya kumuendeleza Mtanzania kimapato na kuondokana na umaskini uliokithiri. Changamoto zipo nyingi lakini Serikali katika kipindi kijacho, iweke mkakati wa kuzitatua na kuweka usimamizi mkubwa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Kambi ya Upinzani, ilisema kuwa Mtanzania tokea miaka ya nyuma hadi leo hivi hajaondokana na umaskini ila anaendelea kuwa maskini. Tutakumbuka kuwa Serikali imetoa fursa mbalimbali kwa wawekezaji kuingia nchini yakiwemo makampuni mbalimbali. Wananchi hivi sasa wamefaidika na suala la uuzaji wa viwanja kupitia hatimiliki za viwanja walizonazo, pia wapo Watanzania wanaondelea kuuza nyumba kwa bei za juu sana na wamefaidika na viwanja hivyo na wameweza kukua kiuchumi kwa kiwango cha juu sana kuliko walivyokuwa hapo nyuma. Zipo changamoto ambazo sasa hivi Serikali wanatakiwa kuzishughulikia kwa kuweka usimamizi katika maeneo mengine ambayo wananchi wanatakiwa kupewa fidia stahili.

Mheshimiwa Spika, wananchi wameweza kufaidika na uwezeshwaji wa wananchi kiuchumi kwa kutolewa mikopo kupitia mfuko wa uwezeshwaji. Serikali inatakiwa kuweka usimamizi na ufuatiliaji na kuangalia changamoto zilizojitokeza katika utekekelzaji wa mifuko hiyo. Pia kuwe na ufuatiliaji wa urejeshwaji wa fedha ili wengine waliobaki nao wafaidike. Elimu ya ujasiriamali kabla ya kutoa fedha hizo ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, tumeweza kupatiwa umeme ambao ulikuwa unasuasua kwa muda mrefu kisiwani Pemba. Mradi wa umeme kupitia baharini kutoka Pangani Tanga hadi Kisiwani Pemba. Pia tulipokuwa tunapitisha Sheria ya Madini katika Bunge hili tumeona vipengele mbalimbali ambavyo vinakusudia kumuendeleza kimapato mchimbaji wa kawaida. Serikali ihimize suala la ufuatiliaji na usimamizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, Serikali imejitahidi kujenga shule mbalimbali katika Mikoa na Wilaya na kutekeleza suala zima la kutokomeza ujinga nchini. Naomba Serikali iweke usimamizi na ufuatiliaji katika utuoaji wa mikopo kupitia Bodi ya Elimu. Mikopo ya Elimu ya Juu, inayotolewa haiko sawa katika utekelezaji. Changamoto zinazojitokeza ikiwemo kuongezwa fedha kwa ajili hiyo zishughukiwe kwa kina. Suala la ubinafsi katika utoaji mikopo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kujenga *hostel* katika Shule za Sekondari ili kiuondoa tatizo la ubebaji mimba kwa wanafunzi. Pia kuondoa vichocheo vya kuleta uhuni kwa wanafunzi wawapo vichochoroni na pia kujenga maabara mashuleni.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kuhusu suala la Jeshi la Polisi. Naipongeza Mifuko ya Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*, kwa kuingia mkataba na Serikali na kujenga nyumba za Askari hawa katika maeneo mbalimbali. Yapo majengo hayo Mjini Dar es Salaam na kule Zanzibar, Ziwani, Unguja na Limbani Pemba.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kuwalipa Askari hawa madeni yao wanayodai kwa kipindi kirefu ili kuwapa moyo katika utekelezaji wa kazi zao. Tutakumbuka kuwa Askari hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, katika kuleta ulinzi wa Taifa letu na usalama wa raia na mali zao na kipindi hiki kitakuwa na kazi ngumu ya uchaguzi wa Taifa letu. Askari hawa tutawatuma katika maeneo mbalimbali nchini, naiomba Serikali kuweka utaratibu maalum na wa kipekee wa kuwawezesha na kuwalipa madeni yao wanayodai ili kufanya kazi kwa utulivu zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Nimpongeze sana kwa hotuba yake nzuri. Pamoja na pongezi hizo, ninaomba nikumbushie suala la usambazaji wa umeme katika Jimbo la Kondoa Kusini. Serikali ilipanga kusambaza umeme katika vijiji 10 vya Dalai, Tandala, Churuka, Jangalo, Itolwa, Mlongia, Mapango, Mwaikisabe, Mwailanje na Isusumya kupitia miridi ya *REA* na *MCC*. Mradi wa kupeleka umeme katika kijiji cha Mwailanje, umeanza mwaka 2008 lakini hadi sasa haujakamilika kwa madai kuwa vifaa havipatikani. Ninaomba vifaa vipatikane mapema ili wananchi wa Kijiji hiki wafikishiwe huduma hii haraka.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kijiji cha Churuka, kimetengewa fedha na Shirika la *TANESCO*, kwa lengo la kupeleka umeme kijijini hapo. Mradi huu pia haujaanza kwa madai ya ukosefu wa vifaa. Ninaomba tatizo hili lishughulikiwe ili mradi huu uanze kutekelezwa. Vijiji nane vilivyobaki, viko chini ya mradi wa *MCC*. Ninaishukuru Serikali kwa kutupa mradi huu, hata hivyo mradi huu umechelewa sana kuanza kutekelezwa. Kwa heshima zote, ninaomba Serikali iharakishe utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia haya machache, ninaomba nimalizie kwa kuunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kumpongeza sana Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu, kwa uwezo wake mkubwa aliouonesha tangu alipoteuliwa kushika nafasi

hiyo na kuthibitishwa na Bunge akiwa Mtendaji Mkuu bila kusahau uwezo wake wa kujibu maswali ya papo kwa papo kila Alhamisi.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninawapongeza Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Celina Kombani, mwanamke mwenzetu aliyeonyesha uwezo mkubwa katika dhamana aliyopewa na Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Ni matumaini yangu, Mungu yu pamoja naye, wapiga kura wake watamrudisha Bungeni na Mheshimiwa Rais atampa tena heshima hiyo, amen.

Mheshimiwa Spika, pongezi zingine zimwendee Mheshimiwa Philip Marmo, Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Shughuli za Bunge, kwa uwezo mkubwa aliuoonesha katika kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kutekeleza Ilani ya Uchaguzi. Naye nina hakika atarudi tena Bungeni, Mungu awa naye.

Mheshimiwa Spika, sitakuwa na fadhili endapo sitatoa sifa kwa Ndugu yangu, Bwana Lyimo, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa uwezo wake mkubwa kiutendaji. Ndugu Mama Maimuna Tarishi, Katibu Mkuu, Wizara ya TAMISEMI, kwa umakini wake wa utendaji ndani ya Wizara hiyo. Vilevile nimalizie pongezi hizi kwa watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii ambayo imeainishwa barabara kwa lengo kuu la kutekeleza Ilani ya Uchaguzi, ninawatakia ushirikiano na juhudi kubwa katika kutekekeza azma yao.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa elimu ya ujasiriamali bado haijawafikia wanawake ipasavyo. Hivyo ninaiomba Serikali kutenga fedha za kutosha kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii, ili waweze kununua pikipiki kama sio magari waweze kuwafikia akina mama vijijini na kuwapa elimu hii ambayo itawasaidia sana kuendesha miradi yao bila kupata hasara au kula mitaji.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuijulisha Serikali kuwa wanawake, wengi hawajapata mikopo hii ya JK kwa sababu wengi wameshindwa kutekeleza masharti ya mikopo kwani ni magumu kwao. Mfano Hati ya Nyumba, wengi hawana Hati hizo. Wanataka wawe na mali za kudumu, wengi hawana. Hivyo, ninaiomba Serikali ilegeze masharti ili wanawake waweze kukopesheka. Ni vema fedha nyingi zipelekwe kwenye *SACCOS* na *SACCOS* hizo zianzishwe kwa kila Kijiji na Kata na ziwe chini ya usimamizi wa watendaji wa Serikali. Hii itasaidia wanawake kukopa kwenye *SACCOS* hizi.

Mheshimiwa Spika, nimefuatilia taarifa au hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, sijaona mkakati uliowekwa kwa ajili ya vijana kuhusu kuwawezesha vijana kujiajiri ama kupata ajira. Ninaamini kipaumbele kiliwekwa kwani wengi wao wamejiunga na vyuo kupata mafunzo, wapo pia wengi wamepata ajira na wengi wamepata mikopo ili waweze kupata mitaji lakini bado kuna wimbi kubwa la vijana ambao hawana mwelekeo. Ninaiomba Serikali ieleze kupitia bajeti hii vijana watanufaika nini ikiwa wanahitaji msingi bora na imara kuwanusuru kujiunga na madawa ya kulevya, uzururaji na kujiunga na ujambazi. Ni vema wakati wa majumuisho vijana wakasikia ni wenzao wangapi wamenufaika na huduma ya Serikali ya ajira au mikopo.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu tangu ilivyoainishwa kwenye Sera ya Ukimwi ya mwaka 2001 kuhusu kuanzisha Mfuko wa *Aids Trust Fund* ambao utakuwa ni chanzo kitakachakuwa endelevu kwa huduma za Ukimwi. Ninaomba kuelezwa lini huduma ya kuanzisha chanzo hiki kitaanza ili tuweze kuwa na chanzo cha kudumu katika kupambana na Ukimwi ukizingatia kwamba wahisani wengi wanaendelea kupunguza kiwango cha uchangiaji.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe wito kwa wanasiasa wote watumie majukwaa yao kuhamasisha wananchi kupambana na Ukimwi. Hii itasaidia sana kwani wapiga kura wengi husikiliza sana viongozi waliowachagua wao. Vile vile itadhihirisha wazi kuwa janga la Ukimwi ni la kila mtu.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii, nikiwa Kamishna wa *TACAIDS*, kuwahabarisha Wabunge wenzangu, viongozi wote na wadau mbalimbali kuwa *TACAIDS* sio kweli kuwa ni chanzo cha fedha, ni chombo tu cha kuratibu shughuli za Ukimwi nchini. Hivyo, ninaomba Serikali kuongeza kiwango cha pesa kinachotengwa kwa ajili ya *TACAIDS* pamoja na wahisani mbalimbali ili kuongeza nguvu ya kupambana na janga hili la Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wazo kwa Serikali kuwa kazi hasa ya kupambana na Ukimwi, uko ngazi ya Wilaya, Tarafa, Kata na Vijiji. Hivyo basi, ili tuweze kusimamia vema fedha za Ukimwi, nyingi zinazopelekwa vijijini, ni vema tuwe na Waratibu Wasaidizi ngazi ya Wilaya ambao watafanya kazi ya kutambua waathirika, yatima na mambo mbalimbali yanayokwamisha jitihada za kupambana na Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri ufuatao kwa Serikali:-

(i) Itoe maelekezo kwa sekta zote kuona umuhimu wa kutenga fedha za Ukimwi na kutekeleza kwa kupitia dhumuni “A” kwa mpango wa bajeti;

(ii) Vyuo Vikuu kuanzisha Mradi Maalum wa Ukimwi na uwe ni sehemu moja ya upangaji maendeleo ya Vyuo Vikuu; na

(iii) Kuwepo na msukumo tofauti wa huduma za kinga na tiba ya Ukimwi kwa kundi la Watu Wenye Ulemavu kwani mahitaji yao ni ya pekee.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuikumbusha Serikali kuwa kuwepo kwa taa za barabarani, kunachangia sana kuboresha mji au Manispaa yoyote. Hii inafanya mji wote kupendeza hasa wakati wa usiku na kusaidia suala la ulinzi. Hivyo, natoa ombi kuwa fedha za barabara zinazotolewa kupitia Halmashauri ziweze pia kufanya kazi ya kuweka taa za barabarani katika Manispaa ya Singida.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuihabarisha Serikali kuwa, Wakuu wa Idara wengi wanakaa kituo kimoja muda mrefu na hivyo kulewa na mazingira. Mfano, Bwana

Afya wa Manispaa ya Singida na Wakuu wa Vitengo, hospitali ya Wilaya ya Iramba (Kiomboi). Ninaiomba Serikali kufuatilia na kuwahamisha kwani wameolewa na mazingira na hawana tija tena.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninapenda kumalizia kwa kuunga mkono hoja na kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Singida na wananchi kwa ujumla, kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakionesha imani kwangu na kuendelea kunipa ushirikiano. Ni matumaini yangu kuwa watanirudisha tena Bungeni kwa kura za heshima.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, kwa kusimamia kwa umahiri mkubwa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Nawapongeza pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Mheshimiwa Celina Kombani, Naibu Waziri, Mheshimiwa Aggrey Mwanri kadhalika watendaji wote wa Ofisi hiyo, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Maimuna Tarishi, kwa utendaji wa kuridhisha kwa kipindi chote cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2009/2010, Serikali iliahidi kufanya mdahalo kuhusu Serikali kuhamia rasmi Mkoani Dodoma. Mdahalo ambao ungefanyika nchi nzima kwa nia ya kupata maoni ya wananchi. Ninaomba kujua mpango huo wa kufanya mdahalo umeishia wapi na je Serikali bado ina nia ya kufanaya mdahalo katika mwaka huu wa fedha?

Mheshimiwa Spika, nilisoma katika gazeti moja la hapa nchini lililomkariri Waziri wa Nchi, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Marmo, kuwa Serikali kuhamia Dodoma kama Makao Makuu sio rahisi kutokana na gharama kuwa kubwa. Je, kauli hiyo ni kweli? Kama ni kweli, ninaomba Serikali iseme rasmi kwa wananchi ili kieleweke.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Gharama za Uchaguzi. Nashauri Msajili wa Vyama vya Siasa kuelimisha jamii kabla ya uchaguzi na pia sheria hiyo itafsiriwe kwa Kiswahili ili wananchi walio wengi waelewe vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2009/2010, niliomba Serikali kufikiria namna ya kutoa upendeleo maalum kwa Hospitali ya Mkoa wa Dodoma kwa kuleta wataalam kwa mfano Madaktari, Manesi, vifaa tiba na kadhalika kwa kuwa hospitali hii huwahudumia viongozi wa Kitaifa wakati wa mikutano mikubwa inayofanyika mkoani hapa. Naendelea kuleta kilio hiki cha wananchi wa Dodoma kwa Serikali hii Tukufu. Hospitali ipanuliwe, tuletewe Madaktari Bingwa wa kutosha kadhalika na vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, kilio cha kugawa Wilaya ya Kondoa kutokana na ukubwa wake, ni cha muda mrefu. Viongozi Wakuu wa Nchi waliotembelea Wilaya hiyo, walielezwa. Nia na lengo, ni namna wananchi wanavyoweza kupata huduma kwa urahisi na kwa karibu zaidi. Naomba kilio hiki cha wananchi kitekelezwe sasa maana ni cha muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mjumbe katika Kamati ya *POAC,* tulipokutana na Shirika la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, lilijitokeza suala la uwekaji saini makubaliano ya mkopo wa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Sisi Wabunge tulijiuliza, tatizo ni nini, ni nini kinachokwamisha makubaliano hayo yasisainiwe lakini bila kupata majibu. Kama ni kweli, huku ni kuwavunja moyo watendaji. Nashauri suala hili lifuatiliwe na kumalizika kwani siyo suala zito.

Mheshimiwa Spika, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, kwa kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, kwa umahiri/umakini mkubwa. Mungu aendelee kumbariki ili aendelee kuongoza Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi, Naibu, watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri njema wanayofanya hapa nchini. Kwa namna ya pekee, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kupandisha Mji Mdogo wa Nzega kuwa Halmashauri ya Mji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika hotuba ya Mheshimwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 29, kifungu cha 45 na 46, Serikali itaendelea ujenzi wa barabara zinazoendelea na kukamilisha mchakato wa kutafuta wakandarasi wa miradi mipya. Ningefurahi kupata maelezo sahihi ya barabara za Nzega – Tabora km 116 iliyotangazwa April 2010; Tabora – Urambo km 40 na Tabora – Nyahua – Manyoni.

Mheshimiwa Spika, wakulima wengi wa Tanzania, hulima kwa kuzingatia kilimo cha kubahatisha, naomba juhudi ziongezwe kujenga miundombinu ya skimu za umwagiliaji na ujenzi wa mabwawa. Uzito uwekwe katika mabonde mfano bonde la mto Manonga n.k. Aidha, ruzuku ya pembejeo itolewe kwa wakulima wote nchini hasa wakulima wa mahindi walioko Tabora – Nzega na huduma ya mifugo iongezewe mkazo ili kuboresha miundombinu ya malambo, majosho na minada. Napendekeza kubadili mfumo wa uuzaji wa mifugo uzingatie uzito/kilo.

Mheshimiwa Spika, Mashirika ya TRC na ATC, ambayo ni ya usafirishaji wa mizigo na watu, kwa sasa yamedorora sana kiutendaji na ufanisi na hivyo kufanya mdororo wa usafiri hasa katika maeneo ya Mikoa ya Magharibi na pia katika nchi jirani zetu za Kanda ya Maziwa Makuu. Je, kuna ugumu gani katika uanzishwaji wa treni yetu? Ni makubaliano gani mapya yapo baina ya wafanyakazi *(TRC)* na iliyokuwa *TRL*? Ni kitu gani kinachosababisha mdororo wa Shirika la Ndege? Ni mpango gani utafanywa kuinusuru *ATC*?

Mheshimiwa Spika, soko la mifugo yetu bado ni la ubabaishaji na hata kuwapunja wafugaji wetu. Utaratibu wa kununua au kuuza mifugo kwa mnada, ni kwa bei ya kubahatisha. Mazao na hata bidhaa zingine zinauzwa kwa utaratibu unaoelezeka,

napendekeza mauzo yawe ya kutumia mizani (Kilo). Pia ukarabati wa miundombinu ya majosho, malambo, minada na viwanda vya nyama, upewe kipaumbele cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata Halmashauri ya Mji Mdogo wa Ndala na Nata. Nawatakia kheri na baraka katika kazi zenu.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mheshimiwa Phillip Marmo, Mheshimiwa Cellina Kombani, Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Naibu Waziri, kwa hotuba nzuri na kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na ofisi yake katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Aidha, napenda niwapongeze Makatibu Wakuu, Peniel Lyimo na Maimuna Tarishi, kwa kufanya kazi nzuri sana. Nawapongeza pia Manaibu Katibu Wakuu wote wa Wizara zote chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wote wanafanya kazi nzuri sana. Napenda kupitia Bunge hili Tukufu, kuwapa pongezi kwa juhudi zilizotukuka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha uliopita, tuliomba TAMISEMI watusaidie kukamilisha barabara za Kiruche – Mwero – Butu na Msangeni – Chunguli – Butu ambazo uchimbaji wake umekamilika kwa kutumia Shs.1.25 bilioni na zimekamilika lakini hazitumiki kwa kuwa baada ya mvua kubwa za vuli na masika mwaka 2009/2010, ngema zimeziba barabara hizo na sehemu zingine barabara zimekatika. Tumeomba Shs.160 milioni kutoka Mfuko wa Barabara. Naomba sana fedha hizi zitolewe ili barabara hizi zisikae bila kutumika baada ya fedha nyingi kutumika kuzijenga.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu jinsi alivyoniokoa na kuniponya na tukio la majambazi tarehe 16/05/2010 Wilayani Bukombe.

Namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshmiwa Spika, kwa jinsi walivyochukua hatua za haraka kunipeleka kwenye huduma *MOI.*

Mheshmiwa Spika nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri, Naibu Waziri wote Ofisi ya Waziri Mkuu, Katibu Mkuu na watendaji kwa kuandaa hotuba hizi na jinsi wanavyosimamia Serikali vizuri.

Mchango wangu nauelekeza katika maeneo yafuatayo; kwanza ni kuhusu Kilimo Kwanza. Serikali imefanya vizuri sana katika Wilaya ya Bukombe. Kwa mara ya kwanza Bukombe imepata pembejeo za ruzuku. Nashauri Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka pembejeo Bukombe kuanza mwezi wa tisa kwani zikicheleweshа haiwasaidii wakulima.

Pia Serikali ifanye mpango wa kuanzisha *SGR* ili wanunue mazao eneo hilo, Serikali iweke utaratibu wa namna ya kununua *Power Tillers,* bei za *power tiller*s baadhi

ya maeneo ziko juu sana. Ushauri wangu wa mwisho kuhusu Kilimo Kwanza, pembejeo kwa ajili ya zao la Tumbaku Serikali iboreshe Wakulima wa Bukombe wameteseka sana.

Ombi langu naiomba Serikali ianzishe miradi mingi ya umwagiliaji Bukombe kwani ni mradi mmoja tu mkubwa uliopo wa Bugelenga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu biashara na masoko naomba Serikali iangalie kurekebisha mfumuko wa bei. Je, Serikali ina mpango gani wa kuoanisha bei ya mazao kwa wakulima na bei ya bidhaa madukani?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi bei ya bidhaa madukani iko juu sana je, suluhu yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu awaambie wana Bukombe kwa nini hafanyi ziara Bukombe ili akatoe majibu ya umeme? Hivi ni halali kuomba umeme kila mwaka wa Bajeti? Mheshimiwa Waziri Mkuu anaona ugumu gani kutoa kauli ya umeme Bukombe?

Mheshimiwa Spika, nimejitahidi kuwajibu wananchi kwa kuwaambia mfululizo wa majanga Kitaifa kwa nini Waziri Mkuu (Serikali) isitoe kauli?

Kuhusu madini naiomba Serikali iendelee kuwasaidia Katente wachimba madini – Bukombe.

Mheshimiwa Spika, suala la utawala bora naipongeza Serikali kwa kuongeza Kata, Vijiji, Vitongoji na Jimbo, Mungu aibariki Serikali ya CCM kupitia umahiri wa usimamizi wenu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu polisi Serikali iangalie umakini wa baadhi ya askari wanaopewa madaraka, kwani wapo askari polisi wasio waadilifu, nashangaa kwa nini Serikali haiwachukulii hatua ikiwa ni pamoja na kuwavua madaraka? Kama Serikali inafanya basi wasio waadilifu toka Bukombe huwa hawachukuliwi hatua tofauti na kuhamishwa kwa cheo chake au kupandishwa. Hilo haliwafanyi wasio waadilifu wajue kuwa hata akikosea hapa atahamishwa tu.

Mheshimiwa Spika, pia naishukuru Serikali kukubali kutoa shilingi 315,000,000/= za ujenzi wa barabara ya Maguta – Kabanga – Nyamwiga. Ombi langu kwa Serikali iwahakikishie wananchi wa Bukombe ni lini fedha hizi zitaanza kupelekwa kujenga barabara hiyo? Pia naomba barabara ya Buntubili – Bulega Kakoyoyo – Lulembela waipandishe na kuwa ya Mkoa pamoja na barabara ya Masumbwe – Lugunga – Mbogwe – Uvumwa kwa nini hazipandishwi?

Mheshimiwa Spika, suala la matumizi ya fedha za Serikali, pamoja na miradi kutekelezwa bado matumizi mabaya ni makubwa mno kwenye Halmashauri. Kitengo cha Manunuzi kinasababisha uvujaji mkubwa mno wa rasilimali za Serikali.

Nashauri Serikali itumie Wakala wa Manunuzi wa Serikali kusambaza vifaa kwenye Ofisi zake. Idara ya Ukaguzi iendelee kuimarishwa, kwani baadhi ya Wakurugenzi huwadhibiti wakaguzi wa ndani na kuwaambia waondoe hoja mbaya zisiwafikie Waheshimiwa Madiwani. Idara hii ijitegemee isiwe chini ya Mkurugenzi Mtendaji. Pia Serikali iangalie upya muundo wa bodi ya *tender* kwani ni vizuri Waheshimiwa Madiwani wakawa wajumbe ili kuweka uwazi zaidi pamoja na viongozi wa madhebu.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati wa kuhitimisha awapatie ufafanuzi wananchi wa Bukombe na Watanzania yafuatayo:-

Je, ni lini mradi wa umeme Bukombe utaanza kujengwa? Je, kwa nini Mheshmiwa Waziri Mkuu hataki kutoa kauli juu ya umeme huo? Serikali iko tayari kupeleka pembejeo za ruzuku Bukombe wakati kilimo kinaanza badala ya kupeleka mwishoni mwa msimu? Ni lini Serikali itapeleka *SGR* Bukombe kununua mazao ya wakulima?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inawaambia nini wakulima wa tumbaku juu ya pembejeo? Serikali itaanza lini kutoa fedha za barabara Maguta – Kabanga – Nyahwiga kama tulivyoahidiwa?

Mwisho naipongeza Serikali kwa ufanisi mkubwa wa kuongeza Sekondari Bukombe, Maabara katika Sekondari 23, vyumba 69 na Mabweni katika Sekondari 10. Ombi langu ni kuwa mtusaidie vifaa kwenye maabara hizo ili kuwatia moyo Wanabukombe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwani utendaji wa Serikali ni mzuri.

**MHE. DR. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri Mkuu na kumshukuru kwa uongozi wake na Ofisi yake na pia kwa kusimamia shughuli za Serikali nzima, Mungu ampe afya njema.

Napenda vilevile kuwapongeza Mawaziri na Naibu Waziri walio chini ya Ofisi yake kwa kazi nzuri pamoja na wataalam na watendaji chini ya Makatibu Wakuu wote wawili.

Mheshimiwa Spika, suala la fidia ya wananchi baada ya mji wa Katesh kuwa mji umegeuka kuwa wa kisiasa na umeleta chuki kati ya wananchi na Serikali hata na Mbunge. Kiasi cha fidia kimeletwa Ofisi yako (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) ili tuweze kupewa *Special Fund* kwani hata katika Bajeti ya Wilaya iliondolewa ili kukidhi haja ya *ceiling* iliyowekwa.

Tafadhali sana naomba muisaidie Halmashauri kwani wananchi walilalamika wakati Mheshmiwa Rais na Mheshimiwa Makamu wa Rais walipotembelea Wilaya. Nakumbuka suala hili lililetwa kwako na wananchi pamoja na *DED* waliomba usaidie. Natanguliza shukrani.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ambayo imeainisha mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi pamoja na kutoa dira ya utekelezaji kwa kipindi cha mwaka 2010/2011. Aidha, nimpongeze sana kwa utendaji uliotukuka katika kumsaidia Mheshimiwa Rais na kuwatumikia Watanzania kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, nimpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote kwa hotuba nzuri na uhodari wao wa utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa njia ya pekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi yake nzuri ya kuiongoza Serikali ya Awamu ya Nne kwa mafanikio makubwa

ambayo yanaonekana kwa mfano uboreshaji wa huduma za jamii kwa kiwango kikubwa, miundombinu, mawasiliano, kilimo na ulinzi na usalama pamoja na utulivu wa kisiasa uliopo.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imepata mafanikio makubwa ya kiuchumi na nyanja nyingine za maendeleo kutokana na ushirikiano mkubwa uliopo kati ya wananchi na Serikali yao. Hii inadhihirishwa na jinsi wananchi wamechangia kwa hali na mali ujenzi wa madarasa ya shule za msingi na sekondari na ujenzi wa zahanati na vituo vya afya pamoja na kuchimba barabara katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio ya maendeleo napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuwawezesha wanawake kwa vitendo, ikidhihirishwa na jinsi ambavyo amewateua wanawake katika nafasi mbalimbali kama majaji wanawake, wakuu wa mikoa, wakurugenzi na kadhalika. Aidha, Mheshimiwa Rais amesaidia sana uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Tanzania na bado ameendelea kuisaidia kwa kutoa maelekezo kwamba benki iendelee kupewa ruzuku na Serikali kwa nia ya kuiimarisha benki yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi naomba nizungumzie changamoto chache ambazo zinakuwa kero kwa wananchi wa Morogoro Vijijini kama ifuatavyo:-

Kwanza ni elimu, naomba tuongezewe walimu katika shule za kata ya Tegelero, Kidugalo, Tonungwa na Mkulasi.

Mheshimiwa Spika, walimu wengi sana wamerundikana mjini. Naomba wapunguzwe wapelekwe vijijini hususan shule za kata ya Tegelero.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara, kata ya Tegelero haina barabara. Hivi sasa wananchi wanachimba barabara kwa mikono yao. Naomba Serikali iwasaidie kulipua mawe na miamba pamoja na kuwasaidia madaraja na mitaro ya maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara hii utasaidia sana kuboresha masoko ya mazao na uboreshaji wa huduma za jamii, kwa mfano walimu wanakimbia kutokana na matatizo ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la afya wananchi wamejenga zahanati na vituo vya afya lakini vingine vimefungwa kwa sababu hakuna wahudumu na dawa. Naomba hili liangaliwe kwa jicho la huruma kwani vifo vya wanawake wajawazito na watoto vimeongezeka katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masoko ya mazao. Katika maeneo ya milimani kuna maeneo mengi ambayo sasa wananchi wamekata tamaa ya kulima kwa sababu ya ukosefu wa masoko. Kwa mfano katika Kata ya Tegelero wananchi wameacha kutunza mashamba ya karafuu, mdarasini na hiliki kwa sababu hakuna wanunuzi na sababu kubwa ikiwa ukosefu barabara.

Kuhusu maji, maeneo mengi hayana maji kabisa au maji wanayopata siyo ya kiwango cha kutumiwa na binadamu. Maeneo mengine kama Mkulabi lambo pekee lililokuwa chanzo cha maji limebomoka. Naomba hilo lambo lifanyiwe matengenezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mawasiliano maeneo ya Mkulabi, Tonungwa na Kiloka hakuna mtambo wowote wa simu. Eneo la Kiloka limezungukwa na mlima Ng'allo

ambako mvua nyingi kumekuwepo na matukio ya ajali na ujambazi na na waathirika wanashindwa kuomba msaada kutokana na kutokuwepo kwa mtandao wa mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, suala la ulinzi na usalama pamoja na kuwepo kwa vituo vya polisi lakini hawana usafiri hivyo wanashindwa kutoa huduma kama inavyotarajiwa. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aangalie uwezekano wa hawa askari kupata angalau pikipiki moja kwa kila kituo hususan Ngerengere na Mkuyuni.

Mheshimiwa Spika, changamoto ni nyingi lakini nilizoona kuwa ni kero kubwa ni hizo nilizozizungumzia. Naomba wahusika wazione na wazipe uzito unaofaa kwani eneo la Morogoro Vijijini bado limebaki nyuma kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. USSI AME PANDU:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na yenye matumaini kwa Watanzania, lakini pia ni hotuba ambayo inatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muungano nataka kuchukua nafasi hii kuupongeza Muungano wetu ambao umedumu na umekuwa ni mfano katika Bara la Afrika, pia nipongeze juhudi za Serikali zote mbili ambazo bado vikao vinafanyika na kuendelea kutatua kero mbalimbali kwa maslahi ya Muungano huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Chuo cha Sayansi ya Bahari Buyu Zanzibar, nikiwa kama Mbunge na kazi moja ya Mbunge ni kuisimamia Serikali jinsi inavyofanya kazi zake. Ujenzi wa Taasisi hiyo ya Sayansi ya Bahari ambayo ujenzi wake sasa umesimama kwa muda mrefu na mkandarasi tayari ameshaondoka kwenye *site* hiyo, baada ya Serikali kushindwa kutoa pesa kwa ajili ya ujenzi huo, lakini pia Serikali ilishindwa kutoa dhamana ya mkopo kutoka *CRDB* ambao wao kama benki walikuwa wako tayari kukopesha fedha kwa ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri Mkuu kama msimamizi Mkuu wa shughuli za Serikali unasemaje kuhusu ujenzi huo ambao sasa umeachwa na fedha nyingi za walipa kodi zimeshapotea?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati wa majumuisho kupata jibu au ufumbuzi wa tatizo hilo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri Mkuu.

Kwanza naishukuru Serikali kwa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kiwango kikubwa. Je, Waziri Mkuu ni kwa nini Wizaya ya Habari, Utamaduni na Michezo zisigawanywe? Kwa kuwa katika ukurasa wa 48, umezungumza habari tu, utamaduni haukuwa na la kusema. Sanaa ya nchi hii inatambuliwa inapotumika tu, lakini haina kipaumbele Serikalini. Je, ni kwa nini mpaka sasa hakuna Bodi ya *COSOTA?* Je, baada ya tamko la Waziri Mkuu, Serikali imesema kiasi gani? Na fedha hizo zimefanya nini?

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuweka kipaumbele Kilimo Kwanza lakini pia kwa kutoa ushuru wa mafuta ya alizeti na mashudu, hivyo naomba kuhusu mikopo ya pembejeo za kilimo kama trekta masharti yapunguzwe kwa kuwataka wawe

na ekari 50 au zaidi kwa pamoja kwani wengi walioungana wanakuwa na mashamba yalioko mbali mbali, hayakuungana.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa ajira kwa vijana kwani zilitamkwa ajira milioni moja lakini ukiwahesabu vijana wa pikipiki tu nchi nzima na bajaji wanaweza wakafika milioni moja hivyo lengo limetimia na zaidi. Nashauri waendesha pikipiki, wawe na leseni.

Pia napongeza jeshi la polisi kwa utendaji kazi wake japo kwa hali ya mazingira magumu hivyo naiomba Serikali itoe kipaumbele kuwapatia usafiri wa kutosha, mfano Singida gari ni moja tu na hata Mheshimiwa Waziri Mkuu ulipotembelea Singida gari za *escort* ziliharibikia njiani.

Mheshimiwa Spika, gari ya Dodoma ilipotupokea nayo ikaanza kutoa moshi, ilibidi iegeshwe pembeni. Tafadhali naomba kama tumepunguza kununua magari kwenye sekta zingine fedha hizo ziangalie polisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu afya, naomba pikipiki za miguu mitatu mwaka huu zinunuliwe isiwe kwa maneno ili zisaidie kuwaokoa wanawake wajawazito kufika kwa haraka kwenye vituo vya afya. Ahsante

Mheshimia Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kuwa mzima.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe, Naibu wako na Wenyeviti wote kwa jinsi mnavyoliendesha Bunge kwa viwango.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kuhusu pembejeo za kilimo, wananchi wengi hasa wa vijijini hawapati pembejeo na wakipata basi si kwa wakati kwa hiyo, ili kufikia lengo la kilimo kwanza ni lazima tuwafikie wananchi wote hasa katika ile mikoa ya *"big 4"* ili waweze kulima kwa uhakika na kupatikana chakula.

Vile vile tuwaandalie wananchi masoko ya uhakika ili hicho Kilimo Kwanza na pembejeo zinazotolewa zilete faisa kwani tukitoa pembejeo nyingi na hakuna masoko mazao yote yataharibikia shambani na Kilimo Kwanza kitakua hakileti faida yoyote. Naiomba vile vile Serikali iwaandalie miundombinu ya uhakika ili wananchi wayafikie masoko hayo.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana watoa hoja hii. Nashukuru sana. Ahsante.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, dhana ya Kilimo Kwanza KiBajeti haikupewa msukumo stahaki. Kutengwa jumla ya shilingi 103,957,371,00/= kwa maendeleo kati ya shilingi 253,335,014,000/= kwa Bajeti yote kwa kweli ni mzaha na kweli tunacheza na uhai wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, Kilimo Kwanza, kama hilo halitoshi, kati ya fedha hizo zilizotengwa za maendeleo ni shilingi 3,916,109,000/= ni fedha za ndani na shilingi 100,335,662,000/= ni fedha kutoka nje. Ni dhahiri kuwa Kilimo Kwanza ni ndoto za mchana.

Mheshimiwa Spika, hivi nani asiyejua tatizo la fedha za wafadhili na upatikanaji wake kuwa ni janga? Ni mara ngapi fedha ama hazipatikani kwa wakati au hazipatikani

kabisa? Tanzania lazima tujifunze tuache kuweka Bajeti hasa ya kilimo na kutegemea wafadhili.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni kila kitu, kwa Watanzania ni uchumi, ajira, elimu, matibabu, viwanda na kadhalika na kama hayo hayatoshi, kilimo ni uhuru na utawala! Nchi omba omba haziwezi kuheshimika, haina uhuru wa kutosha, haipaswi sekta ya kilimo kuwekwa pembeni na kupuuzwa kwa mtindo huu wa dhana ya Kilimo Kwanza na mapunduzi ya kijani haitakuwepo, yatakuwa kwenye makabrasha na mikutano ya hadhara tu.

Mheshimiwa Spika, hivi nani hajui kuwa viwanda ni kilimo, nani hajui kuwa mifugo ni kilimo, nani hajui kuwa misitu ni kilimo, nani hajui kuwa muhimili wa maisha kwa kila binadamu ni chakula na chakula ni kilimo? Nani hajui kuwa kilimo ni chakula na chakula ni afya, na afya ni utawala, na kwa kweli ndio unaotuweka hapa?

Mheshimiwa Spika, askari, sio jeshi, polisi, Waziri, Katibu Mkuu na kadhalika hata mimi na wewe kama nchi itaingia njaa hakuna atakayebaki ofisini au atakayekuwa tayari kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, hebu kama hatuoni basi hata kusikia, vipi leo Misri (nchi yenye jangwa), Israel, Libya zinazolisha na kujitosheleza kwa chakula na kuuza nje? Sisi Tanzania tuna kila neema tuliyojaaliwa, ardhi nzuri je, zaidi ya hekta milioni 44 ni nzuri kwa umwagiliaji na kilimo kwa ujumla wake. Sisi tunalima chini ya asilimia 13% tu. Nchi yetu ina mifugo ya kutosha, maji, kwa maana ya mito, mabwawa na hata mvua zinanyesha kwa vipindi muafaka. Nini tunataka? Maji tuliyonayo mfano ya Ziwa Victoria ndio yanayoneemesha nchi za Kaskazini na Jangwa la Sahara, sisi tunabaki watizamaji.

Mheshimiwa Spika, mimi haya ni moja ya mchango wangu, Serikali ijipange tena kuzidisha Bajeti ya kilimo na iandae mpango thabiti wa kuunganisha programu za kilimo na ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, lingine ni sekta ya uvuvi, sekta hii ni muhimu sana si kwa lishe tu, bali hata kiuchumi. Uvuvi unaajiri si chini ya Watanzania milioni 14 kwenye ukanda wa Pwani/Bahari, nguvu ya bahari kwa maana ya kutoa samaki inapungua. Ni vyema wananchi wakawezeshwa kupatiwa zana kwa uvuvi wa maji makuu na utaalamu wa usindikaji samaki viwandani, sio hivyo tu, bali wafundishwe ufugaji wa samaki wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, uvuvi si ajira bali ni lishe ya kutosha kwa binadamu, pia ni moja ya pembejeo kwenye viwanda vya kutengenezea chakula cha kuku. Ahsante.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi nyingi kutokana na kazi nzuri inayofanywa na Serikali yetu, naomba Bajeti ya mwaka 2011/2012 itilie maanani masuala yafuatayo:-

Kwanza kupambana na umaskini. Mkakati mzuri wa kupambana na umaskini ni ule unaoelekeza mapambano katika maeneo yaliyo maskini. Hivyo rasilimali kubwa zitengwe katika maeneo husika, kwa mfano Jimbo la Mwibara ndilo lililo maskini zaidi, lakini rasilimali zinazotolewa kwa ajili ya kupambana na changamoto zake ni kidogo sana.

Pili, tutengeneze mfumo wa uwajibikaji kuanzia ngazi ya tawi, kata hadi wilaya ili kuhakikisha kwamba rasilimali zinazotolewa zinafanyakazi na kuleta matokeo yaliyolengwa. Mfumo uliopo sasa hautasaidii na badala yake unachochea rushwa na ufisadi. Tatu, tuwachukulie hatua za kinidhamu pamoja na za kisheria watendaji mafisadi na wala rushwa ili kulinda rasilimali zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya wananchi.

Mheshimiwa Spika kuhusu utawala bora na wa sheria, kwanza tufanye maamuzi mara moja hasa pale ambapo hapahitajiki rasilimali kama fedha ili kurahisisha utendaji kazi na uwajibikaji. Pili, tufanye mabadiliko ya kimfumo katika Jeshi la Polisi na Mahakama zetu ili kuondoa dhuruma, unyanyasaji, rushwa na ufisadi. Tukumbuke kuwa wananchi wa vijijini ambao ndiyo wengi wanapata shida sana wanapokwenda kupata haki zao kwa kutumia vyombo hivi viwili vya dola.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa TAMISEMI, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na wengine wote walioandaa hotuba hii. Aidha, naipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa kazi kubwa iliyofanya kwa kusimamia kazi nyingi ambazo zimeonekana kwa macho kwa mfano Chuo Kikuu cha Dodoma, ujenzi wa shule za sekondari za kata na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Dr. Jakaya Kikwete, kwa jitihada zake binafsi za kuiongoza nchi hii kwa mafanikio makubwa kwa amani, usalama na utulivu. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusimamia kazi za maendeleo ya wananchi, kwa muda mfupi alikaa kwenye nafasi hii, lakini vile vile kuonesha uwezo mkubwa na umahiri aliouonesha kwenye kutekeleza wajibu wake. Vile vile nalipongeza Baraza la Mawaziiri na Mawaziri wote, kwa kuwajibika vyema kila Waziri na Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, nawaombea kila Waziri, Naibu Mawaziri na Wabunge wote wakachaguliwe na warudi tena Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie yale ninayoona. Kilimo kwanza, naamini kilimo kwanza ni kilimo cha kufuata kanuni za kilimo kwa kutumia pembejeo za kisasa na kupata mavuno mengi kutoka kwenye eneo dogo kwa mfano eka moja kuzalisha magunia zaidi ya 30.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu elimu zaidi itolewe kwa wananchi/wakulima, kuwepo na usimamizi kwa wananchi kupatiwa mikopo hiyo ya kununua pembejeo. Pia mashamba darasa yawe mashamba makubwa badala ya kulima vishamba vidogo ambavyo havina matokeo makubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mifugo tunaishauri Serikali iongeze jitihada katika kuboresha ufugaji ili wananchi waondokane na uchungaji waingie kwenye ufugaji wa kisasa ili mifugo hii iwapunguzie umaskini na waweze kupata tija. Pili, wafugaji wapewe elimu ya ufugaji bora ili waweze kuelewa umuhimu wa ufugaji bora kwani wakielewa ni rahisi kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi, naipongeza Serikali kwa mipango mizuri ya matumizi ya ardhi na hasa ile ya kujenga nyumba za viwango tofauti na hasa zile za kiwango cha chini na watauziwa wananchi wa hali ya chini. Tunaiomba Serikali iongeze idadi ya kujenga nyumba hasa kwa Mji wa Dodoma

kwani watu wengi wanahamia Dodoma wakiwepo watumishi wa vitengo mbalimbali vya Serikali, Vyuo Vikuu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyuo Vikuu, tunaishukuru Serikali kwa kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma kwa muda mfupi na kuchukua wanafunzi zaidi ya 15,000. Ombi langu ni Serikali iangalie kukipandisha daraja Chuo cha Mipango kuwa Chuo Kikuu Kishirika cha Chuo Kikuu cha Dodoma. Vile vile kipo Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo na Chuo cha Madini, Serikali vipandishwe daraja. Pamoja na Chuo cha Kukata Nyama nacho kiboreshwe ili kitoe wanafunzi wengi waweze kuhudumia maduka ya nyama.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru kwa kupandisha kiwango cha posho ya Waheshimiwa Madiwani, hata hivyo naiomba Serikali kuongeza ifikirie suala la kuwakopesha madiwani ama gari au pikipiki.

Mheshimiwa Spika, wenyeviti wa vijiji, tunaomba Serikali ifikirie posho ndogo kwa ajili yao kwani hawa ndio wachapakazi wakubwa. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja ya hotuba ya Waziri Mkuu katika kuleta Bajeti yake ndani ya Bunge hili Tukufu. Naipongeza hotuba hii wakiwemo yeye mwenyewe Waziri Mkuu, Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Naibu Waziri TAMISEMI Mheshimiwa Aggrey Mwanri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watoto kukaa chini katika shule za msingi nchini, nitoe pongezi kwenye Wizara ya Elimu kwa kujenga madarasa mengi na mazuri, kuingiza wanafunzi/watoto wengi darasa la kwanza, kwa asilimia kubwa. Tatizo lililopo watoto hao huanza shule na hukuta madarasa tupu yasiyo na madawati na wala vitabu vya kuanzia shule. Mtoto aanzapo shule kwa kukaa chini, si rahisi akaweza kuandika vizuri mara apatapo dawati baadae.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuwa nchi yetu inayo misitu ya Serikali inayoridhisha kabisa ikiwemo misitu kwa mfano Buhindi, Sengerema Mwanza au misitu iliyoko Mkoa wa Iringa pale Njombe na mingine nchini. Kama misitu hiyo ingetumika vizuri kwa *operation* maalum (muda maalum) kungetengenezwa madawati ya kutosha na watoto wetu wangetoka chini na kukalia mdawati. Fedha katika shule zetu za msingi wanazo na hata pesa za matengenezo wanazo. Hivyo naishauri Serikali ilichukue wazo hili ikibidi hata kwa awamu hadi zoezi kukamilika, naamini inawezekana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya kilimo kwanza ni sehemu ya hakika kuondoa umaskini wa wananchi wetu hususani wa vijijini. Ninapotafakari kuhusu jambo hili najiuliza maswali mengi, miomgoni mwa maswali ninayojiuliza ni pamoja na kwa kiasi gani wakulima wadogo wadogo wa vijijini kama Kilimanjaro ambao wengi wao wanamiliki vihamba/mashamba yenye ukubwa wa nusu eka mpaka eka 2 hadi 5, wanaokuwa na kuhamasika kuhusu kilimo kwanza? Eneo la kutosha liko wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi gani wako tayari kubadili kilimo cha mazoea kwenye vihamba vyao? Je, wakielekezwa na kufundishwa kanuni bora za kilimo wako tayari kuzitekeleza? Mfano, kung'oa migomba na kuotesha miche bora ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, ukitembea katika mkoa, utaona wakulima wachache wadogo wanaovuna mavuno ya kutosha kutoka vishamba vidogo. Jambo la kusikitisha ni kwamba wako majirani wa wakulima wa aina hii ambao hawatunzi vihamba vyao au mifugo yao vizuri na uzalishaji wao ni kiwango cha chini sana hata haitoshelezi chakula chao.

Mheshimiwa Spika, wakulima ninaowazungumzia hapa wanajulikana kama wakulima wadogo wadogo na kilimo chao ni cha kujikimu ni jinsi gani wataelemishwa na kuhamasishwa ili watoke sasa kwenye kilimo cha kujikimu na wajihusishe na kilimo kwanza? Wizara ya Kilimo na Ushirika ikitekeleza nguzo nyingine za kilimo kwanza bila kuwahamasisha wakulima wadogo hadi waamue kutumia mtaji wao wa nguvukazi na akili zao kwenye kilimo, hatutaweza kuwabadili.

Mheshimiwa Spika, wakulima wadogo ambao hawajaamsha ari ya kubadili maisha yao kwa kuboresha kilimo chao, wanapopewa msaada wa ruzuku ya pembejeo, wanauza vocha wapate fedha. Wakulima waliohamasika wako tayari kuandamana hadi ofisi yoyote kudai stahili zao za ruzuku ya mbegu, mbolea au dawa.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuwepo mpango wa uhamasishaji na tutengewe fedha za uwezeshaji. Napendekeza Wizara ya Kilimo na Chakula ishirikiane na TAMISEMI kuandaa na kutekeleza programu maalum ya kubadili mtazamo wa wakulima wetu wadogo vijijini kuhusu kilimo. Wakulima hawa wakishaandaliwa na kuwa tayari kubadili kilimo chao cha sasa, ndipo wataalam wa ugani waliowezeshwa vizuri wawasaidie kilimo chao kiwe na tija.

Mheshimiwa Spika, programu ya kubadili picha ya kilimo kwenye vichwa vya wakulima wadogo itakuwa na gharama zake, lakini gharama hizi ni za lazima na hazikwepeki. Hizi ni za lazima ili kilimo kwanza kifanikiwe.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipata nafasi hii. Kwanza kabisa napenda nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika, kwa kazi nzuri unayoifanyua ya kuliendesha Bunge kwa kasi na viwango.

Pili, nimpongeze Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri Mkuu kama manahodha wa nchi yetu kwa utendaji wao mzuri wa kazi ambao umewezesha kuifikisha Awamu ya Nne salama kipindi cha uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, naendelea kumwomba Mwenyezi Mungu azidi kuwapatia ninyi viongozi wetu afya njema ya roho na ya mwili pamoja na sisi wananchi ili tuweze kuendeleza vizuri kazi ya utumishi na kuidumisha amani.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa mambo mengi makubwa ambayo imeyafanya kwa kipindi cha miaka mitano ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Daraja la Umoja, ujenzi wa barabara ya Kibiti - Lindi, uanzishaji wa mfumo wa stakabadhi ghalani, pamoja na kutunga sheria mbalimbali. Lakini hata hivyo mafanikio yatokanayo na jitihada za Serikali hayawagusi wananchi walio wengi kutokana na kasi kubwa ya ongezeko la watu. Kutokana na hilo napenda sasa nianzie mchango wangu kwa kutoa ushauri katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naishauri Serikali ielekeze nguvu zake kwenye kitengo cha uzazi wa mpango ambao utasaidia kupunguza vifo vya uzazi pamoja na kudhibiti kasi ya ongezeko la watu. Pili, Serikali ijaribu kutumia uzoefu wa mikakati waliojiwekea hospitali ya Mkoa wa Dodoma, mmojawapo ni kuboresha maslahi ya wauguzi ambapo takwimu zinaonesha kuwa hospitali hiyo imefanikiwa kwa kiasi fulani kupunguza vifo vya uzazi. Uzoefu wa hospitali ya Dodoma usambazwe katika mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu mwingine ni kuiomba Serikali ijitahidi sana kuwafuatilia wale watendaji wanaokwamisha maendeleo kwa kuchanganya utendaji na siasa, kweli hili ni tatizo kubwa na lina athari hasa kwa maendeleo ya wananchi. Suala hili linaweza kuwa ni sababu mojawapo ya kushindwa kuzitumia rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna tatizo ambalo ni kero kubwa kwa wananchi wengi. Baadhi ya mamlaka za Serikali zimeshindwa kutimiza ipasavyo wajibu wao kwa jamii kwa kiasi ambacho imebidi baadhi yao kufuatilia stahili zao katika ofisi ya Waziri Mkuu. Malalamiko ya wananchi ni kwamba mamlaka husika wakati mwingine zimekuwa hazijibu barua na pengine kuwapiga dana dana wale wanaofuatilia haki zao pasipo mafanikio kwa muda wa miaka kadhaa.

Aidha, wananchi hawa wamenituma nimpe shukrani na pongezi nyingi Mheshimiwa Waziri Mkuu kwani ofisi yake imekuwa makini na imekuwa ikitatua matatizo yao kwa muda mfupi na kwa kiasi kisichotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, barua zimejibiwa kwa ukarimu kwa muda usiozidi wiki moja, wenye kupunjwa mafao walilipwa kwa maelekezo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, pia kero nyingine mbalimbali zilipatiwa ufumbuzi, hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pamoja na pongezi hizi naishauri Serikali izifuatilie mamlaka zinazoshindwa kutimiza wajibu wake kwa wananchi kwani baadaye wananchi wanaweza kukatishwa tamaa kwa tabia hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho ningeishauri Serikali iweke utaratibu wa kuwapongeza watendaji wanaofanya kazi nzuri na kuwapa karipio wale wanaoshindwa kutimiza wajibu wao kwa uzembe. Taarifa za kila mwezi kutoka halmashauri zetu zifuatiliwe kwa makini ili matatizo yatatuliwe mapema. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, napongeza hotuba na kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uanzishwaji wa Halmashauri ya Igalula, taratibu zote kuanzia wananchi wa Jimbo hadi vijiji, kata hadi halmashauri na mkoa wanaunga mkono uanzishwaji wa halmashauri hiyo, maelekezo yote kuhusu uanzishwaji umekamilika na taarifa zote zimeletwa TAMISEMI. Wananchi wanasubiri hatma yake kwani sasa ni miezi nane tangu taarifa iletwe; na ni ofisi yako tu inangojewa kutoa tamko baada ya kuifanyia kazi. Ulipotembelea Kijiji cha Kigue Jimboni Igalula, ulilikuta suala hili na ukasema, tuendelee na taratibu zote limefikia wapi suala hili?

Mheshimiwa Spika, tamko la wafanyakazi wa reli ya kati kuwa Serikali iliwambia tarehe 15 Juni wataanza kazi ya treni ya abiria, leo ni tarehe 18 Juni vipi?

Kuhusu ujenzi wa majengo ya zahanati, yamekamilika mengi lakini hayafanyi kazi na yameanza kuharibika si chini ya miaka mitatu sasa, wafanyakazi hawajapelekwa, lini wafanyakazi watapatikana na ukarabati huo wa majengo utafanywa na nani kwani wananchi walikwishachangia 20% yao katika ujenzi huo. Nawasilisha.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu nzima kwa yote waliotufanyia. Hongera sana na ninawaombea afya njema, maisha marefu Serikali yote ya Awamu ya Nne ambayo inaongozwa na Rais wetu kipenzi, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana kwa yote waliyofanya nikitaja machache kama upande wa elimu za sekondari, kweli Jimbo langu lilikuwa na shule za sekondari mbili tu wakati Awamu ya Nne ikichukua madaraka nami nikiwa Mbunge wa Jimbo. Lakini kwa uongozi wa Awamu ya Nne, nami nikiwa Mbunge wa Jimbo la Bukene, tukishirikiana na wananchi wa Jimbo la Bukene, tumeweza kujenga shule kila kata katika kata kumi na sita za jimbo, ukitoa zile zilizokuwepo mbili yaani shule ya sekondari ya Kilina, shule ya sekondari ya Itobo. Zile zingine 16 tumejenga kwa ushirikiano, nami nimetoa matofali ya chumba kimoja kwa kila kata.

Mheshimiwa Spika, tunachoomba hapa ni walimu, tuna upungufu wa walimu. Kuna shule zingine zina mwalimu mmoja tu. Kwa matumaini sana kwani Roma haijajengwa siku moja, basi naamini Serikali itatuletea walimu angalau wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi nimesemea barabara ambazo ahadi za Rais katika barabara ya kutoka Tabora/Maambali/Bukene/Itobo/Bukwimba/Kahama. Hii pia ni barabara iko kwenye T.3 ikifika Nzega lami inaishia, inaingia kwenye kiwango cha changarawe. Nashukuru kwa ahadi ya Rais, hongera sana kwa utekelezaji huo wa ahadi.

Mheshimiwa Spika, naomba barabara hizi hasa ile *T3* toka Dar es Salaam itoke Nzega kwenda Kahama kupitia Itobo/Bukwimba iwe ya lami ni kipande kidogo sana. Pili, ile inaendelea toka Itobo/Bukeni/Maambali/Tabora nayo iwe ya lami. Naomba sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme wa kutoka Nzega/Bukene. Naipongeza na nashukuru sasa kazi imeanza, ila watu wanasema danganya toto. Naomba hitimisho liwepo tupate *'live'* umeme ili kuwafanya wananchi wawe na imani zaidi na Serikali yao na wapinzani wetu wakose la kusema. Ni kipande kidogo sana kilomita 48 tu jamani, hebu Serikali ifumbe macho ilete umeme yaani ihitimishe. Tuna Igembesabo ambayo inashindwa kukoboa mchele na hali tuna mashine, sababu umeme. Naomba sana hitimisho ili nasi tujikwamue kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa bwawa kubwa la Kahama ya Nhalanga/Mogwa. Nashukuru ingawa kuna matatizo ya aliyepewa *tender*, lakini najua tutafanikiwa na wananchi wanangojea hitimisho tu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru zaidi kwa maji katika vijiji kumi kwangu viko sita na kazi imeanza kule Sigili, Buhundo, Ikindwa, Itobo, Mwamala, Nawa na Mahene.

Mheshimiwa Spika, naomba nipatiwe halmashauri na baadaye wilaya. Wilaya yetu na halmashauri ziko kata 37, nyingi mno. Tunaomba nasi tujipikie wenyewe Bukene.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wananchi wangu na nawaomba wakati muafaka ukifika, tushirikiane kwa kunirudisha ili niweze kuendelea kuwawakilisha. Najua wengi wanapitapita sasa hivi, ila waamini wanajua, mume anakuja wakati wa *Xmas* tu na mume uliye naye siku zote nani anawafaa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa sungusungu kunipa ukamanda mkuu, nami nimewapa pikipiki mbili ambazo wanafanya kazi pamoja na polisi jamii yaani pikipiki hizi zinasaidia kwenye doria. Nafurahi sana na hongera kwa ushirikiano huo.

Mheshimiwa Spika , naomba kuwasilisha.

**MHE. HALIMA M. MAMUYA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuanza kuunga mkono hoja hii ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na kumpongeza yeye na watumishi wa ofisi yake kuanzia kwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa kusimamia kazi za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nauelekeza katika maeneo mawili moja ni yale niliyotumiwa na pili ni ushauri wangu kwa Serikali kama nilivyotumwa na wananchi wa Arusha na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, wanawake wa jamii ya wafugaji wamenituma kuiomba Serikali kuwakumbuka na kuwapa nao *stimulus package* kutokana na wao kuathirika kwa ukame uliotokana na mabadiliko ya hali hewa. Ukame huo ulisababisha njaa na vifo vya mifugo. Wanawake hawa wanaishukuru sana Serikali kwa chakula na wanaomba *stimulus package* hiyo ili waweze kurudi tena katika harakati za kupambana na umaskini.

Wananchi wa Arusha wanataka kujua kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu ni lini Serikali itapanga kujenga Hospitali ya mkoa kwani *Mount Meru Hospital* ilikuwa ni hospitali ya manispaa ya Arusha na kwa sasa imezidiwa na hospitali na vituo vya afya 263 ambavyo vyote vinaitegemea.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Arusha mjini wanataka kujua Serikali imetenga kiasi gani kwa matengenezo ya barabara za mjini ili kupunguza msongamano wa magari na kupata barabra zenye hadhi ya jiji.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Arusha wanataka kauli ya Serikali katika kufufua viwanda vilivyo Arusha nini hatma ya kiwanda cha *General Tyre?* Kimeuzwa au kitaendeshwa na Serikali?

Maombi binafsi ni kuwa namuomba Waziri Mkuu katika kuhitimisha hotuba yake atoe agizo kuwa sasa maafisa mipango miji wasiguse maeneo yote ya wazi pamoja na makaburi na vilima vyenye uoto wa asili vinavyozunguka miji ili vibaki kama vilivyo na wasibadilishe matumizi yake ili yabaki kama *green areas.*

Naomba Serikali ibuni mikakati wa kudumu ya kuwa na mfuko wa hifadhi ya mazingira badala ya kutegemea fedha za wafadhili tu katika hifadhi ya mazingira. Mfuko huu usaidie pia katika kufidia wanaoathirika na matokeo ya mabadiliko ya hali ya hewa.

Naomba Serikali itafute njia au utaratibu wa kuonyesha kiasi cha mchango wa wananchi katika miradi ya maendeleo ambayo imepangiwa fedha za Serikali na wafadhili

ili kuweza kuwaonyesha wafadhili mchango wa wananchi na kuwatia moyo Watanzania kuwa wao ni wafadhilli wakubwa wa maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba majibu.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, tunaomba barabara ya Mbande - Kongwa – Mpwapwa iwekwe lami.

Kuhusu elimu, upungufu wa nyumba za walimu ni mkubwa sana pia madawati na kuna uhaba mkubwa sana wa vitabu vya ziada na kiada. Walimu wa shule za sekondari haba sana.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa afya kwa maana ya manesi na madaktari ni wachache sana, tumejenga zahanati na baadhi hazijafunguliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miiji midogo, mji mdogo wa Kongwa haujawa *operational* mji mdogo wakati Kibaigwa umeanza, miji midogo nchini itengewe Bajeti kipekee ili kuondosha mamlaka hizo.

Mheshimiwa Spika, suala la maji, vijiji zaidi ya 40 kati ya 85 bado havina chanzo chochote cha hakika cha maji salama. Kuhusu kilimo, tunahitaji mbegu ya mtama mapema kabla ya msimu.

Mheshimiwa Spika, hali ya ukame na njaa inaendelea kwa wilaya ya Kongwa kwa mwaka 2010. Kuanzia Septemba mwaka huu patahitajika chakula cha njaa.

Mheshimiwa Spika, mgao wa kata na vijiji, kwa mgao ujao wa kata naomba kata zifuatazo zianzishwe, Banyibanyi, Laikalo, Ibwaga, Mbande, Tubugwe, Mseta na Ndalibo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa utendaji mzuri wa kazi.

Kwa kuwa katika halmashauri nyingi kuna ubadhilifu na matumizi mabaya ya fedha na madaraka na mara nyingi watendaji hao wanapofanya makosa hayo wanahamishwa na kupelekwa kwenye halmashauri nyingine ni kwa nini watendaji hao waendelee kufanyakazi badala ya kufukuzwa au kuachishwa kazi kwani kuendelea kuwahamisha kutoka kituo kimoja kwenda kingine ni kulea uozo, kama ni wasomi wako wengi siku hizi.

Mheshimiwa Spika, suala la ujambazi, hali bado sio nzuri pamoja na jitihada za Jeshi la Polisi na Serikali kwa ujumla kupambana na ujambazi. Niliwahi kuzungumzia jambo hili wakati nikichangia Bajeri ya mwaka 2006/2007 na nikaomba Serikali iangalie uwezekano wa kutumia vikosi vyetu vya ulinzi kusaidiana na polisi kupambana na uhalifu huu, kwani hivi sasa silaha ziko nyingi sana mtaani tena za kivita unaweza kuporwa simu au mkoba na mporaji anatumia bastola lakini wanaoporwa majumbani na hata barabarani ni wengi na waporaji wanatembea kwa makundi na kufanya uhalifu huo tatizo linaloonekana ni uchache wa askari polisi.

Naiomba tena Serikali iangalie uwezekano wa kutumia vikosi vya ulinzi kupambana na majambazi yaliyokithiri Kinondoni na nchi nzima. Naunga mkono hoja.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imezingatia hali halisi ilivyo sasa kiuchumi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuongoza ni kuonyesha njia, nawashukuru sana Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri Kiongozi, Mheshimiwa Shamsa Vuai Nahodha, Katibu Mkuu wa CCM, Mheshimiwa Yussuf Makamba, Mawaziri na viongozi wote katika ngazi ya Mkoa na Wilaya ambao kwa nyakati tofauti walitembelea Jimbo la Mikumi kutuonyesha njia ya kutekeleza majukumu ya kujiletea maendeleo kwa michango ya wananchi pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nawashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Mikumi kwa kunichagua Mbunge mwaka 2005. Heshima hii nitaienze daima, nafurahi kutamka kutokana na ushirikiano wao, pamoja tumefanikiwa kutekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2005 kwa kiwango kikubwa kama ifuatavyo, shule nyingi za msingi na za sekondari na kwa kiasi nyumba za walimu zimejengwa.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa vituo viwili vya afya vya Ulaya na Mhovu katika tarafa za Ulaya na Mikumi umefanywa pamoja na ujenzi wa Wodi ya Wazazi katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Waziri Mheshimiwa Celina Kombani aliahidi Bungeni kuwa maombi ya magari ya kubebea wagonjwa kwa vituo hivi viwili lilikubaliwa mwaka jana hivyo naomba wakati wa kuhitimisha hoja yake Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 vituo hivi vitapewa kipaumbele kupatiwa magari yaliyoahidiwa.

Kituo cha Afya cha Mikumi kilipandishwa hadhi kuwa Hospitali mwaka 2008, inaitwa Hospitali ya *St. Kizito,* tunaishukuru sana Serikali kwa sasa hospitali hii inahitaji sana jokofu la kuhifadhia miili mitano ya watu wanaofariki. Hii ni kutokana na kuhudumia zaidi ya wagonjwa 100,000 katika tarafa ya Mikumi na pia kutokana na ajali nyingi zinazotokea katika barabara nne zinazokutana Mikumi.

Mheshimiwa Spika, usalama ulioboreshwa kwa Serikali kutoa gari mbili, moja mpya kwa kituo cha Polisi Mikumi na moja chakavu kwa kituo cha Polisi Kilombero kilichopo katika eneo la kiwanda cha sukari cha Kilombero tunaishukuru sana Serikali lakini ujambazi wa kutega magogo katika barabara umeongezeka sana. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iongeze gari moja la kuaminika kituo cha Polisi Mikumi ili kuimarisha ulinzi hasa nyakati za usiku.

Mheshimiwa Spika, Serikali imewezesha *TANESCO* kupeleka umeme katika kata tatu za Mabwerebwere, Masanze na Kilangali ambapo kata nne za Zombo, Ulaya, Kisanga na Malolo zimeingizwa katika mpango wa kusambaza umeme vijijini. Tunaishukuru sana Serikali kwa hatua hizi za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji, naishukuru sana Serikali kuridhia kutoa shilingi milioni 60 kwa ajili ya kuchimba visima virefu vinne katika mji mdogo wa Mikumi, napenda Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitia Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Maji na Umwagiliaji aliyetoa ahadi hii alitaarifu Bunge lako na wananchi wa Mikumi wasikie ni lini uchimbaji wa visima hivi utaaanza?

Kuhusu kilimo cha miwa wananchi wanaipongeza na kuishukuru Serikali kwa kuwajali kwa kufuta *VAT* kwenye usafirishaji wa miwa kwenda kiwandani, shukrani zao zitajionesha katika uchaguzi ujao.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa kukubali hoja niliyoitoa ya kupima upya mipaka baina ya mbuga ya wanyama ya Mikumi na vijiji vyote vinavyopakana na vyuo hususan vijiji vya Mikumi, Lumango, Ruhembe, Kihelezo, kidogo basi na Kitate. Upimaji huu utaondoa utata na ugomvi usioisha baina ya wanavijiji na askari wa hifadhi. Nampongeza sana Mheshimiwa Chiligati kwa kulipa umuhimu mkubwa suala hili kwa faida mtambuka za kulinda rasilimali misitu na wanyamapori zitapatikana kupitia utalii kuimarika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizi nawapongeza *TANAPA* kwa misaada mbalimbali iliyotolewa kwa vijiji mbalimbali, ujenzi wa shule, ujenzi wa maabara, lakini pongezi halisi ni kwa Serikali inayoiongoza *TANAPA* kwa kuyatenda hayo.

Mheshimiwa Spika, kama ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 iliyoainishwa kuwa barabara ya Mikumi - Kilosa itafikia hatua ya usanifu yakinifu wa kina ingefikiwa hivi sasa! Hatua hii ndio uliyofikiwa sasa, naipongeza Serikali na kuiomba ijitahidi kutafuta fedha ili ujenzi uanze mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mawasiliano ya simu katika jimbo ni kata tatu tu kati ya kata 12 jimboni ambazo hazina mawasiliano ya simu za mkononi, naiomba Serikali iwashawishi makampuni ya simu kupeleka mawasiliano katika kata hizi tatu zilizobaki ili mtandao wa mawasiliano uwezeshe ufanisi mkubwa wa shughuli mtambuka za kimaendeleo na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha changamoto nilizopokea kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Mikumi kama ifuatavyo:-

Kwanza, Serikali inaombwa kuwalipa kifuta jacho kwa wahanga waliohamishwa milimani katika kijiji cha Ruaha, kutokana na ahadi ya Serikali Wilaya ya Kilosa iliyopitia Afisa Mwandamizi wa Halmashauri ya Kilosa aliyewaahidi wahanga hao kuwa makubali kuteremka toka milimani kwa vile Serikali ingewalipa fidia akawapa fomu za kujaza mali zao na mimea, na wakashuka, kilichofuata hawakulipwa chochote licha ya kupelekwa maeneo mengine yenye mafuriko kulima jambo ambalo liliwatetea hasara inayowatesa mpaka sasa kwa kukosa makazi. Naishauri Serikali itoe hata *a token offer* ya kuonyesha Serikali inajali matatizo yaliyowapata.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya *LAAC* imebaini kuwa Serikali haijalipa sehemu yao ya mchango wa pamoja na mwekezji aliyenunua Kiwanda cha Sukari Kilombero uliopaswa kutumika kukamilisha malipo kwa wafanyakazi waliopunguzwa kazi mwaka 2000. Kwa kuwa nimepewa kero hii na wafanyakazi nilipowatembelea hivi karibuni, naiomba sana Serikali iwaondolee mnuno mkubwa uliopo katika jamii kwa kuliacha

suala hili kwa miaka mingi. Nitajitahidi kulifuatilia lakini, namuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati akihitimisha hotuba yake atoe tamko kuhusu hatima ya malipo haya.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kata za Ulaya, Zombo, Kilangali, Mawawe na Mabwerebere wanaiomba Serikali yafuatayo, kwanza nini hatma ya tathmini ya Serikali kuhusu orodha ya mashamba yaliyotelekezwa kwa miaka mingi ambayo inawanyima ushiriki kamilifu katika kutekeleza kilimo kwanza?

Mheshimiwa Spika, nini muongozo wa Serikali sasa kuhusu kuyatengeneza maeneo ya wakulima na wafugaji kupitia sheria mbili za maeneo ya malisho kwa mifugo na ya chakula cha mifugo kupitishwa? Tatizo lililopo ni kwamba hivi sasa wafugaji wameongezeka sana kiasi wameingia hata katika hifadhi za misitu ya Ukwira.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilosa iliomba igawanywe tangu miaka mingi iliyopita, je wazo hili limefutwa au ni lini uamuzi utatolewa ili kusogeza karibu zaidi huduma kwa wananchi ili ufanisi katika utekelezaji wa majukumu uongezeke?

Mheshimiwa Spika, jamii ya kijiji cha Ruaha, watu binafsi na hasa wafanyakazi wa Kampuni ya Sukari Kilombero wameniomba niiulize Serikali kuwa katika ubinafsishaji wa kampuni na rasilimali zake za majengo, shule iitwayo Malecela Sekondari *(form I - form IV)*na majengo yake yote yalijengwa kwa michango ya wafanyakazi na sasa wawekezaji wameiuza shule hiyo, nini hatma ya michango yao ambayo ndiyo iliyojenga shule hiyo? Na ni kwa sababu zipi wawekezaji hawakujulishwa kuwa shule ya Malecela ya Sekondari imejengwa kwa nguvu za wafanyakazi?

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya mchango huu naomba kurudia kuunga mkono hoja na kumuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa matamko kwa maeneo niliyomuomba afanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya na hivyo kushiriki katika kikao cha leo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu, viongozi wa chama changu cha *CUF (The Civic United Front)* pamoja na viongozi wetu wa Kambi ya Upinzani hapa Bungeni kwa kutuongoza vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kukupongeza wewe, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge vizuri. Halikadhalika, nampongeza Waziri Mkuu pamoja na Watendaji wote walioko chini yake kwa kuandaa na kuwasilisha bajeti hii hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya amani na utulivu na kazi ya Jeshi la Polisi ni kulinda raia na mali zao. Hivi karibuni kumejitokeza matukio ya raia wema kuvamia Vituo vya Polisi na kuumiza baadhi ya askari, lakini pia na Polisi kuchukua hatua mikononi kiasi cha kuwaumiza raia na hata vifo vya raia kutokea mikononi mwa Polisi. Je, Serikali inasema nini kuhusu matukio ya namna hii? Je, Serikali haioni

kwamba hali hii ikiendelea hivi hivi ile amani na utulivu uliopo unaweza kutoweka na hivyo kuleta maafa makubwa kwa pande zote?

Mheshimiwa Spika, katika Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliopelekea kupatikana kwa Tanzania kulikuwa na mambo 11, lakini yameongezeka hadi kufikia mambo 22. Je, kutoka mambo 11 hadi 22 ya Muungano kulichukua muda mfupi, ni kwa nini kupatikana kwa ufumbuzi wa kero za Muunganzo kunachukua muda mrefu kiasi kwamba wananchi wanaanza kukata tamaa? Mfano ni mgao wa 4.5 ambao hadi leo haujapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar ina mfuko wake wa fedha kwa mambo ambayo sio ya Muungano. Je, Tanzania Bara inatumia mfuko gani kwa mambo ambayo sio ya muungano?

Mheshimiwa Spika, hali ya uchumi katika miaka ya 80 ilikuwa juu kwa wananchi wa Zanzibar na chini kwa wananchi wa Tanzania Bara, lakini kadri miaka inavyokwenda, hali imekuwa kinyume chake, yaani wananchi wa Zanzibar wanashuka na wa Tanzania Bara wanapanda (Uchumi wao unaongezeka au kipato kwa kila mwananchi). Je, Serikali ya Muungano inaona hali hii na ina mpango gani kuisaidia Zanzibar iweze kunyanyua kipato kwa wananchi wake?

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeingia katika mageuzi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii na katika mfumo wa ukweli na uwazi *(Truth and Transparency).* Pia imeingia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa, lakini Katiba inayotumika ni ile ile ya chama kimoja. Wakati umefika sasa kuwa na Katiba mpya ambayo ni *"flexible"* (yenye kubadilika) kuendana na wakati badala ya kuendelea na Katiba ya sasa ambayo ni *"rigid"* (isiyo badilika) wakati nchi imeingia katika mageuzi mbalimbali kama nilivyokwishaeleza hapo juu.

Mheshimiwa Spika, katika chaguzi zilizopita, vyombo vya dola vilikuwa vikiegemea na kukisaidia sana Chama Tawala na hivyo kuwanyanyasa na kuwadhalilisha wafuasi wa vyama vingine vya siasa hasa kule Zanzibar. Je, Serikali imejiandaa vipi kuhakikisha kwamba Uchaguzi Mkuu wa 2010 unakuwa huru na wa haki na kwamba wananchi wote watakuwa katika hali ya amani na usalama na kuweza kuitumia haki yao bila ya uzalishaji au ukandamizwaji wa aina yoyote?

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mazingira gani kwa wawekezaji ili dhana ya Kilimo Kwanza iweze kutekelezeka na hivyo kutuwezesha kupata chakula cha kutosha kupata ziada ya kuuza nje na kuweza kukuza uchumi? Serikali inasema nini kuhusu usindikaji wa mazao mbalimbali badala ya kuuza kama mali ghafi au kuyaacha yakaoza mashambani?

Mheshimiwa Spika, tatizo la wakulima na wafugaji limepatiwa ufumbuzi gani katika maeneo mbalimbali hapa nchini ili kuondoa mapigano na mauaji baina ya wakulima na wafugaji?

Mheshimiwa Spika, kujenga mashule katika maeneo mbalimbal hapa nchini ni hatua moja muhimu, lakini kuwa na walimu wa kutosha na wenye sifa ni muhimu zaidi, pia kupatikana kwa vifaa vya kufundishia na kusoma ni muhimu sana. Serikali imejipanga vipi kukabiliana na matatizo haya ili lengo liweze kufikiwa?

Mheshimiwa Spika, mafao ya wastaafu yaangaliwe upya na yatolewe kwa wakati kwani wastaafu wanadhalilika sana wakiwa wameitumikia nchi hii kwa imani kubwa.

Mheshimiwa Spika, wanaolipa kodi katika nchi ni kama watu 1,570,000 kati ya mamilioni kadhaa ya Watanzania. Serikali inapaswa kuwa makini zaidi katika suala zima la kukusanya kodi hapa nchini.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naomba nipate maelezo kuhusu Barabara ya Nyambiti – Malya.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuendelea kupongeza hotuba hii nzuri. Kwa maana nyingine, nakupongeza wewe, Mawaziri wako, Manaibu Mawaziri wako, Makatibu Wakuu na wale wote ambao wameshiriki katika kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchangia kwa kuongea, bado nina haya machache. Kwanza, naomba sana tujitahidi kwa njia yoyote ile hata ya *BOT* ifunguliwe barabara ya Bagamoyo – Saadani - Pangani. Hii barabara ni muhimu sana kwa sisi watu wa mwambao hasa baada ya hii barabara ya Tanga – Hororo kujengwa. Utalii wa ufukweni na hata kibiashara pia itapunguza msongamano wa barabara hii moja tunayotumia wote Dar es Salaam – Arusha, Dar es Salaam – Tanga.

Pili, naomba wenzetu wa *NMB* wajaribu kuona angalau kila Makao ya Wilaya kama hakuna Tawi basi kuwe na *ATM*. Natoa mfano Utete – Rufiji, Mlandizi – Kibaha Vijijini, lakini pia hata Ikwiriri.

Mheshimiwa Spika, lingine naomba sana tena sana pamoja na matatizo yote ya fedha, tujitahidi kila tutakapopata fedha kidogo tujenge, tujitahidi kila tutakapopata fedha kidogo tujenge mabweni Shule za Sekondari za Wasichana. Hii naamini itapunguza hizi mimba kwa wasichana wetu. Sisi kama wazazi, tupo tayari kushiriikiana kama tunavyoshirikiana kwenye madarasa na nyumba za waalimu.

Mwisho, naomba tena tufikiriwe kupewa mji mdogo Kilindoni Mafia. Tunashukuru kwa Kata mpya mlizotupa Mkoa wa Pwani. Tunaamini maendeleo yatakuwepo na Mungu akipenda tutakua pamoja kushirikiana kuona tunasaidiana kwenye ujenzi wa Taifa letu. Ahsante, nakubali tumefanya mengi, sina sababu ya kuwa na wasiwasi wa utendaji wenu.

Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, Kilimo Kwanza ni tumaini kubwa kwa maendeleo ya nchi yetu. Ni tegemeo kubwa kwa ajili ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania na hasa wakulima wenyewe.

Wananchi wa Mkoa wa Lindi na Wilaya zake hususan Kilwa wana kero za muda mrefu hasa katika zao la ufuta na korosho, ambapo hivi sasa wafanyabiashara walikuwa wakinunua ufuta kwa bei ya Sh. 1,300/= toka kwa wakulima. Lakini hawa wanunuzi wa bei hii wamezuiliwa watakuwa wakulima kwa lazima wauze ufuta wao kwa Chama cha

Ushirika kwa Sh. 700/= kitu ambacho wakulima hawataki na wamediriki kufanya maandamano siku ya Jumapili ya tarehe 13 Juni, 2010.

Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alirekebishe suala hili, kwani wanunuzi hawa wanapata vibali toka Halmashauri ya Wilaya na ni maamuzi ya *Full Council,* kwa nini uongozi wa Mkoa unalazimisha? Kilimo Kwanza ni kwa ajili ya kumnufaisha nani? Sh.1,300 ni bora zaidi ya Sh. 700/= ya Chama cha Ushirika. Wakulima wetu hawatendewi haki.

Mheshimiwa Spika, Mwanasheria wa Serikali wa Halmashuri kama hawawezi kutoa maamuzi sahihi, hana faida ndani ya Halmashauri husika. Ni sawa na kutokuwa na Mwanasheri huyo.

Mwanasheria wa Halmashauri wa Wilaya ya Kilwa ameshindwa kuona ukweli wa kutoa uamuzi wa Wajumbe watatu batili ambao wameteuliwa kinyume cha sheria. Mmoja wa viti maalum alikuwa ndani ya kifungo, na wajumbe waliobaki hawakuwa na sifa za kuteuliwa kulingana na maelezo ya vifungu vya sheria, wao sio Wajumbe wa Halmashauri, ni wajumbe waliookotwa, sio kisheria.

Mwanasheria alisema malalamikio haya yapelekwe Mahakamani, kwani hana uwezo nayo. *RAS* naye alisema malalamiko ni sahihi, lakini haziwezi siasa za Kilwa. Nilimweleza Mheshimiwa Waziri wa Tamisemi kwa mdomo (ana kwa ana) akanishauri nimwandikie, lakini hadi leo hii ni kimya. naomba ufumbuzi wa suala hili.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Kilwa ni vurugu tupu. Kuhusu mapato Halmashauri hii ina vyanzo vingi vizuri vya ukusanyaji wa mapato. Mapato haya yanapokusanya Vijiji huvuka lengo kuliko yakikusanywa na Mawakala wawekwao na Halmashauri. Hivi sasa wanataka kuvinyang’anya kwa vile hawapati mwanya wa kuziiba fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, ninashauri kwamba yule akusanyaye mapato zaidi na kuvuka lengo la makisio ndiye anayefaa. Pia nawashari waitupie jicho Halmashauri hii kwani vyanzo vya mapato vingine ni siri ya Watendaji na haviko wazi, mfano kiwanda cha Pweza Kilwa Kivinje kifanyiwe ukaguzi maalum.

Mheshimiwa Spika, kuna matumizi mabaya ya fedha za Serikali kwani Mganga Mkuu wa Hospital ya Wilaya Kilwa Kivinje ana zaidi ya mwaka sasa anaishi hotelini wakati nyumba ipo na ipo safi iliyokarabatiwa. Nashauri ashauriwe kwenda kuishi katika nyumba hiyo ili kuokoa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuiendeleza miradi ya *TASAF* lakini kuna tatizo moja ambalo naomba lifanyiwe kazi. Mnamo mwezi Desemba, vijiji vipatavyo vinane vilipata fedha ambazo walikuwa wameomba baada ya kuibiwa miradi. Cha kushangaza, Vijiji hivyo vilipoingiziwa fedha hizo na walipokwenda kupata ruhusa ya kuzichukua ili waendeleze miradi yao waliyoibiwa, waliambiwa kwamba wazitoe fedha hizo na kuzirudisha TASAF kwani zililetwa kwa makosa na sio zao. Kwa hiyo, fedha hizo zilirudishwa TASAF Wilayani kukiwa na maswali kadhaa. Nilifuatilia na nilielezwa amri ilitoka Mkoani.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza zaidi baada ya maswali mengi, fedha hizo hadi wakati naelekea katika Kamati tarehe 24 Mei, 2010 fedha hizo zilikuwa bado katika *account* ya *TASAF* ya Wilaya bila maelezo. Naiomba Serikali ilifanyie uchunguzi suala hili ili kuona fedha hizi zilipotea vipi hadi zikaingia katika *account* za vikundi vinane vya Wilaya ya Kilwa? Ni kwanini hadi leo hazijapelekwa kwa wahusika?

**MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake inayotoa mwelekeo na hatua ambazo Serikali inachukua kuimarisha uchumi pamoja na kupambana na umasikini na uboreshaji wa huduma za jamii. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Nchi TAMISEMI, kwa juhudi zake za kusimamia shughuli za Tawala za Mikoa na Serikali ya Mitaa. Nampongeza pia Mheshimiwa Philip Marmo Waziri wa nchi anayesimamia masuala ya Bunge na Sera kwa umakini wake katika eneo hili.

Mheshimwa Spika, nami napenda kuchangia mawazo yangu kwenye eneo la usimamizi na usafi wa mazingira katika miji yetu.

Mheshimiwa Spika, hali ya usafi katika miji yetu hairidhishi, watendaji kwenye Halmashauri mbalimbali wamekuwa wepesi wa kujitetea na kutoa sababu kadhaa za kutokutekeleza wajibu wao, lakini kimsingi sababu hizo hazitoshelezi, kwani hayo wamefanya vizuri na mafanikio yameonekana. Mafanikio hayo wala siyo kwa sababu wamekuwa na vitendea kazi vingi, bali ni kwa ajili ya kusimamia na kuzingatia sheria zao ndogo ndogo wanazotunga. Usimamizi huo ni pamoja na kutoa adhabu kwa wanaovunja hizo sheria.

Hivyo basi, ili Halmashauri zote zitekeleze wajibu wao ningependekeza Ofisi ya Waziri Mkuu ifikirie namna ya kutoa adhabu kwa Halmashauri zinazofanya vibaya kama ambavyo zawadi zimekuwa zikitolewa kwa zile zinazofanya vizuri. Bila kuchukua hatua kama hiyo, hatuwezi kufanikiwa. Mafanikio yanaweza kupatikana iwapo nia ipo. Mfano mzuri ni hivi majuzi Jiji la Dar es Salaam lilipokuwa mwenyeji wa Mkutano wa Uchumi Duniani *(World Economic Forum)* Jiji likawa safi, lakini cha kusikitisha baada ya ugeni ule hali imerejea kama awali.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais, ilielekeza kuajiriwa kwa Maafisa Mazingira kwa Halmashauri zote na Wilaya zote, lakini cha kukatisha tamaa ni kwamba bado baadhi ya Wilaya na Halmashauri hazijatekeleza agizo hilo bila ya sababu yoyote ya msingi. Badala ya kuajiri Maafisa Mazingira wamekamilisha kazi hizo kwa Maafisa wengine walioajiriwa kwa nafasi nyingine.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa taka ngumu umeendelea kwa kero na hali ya kwenye madampo ni mbaya. Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa kanuni kadhaa za usimamizi wa taka ngumu lakini bado Halmashauri zimeshindwa kusimamia utekelezaji wake, kwa mfano suala la kutenganisha taka pale zinapozalishwa bado halijafanyiwa kazi. Aidha, ofisi ya Makamu wa Rais imetayarisha kanuni za kudhibiti kelele mijini *(noise pollution).* Tunaomba Halmashauri ifuatilie na kuwabana wale wanaosababisha kelele hizo ikiwa ni pamoja na kupiga miziki usiku kwa sauti kubwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea na maandalizi ya *"Enviroment Master Plan"* kwa Jiji la Dar es Salaam, Mwanza na Arusha. Ni matarajio ya Ofisi kuwa mpango huu unaoandaliwa kwa msaada wa Serikali ya Korea utakuwa chachu na kuigwa na Miji mingine.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa hotuba zao nzuri. Pia nachukuwa nafasi hii kuishukuru Serikalli ya Chama cha Mapinduzi kwa kuinua hadhi ya Kata ya Makongorosi Wilayani Chunya kuwa mamlaka ya mji mdogo. Kitendo hiki kinasogeza maendeleo karibu na wananchi. Sasa baada ya kuwa Mamlaka ya Mji mdogo kuna Baraza la Wenyeviti wa Mitaa na hilo Baraza lina Mwenyekiti wake. Hii ina maana kuwa ile *W.D.C* ya Kata haipo tena na Mheshimwa Diwani hana nafasi tena kuwa mwenyekiti wa *W.D.C.*

Namwomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI atoe ufafanuzi kuwa katika Uchaguzi Mkuu ujao, tutachagua Diwani pale kwenye Mamlaka ya mji mdogo? Je, huyo Mheshimiwa Diwani akiwapo atakuwa na *role* gani pale kwenye Mamlaka?

Naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, ni juhudi gani za makusudi zinazofanywa kuhakikisha kiwanda cha *General Tyre* kinafufuka? Ni jambo la aibu ukiangalia Serikali ilivyo na magari mengi na tairi (mipira) lazima ibadilishwe kila baada ya kilometa15,000 au kila baada ya miezi sita. Je, kwa magari ya Serikali matairi yake yanatoka wapi? Ni aibu kama yanatoka Firestine ambayo kiwanda hicho ni sawa kabisa na cha *General Tyre* tena chetu kilikuwa kinazalisha matairi yenye ubora zaidi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, *TEMESA* iliwekwa ili kutengeneza magari ya Serikali, kuna tatizo gani, hivi majuzi tulisikia magari ya Mheshimiwa Rais kule Moshi yaliwekwa *diesel* chafu? Je, vile visima vilivyojengwa kila Mkoa kwa ajili ya kujaza mafuta magari ya Serikali vimekwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na mabadiliko ya hali ya hewa kwa sababu ya tabia nchi. Cha kusikitisha, Askari Polisi hapa Dodoma mpaka leo bado nyumba za baadhi yao ni zile zinaoitwa *(Full suit),* zimejengwa kwa bati kuanzia juu mpaka chini, ukizingatia hapa Dodoma jinsi jua linavyowaka, hivi askari huyu jioni yeye na familia yake walale usiku mzima ndani ya fukuto hili halafu tutegemee aje kazini afanye kazi yake kwa ufanisi? Ni lini Askari hawa watajengewa nyumba za uhakika? Ni aibu kwa Serikali kwa kutowajali askari hawa ambao hata vyoo na bafu za kutosha hawana.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam ni kioo cha nchi yetu, lakini ni kitu cha aibu kwa Serikali kushindwa kusimamia usafi wa Jiji letu. Moja, magari yote yanayozoa taka yanatakiwa yapelekwe kwenye vyuma chakavu kwa sababu badala ya kuzoa taka huwa yanasambaza taka na hii inapelekea magonjwa ya mlipuko kutoisha katika Jiji. Hivi kuna tatizo gani Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuja katika Manispaa ya Moshi mjini chini ya uongozi wa Mbunge wa pale Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, imekuwa ikiongoza kwa usafi na hata kupata tuzo duniani, wajue wajifunze.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa ajili ya kusambaza *net* kwa ajili ya kuzuia ugonjwa wa Malaria, lakini Serikali inatakiwa iende zaidi kwa kutafuta ni jinsi gani ya kuuwa mazalia ya mbu.

**MHE. SHOKA KHAMISI JUMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima wa afya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hotuba ya Waziri Mkuu ni kuwa amezungumzia mambo mengi sana lakini mimi nitaongelea baadhi tu ya mambo hayo. Kwanza, nitaanza na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni chombo muhimu sana na kinachotakiwa kutoa haki sawa kwa wote na kisiwe na upendeleo wa aina yoyote. Kuhusu uchaguzi wa mwaka wa 2010, Tume ya Taifa ihakikishe kuwa inatoa matokeo ya uchaguzi haraka iwezekanavyo ha kusiwe na sababu yoyote kuwa kura zimeshahesabiwa, lakini zisifanyiwe majumuisho mpaka siku ya pili hasa kwa Majimbo madogo madogo kama vile ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, tunaisifia Marekani kwa kutoa matokeo mapema na ilhali na sisi kwa baadhi ya maeneo tunaweza kufanya hivyo kama nilivyoeleza hapo juu.

Mheshimiwa Spika, kwanini Tume ya Taifa ya Uchaguzi isiandikishe wapigakura wake wa Jamhuri ya Muungano na badala yake inatumia wakala (Tume ya Uchaguzi) ambaye amehakikiwa na kukutwa kuna wapiga kura hewa laki moja? Uchaguzi unapoharibika, Zanzibar vile vile unaharibika na Bara kutokana na ubovu wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, napenda niongelee kuhusu kuhamia Dodoma. Kuhusu kuhamia Dodoma mimi naona tutachukua muda mrefu kwani tokea tulipoanza kutaka kuhamia Dodoma mpaka leo inasikitisha kwamb mpaka leo hii bado hatujahamia Dodoma. Sasa ikiwa bado hatujawa tayari kwanini hatubadilishi misimamo tukabaki Dar es Salaam? Kwani kubaki Dar es Salaam kuna ubaya gani ? Ahsante.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunilinda hadi kufikia siku ya leo. Nazidi kumwomba azidi kunirefushia baraka ya kuendelea kuishi kwa miaka mingi zaidi ijayo. Aidha, ninamwomba Mwenyezi Mungu awaongezee baraka ya kila mmoja wao maisha marefu na baraka ya maendeleo kwa Jimbo letu la Kwimba.

Pili, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Awamu ya Nne kwa ujumla kwa mafanikio yote yaliyopatikana kwa kipindi chote hiki tangu uongozi wake uingie madarakani. Napenda zaidi kuipongeza Serikali ya Awamu hii kwa mafanikio yote yaliyotokea katika Jimbo langu la Kwimba. Nampongeza pia kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wapigakura wangu Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote walioko chini ya Wizara yake kwa utekelezaji mzuri wa mipango na maazimio kama yalivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, matokeo yake yakiwa ni baadhi ya mafanikio hayo, baadhi yake ni haya niliyoyataja hapa chini ndani ya Jimbo langu.

(1) Maji ya mradi wa maji kutoka ziwa Victoria kufikishwa katika Jimbo langu hususani katika Tarafa ya mwanashimba, mradi ambaio unaendelea kutekelezwa hadi leo.

(2) Mradi wa umeme sasa unaojadilika wa kufukisha umeme Hungumalwa, Ilula hadi Shilima na maandalizi yake yanaendele vyema.

(3) Kielimu, Kata zote kila moja ina Shule ya Sekondari na baadhi zina shule mbili na tayari Jimbo lina shule za *"A" level* mbili, moja ya wavulana na moja ya wasichana na shule hizi zimefanya vyema japokuwa bado hazijapata walimu wa kutosha.

(4) Katika kipindi hiki, tangu mwaka 2006 Zahanati saba zinakarabatiwa na huduma zake za utaoji wa huduma kuboreshwa.

(5) Barabara nyingi mpya zimejengwa, nyingine zimekarabatiwa na barabara mbili kupandishwa daraja kutoka kuwa za Halmashauri na kuwa za Mkoa.

Mheshimiwa Spika, mambo haya ndiyo yananitia moyo mimi na wapigakura wangu kuwa CCM bado ni chama cha watu tena watu wengi wanahitaji na kinawajali. Mafanikio haya ndiyo yawapayo nguvu wapigakura wangu kushawishika na kusema hadharani kuwa watakichagua tena chama hiki katika uchaguzi ujao iwapo kitafika kuwaomba ridhaa ya kuongoza tena. Watakichagua kwa kuyatimiza mengi kilichowaahidi na kuamini kuwa kitaendelea kutekeleza haya na mengine mengi kikipewa fursa.

MheshimiwaSpika, katika michakato mbalimbali ya mambo kukutana na changamoto, matatizo ni jambo la kawaida kabisa. Changamoto yaweza kukufanya ubadilishe mbinu au kucheleweshа mipango yako ulivyokuwa umejipangia. Kubadilisha mbinu au kucheleweshа mipango siyo lazima kuitwe kushindwa. Aidha, kukutana na changamoto katika mchakato wa utekelezaji wa jambo ni jambo la kawaida kabisa. Itokeapo ni vyema ikafanyiwa tu uchaguzi, kama ni kosa la kibinadamu linasameheka, kama ni uzembe nao ukatafutiwa dawa. Dawa bora ni kupewa fursa nyingine ili lengo lengwa liweze kufikiwa kwa manufaa ya wengi. Ni imani ya wananchi wengi kuamini kuwa yaliyoelekezwa ni mengi na malengo yalikuwa mazuri, ni vyema yakafikiwa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa ofisi kubwa kama hii ya Watendaji mbalimbali wenye maadili tofauti tofauti na malezi mbalimbali siyo rahisi wote kuwa na roho safi ya uadilifu. Ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote walio chini yake ni kuwaangalia mara kwa mara watumishi walio chini yao. Baadhi yao siyo watumishi bora. Ni vyema kila wanaogunduliwa na udhaifu wawekwe pembeni kwa kuwa wanaharibu sifa nzuri ya viongozi walioko juu. Sio vyema mtumishi akahamishwa katika Halmashauri ya Wilaya tatu, nne, hata tano tena kwa kashfa akaendelea kubaki katika ajira na kuendelea kupandishwa nyadhifa.

Aidha, wakati umefika wa kuziangalia upya kanuni za utumishi na taratibu za kuthibitisha. Inavyoelekea, wanaotegemea huduma ya mtumishi hawana nafasi ya moja kwa moja ya kuchangia katika kumtathmini mtumishi anayewahudumia. Mwenye uamuzi wa tathmini ya kazi ya mtumishi sio vyema sana akawa mtu ambaye hahudumiwi na mtumishi huyo. Nafasi itolewe tena ya kutosha kwa mpokea huduma.

Naunga mkono hoja hii, ninawatakia Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri na Watendaji wote kheri.

**MHE. MUSTAPHA H. MKULO:** Mheshimiwa Spika, tumepata taarifa kuwa Wilaya ya Kilosa itagawanywa na kwamba kutazaliwa Wilaya mpya ya Gairo. Taarifa hii bado haiko rasmi. Uamuzi huu unamaanisha kuwa Kata ya Dumila, Magole, Magubike, Mamboya na Berega zitakuwa katika Jimbo la Gairo Wilaya ya Gairo. Kwa hiyo, Jimbo la Kilosa litapungukiwa na Kata tano. Katika kikao cha *RCC* iliamuliwa kuwa Kata za Masanze, Kilangali, Mabwerebwere na Zombo zihamishiwe Jimbo la Kilosa pamoja na Kata ya Msowero.

Nashauri kuwa uamuzi huu uwe rasmi, utangazwe ili Tume ya Uchaguzi ibadili mipaka ya majimbo ya Kilosa na Mikumi katika itakayokuwa Wilaya mpya ya Kilosa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia kwa asilimia mia moja.

**MHE. ABASI Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tena kupongeza hotuba ya Mheshimiwa Mkuu na Waziri wa Tamisemi na wafanyakazi wote na wa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchangia kwa mdomo, lakini nimeona mambo muhimu niyaandike ili niyape uzito wake. Tatizo la fidia kwa eneo la Kurasini, Mtaa wa Kurasini, Mtaa wa Kiungani na Mtaa wa Mivinjeni kuna tatizo la fidia na tatizo la watu kutopewa viwanjwa kama walivyoahidiwa. Tatizo hilo Wizara wanalijua na tatizo kubwa kwa sasa liko Ofisi ya Katibu Mkuu toka achaguliwe Katibu Mkuu wa sasa, zoezi hili kama limesimama.

Mheshimiwa Spika, naomba lipewe uzito wa hali ya juu, kinyume cha hapo mimi na chama changu tutakuwa kwenye mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu, ilizungumzia jinsi umuhimu wa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa ni muhimu. Sasa Serikali ikaona umuhimu wa kuhakikisha Wenyeviti na Watendaji wanapata vitendea kazi vikiwepo ofisi, vifaa vya ofisi na usafiri wa pikipiki au baiskeli.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia kwa wananchi wa barabara ya *Kilwa Road,* wananchi wa *Kilwa Road* walifungua kesi mwaka 2004. Tarehe 15 Aprili, 2008 Mahakama ikaamuru wananchi hao walipwe fidia zao kutokana na ujenzi wa Kilwa Road, lakini hadi leo wananchi hao hawajalipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Temeke kwa ujenzi wa barabara ya *Davis Corner* hadi *Jet club*. Tunaomba Serikali iharakishe kulipa fidia kwa wananchi ambao mali zao zinatakiwa zipishe ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha wavuvi Mtoni tunalo tatizo la ndugu zetu wa Tazara kuuza maeneo hadi kusababisha njia za maji kuziba, husababisha nyumba kuanguka na watu wengi kukosa makazi. Niliomba Wizarani waitie kwenye ule mpango wa Kurasini, hatimaye eneo lile liuzwe. Wizara ilikubali, lakini muda umekuwa mrefu na wananchi wa kijiji cha wavuvi wamekuwa wakiishi katika mateso makubwa. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie kulisukuma hilo na Mungu akijalia nafasi, wananchi wa Kijiji cha Wavuvi wanamkaribisha atembelee Kijiji cha Wavuvi.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia suala la uvuvi na wavuvi wadogo wadogo wamekuwa sasa wakichomewa nyavu na vifaa vyao vya uvuvi. Ni wazo zuri, lakini tungeona njia mbadala kwa kusaidia hao wavuvi wadogo wadogo, wangekopeshwa vifaa na nyenzo mbali mbali zinazohusiana na uvuvi kama Serikali inavyofanya kwa wachimbaji wadogo wadogo kwa kuwatengea fungu maalum kuwawezesha katika kazi zao.

Msongamano wa barabara za Dar es Salaam, Mheshimwa Waziri Mkuu, bajeti inaonyesha Serikali imetenga pesa nyingi kwa ajili ya barabara, lakini ni muhimu sasa Serikali ikafanya upendeleo maalum katika bajeti yake ya barabara Mkoa wa Dar es Salaam kama tulivyotoa umuhimu katika Kilimo Kwanza. Pia Serikali ni muhimu katika bajeti hii ikasema neno kuhusu Daraja la Kigamboni.

Mwisho, tunamwombea afya njema Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi - Mheshimiwa Celina Kombani na Naibu Waziri wa Nchi na Makatibu wote pamoja na wafanyakazi wako wote.

**MHE. JOHN M.CHEYO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Peter Kayanza Pinda na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Mheshimiwa Celina Kombani na Waziri wa Nchi - Mheshimiwa Marmo kwa kazi nzuri wanazofanya tangu wameshika madaraka walionayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maoni yangu juu ya hotuba kwa maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatia uzoefu tuliopata kutoka bajeti ya *CAG,* ni vizuri Serikali ikatoa uhuru zaidi kwa Bunge. Napendekeza kama ilivyo bajeti ya *CAG* inaidhinishwa na Kamati ya Bunge kwa kushauriana na Wizara ya Fedha *(Consultative Meeting)* na mara ikikubaliwa, basi Wizara isigeuze. Aidha, utaratibu huu ukubalike pia kwa muhimili wa Mahakama. Jambo hili litatoa uhuru wa uhakika wa muhimili hii kupanga shughuli zao za kutunga na kutoa haki.

Mheshimiwa Spika, katika dhana ya Kilimo Kwanza, barabara Vijijini ni mkombozi na masikini walio Vijijini. Mfano, tunao Bariadi Mashariki kufunguliwa kwa Tarafa ya Gombasingu na barabara la Bariadi – Gombasingu Meatu - Ng’wanhunzi kumeongeza ubora wa maisha ya watu wengi sana na kuchochea biashara kati ya Wilaya ya Bariadi na Meatu. Tunapaswa kutoa kipaumbele kwa barabara Vijijini, kwa Bariadi Daraja la Gamaroha na Kata ya Mhunze na Bukingwaminzi Kata ya Zagaye. Naomba Serikali itusaidie kutupa fedha ya kutosha. Madaraja haya ni muhimu sana kwa uchumi wa huduma ya afya. Mhunze ni wakulima wazuri sana wa pamba na mahindi na wakati wa msimu malori ya mazao hushindwa kusafirishwa kwenda kwenye masoko.

Mheshimiwa Spika, aidha, uzoefu wa matumizi ya fedha kwenye sekta hii ni kuoanisha kufika kwa fedha na masika ya mvua. Nashauri fedha itolewe kuzingatia mazingira ya mvua. Aidha, utaratibu wa Sheria ya Ununuzi uelezwe vizuri kwa sababu siyo lazima hata kwa miradi midogo, mlolongo mrefu wa tenda lazima zifuatwe. Inakubalika kutumia makandarasi wanaojulikana katika Halmashauri kufanya kazi nzuri, huwa ndiyo wachaguliwe kufanya kazi kama wakati muafaka ukizingatia majira.

Mheshimiwa Spika, mimi nimefarijika sana na msimamo wa Rais kwamba yeyote atakayeharibu uchaguzi, atachukuliwa hatua kali za kinidhamu na sheria. Naomba mtazamo huu utekelezwe kwa dhati. Kuharibu uchaguzi kwa uzembe kama vile kununua

shahada, kutojumlisha kura, kutokemea fujo na rushwa kuachiwa kutawala uchaguzi ni mwanzo wa kutokuwa na amani.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea kuhusu bei ya pamba na malipo ya *Cess*. Napenda kuishauri Serikali kwamba bei ya pamba isiwe chini ya Sh. 700/= kwa kilogram, gharama za maisha ni kubwa sana na kwamba ndiyo chanzo kikuu cha fedha cha takiribani watu milioni 10. Shinyanga ni Mkoa ulio chini sana kimapato kwa wananchi Serikali mwaka jana Serikali ilitoa ruzuku ya Sh 80/= kwa kilogram. Jambo hili lilihamasisha wakulima kulima zaidi na kwa hiyo, bei nzuri itawapa hamasa. Kuna kila sababu bei isiwe chini ya Sh. 700/= kwa kilogram, baadhi ya sababu ni kama zifuatazo:-

- Bei ya ulimwengu ni juu na *exchange rate* ni nzuri;
- Mashudu na Mafuta yamesamehewa *VAT ;*
- Tusipo weka bei nzuri, zao la pamba litatoweka na wakulima watalima choroko ambazo sasa zinauzwa kwa bei nzuri sana.

Aidha, Serikali isijivue jukumu la kusaidia kudai *cess* kwa wananunuzi wa pamba. Bila msaada wa kauli kali ya Serikali kuu, Halmashauri haitapata mapato.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu na Waziri wa Nchi (TAMISEMI) kwa kuwasilisha hotuba nzuri na kwa ufasaha. Nampongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Mheshimiwa Philip Marmo, Naibu Waziri - Aggrey Mwanri kwa kuandaa hotuba nzuri ambayo inatoa matumaini kwa Watanzania walio wengi.

Napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne, Serikali ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Serikali ya CCM kwa miradi mingi mizuri iliyotekelezwa kwenye Jamii. Ilani ya CCM imetekelezwa vizuri sana. Wote mmeshuhudia shule nyingi za Sekondari zimejengwa. Serikali imetoa fedha na wananchi wamechangia nguvu zao. Nawapongeza wananchi kwa kuchangia nguvu zao kwenye miradi ya maendeleo kama miradi ya maji, barabara, shule na kadhalika. Shule zilizojengwa ndio zinabeba watoto wetu ambao kama siyo hizo shule, basi wangeishia kuwa vibaka. Watakaohitimu kwenye Sekondari hizi, watakuwa na uelewa kuliko walioishia Darasa la Saba na hawa ndio watailetea maendeleo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma. Ni Chuo kizuri, kikubwa kuliko vyote Kusini mwa Sahara. Kikikamilika kitatoa Walimu pamoja na wataalam wengine wapatao 40,000. Hawa ndio watakaoiondoa nchi yetu kwenye matatizo mengi ya ukosefu wa wataalam. Tunajivunia ukweli kwamba Chuo hiki kimejengwa bila kutegemea fedha za wafadhili/mikopo kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuhimiza sera ya ushirika wa akiba na mikopo. Watu wengi wameitikia wamejiunga. Mkoani Kagera, tumeanzisha *Saccos* tisa za wanawake. Leo hii katika kipindi cha miaka minne tu, wameshakopeshana zaidi ya shilingi billioni 2.6. Ili wakopaji waweze kukopa na kufaidika na mikopo hiyo, napendekeza Serikali itoe elimu ya kutosha ya mkopo na ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, Serikali itahimiza uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika wa Ujenzi wa Nyumba. Mkoa wa Kagera tumeshaanza, kuna Ushirika wa akina mama wa kujengeana majumba. Ushirika huo uko Muleba, Bukoba, Missenyi na Karagwe. Baadhi wameshapatiwa na viwanja. Awamu ya pili, tutaanzisha katika Wilaya ya Chato, Biharamulo na Ngara.

Je, ni Benki zipi au Taasisi zipi zitakazotoa mikopo ya muda mrefu ili hawa wanaushirika wa Ujenzi wa Nyumba, wakope wajenge Nyumba na kurejesha mikopo hiyo katika kipindi kirefu miaka 15 – 25? Naomba jibu ili waanze kujenga.

Mheshimiwa Spika, mtikisiko wa uchumi ulisababisha Vyama Vikuu vya Ushirika na Makampuni ya Watu binafsi kuuza kahawa kwa bei ndogo na hivyo kupata hasara kubwa. Kwa kupitia *Stimulus Package*, Serikali iliahidi kuwapunguzia makali kwa kuwalipa hasara waliyopata, na madeni ya Benki. Hadi leo hii zaidi ya makampuni 75% hawakupata, hata hawakujibiwa ili wajue nini kinaendelea.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini haya makampuni yatalipiwa hizo hasara na mikopo ya Benki isiyolipika ili waweze kuimarika kiuchumi na kupata uwezo wa kununua kahawa za wakulima kwenye msimu ufuatao?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri yenye matumaini kwa wananchi. Pia nawapongeza timu nzima ya Mawaziri na Naibu Mawaziri na Watendaji wote wa TAMISEMI. Nikiri tu kwamba, mimi binafsi nafurahia ushirikiano mkubwa ambao nimeupata katika kipindi hiki cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, nimefurahia sana kwa Serikali kwa bajeti ya mwaka huu ambayo inalenga kutekeleza sera ya afya ya mwaka 2007 inayokusudia kuimarisha huduma za afya Vijijini. Huduma iliyokusudia kutoa tiba na kinga, kwa kusambaza dawa mseto za malaria kwa vituo vyote, jambo ambalo ni jema sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa za Serikali katika kuboresha huduma za afya, sekta hii bado inakumbwa na changamoto mbalimbali mfano upungufu wa madawa, upungufu wa watumishi wa afya na upungufu wa vitendea kazi.

Nikianza na changamoto ya kwanza, Jimbo la Busanda lina idadi kubwa ya watu kutokana na shughuli za uchimbaji na uvuvi ambao unakusanya watu wengi kutoka sehemu mbalimbali. Mgao wa madawa tunaopata hautoshelezi kabisa mahitaji ya wananchi. Hii nililibaini wakati wa ziara zangu Jimboni nilipotembelea Zahanati ya Kaseme, moja ya Zahanati katika Jimbo la Busanda. Ilinihuzunisha kuona mgojwa wa malaria hakupewa dawa za malaria kwa sababu hazikuwepo. Nimejaribu kufuatilia suala hili kwa Zahanati nyingine na kubaini kuwa tatizo hili ni sugu na ni kero kubwa kwa wananchi.

Ombi langu kwa Serikali ni kwamba ione uwezekano wa kutoa kipaumbele kwa maeneo yaliyo katika maeneo ya uchimbaji madini na uvuvi, kuongeza kiasi cha dawa kulingana na idadi ya watu. Hii itapunguza kero kwa wananchi kutokupata dawa.

Jambo la pili ni upungufu wa Watumishi katika Zahanati za Vijijini. Ninaomba Serikali iangalie namna ya kuongeza watumishi wengi ili huduma kwa wananchi Vijijni ziweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika jambo la tatu, ni upungufu wa vitendea kazi kama vile *solar*. Upungufu au ukosefu wa vitanda, magodoro, vifaa vya kuchemshia sindano na ukosefu wa maji. Ninaomba Wizara ya Afya iangalie uwezekano wa kuweka *solar* kwa ajili ya mwanga ili kurahisisha utoaji huduma katika Zahanati hizi. Kwa sasa ni kero kubwa sana vijijini, wakati mwingine wagonjwa wanachangia fedha kwa ajili ya kununua mafuta ya taa, na wengi wanaopata taabu hizi ni akina mama wengi wanaokwenda kwa ajili ya kujifungua.

Mheshimiwa Spika, katika Zahanati hizi, maji ni muhimu sana. Zahanati za Vijijini hazina huduma ya maji. Hivyo, ninaomba Serikali iangalie uwezekano wa kuchimba kisima kwa kila Zahanati ili kurahisisha utoaji wa huduma. Maji ni muhimu sana kwa ajili ya usafi wa mazingira kwa ujumla. Ninaomba Serikali iangalie namna ya kufufua changamoto nilizozitaja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA SALEH NGOZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, kwa hotuba yake nzuri iliyojaa hekima na upendo. Pia tumeshuhudia anavyoshirikiana na Mawaziri, Manaibu Waziri na sisi Wabunge na kuleta ufanisi mkubwa ndani ya Bunge letu Tukufu. Ukweli ni kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kiongozi shupavu na wa kupigiwa mfano. Mwenyezi Mungu ambariki ampe afya njema, aendelee kulitumikia Taifa hili na wananchi wake, akiwa na wadhifa huo huo kwa kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniteua mimi kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ahsante sana. Namtakia kila la kheri na maisha marefu ili Watanzania tuendelee kuneemeka na uongozi wake uliotukuka ndani ya nchi na nje ya nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya Mrisho Kikwete ni kiongozi ambaye ameijengea nchi yetu heshima kubwa katika jamii ya Kimataifa na wote tunashuhudia alivyo hodari na mvumilivu. Ni mtu aliyejaa roho kubwa na upendo kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, tumtakie kila kheri katika uchaguzi Mkuu ujao uwe wa amani na utulivu ndani ya nchi ili CCM turudi madarakani na hatimaye Rais wetu mpendwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete aendelee kuiongoza nchi ya Tanzania kwa vipindi vyote. Mwenyezi Mungu amjalie. "CCM ushindi ni lazima."

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mchango wangu kuwa ni lazima tujivunie viongozi wetu. Wakuu wa nchi walipita na kiongozi Mkuu wa sasa Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anazoendelea nazo.

Mheshimiwa Spika, tumeona mafanikio makubwa aliyokwishayafanya ndani ya nchi yetu na nje ya nchi ambayo hayana mfano. Amekuwa mstari wa mbele katika kuliletea Taifa la Tanzania maendeleo makubwa kwa ajili ya wananchi wake. Shule zimejengwa, Hospital, Zahanati vijijini, barabara za kuunganisha Mikoa zimejengwa, madaraja, baadhi ya Mikoa ambayo haikuwa na umeme sasa upo. Katika mambo makubwa aliyoyafanya na anaendelea kufanya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambacho ni cha Kimataifa.

Kujengwa kwa Chuo hicho kumebadilisha sura ya Mkoa wa Dodoma kuwa Jiji zuri la kupigiwa mfano. Yote hayo yamefanyika kwa muda mfupi chini ya uongozi wake Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia tukumbuke kuwa mtafutaji wa yote hayo ni yeye peke yake na nchi hii ni kubwa, anastahili pongezi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. FATMA OTHMANI ALI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wake wote. Mimi mchango wangu upo kwa Wizara ya Afya. Serikali imejitahidi sana kuhusu kutoa elimu ya Ukimwi mpaka Vijijini na ni matumaini yetu kuwa watu wengi imewafikia elimu hiyo, lakini kuna tatizo kubwa la malaria ambalo bado elimu kubwa iko mijini tu, kwenye Vijiji bado inaendelea kuwaathiri wananchi hasa watoto kwani dawa zinazotolewa huwa zinawaathiri kwa kutoa madonda ndani ya mwili. Ningeomba Serikali ikalichunguza na kulipatia ufumbuzi suala la malaria na dawa zinazotolewa.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, ni ile hali ya Wizara ya Habari na Utamaduni. Hali yetu ya utamaduni bado iko nyuma kwa kuwaona wasanii wetu wa kizazi kipya mavazi wanayovaa wakiwa kwenye majukwaa.

Ningependa kutoa ushauri wakati kukitokea shughuli maalum na wao wakishirikishwa, basi waambiwe wavae mavazi ya heshima kwani inakuwa aibu wakati nyinyi viongozi wetu mko mbele ya sherehe yoyote ile na vijana wetu wanavaa nguo ambazo hazistahili na hata hizi nyimbo zetu zinazoimbwa na vikundi vya taarabu za kisasa ningeomba kabla hazijatoka kwenye vyombo vya habari zingechunguzwa kwanza, kwani hizi sasa zimeibuka nyimbo za taarabu na maigizo yake hayafanani kabisa na mila na desturi zetu, bora zifanyiwe sensa kwanza.

Kuhusu Wizara ya Habari, majengo ya utangazaji wa redio ya *TBC1* hayaridhishi hasa ukifikiria ile ndio redio ya wananchi wengi wa Mijini na Vijijini, ni aibu jengo linavuja na wala ndani halina ubora la kuwa redio ya Taifa. Mbele ya jengo la *TBC1 Television* kuna jengo ambalo halijamalizika na Kamati ya Maendeleo ya Jamii ilipotembelea *TBC1 T.V* waliambiwa kwamba tayari Wizara imeliomba jengo hilo kwa ajili ya kutengenezwa maofisi pamoja na studio za radio na TV: Je, jengo lile mpaka hivi sasa inashindikana nini kuwapo *TBC1* ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani, nampongeza sana *IGP* kwa kuanzisha ulinzi shirikishi au Polisi Jamii, lakini bado kuna matatizo ya raia kutokujua vizuri ulinzi shirikishi ni nini kwani kuna Vijiji, hawa raia waliojitolea kufanya huo ulinzi huchukua sheria mikononi mwao kwa kuwahoji watu wanaokwenda usiku bila kujua, wengine wanakwenda kwa shida kama hospitali au umetokea msiba wao huwapiga au kuwarudisha wanakotoka. Ningeomba sana huo ulinzi shirikishi utolewe elimu ya kutosha.

Kuhusu nyumba za Polisi ambazo zilizojengwa, mbona kuna malalamiko kwamba nyumba hizi hazitoki bure, lazima utoe pesa kwa yule anayehusika? Ningeomba suala hili lifuatiliwe kwani kama halina ukweli, basi linalitia kasoro Jeshi letu la Polisi.

Vile vile namwomba Waziri afikirie pindi itapata vitendea kazi kwa mwaka huo, afikirie Vituo vya Polisi Zanzibar kwani vituo vingi vya Zanzibar havina vitendea kazi muhimu, kama redio za mawasiliano, pingu pamoja na magari. Kuhusu michezo, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya ndani, naomba suala la michezo ndani ya Jeshi alitilie mkazo kwani michezo ni furaha na michezo ni moja ya kuwajenga maaskari wetu. Naomba kwenye Jeshi la Polisi michezo irudi kama zamani kwa kufanya mashindano ya vikosi kwa vikosi huko Moshi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. SALIM YUSSUF MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kufika katika kikao hiki cha Bunge na kuendelea kutekeleza majukumu yetu vyema.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukushukuru wewe, Naibu Spika na Wenyeviti kwa kuliendesha vyema Bunge letu. Napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu; Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge; Waziri wa TAMISEMI, Naibu wake pamoja na Watendaji wao wote.

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa hii kauli ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Kwa tafsiri ndogo tu ya maisha bora ni kuwa mtu aweze kupata chakula cha kawaida bila ya matatizo, aweze kupata matibabu mazuri, aweze kumsomesha au kuwasomesha watoto wake vizuri na kadhalika. Lakini Watanzaia walio wengi wanaishi kwa chini ya dola moja kwa siku ingawa kwa mujibu wa maelezo ya bajeti ya Serikali, wastani wa pato la kila Mtanzania ni Sh. 2,000/= tu kwa siku. Hata kiasi hicho ni kidogo sana ukilinganisha na maisha yalivyopanda. Kwa hali hiyo, maisha bora kwa kila Mtanzania hayatapatikana bali kuna maisha bora kwa baadhi ya Watanzania, tena walio wachache. Kwa hiyoi, nashauri ni vyema Serikali iache kutumia kauli ambazo kwa dhahiri utekelezaji wake ni ndoto.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni maskini sana na kuna msemo unaosema: "Maskini hana fahari". Watanzania tumezidiwa na fahari. Kwa hali hiyo, ni lazima tubane matumizi yetu na hasa yale yasio ya lazima ili tupate fedha nyingi, zitumike katika kujiletea maendeleo katika bajeti zetu zote, fedha za matumizi mengineyo *(OC)* zimekuwa nyingi mno kuliko zile za maendeleo. Nakubali kwamba matumizi mengineyo lazima yawepo, lakini ya Tanzania yamekuwa mno.

Tunawategemea sana wafadhili hata kwa matumizi yetu ya kawaida. Tukumbuke kuwa cha kupewa hakikumalizii haja yako. Kwa hali hii hata hao wafadhili wanaweza

kutuzunguka bila ya kujitambua tukajiona/tukajikuta tumeingia katika mtego wao. Kwani akufadhiilie ni bwana wako.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu achukue hatua za makusudi kupunguza au kuondoa kabisa baadhi ya mafungu ya bajeti ili kupata fedha zitakazosaidia katika shughuli zetu za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka sasa kuangalia baadhi ya sheria zetu za utumishi. Baadhi ya Watumishi wamekuwa na jeuri, kiburi na hata kuwa mafedhuli kutokana na kujiona kwamba labda sheria inamlinda sana, inampa uwezo mkubwa kufanya mambo na hata kuwa ni vigumu kumuajibisha. Nadhani kwa hali hiyo hata utekelezaji wa majukumu kwa watumishi wengi unapungua na hivyo kujali maslahi yao binafsi kuliko ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ahsante sana.

**MHE. KHADIJA S. AL–QASSMY:** Mheshimiwa Spika, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa mzima na kuweza kuchangia bajeti hii ya Waziri Mkuu iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe, Naibu Spika na Wenyeviti wako wote kwa jinsi mnavyoliendesha Bunge hili kwa viwango. Mwenyezi Mungu awabariki muwe na moyo huo huo wa uzalendo.

Mheshimiwa spika, napenda kuchangia kuhusu elimu. Nashukuru sana kuwa Serikali imeshirikiana sana na wananchi, wamejenga shule nyingi katika Kata mbalimbali, inahitaji pongezi. Lakini kinachosikitisha ni kuwa walimu, maabara na nyumba za walimu havitoshi kabisa kiasi kwamba kinachangia sana watoto kukosa la kufanya na kushawishika kuweza kupata mimba kwa wingi kwani hawana la kufanya, mara nyingi wanakaa na kutazamana tu kwa kukosa walimu. Naomba Serikali itilie sana maanani suala la Walimu kwani bila Walimu hakuna elimu.

Mheshimiwa Spika, maabara ndio inayozaa wana Sayansi wengi. Leo utaona wanafunzi wengi hawavutiki na somo hili kutokana na kukosekana na nyenzo muhimu ambayo ingeweza kuwapa ari ya kufanya vitendo *(Practical)* katika somo wanalosoma, sio *theory* tu.

Mheshmiwa Spika, katika Vijiji vingi kuna mazingira magumu ya kuishi hasa nyumba. Sasa ukiangalia mwalimu amesoma kwa taabu sana, baada ya taabu aliyopata kutafuta elimu ili apate maisha mazuri, Serikali haiwatengenezei mazingira mazuri ya maisha. Kwa hiyo, kutokana na kutokuwa na motisha, fani hiyo imekosa sifa ya kupendwa na watu wengi, ndio maana walimu wengi wakienda vijijini hawakai.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kujitahidi sana juu ya kuboresha mambo ya afya, lakini bado wananchi wengi hasa akina mama na watoto wanapoteza maisha kutokana na kukosekana mambo muhimu kama vifaa vya kujifungulia, damu salama Vijijini, kwani hakuna umeme wa kuhifadhia damu hiyo.

Mheshimiwa Spika, vile vile vipimo muhimu ni ghali sana kiasi kwamba mwananchi sio rahisi kutambua maradhi yake mapema kutokana na ughali wa vipimo

hivyo. Naiomba Serikali ielimishe wananchi kupima afya zao mapema na vile vile Serikali wajitahidi sana kuleta vipimo muhimu na viwe bei nafuu ambayo wananchi wataweza kupima afya zao kwa urahisi na kutambulika ugonjwa mapema ili aweze kutibika mapema.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho muhimu sana ni kwamba Serikali iweke mazingira mazuri kwenye uchaguzi ili nchi hii isije ikatumbukia kwenye machafuko yaliyokuwa sio ya lazima kwani nchi nyingi za jirani zinaingia katika mitihani ya machafuko kutokana na kuwa na uchaguzi uliokuwa sio wa haki na huru hasa ukizingatia Tume ya Uchaguzi inachaguliwa na Chama Tawala tu. Imefika wakati sasa wa kuchagua Tume huru ya Vyama vyote viridhike, kwani suala hili Wapinzani wameshalipigia kelele sana na kufanya maandamano kuomba jambo hili, kwanini Serikali ina kigugumizi kuleta Tume huru na inakubalika 92% kwa mujibu wa Chama Tawala na ushindi wa Serikali za Mitaa?

Mheshimiwa Spika, sina budi kuwapongeza wote walioandaa hotuba ya bajeti hii na kwa umuhimu mkubwa, naipongeza sana hotuba ya bajeti ya Upinzani kwa maoni yake na kuweza kuisaidia Serikali ili iweze kutimiza wajibu wake kwa umakini mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ahsante.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Awali ya yote, napenda nimpongeze Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Katibu Mkuu kwa maandalizi fasaha ya hotuba zote mbili.

Hoja yangu itahusu katika maeneo mawili ambayo katika majumuisho ningependa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) atufafanulie yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, uongozi katika miji midogo haujawa bayana sana. Mji wa Ifakara ulitangazwa kuwa mji mdogo miaka mingi iliyopita. Tulipofanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka jana Septemba, hawakuchaguliwa Wenyeviti wa Vijiji wala Wenyeviti wa Mitaa kwa maana ya mji kuwa mdogo. Kwa maana hiyo, kuna *"gap"* katika uongozi ambapo viongozi wa vitongoji ndiyo wanaoshikilia mambo yote ikiwa na ukusanyaji wa mapato ambayo kwa namna fulani yanaweza yakakosa udhibiti.

Pamoja na kwamba Mkurugenzi Mtendaji wa muda aliteuliwa (*former District Water Engineer* ambaye amehamishiwa Bagamoyo), lakini mfumo wa kiutawala wa mji mdogo haujaanza rasmi. Naomba Waziri katika majumuisho atuongoze katika jambo hili. Kama haitawezekana, basi niitishe uchaguzi wa kupata Wenyeviti wa Vijiji. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingi za Halmashauri zimebaki kuwa za Halmashauri bila kupanda hadhi baada ya kuzikagua mwaka hadi mwaka.

Katika Wilaya yangu barabara ya Namwawala – Mafu ya kilometa 18 ina daraja Mto Ruipa ambalo kwa fedha za barabara zinazokwenda Halmashauri ya Wilaya Kilombero, hawataweza kujenga barabara ile hata kidogo. Hali kadhalika kuna barabara

ya Taweta – Tanganyika, kilometa 18 kuna daraja la Mto Mfuji. Daraja ambalo haliwezi kujengwa kwa uwezo wa Halmashauri.

Je, Waziri haoni kuwa itakuwa vema, ku-*review* barabara hizi ili pafanyike kama Wizara ya Miundombinu ya kupandisha hadhi barabara na zikawa za *TANROADS*? Ahsante.

**SPIKA:** Namwita sasa Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ili kwa dakika 10 aweze kuchangia baadhi ya yale yaliyojitokeza katika mchango wa Waheshimiwa Wabunge kuhusu sekta ya elimu ndani ya Hotuba ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa hii nafasi ya kutoa ufafanuzi kidogo katika maeneo ambayo yamejitokeza kutoka kwenye sekta ya elimu katika hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ningependa nami kabla sijaanza kutoa hoja hii nikupongezee wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wetu wa Bunge kwa kazi nzuri mnayofanya ya kuongoza Bunge letu. Kwa kweli Bunge letu linakwenda kwa viwango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hoja hii ambayo ni nzuri sana. Imelenga katika kutuonyesha tumetoka wapi, tuko wapi na tunakwenda wapi. Nichukue fursa hii kuwapongeza pia Mheshimiwa Waziri Philip Marmo, Mheshimiwa Celina Kombani na Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kwa kumsaidia vizuri Mheshimiwa Waziri Mkuu. Napenda pia nirekodi shukrani zangu na pongezi kwa wafanyakazi wote wa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri pia uniruhusu niwashukuru sana wananchi wa Mwanga kwa kuniunga mkono kwa nguvu zao zote katika kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi. Niseme kwamba katika kipindi hiki Ilani yetu tumeitekeleza kwa zaidi ya asilimia 95.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo nawaomba sana wananchi wa Mwanga waendelee kuniunga mkono na kunirudisha hapa Bungeni kwa kishindo katika mwaka 2010 – 2015.

Mheshimiwa Spika, katika hoja zilizojitokeza kwa nguvu hapa ni hoja ya uboreshaji wa elimu ya msingi na sekondari na maeneo ambayo ni muhimu katika hoja hii yamekuwa ni kusomesha walimu, kuwa na maabara katika shule, kujenga nyumba za walimu na kupeleka vitabu mashuleni. Napenda sana niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliosema na hata wale waliochangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba ni dhahiri kwamba Waheshimiwa Wabunge, wanafuatilia kwa makini sana maendeleo ya elimu hapa nchini na ni vizuri tujipongeze kwa kweli kwa hatua kubwa ambayo tumefikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika elimu ya msingi sasa tumefikia uandikishaji wa wanafunzi wa rika lengwa wamefikia asilimia 97. Tumebakiza asilimia tatu ambayo tunahangaika nayo na nina uhakika kwamba mpaka tunafika mwaka 2015 hii asilimia tatu kwa sehemu kubwa tutakuwa tumeifikisha shuleni.

Moja ya mambo haya ni walimu, walimu. Mtakumbuka katika mwaka 2009 katika eneo la shule ya msingi tumepeleka walimu 14,800. Hili ni jeshi kubwa sana la walimu ambao tumelipeleka shuleni. Katika kiwango cha elimu ya sekondari tumepeleka walimu 11,140 katika shule za Sekondari wastani wa walimu wanne katika kila shule ya umma.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba upelekaji wa walimu shule za sekondari na shule na msingi unakuwa endelevu, Serikali imejenga msingi mkubwa sana wa kufundisha walimu katika vyuo mbalimbali hapa nchini. Mwaka 2005 tulikuwa na Vyuo vya Walimu 34 peke yake na wako wanafunzi katika vyuo 77. (*Makofi*)

Kwa hiyo, katika ngazi ya ufundishaji wa walimu watakaofundisha elimu ya msingi katika vyuo vya Serikali wako wanafunzi walioandikishwa wa mwaka wa kwanza na mwaka wa pili, 15,572 kwa maana kila mwaka walimu 7000 na ushee wako tayari kuondoka vyuoni na kwenda kufundisha. Katika vyuo vya watu binafsi wameandikishwa walimu wa cheti 12,529. Jumla ya wanafunzi walimu tulionao shuleni ni 28,100. Ni hatua kubwa sana na hii inaonyesha kwamba tunakwenda kulitatua tatizo hili la walimu kwa mara moja katika kipindi hiki hiki cha miaka mitano iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya *diploma* jumla ya wanafunzi walimu walioko kwenye vyuo vya Serikali na vile vya binafsi ni 13,887, hii ni ngazi kubwa sana. Hivi sasa hatuna walimu ambao wanakwenda chuoni kwa mwaka mmoja halafu waende shuleni kwa sababu vyuo sasa tumejenga uwezo mkubwa wa kupeleka walimu shuleni ambao wanatosha kushika nafasi hizo zilizoko wazi mpaka wengine nao wafuate. Kwa hiyo, kila mwaka katika ngazi ya Sekondari tutakuwa na uwezo wa kupeleka walimu watano kwenye kila shule Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka huu wa masomo unaomalizika katika vyuo vikuu hapa nchini vyuo vikuu vya umma na vyuo vikuu vya binafsi wameandikishwa walimu wanafunzi wanaochukua shahada za *BA Education au BSC Educatio*n au masomo ya elimu katika mchanganuo ambao unatolewa katika vyuo vikuu walioandikishwa kwenye mwaka huu unaokwisha ni 11,500 na mwaka huu wataandikishwa wengine 11,500 na mwaka unaofuata hivyo hivyo. Kwa hiyo, tuko katika hatua kwa kweli ya kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, nakuomba kupitia kwako na kupitia kwenye Bunge lako Tukufu niwaarifu Watanzania kwamba tatizo hili la walimu sasa tumefikia kiwango tutakuwa juu yake *(on top of this problem).*

Mheshimiwa Spika, matatizo mengine ya shule za Sekondari yanahusu maabara, yanahusu nyumba za walimu, yanahusu vitabu shuleni. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kuanzia Julai 1 mwaka huu kwa maana ya bajeti hii ambayo tunaisoma sasa tutaanza utekelezaji wa mradi wa maendeleo wa elimu ya sekondari, awamu ya pili. Katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa mradi huu tutajenga maabara na kuweka vifaa ndani ya maabara, tutajenga nyumba za walimu na tutapeleka vitabu shuleni. Ni matumaini ya Serikali kwamba mwisho wa utekelezaji wa mradi huu utaziona shule zetu zikiwa zinapeta katika taaluma na maeneo mengine muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mchungaji Mwanjali wa Mbeya Vijijini alitoa hoja kuhusu upanuzi wa Chuo cha Ufundi na Sayansi cha Mbeya. Nilikuwa nataka kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba mipango ya mbele ya Chuo cha Sayansi na Teknolojia kule Mbeya ni kukigeuza kiwe Chuo Kikuu. Kwa hiyo, matayarisho ya kufanya hivyo ni sasa. Moja ya matayarisho makubwa ni kukipatia ardhi ya kutosha ili kiweze kugeuzwa kwa urahisi kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, suala la walimu katika shule ya sekondari ya Tabora tumelishughulikia kama ambavyo tuliagizwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kundi la kwanza la walimu wa Sayansi na Hesabu wameshapelekwa na hivi tunavyogawa walimu katika kipindi hiki cha mwezi Mei, Juni, Julai kwa mwaka 2010/2011 walimu wa ziada watapelekwa kule kwenye shule ya sekondari ya Tabora.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kujibu baadhi ya hoja zilizojitokeza wakati wa kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nakushukuru kunipa nafasi hii kwa sababu nisingejibu leo ningejibu siku ambayo nitatoa bajeti yangu tarehe 28. Pia nikupongeze kwa uongozi wako mahiri katika ukumbi huu. Vile vile namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuniongoza na kunielekeza, nimejifunza mengi, lakini vile vile kwa hotuba nzuri ambayo aliitoa hapa juzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia katika sekta ya afya ni watu 20 katika kipindi nilichopewa cha dakika kumi sidhani kama naweza nikajibu yote. Lakini nitajaribu. Nianze na hoja ya Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini ambaye alizungumzia suala la Hospitali ya Mkoa wa Mara. Aliileta kwanza kama swali la moja kwa moja kwa Waziri Mkuu tarehe 10 lakini pia alipochangia alilizungumzia hilo. Hii ni Hospitali ambayo ilianzishwa kwa juhudi ya wananchi, waliamua kujenga hii hospitali mwaka 1975 wakajenga mpaka ghorofa ya kwanza halafu nguvu nadhani zikaisha na ikawa kama imetelekezwa mpaka mwaka 2007 ambapo Askofu alionyesha nia ya kuweza

kuiendeleza. Walikuja kumwona Waziri Mkuu hapa Dodoma, ilikuwa kipindi cha Bunge mwaka 2007 na ikakubaliwa kwamba kanisa lipewe hiyo Hospitali na kuindeleza.

Lakini mpaka mwaka jana hakuna chochote kilichoendelea. Inaelekea kulikuwa kuna mvutano askofu alitaka apewe hati ili amiliki kabisa hili eneo na kulikuwa na suala la fidia kwa watu ambao waliondolewa kwenye lile eneo. Sasa katika mazungumzo ya *RCC* mwaka jana walipewa miezi sita kwamba ikiwa Askofu atakuwa hajaanza kuendeleza katika kipindi cha miezi sita basi lile jengo litachukuliwa. Mwezi wa nne mwaka huu kanisa likawaandikia Mkoa kwamba wana *withdraw* na hawataki tena kuendeleza ujenzi. Kwa hiyo, hapa kuna suala la fidia la shilingi 35,000 milioni ambalo Mkoa unaangalia kuweza kuwapa lakini wameamua Mkoani kujenga wenyewe.

Wameunda Kamati ya watu 22 kusimamia uendelezaji wa ujenzi. Kwa hiyo, kama Serikali tunasubiri hayo yatakayotoka kwenye hiyo Kamati ili tujue tunaweza tukasaidia vipi.

Lakini tukumbuke tu kwamba, kuna Hospitali nyingi za Mikoa ambazo zinajengwa hivi sana na utaratibu utakuwa ule ule Manyara tunajenga, Mbeya tunajenga na Singida vile vile tunajenga. Tutajumuisha hii hospitali kwa kadri ya uwezo wa fedha utakavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo alipendekeza kwamba waratibu wa Ukimwi waajiriwe kila Wilaya. Tunachojibu ni kwamba Wilaya nyingi kama siyo zote zinao Waratibu wa UKIMWI. Hawa wanafanya kazi kwa karibu na kushirikiana na waratibu wa Mkoa katika masuala ya UKIMWI.

Lakini kama kuna Wilaya ambayo haina basi wateue huyo mratibu kutoka miongoni mwa watumishi wa afya wa Wilaya. Wabunge watatu kutoka Mkoa wa Singida Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Juma Killimbah na Mheshimiwa Paul Lwanji waliomba Serikali itafute njia mbadala ya kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida kwa muda mfupi. Serikali inajibu kwamba tunakubaliana nao, itakuwa vema kwamba hiyo Serikali ikakamilishwa mapema ili iweze kutoa huduma kwa wananchi.

Kwa kupitia Mkoa mwaka huu zimetengwa shilingi bilioni mbili kwenye bajeti ya mwaka 2010/2011. Lakini jumla ya fedha zinazohitajika ni bilioni 3.7 ambazo tunajaribu kuzitafuta na tumeongea na Mifuko kama *NSSF* hata Mfuko wa Bima ya Afya kuangalia kama tunaweza tukapata fedha huko ili tumalize hatua ya pili ya ujenzi. Pia tunawasiliana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida kwa sababu ni kiungo muhimu katika mambo ya fedha.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa alisema Halmashauri imetenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Mkoa, wananchi waliopisha ujenzi huo walipwe haraka haki zao na ujenzi uanze haraka. Ningependa kuwapongeza wananchi wa Shinyanga. Eneo nalifahamu maana yake nilikuwa Mganga wa Wilaya pale. Sisi

tunasema kwamba tutawasiliana na Serikali ya Mkoa wa Shinyanga ili tathmini ya fidia ifanywe na hayo madai yalipwe haraka.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Said Juma Nkumba walisema Tabora ni ya mwisho kwa huduma za afya. Ina vituo vichache vya huduma ya afya na pia watumishi ni wachache. Katika mpango mzima wa MAM ni azma ya Serikali kusogeza huduma kwa wananchi. Hii ni pamoja na kuimarisha vituo vilivyopo, kuongeza vituo vipya katika maeneo ambako hakuna huduma hiyo na kuendelea kupanga watalaam wa afya ili waweze kutoa huduma kwa wananchi wakiwemo wale wa Mkoa. Tukumbuke kwamba dhana nzima inayotokana na Ilani ni kwamba maendeleo yataletwa na sisi wenyewe. Ningeomba Halmashauri ziibue hiyo miradi ya kujenga zahanati na vituo vya afya waiweke kwenye *Comprehensive Councils Plans* halafu zitakwenda moja kwa moja mpaka kunakohusika na fedha kutengwa.

Halafu Mheshimiwa Lucy F. Owenya alisema kuna mlipuko wa *dank fever* ambayo watu wanapata homa kali, naomba Wizara ya Afya itoe tamko ili kuwaondolea hofu wageni na watalii. Nikiri kwamba niliongea na Mama Owenya kuhusu hilo. Ni kweli kumekuwepo na taarifa kwamba ugonjwa wa homa umeingia hapa nchini na taarifa za awali zilitolewa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Zanzibar. Mpaka sasa tumekuwa na wagonjwa 79 waliohisiwa kwamba wana homa hiyo na ni 27 tu waliopimwa wakaonekana kwamba wana huo ugonjwa kimaabara. Tulichukua hatua zinazohusika na tunaandaa tamko rasmi ambalo tutalitoa katika siku chache zijazo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Manyanya alisema Serikali ihakikishe kuwa dawa za uzazi wa mpango zinapatikana. Wizara inatambua kwamba kuwa na mpango mzuri wa uzazi wa mpango ni kuboresha, yaani nikuwekeza katika afya ya mama na mtoto. Nchi nyingi ambazo zina mpango ambao ni madhubuti kama Mauritius, afya ya akinamama imeboreka sana na sisi tumeliona hilo mwezi Machi, mwaka huu tulizindua mpango wa uzazi uliokasimiwa yaani *coasted national family planning implementation plan* ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, Lengo letu ni kuboresha hotuba kwa watumiaji, mwaka uliopita tulitenga kiasi cha shilingi bilioni 11 na zoezi la kutambua mahitaji halisi pia litafanyiwa kazi katika mwaka huu wa fedha. Mheshimiwa Ladiana Mafuru Mng’ong’o alisema Serikali ianzishe mfuko wa mapambano dhidi ya UKIMWI. Majibu yetu ni kwamba katika mgawanyo wa majukumu kati ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Tume ya Kudhibiti UKIMWI, suala la kutafuta rasilimali kwa ajili ya witikio wa Taifa dhidi ya UKIMWI linaratibiwa na Tume ya Kudhibiti Ukimwi yaani *TACAIDS*.

Mheshimiwa Spika, *TACAIDS* imeanza mchakato utakaowezesha uanzishaji wa Mfuko huu, wanachambua ili wapate uzoefu kutoka taasisi na mashirika yaliyoko ndani na nje ya nchi ambayo yana uzoefu na mifuko kama hii na natambua kwamba mama Mng’ong’o amekuwa Mjumbe wa Bodi kwa muda mrefu katika Bodi hii ya *TACAIDS*. Aidha, *TACAIDS* wamefanya mawasiliano na *TRA* ili wapate ushauri, wasije kugongana

na sheria katika kupata hayo mapato. Vile vile kutokana na sheria iliyounda *TACAIDS*, kuna haja ya kuomba marekebisho yafanyike ili kuongeza kipengele cha kuwaruhusu kuanzisha mfuko, katika sheria iliyoanzisha suala la Mfuko halikuwepo, kwa hiyo, itabidi irekebishwe.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mramba alisema Serikali iwe na mkakati madhubuti wa upatikanaji wa dawa katika mahospitali yote. Tunajibu kwamba Wizara imeweka mikakati ya kuboresha upatikanaji wa dawa, vifaa, tiba na vitendanishi katika sehemu zote za kutolea huduma. Tumebadilisha mfumo kutoka ule wa *kits*, sasa hivi Mganga Mkuu wa kituo yeye anaagiza dawa na vifaa kulingana na mahitaji na mgao wa fedha aliopewa.

Mheshimiwa Spika, sheria ilikuwa inaagiza kwamba *MSD* ipeleke dawa mpaka Halmashauri, lakini tulifanya utafiti na kwa kuangalia kwamba *what would it take* kama *MSD* watafuatilia dawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ni kengele ya pili. Basi malizia kama sentensi mbili za mwisho.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, basi niwaombe msamaha wale ambao sijajibu hoja zao, nitakuja nijibu wakati wa bajeti yangu. Lakini nimalizie tu hili la madawa kwamba tulifanya utafiti kuangalia, je, *MSD* ikifuatilia dawa mpaka kwa mlaji wa mwisho badala ya kufikia kwenye Halmashauri na hiyo imeonekana inawezekana na ndio mpango ambao tunaingia kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ili niweze kutumia dakika kumi ulizonipa kujibu masuala machache tu ambayo yatawezekana, lakini kabla sijaanza kusema hayo, ningependa kuwaambia wananchi wa Wilaya ya Muleba ambao matatizo yao yanahusu mnyauko wa migomba yalielezwa hapa na Mbunge wao tena kwa nguvu nyingi sana akichanganya pamoja na utani kwa sababu yeye ni mtani wangu. Lakini ukiondoa utani nataka kuwaambia tu wakulima wa Muleba kwamba ule mnyauko fizari ni ugonjwa ambao haujapata tiba.

Watafiti wetu wanaendelea kutafuta namna ambayo watashughulika na ugonjwa huo lakini ushauri ambao tunawapa sasa hivi, kwamba dalili za mnyauko zinapotokea katika mashamba yao waweze kungoa yale mashina na kuyateketeza, kwa sababu kwa kufanya hivyo wanazuia ule ugonjwa usiweze kuenea. Huo ndio mnyauko ambao sisi Wizara ya Kilimo tunaweza kuushughulikia, lakini mnyauko mwingine wa kisiasa ulioko kule Muleba unaweza kumalizwa na wananchi wa Muleba wenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ningependa kujibu baadhi ya mambo ambayo yamezungumzwa hapa ambayo yametokana na hotuba ya Waziri Mkuu. Moja

kubwa ambalo limezungumzwa sana limehusu kwanza kauli mbiu ya kilimo kwanza, wako watu ambao wamehoji baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kwamba kilimo kwanza si chochote. Lakini kilimo kwanza ni azma ya nchi ambayo inasema kuanzia sasa kwenda mbele, haya ndio utakayoyafanya. Kwa hiyo, kwa kweli kusema si chochote na kuhukumu azma yote kwa bajeti ya mwaka mmoja au miwili, sidhani kama tunajitendea haki.

Mheshimiwa Spika, nadhani Kilimo Kwanza kinazungumza habari ya kujumuisha sekta nyingi kushiriki na bajeti hii ina sekta ambazo zinashiriki katika kilimo kwanza. Fedha zilizopelekwa miundombinu zinatengeneza barabara katika maeneo ambayo ukiyafungua kilimo kinakua kwa haraka na soko la ndani linakuwa, kwa hiyo, linasaidia kukuza kilimo. Ukizungumzia masuala ya viwanda na nia yetu kubwa ya kutaka kukaribisha wawekezaji ili wawekeze katika viwanda vya kuongeza thamani, tunazungumza juu ya kukuza kilimo kwa sababu unaongeza ubora na kwa hiyo, unaongeza bei ya mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, ukizungumza juu ya barabara za vijijini, unazungumza juu ya kilimo kwanza kwa sababu zinafungua maeneo ya vijijini ili yaweze kuongeza uzalishaji na kufikisha mazao kwenye masoko. Nadhani zana hii ni nzuri na imegawanya kazi hizi kwa sekta sio za Serikali tu, kuna *private* sekta ambayo inatakiwa na yenyewe ishiriki na kwenye Mkutano uliomalizika wa *World Economic Forum* kuna *private sector* baada ya kuelewa vizuri dhana ya kilimo kwanza iliyotangazwa hapa nchini, kuna makampuni manane makubwa ya dunia ambayo yalijitoa na kujiandikisha kwamba yako tayari kushirikiana na Serikali katika jambo hili kwa kuendeleza kitu kinaitwa *Southern Highlands Agricultural Corridor* na hawa watu sio kama walisema tu halafu wakaondoka.

Juzi tarehe 8, Juni, 2010 Kamati Maalum ya watu hawa walikutana Dodoma chini ya Uenyekiti wangu na Mwenyekiti Mwenza ambaye anatokana na kampuni kubwa ya *UNILIVER*, tumezungumza na sasa tuko kwenye mchakato wa kuweka utaratibu wa namna ambavyo tunaweza kushirikisha sekta binafsi katika kukuza kilimo kwa maana ya mfumo wa kilimo kwanza. Kwa hiyo, si kama ni jambo tu limesemwa, hapana, ni jambo ambalo linatekelezeka na Serikali iko makini katika kuona kwamba tuko makini, tunasimamia jambo hili kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, ukiondoa hilo, liko jambo la pembejeo ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi, Mheshimiwa Zambi, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Jackson Makweta, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale na wengine wengi pamoja na Mheshimiwa Chenge, wote wamezungumzia suala hili la mfumo wa upelekaji wa mbolea kwa kutumia ruzuku. Ningependa kutumia nafasi hii kusema kwamba tumefanya hatua hii kama uboreshaji wa hali ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, zamani ilikuwa ni makampuni ndio yanapeleka Mikoani halafu yanapata *certifcate* kwamba yameuza mbolea, halafu yanalipwa na Serikali. Lakini ilikuwa vigumu sana kujua nani hasa mkulima, nani ambaye amepata hiyo ruzuku, ndio maana tukabadili, tukasema sasa tutoe vocha na vocha hii iende kwa mkulima na mkulima yeye awe na mamlaka ya kupata ile mbolea, Serikali tuwe tunamlipia tukijua yeye ndiye aliyepata hiyo ruzuku. Hiyo ndio tuliyofanya.

Mheshimiwa Spika, nadhani ni *innovative* na tunaweza kusema wakulima wangapi wanapata mbolea, tulianza na laki saba na nusu, tukaenda kwenye milioni moja na nusu, msimu unaokuja tutakwenda mpaka kwenye milioni mbili hasa kwa mazao ya chakula na laki tano zaidi kwa mazao mengine. Lakini hiyo ni nje ya mifumo ya kutoa ruzuku kwa ajili ya miche ya chai, miche ya kahawa, madawa ya pamba, madawa ya korosho, yote hayo. Hilo linajibu kidogo swali lililoulizwa kwamba kwa nini ruzuku isiwe ya nchi nzima, nadhani tumekwenda mbali sana, tumefikia karibu nchi nzima. Hivi nchi hii iko wapi? Hatuwezi kumfikia kila mtu kweli, lakini nchi nzima kwa sababu tunatoa ruzuku kwa Mikoa yote 20 ukiondoa Dar es Salaam ambao si Mkoa wa kilimo. Kwa hiyo, ukisema twende nchi nzima, nasema sawa, ndio lengo kuu na jitihada ni kwenda huko kwenye nchi nzima. Tulianza na Mikoa sita, *actualy* tulianza na Mikoa minne ya Nyanda za Juu Kusini, tukaongeza Morogoro na Kigoma lakini baadaye tumekwenda katika Mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengine katika Mikoa mingine ambayo yana hali ya hewa inayolingana kabisa na ile ya Nyanda za Juu Kusini. Kwa mfano, ukienda Bukombe katika Mkoa wa Shinyanga au uende Sengerema au Geita katika Mkoa wa Mwanza au Chato katika Mkoa wa Kagera au Karagwe, Kagera na Mikoa mingine ambayo inahudumiwa katika Wilaya mbalimbali kama Serengeti au Tarime katika Mkoa wa Mara, yote ina hali ya hewa inayokaribiana sana.

Kwa hiyo, katika kupanua mpango huu tumekwenda mpaka katika maeneo yale na shabaha yetu ni kuzalisha chakula katika maeneo hayo ili kiwe karibu zaidi na walaji kwa sababu kwenye maeneo hayo yana upungufu wa chakula kila mwaka. Kwa hiyo, badala la ku-move chakula kwenda kusini basi yapelekwe. Basi mfumo huu unakaribia kufika kwa wakulima wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa ni la zana. Katika hili walisema kwamba, tusipeleke *power tillers* kila mahali, maana kuna maeneo mengine hazifai. Nasema maamuzi ya zana aina gani yafanywe kule kule ambako zana zinanunuliwa. Kama kuna Wilaya inaona *power tiller* haziwezi kufaa kule, basi wafanye kitu ambacho kinafaa kule, isiwe ni kwamba lazima tu *power tiller* zipelekwe kila mahali. Lakini siamini kama *power tiller* hii inaweza kuwa na mahali fulani haifai kabisa. Inaweza kuwa katika udongo fulani hazifai na inaweza kuwa katika udongo fulani zinafaa. Tena hii inafaa sana kwa kilimo cha mpunga katika majaruba. Na kilimo hiki cha mpunga kinalimwa katika maeneo mengi sana. Kwa hiyo, sidhani kama hili ni jambo la ajabu sana.

Mheshimiwa Spika, lingine lililozungumzwa linahusu bei ya pamba na kadhalika, liliulizwa na rafiki yangu Shibiliti pale alikuwa anapiga mahesabu anaonesha bei ya soko la dunia ikoje, haya mengine tutayajadili zaidi wakati nitakapowasilisha hotuba yangu ambayo inakuja tarehe 22, Juni, 2010, siku chache tu zijazo. Kwa hiyo, nafikiri tuwe wastahimilivu, tutapata nafasi ya kujibu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kuna hoja iliyouliza tunawafanya nini watu ambao wanavuruga mpango wa upelekaji wa ruzuku au wanatumia zile ruzuku kuiba. Hawa ni wezi kama wezi wengine. Ukiiba huwezi tena kuweka sera gani, unakamatwa unapelekwa katika vyombo vya dola na vyombo vya dola vipo kila mahali hata Mbozi vipo kule Mbeya, wengine waliofanya madudu haya kule Sumbawanga wanachunguzwa hivi sasa na watachukuliwa hatua za kisheria na hiyo ndio kazi yenyewe ya Polisi kuhakikisha kwamba wanaofanya uhalifu wa namna hiyo wanachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo bila kungoja kengele ya pili nakushukuru sana, huo ndio mchango wetu kama ulivyotolewa hapa katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uwasilishaji wake mzuri wa hoja ambayo ameiwasilisha kwa umakini na kwa kina kwa namna ambayo imetupa matumaini Serikalini lakini pia kwa wananchi wote wa Tanzania. Nichukue nafasi hii pia kuwapa pongezi nyingi sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Celina Kombani; Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge na Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Mwanri, Makatibu Wakuu na watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri ambayo wameifanya iliyomwezesha Mheshimiwa Waziri Mkuu kuweza kuwasilisha vizuri hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kuwashukuru Wabunge wote ambao wamechangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini pia wale ambao katika kuchangia kwao wamegusia masuala ya miundombinu. Naomba nitangulize kusema, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, katika michango ya Wabunge ambao wamegusia sekta ya miundombinu kuna maeneo kama manne hivi ambayo ningependa niyatolee ufafanuzi angalau kwa muhtasari. Kuna eneo la barabara, kuna eneo la viwanja vya ndege hasa uwanja wa ndege wa Songwe, kuna eneo la usafiri wa anga, bandari na reli na pia kuna suala mahsusi kuhusu daraja la Kigamboni. Nikianza na eneo la barabara, hili limechangiwa na Wabunge wengi. Karibu kila aliyeongelea sekta ya miundombinu, alichangia kuhusu hoja ya barabara na nashukuru. Nafarijika sana kujua kwamba Wabunge wengi walitoa pongezi sana kwa kazi kubwa ambayo Serikali ya Awamu ya Nne imefanya katika ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Spika, wametoa pongezi Wabunge wengi wakiwemo ni Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Charles Ogesa Mlingwa, Mheshimiwa Haroub Masoud, Mheshimiwa Gosbet Blandes, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Mwinchoumu Msomi, Mheshimiwa Riziki Saidi Lulida, Mheshimiwa Paschal Constantine Degera.

Pongezi hizo tumezipokea pia kutoka kwa Mheshimiwa Mtemvu, Mheshimiwa Shibiliti, Mheshimiwa Nkumba, Mheshimiwa Kimbau, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Mchemba na Mheshimiwa Missanga, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Kimaro, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Njwayo, Mheshimiwa Gulamabbas Dewji, Mheshimiwa Katagira, Mheshimiwa Marombwa na Mheshimiwa Mwenegoha na wengine wengi ambao walichangia lakini wametoa pongezi nyingi kuhusu ujenzi huu wa barabara.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna masuala mahsusi, kama la Mheshimiwa George Lubeleje ambaye amezungumzia Mfuko wa Barabara na kwamba hoja yake ilikuwa kwamba Mfuko huu wa Barabara uongezewe mgao wa fedha kutoka mgao wa sasa wa asilimia 30 kwenda asilimia 40. Ufafanuzi ambao naweza nikautoa hapa ni kwamba Serikali itafanya utafiti wa kina ili kubaini mahitaji halisi ya matengenezo ya barabara kwa sasa katika barabara kuu, barabara za Mikoa na barabara za Wilaya ili tuweze kufahamu kwa uhakika mahitaji ya fedha za maendeleo kwa mitandao ya barabara hizi.

Matokeo hayo ya utafiti ndio ambayo yatatoa hali halisi ya mahitaji ya kila mtandao wa barabara ikiwa ni pamoja na zile ambazo zinasimamiwa na Serikali za Mitaa. Hapo ndio tutakapoweza kujua asilimia hii tuweze kuibadilisha kwa namna gani ama tuweke viwango gani kati ya barabara kuu na zile ambazo zinasimamiwa na Halmashauri zetu za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ambalo ni mahususi ni hoja ya Mheshimiwa Mwinchoumu Abdulrahman Msomi ambaye katika hoja yake amesema kwamba Serikali ikamilishe ujenzi wa barabara ya Kilwa na hasa ile kilomita moja ambayo imebaki katika

barabara hiyo eneo la Mbagala mwisho ili kupunguza msongamano wa magari uliokuwepo hivi sasa. Nitoe ufafanuzi tu kwamba maandalizi ya ujenzi wa kipande hicho cha kilomita moja sasa yako katika hatua za mwisho za kumpata mkandarasi. Kwa hiyo, tunatarajia katika mwaka huu mpya wa fedha bila shaka tutaanza kushughulikia kilomita moja iliyobaki ili kuondosha ule msongamano wa magari ambayo yanatokea katika eneo lile la bendera tatu baada ya hapo bila shaka barabara hii italeta ufanisi mzuri zaidi katika kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Paschal Constantine Degera naye alikuwa na hoja maalum ambayo inahusiana na ujenzi wa barabara ya Dodoma hadi Babati. Hoja yake ni kwamba kiwango cha fedha kilichotengwa na Serikali cha shilingi bilioni tisa kwa ujenzi wa barabara hiyo ni kiwango kidogo na amehoji kwamba katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Serikali pia ilitenga kiasi cha fedha cha shilingi bilioni 45 ambazo nazo pia ni kidogo mno na Serikali itekeleze ahadi yake.

Mheshimiwa Spika, Waswahili wanasema ada ya mja hunena, muungwana ni kitendo na sisi katika Serikali hii ni waungwana sana. Tunatenda yale ambayo tumeyaahidi. Hii barabara ni ndefu, ina jumla ya kilomita 260 na katika awamu hii ya kwanza ambayo tutajenga kwa kutumia pesa za Serikali tumetangaza tenda zenye jumla ya kilomita 44. Thamani yake tunatarajia itavuka bilioni 44 kwa maana bilioni hizi 45 tulizoziahidi kwamba mara tu wakandarasi watakapopatikana pesa hizi zitaanza kutumika kwa ajili ya ujenzi. Tutajenga awamu ya kwanza, kipande cha Dodoma-Mayamaya kilomita 24. Babati hadi Bonga kilomita 16 na mchepuo kutoka Bicha kuingia Kondoa kilomita tatu za lami ili ziweze kuunda hii awamu ya kwanza ya ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Serikali iko mbioni kuzungumza na wafadhili mbalimbali. Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi karibuni alipokuwa Japan ameliwasilisha suala hili, Japan na Serikali ya Japan inalitafakari au imekubali kimsingi kuweza kufadhili barabara hiyo. Lakini mchakato unabidi uendelee kwa ajili ya kuweza kupata fedha kutoka Serikali ya Japan kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo. Kwa hiyo, hili tunalishughulikia, tutalifanyia juhudi ili kuhakikisha kwamba linakamilika kwa manufaa ya wananchi siyo tu wa Dodoma na Babati bali kwa wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame ambaye pia imechangiwa na Mheshimiwa Florence Kyendesya na wao wamehoji ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Songwe na hoja ni kwamba Serikali itoe maelezo juu ya ujenzi wa kiwanja hicho. Naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kama ifuatavyo kwamba, utekelezaji wa awamu ya tatu na ni awamu ya mwisho ya ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Songwe unaendelea pamoja na changamoto ambazo zipo.

Mheshimiwa Spika, lakini kazi hiyo hivi sasa inaendelea. Kazi inayofanyika hivi sasa ni pamoja na ujenzi kwa kiwango cha lami, barabara ya kuruka na kutua. Maegesho ya ndege na pia barabara za viungio. Jengo la abiria na ununuzi wa vifaa vya ukaguzi kama vile *X-Ray* navyo viko katika awamu hii na ujenzi wa kiwanja hiki unategemewa

kumalizika kwenye nusu ya mwanzo ya mwaka huu wa 2010/2011. Kwa maana tunatarajia tunapoanza mwaka mpya 2010/2011, kwa kiasi kikubwa ujenzi wa kiwanja hiki uwe umekamilika.

Mheshimiwa Spika, hoja zingine ni za mchanganyiko ambazo zinahusiana na uendeshaji wa Shirika la Reli, Bandari na Shirika la Ndege la Tanzania na hii ni hoja ambayo ameileta Mheshimiwa Ismali Jussa Ladhu. Lakini pia imechangiwa na Waheshimiwa Lucy Owenya na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika. Niseme tu kwa ujumla kwamba upande wa Shirika la Ndege la Tanzania ama *ATCL,* Serikali imejitahidi katika miaka hii michache iliyopita mpaka hivi sasa kutenga pesa kwa kadri ya uwezo wake ili kuliwezesha Shirika hili liendelee. Lakini bado tumeendelea kupata changamoto.

Serikali imechukua maamuzi tayari kwamba tufanye mkakati sasa wa kuliunda upya Shirika la Ndege la Taifa hili. Kwa maana siyo ukarabati wa Shirika lililokuwepo kwa kuwekea viraka, bali ni kufanya mkakati maalum wa kuliunda upya Shirika jipya kwa kushirikisha Sekta binafsi. Kwa hiyo tuko katika mchakato huo wa kuunda Shirika jipya la Ndege la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutakapofikia katika hali nzuri bila shaka tutapata sura ile ambayo wananchi wa Tanzania wataifurahia kwa usafiri wa anga. Ama kuhusu Bandari, Bandari hali yake siyo mbaya, hali ni mzuri. Mchakato wake ni mzuri. Sasa hivi Mamlaka ya Bandari, imeshamaliza *Port Master Plan* ambayo imeainisha maeneo yote ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi kwa ujenzi wa miundombinu ya Bandari.

Mheshimiwa Spika, naona muda umeniishia. Ningependa kuchangia mengi kwa sababu michango imepokewa mpaka dakika hizi za mwisho hivi asubuhi. Naomba nitoe ahadi tu kwamba michango hii yote nitaitolea ufafanuzi wakati nitakapokuwa nawasilisha hoja ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu. Sasa tuna takriban saa moja, yaani dakika zisizozidi 60 ambazo zimegawika kama ifuatavyo, maana yake sasa ndiyo rasmi hoja zinaanza kujibiwa; Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge kwa dakika 15; Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, dakika 15 na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa dakika 30. Kwa hiyo tunaanza na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Marmo, unazo dakika 15.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba nzuri ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Mbunge.

Mheshimiwa Spika, nitachangia katika maeneo ya Sera, Uratibu na Shughuli za Serikali na pia masuala mtambuka kwa kuwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mheshimiwa Waziri mwenyewe watasemea maeneo yanayowahusu na pia Mheshimiwa Waziri Mkuu atatoa maelezo ya Ofisi yetu lakini na pia maelezo ya Serikali kwa ujumla. Eneo la kwanza linahusu kuhamia Dodoma. Waliochangia katika eneo hili ni Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati; Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni na Mheshimiwa Felister Bura, Mbunge wa Viti Maalum, Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla maelezo yetu kwa hoja zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge ni kama ifuatavyo:-

Kuhusu mpango wa kuendeleza na kuharakisha kuhamia Dodoma ni kwamba Serikali inaendelea na juhudi za kuweka mazingira mazuri ya kuhamia Dodoma na hatua ambazo zimechukuliwa mpaka sasa katika muda wa miaka mitano iliyopita ni kama ifuatavyo:-

Kupima viwanja 21,000 katika maeneo mbalimbali na kukamilisha upimaji wa viwanja 3,584 vya zamani na kuandaa hati 5,187 za kumiliki viwanja hapa Dodoma. Kutayarisha mipango kwa maeneo yenye kuhitaji matumizi makubwa ya ardhi na uwekezaji mkubwa kwa Taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma na pia Sekta binafsi. Kukamilisha ujenzi wa barabara ya Dodoma kwenda Manyoni na pia Serikali imepata fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Dodoma-Iringa na Waziri wa Miundombinu sasa hivi ametuelezea kwamba jitihada za kupata fedha za barabara ya Dodoma-Babati inaendelea.

Pia kuongeza huduma za jamii za umma na za watu binafsi kukidhi mahitaji ya mji huu. Aidha, Serikali ina mpango wa kujenga Kituo kipya kikubwa sana cha uchapishaji hapa Dodoma ambacho kitakuwa ndiyo Makao Makuu ya Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Kuhusu Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu kupitwa na wakati na kuhitaji kurekebishwa ili kuondoa kasoro na migogoro baina ya *CDA* na Manispaa ya Dodoma. Ni kwamba Serikali imekwishaanza mchakato wa kurekebisha Sheria husika na Rasimu Waraka wa Baraza la Mawaziri umekwishaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya UKIMWI. Katika eneo hili Waheshimiwa Wabunge waliotoa maoni yao ni Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Rajab Juma. Hoja kuhusu Waratibu wa UKIMWI katika Wilaya imekwishajibiwa na Mheshimiwa Waziri wa Afya. Kuhusu ushauri kwamba Tume ya Kuratibu udhibiti wa dawa za kulevya kuunganishwa na *TACAIDS*, kwa sababu majukumu yao yanafanana. Kimsingi nataka kusema kwamba Tume hizo mbili zina majukumu tofauti.

Mheshimiwa Spika, Tume ya kudhibiti UKIMWI kazi yake ni kuratibu udhibiti na kuzuia maambukizi ya VVU na UKIMWI. Pia kutafuta rasilimali, kutangaza Sera za UKIMWI, kufuatilia na kutathmini maambukizi ya VVU. Lakini kwa upande wa Tume ya kuratibu dawa za kulevya kazi yake ni kuratibu uzuiaji na udhibiti na matumizi wa biashara haramu wa dawa za kulevya. Hata hivyo ni kweli kwamba utumiaji wa dawa za kulevya ni kichocheo cha maambukizi ya VVU hasa kwa watumiaji wa dawa hizo kwa kujidunga sindano na watumiaji kukosa maamuzi sahihi ya kujikinga na UKIMWI. Vyombo hivi vyote vina umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Katika eneo hili wamechangia mawazo Waheshimiwa Wabunge wafuatao:- Kwanza Mheshimiwa Wilbrod Slaa, Msemaji wa Upinzani katika eneo hili, Mheshimiwa Mgana Msindai, Iramba Mashariki; Mheshimiwa Masoud Salum, Mbunge wa Mtambile; Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum. Lakini pia alichangia Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, Mbunge wa Kuteuliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa kuondolewa chini ya TAMISEMI na kuwekwa chini ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Maelezo ni kwamba, Katiba na Sheria ya Uchaguzi inaipa Tume ya Uchaguzi ya Taifa kusimamia uchaguzi wa Rais, uchaguzi wa Wabunge na Madiwani Tanzania Bara. Hivyo Tume haina mamlaka ya kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Uchaguzi huo unasimamiwa na Halmashauri husika chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa Na. (7) na namba (8) za mwaka 1982. Serikali kwa sasa inaamini kwamba, utaratibu huo unakidhi haja na utaendelea kutumika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Uchaguzi kutoa taarifa sahihi ili kuepusha ubambikwaji wa kesi kwa viongozi wa vyama wakati wa uchaguzi. Ni kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi, Sura 343, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepewa mamlaka ya kuandaa maadili ya uchaguzi baada ya kushauriana na vyama na Serikali. Hivi sasa tunapoongea Tume ipo katika mchakato wa kuandaa maadili hayo.

Pamoja na mambo mengine maadili yanakataza ubambikiwaji wa kesi wakati wa uchaguzi. Maadili hayo yakishakamilika yatasambazwa kwa wadau wote ili yaweze kufahamika. Vyama vyote vya Siasa, Serikali ikiwepo, vyombo vya Ulinzi na Usalama na Tume watawajibika kutekeleza maadili haya hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kukemea lugha chafu wakati wa uchaguzi. Lugha chafu wakati wa uchaguzi inakatwa na Sheria za Uchaguzi na Maadili ya Uchaguzi. Serikali haitasita kuchukua hatua kwa atakayekiuka maadili hayo. Pia ilitolewa hoja kwamba Serikali itoe tamko kukemea viongozi wa CCM kwa kuwa wanafuata wananchi kwenye nyumba zao kuwataka wawaonyeshe kadi zao za kupigia kura na wanaandika namba hizo kwenye fomu na daftari zao.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba Vyama vyote vya Siasa vinaruhusiwa kuwafuata wananchi na kuwahamasisha na pia kuwashawishi ili wawapigie

kura. Wajumbe wa vyama hivyo wanaruhusiwa kufanya kampeni nyumba hadi nyumba. Sheria za Uchaguzi hazikatazi vyama kuorodhesha majina ya watu walioandikishwa. Kinachokatazwa ni kuchukua kadi za wapiga kura. Hivyo kuna vyama vinafanya hivyo yaani kuchukua kadi za wapiga kura, basi taarifa zitolewe ili hatua zinazostahili zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchaguzi ule wa Busanda na Biharamulo kuwa kadi za wapiga kura zilichukuliwa kwa nguvu. Taarifa hii ilipelekwa Polisi na baada ya uchunguzi Polisi walibaini kuwa waliolalamikiwa walikuwa wameorodhesha majina tu ya wanachama wao na hawakuchukua kadi yoyote ya mpiga kura kwa kuwa kuorodhesha majina siyo kosa, basi walikuwa wameachiwa.

Napenda kusema hapa kwamba, tutawasilisha hoja hizi kwa njia ya maandishi kwa wahusika na tutahakikisha kwamba majibu yote yatawafikia.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, mimi ni Mbunge wa Mbulu na hivyo napenda kuchukua fursa hii, kuwashukuru sana wananchi wa Mbulu, kwa kunileta katika nyumba hii, muda wote tumeshirikiana nao. Kama alivyosema jana Mheshimiwa Mbunge Mkongwe wa Njombe Kaskazini, Jackson Makwetta, kushukuru pia ni kuomba.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Siha, naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa vile najua nitaongeza *speed,* basi nitamke moja kwa moja kwamba hoja hii naiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii, kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nafasi ya kipindi cha miaka mitano katika Bunge hili na kuweza kushirikiana na wenzangu katika kazi hii ambayo tumeifanya. Kipekee, naomba nichukue nafasi hii, kumshukuru sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani kubwa sana aliyoionesha kwangu, kwa kunipa fursa hii ya kuweza kumshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu na kushauriana katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na katika Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kuchukua nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa namna alivyonilea na kwa namna alivyotuongoza na pia kumshukuru dada yangu Celina Kombani, kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kunielekeza na kuniongoza na kwa ushirikiano alionipa. Pia napenda kuchukua nafasi hii, kuwashukuru sana Wakuu wa Mikoa pamoja na Wakuu wa Wilaya na ndugu zangu Wabunge wote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ushirikiano mkubwa mlionipatia kwa kipindi hiki ambacho tumekuwa wote, cha miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nipende kuchukua nafasi hii, kukupongeza sana kwa kazi nzuri unayoifanya na namna unavyoliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia sitasahau kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Siha na Wilaya ya Siha, kwa imani kubwa waliyonionesha na nina hakika kwamba wataendelea kunionesha imani hiyo; tumekaa vizuri, tumefanya kazi vizuri na nina hakika wataendelea kutoa imani yao kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee, naomba kuchukua nafasi hii, kuishukuru sana familia yangu, mke wangu mpenzi na rafiki yangu sana, Grace Mwanri na watoto wangu, kwa namna ambavyo wamekuwa wanashirikiana na mimi na ninajua mke wangu ananiombea sana na ninamshukuru sana kwa namna anavyoniombea; nataka niseme ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, basi baada ya kusema hayo, yote ya shukrani na wale wengine wote ambao sikuwataja, kwa kweli nataka niseme nawashukuru sana na nimshukuru Mungu sana kwa namna alivyonilea, mimi hapa nataka niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hayati Rais Samora Machel wa Msumbiji, aliwahi kuulizwa, ni nini maana ya mapinduzi? Hayati Rais Samora Machel akasema, naomba kunukuu:-

*"Mapinduzi ni kitendo chochote cha manufaa kinachofanyika kwa haraka na kuleta manufaa kwa jamii inayohusika",* mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, akaulizwa je, unapataje mapinduzi? Akasema, naomba kunukuu:-

*"Ukitaka kupata mapinduzi ya haraka, ni lazima uwe tayari kufanya kazi muda wa ziada"*, mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, akafafanua akasema, kama unafanya kazi mpaka saa 9.30 ndio mwisho wa kazi, ukaondoka ukaenda nyumbani kwako, wewe ni Mkuu wa Wilaya, ni Mbunge, ni Spika, *according to Samora Machel, there is no development, there is no revolution.* Akasema, ukitaka shule, ukitaka maji, ukitaka maziwa, unataka nyama, wananchi wanachotaka kusikia ni sasa vitu hivyo viweze kupatikana. Huyu ni Samora Machel, sio mimi, mimi nataka ku-*quote* tu na kuonesha hali jinsi ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watakaonisaidia hapa maana kumekuwa na mjadala hapa na Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Profesa Magembe, ametoa takwimu hapa akaeleza mambo ambayo yamefanyika katika Wizara ya Elimu na mimi ninataka nisaidie kwa maana kazi yetu sisi ni kuinua kiwango cha mjadala humu ndani, wapo watu wanaofanya utafiti na wanaojua kwamba kama tungesema tusubiri mpaka tupate Walimu wote wanaohitajika katika shule za sekondari na shule za msingi, kama tungengoja mpaka tupate Madaktari wote wanaohitajika katika hospitali katika zahanati, utafiti unaonesha kwamba tungefikia hatua hiyo mwaka 2015, nataka tuweke vizuri. Kwa hiyo, kama unasema kwamba tusubiri mpaka tupate maabara zote, mpaka tupate shule zote,

mpaka tupate Walimu wote wanaohitajika ili tuweze kusomesha watoto wote, hii kazi yote iliyofanyika hapa ingeanza matokeo yake yangeanza kuonekana mwaka wa 2015. Ndio maana nikam-*quote* Samora Machel na *according to him* haya yasingekuwa ni mapinduzi wala yasingekuwa ni maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kazi iliyofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ya kuhakikisha kwamba watoto wanakwenda shule sasa, 50% ya watoto wote wanaomaliza *primary school* wanakwenda sekondari, ni kazi nzuri na kwa maoni yangu mimi, ninaamini kwamba inahitaji sifa kubwa sana, vinginevyo hawa watoto wote wangerudi mtaani. Ninachotaka kusema ni suala la kupata maabara, suala la kupata Walimu, ni kweli kabisa linasaidia sana katika kuinua viwango na *quality* ya elimu katika nchi hii. *Argument* yetu sisi hapa, ni kwamba vyote kwa pamoja ni lazima twende navyo. Ni lazima uanze kupanga na kusema kwamba unawasomesha. Ukitaka mfano mzuri, nenda kaichukue Cuba, wale walipotaka kuwaondoa watu wasiojua kusoma na kuandika katika nchi yao, waliwachukua watu wakawaweka chini ya mwembe, wakachukua ule ubao ambao una mguu wa kiasi hiki, wakawaambia watu wawili wawili watakuwa wanakwenda wanawasomesha wale watu mpaka wajue kusoma na kuandika, chini ya mwembe. Sio kwenye madarasa haya ambayo yanaitwa yebo yebo, vodafasta, sijui nini, aha aha, chini ya mwembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyozungumza, dunia inajua kwamba Madaktari Bingwa katika dunia wanatoka Cuba, ambao wanasoma chini ya mwembe. Ukisoma historia yake ndio hiyo, ukiwasoma akina Fidel Castro, walichofanya walisomesha watoto wao kushoto, kulia na katikati, wakahakikisha kwamba katika muda mfupi sana wameondoa *iliteracy* na mwisho wakaanza kupata Madaktari na wataalamu wengine wote. Tukitaka tuisaidie nchi yetu hii ya Tanzania na kama tunataka tuache urithi katika nchi hii, tusomeshe watoto wetu, tupeleke watoto wetu shule, mbele ya safari suala la *quality* litakwisha na maabara zitajengwa na mambo mengine yote yatafanyika. Kwa hiyo, ukitaka mapinduzi ni lazima ufanye kazi muda wa ziada na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilichofanya ni kufanya kazi muda wa ziada. Mimi ninaamini kwamba kazi nzuri imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niingie katika kujibu maswali kama yalivyoulizwa na Waheshimiwa Wabunge. La kwanza limezungumzwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje, ambaye anazungumzia kuhusu Chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo, kiwezeshwe kifedha ili kiweze kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti. Waliozungumzia pia ni pamoja na Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi na Mheshimiwa Mohamed Missanga. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ushauri huu umezingatiwa na utekelezaji wake unategemea uwezo wa Serikali. Lakini ninataka niseme hapa kwamba tuliondoka hapa tukafuatana na Mheshimiwa Lubeleje pamoja na Kamati yake ya Katiba na Sheria, tukaenda mpaka Hombolo na kazi ambayo inafanyika pale waliipongeza, ni kazi nzuri. Ninawashauri

Wabunge wenzangu, mkipata nafasi, nendeni Hombolo mkaone kazi inayofanyika pale. Ni kazi nzuri na mtaona kwamba haya yanayosemwa na Waheshimiwa Wabunge, tayari yamekuwa *taken on board.* Kwa hiyo, jambo hili limeanza kufanyika na kazi inayofanyika pale ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, tukienda mbele utawala bora, uendeshaji wa miji midogo haueleweki vizuri, hivyo miji hiyo kutokidhi mahitaji ya utoaji wa huduma kwa wananchi. Hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Dokta Lucas Siyame wa Mbozi Magharibi. Tunasema Serikali inaendelea na mchakato wa kurekebisha Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura namba 287, iliyoanzisha Mamlaka ya Miji Midogo ili ziwezeshwe kukidhi mahitaji ya utoaji huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine inahusu usimamizi na matumizi ya mapato ya fedha za Serikali na hoja hii inazungumzia mfumo huu unaohitaji marekebisho, ikiwa ni pamoja na kuona jinsi ya kupunguza wingi wa akaunti za fedha katika Halmashauri za Wilaya. Hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Herbert Mntangi, wa Muheza na majibu yake ni kwamba Serikali imeliona hilo na iko kwenye mchakato wa kuzipunguza, isipokuwa zile zilizofunguliwa kisheria, kama za mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo, hizi tumesema kwamba zitaendelea kufuatana na sheria yenyewe inavyozungumza. Halmashauri zote nchini zimeelekezwa kuwa ifikapo Juni, tarehe 30 mwaka 2011, akaunti zitapunguzwa na kufikia angalau sita kwa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali pia imezungumziwa, Serikali ipunguze gharama za matumizi yake hasa kwa maeneo ya sherehe, tafrija, mapokezi, samani, magari na kadhalika. Hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim na Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya. Tunachosema hapa, suala hili limezingatiwa katika hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi na katika Mwongozo wa Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2010/2011, 2012/2013. Mmemsikia Mheshimiwa akisema kwamba sasa hata matumizi ya simu tutakuwa tunalipia kwa *Pre-paid* kwa maana ya kulipa kama tunavyolipa kwa *Luku.* Pia Serikali imeshatoa mwongozo kwa maana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuhusu warsha na semina kwamba kibali kitatolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu, baada ya kuridhika kuwa semina hizo na warsha hizo, kweli zinatuletea tija.

Mheshimiwa Spika, usimamizi na udhibiti wa mapato umezungumziwa, Serikali isilee uzembe katika maeneo ya kazi. Ipo Halmashauri ambayo imehamishia fedha katika akaunti ya amana, inayozalisha faida pamoja na kununua hisa bila ridhaa ya Halmashauri. Wazo hili limeletwa na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya na hoja ya Mheshimiwa Grace Kiwelu. Tunachojibu hapa, ni kuweka fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika akaunti ya amana, kunahitaji kuzingatia sheria na kanuni na taratibu za fedha zilizowekwa. Kinyume cha hapo, ni ukiukwaji wa sheria na anayefanya hivyo anastahili kuchukuliwa hatua. Tunachosisitiza hapa ni kwamba, kama kuna hela, ukichukua hela, ukaingiza katika *fixed deposit account,* ni lazima mkae kwenye kikao cha Halmashauri na

mseme kwamba mnafanya hivyo na mara nyingi hela zinazotegemewa, ni zile za *own source* ambazo wameweza kuzileta wao wenyewe, michango ya wananchi, ndio wanaweza wakaziingiza pale. Ni lazima kikao kile kiambiwe pia, kwamba hela hizo wakati ile amana itakapokuwa imeiva, itatumika kwa ajili ya kazi gani na inaingia katika *minutes.* Sasa tunaambiwa kwamba katika Halmashauri ya Iringa, alivyosema Mheshimiwa, kuna hilo tatizo. Nataka niahidi hapa, kwa niaba ya Waziri Mkuu, kwamba tutafuatilia jambo hili ili tujue kwa undani kwamba ni kitu gani kilichotokea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uboreshaji wa huduma za jamii, Serikali itatue tatizo kubwa la magari ya wagonjwa. Suala hili limeulizwa na Mheshimiwa Savelina S. Mwijage. Ninachosema ni kwamba Serikali inaendelea kuboresha huduma mbalimbali za afya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Itakumbukwa kuwa, mapema mwaka huu, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi yaani *UNHCR,* imetoa magari mawili ya kubebea wagonjwa katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa huduma za jamii pia umezungumziwa na Mheshimiwa Savelina na jibu lake ni hilo.

Mheshimiwa Spika, jengo linalotarajiwa kufunguliwa katika robo ya kwanza ya mwaka 2010/2011, ili kuweza kutekeleza kwa vitendo Sera za Chama cha Mapinduzi za kuongeza ajira kwa vijana, hii alikuwa anazungumzia kuhusu Serikali ifanye jitihada za kufungua jengo la Wamachinga Dar-es-Salaam, ili kuongeza ajira kwa vijana. Tunajibu hapa na ndio hiyo ninayosema kwamba jengo hilo linatarajiwa kufunguliwa katika robo ya kwanza ya mwaka 2010/2011 ili kuweza kutekeleza kwa vitendo Sera za Chama cha Mapinduzi za kuongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, Eng. Stella Manyanya amezungumzia kuhusu Wakandarasi wa uzoaji taka mijini, walipwe. Serikali ilishatoa maagizo kuhusu kulipwa Wakandarasi wote mjini na imeweka msisitizo katika Mwongozo wa Bajeti ya Mwaka 2010/2011, 2012/2013 kwa taasisi zote ili kuhakikisha mamlaka husika zinalipwa madeni yote na pia kutoendelea kilimbikiza madeni.

Mheshimiwa Manyanya, pia amezungumzia kuhusu zabuni za uzoaji wa taka mjini, zitolewe kwa makampuni ya nje ya nchi kwa sababu makampuni ya ndani yameshindwa kufanya kazi hiyo kwa ufanisi. Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004, inatoa maelekezo ya namna ya upatikanaji wa Mkandarasi wa kutoa huduma mbalimbali katika Halmashauri. Sheria hii haibagui mwombaji wa zabuni. Hata hivyo, ni muhimu kuwaendeleza Watanzania wenye kampuni badala ya kutegemea wazabuni kutoka nje ya nchi. Nasisitiza sheria hii izingatiwe kwa utoaji wa zabuni katika uzoaji wa taka mijini na usimamizi wake uweze kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, la hospitali ya Musoma, limeshajibiwa na Profesa Mwakyusa, kwa hiyo sisi tunazingatia hiyo na kama wanaona kwamba kuna hitaji la kuwa na Hospitali ya Mkoa, basi waingize katika bajeti yao.

Mheshimiwa Spika, kama unavyoona, muda unaniishia hapa, nimalizie, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, alizungumzia kuhusu soko la Tabora. Tunachojibu hapa nia kwamba tumelisikia na tunashauri kwamba, wana Tabora waangalie uwezekano wapate mkopo kutoka katika *Loans Board* ambayo iko katika *TAMISEMI* au *LAPF*. Tunaweza tukazungumza vizuri zaidi na tukasaidiana, kwa sababu nakumbuka swali hili liliwahi kuulizwa na Mheshimiwa Kaboyonga, kwa hiyo, tunaweza tukasaidiana.

Mheshimiwa Spika, naona muda umekwisha, basi naomba niunge mkono hoja. Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, muda ni mfupi. Msemaji anayefuata ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, ana haki yake ya dakika 30. Kama akiamua kuitumia haki hiyo, itakuwa tumepita muda mahsusi wa Bunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 28 (1). Kwa hiyo, natumia Mamlaka mliyonipa chini ya Kanuni ya 28(2), kuongeza muda usiozidi dakika 30 ili kumuwezesha Mheshimiwa Waziri wa Nchi – TAMISEMI, amalize maelezo yake, ambayo nadhani itafika kama saa saba na dakika saba hivi.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, karibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Awali ya yote, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nijibu masuala ya jumla halafu ndio niingie kwenye kwenye suala moja baada ya lingine. Suala la bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, yaani Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Mikoa pamoja na Serikali za Mitaa, naomba kuweka rekodi vizuri, wachangiaji wengi wanasema kwamba 80% ya fedha za Serikali zinaenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, ni 23% tu ya fedha za bajeti ya Serikali ndizo zinazopelekwa kwenye Serikali za Mitaa. *Simple arithmetic,* mimi sijui hesabu vizuri, kwamba bajeti ya Serikali ni shilingi trilioni 11, zinazoenda kwenye Serikali za Mitaa, yaani Mikoa pamoja na Halmashauri ni trilioni 2.7 kwa hiyo, kwa *calculations* hizo mimi nasema kwamba ni 23% na sio 80% kama alivyosema dada yangu Magdalena Sakaya.

Mheshimiwa Spika, la pili, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, alisema kwamba fedha za Serikali za Mitaa, haziwafikii walengwa. Mimi nasema kwamba fedha zinawafikia walengwa na ni wananchi wenyewe. Fedha hizo zinajenga Shule za Sekondari, Shule za Msingi, Vituo vya Afya na Zahanati, zinajenga barabara, ruzuku ya pembejeo, zinajenga visima na mengi mengineyo. Fedha hizi zinatoa huduma za jamii, wanaolengwa ni wananchi. Baada ya kujenga zahanati, anayetibiwa ni mwananchi na ndio mlengwa mwenyewe. Baada ya kujenga shule, anayesoma ni mtoto wa mwananchi

wa Tanzania. Sasa sielewi labda walitaka hayo mabilioni tuwagawie mtu mmoja mmoja? Mimi nafikiri tukitoa huduma za jamii kwa wananchi, kwa kufanya hivyo tumewapa wananchi moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine kwa ujumla ni la kuondoa umasikini. Kaka yangu Mheshimiwa Jussa, ameiosoma Ilani vizuri sana, ukurasa wa 157, akasema kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi, imesema hivi, itaondoa umasikini hatua kwa hatua, naomba kum-*quote* na imeandikwa hivyo. Sasa nikasema ndio, Chama cha Mapinduzi kwa miaka mitano kimeenda hatua kwa hatua. Umaskini hauondolewi kwa mwaka mmoja, miwili wala kumi, umaskini unaondolewa hatua kwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata wenzetu wa Marekeni walioendelea, Uingereza walioendelea, walienda hatua kwa hatua. Zinaitwa nchi zilizoendelea lakini mpaka sasa hivi hawakai wakisema kwamba sisi tumeshaendelea, kwa hiyo, hatufanyi chochote. Wanaendeleza teknolojia, wanaendeleza bajeti, wanafanya kila kitu, kwa ajili ya kuongeza maendeleo, hatuwaiti maskini, lakini maendeleo ni mchakato.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi tumesema, kwa mfano, tumeanza kujenga shule, ni hatua moja hiyo, tumejenga shule za sekondari kutoka 1000 mpaka 3000, hiyo ni hatua, hatua inayofuata, mkakati ameshautoa Prof. Maghembe, kwamba baada ya kujenga hizi shule, zahanati, sasa ndiyo tunaona kwamba tuna upungufu wa Walimu, maabara, wafanyakazi wa afya kama anavyosema Prof. Mwakyusa, kwa hiyo, hizo ndiyo hatua kwa hatua. Mimi nasema kwamba kupanga ni kuchagua hata sisi watu binafsi anaweza ukanunua Shangingi VX lakini anaishi nyumba ya kupanga lakini mwingine anachofanya yeye anajenga nyumba yake nzuri lakini anakalia kiti cha marimba, sasa kupanga ni kuchagua, Chama cha Mapinduzi kiliamua kujenga kwanza nyumba, *furniture* zinafuata baadaye. Kwa hiyo, hizo *furniture*, maabara na madawati, ndiyo hiyo miaka mitano ijayo tutaweza kutekeleza vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni watu kubedha kuhusu maisha bora kwa kila Mtanzania. Maisha bora kwa kila Mtanzania tuyagawanye katika sehemu kuu mbili, kiuchumi na kijamii. Kijamii ndiyo tunajenga shule, Zahanati, barabara, visima, huduma za jamii, zikishakuwa bora, basi kwa kila Mtanzania yanawezekana kwamba kila mtu anaweza akatibiwa, kila mtu anaweza akasoma, akaenda shule, kila mtu anaweza akapata maji ya kisima, ndiyo maisha bora yenyewe. Kiuchumi, mimi nasema kwamba tumejenga barabara, ukishajenga barabara tayari umemwezesha huyo Mtanzania kiuchumi. Ukitoa pembejeo, ina maana kwamba umemwezesha huyo Mtanzania, umempa ruzuku ya pembejeo. Sasa maisha bora kwa kila Mtanzania ana-*determine* mwananchi mwenyewe, wananchi wengine toka asubuhi mpaka jioni anacheza *pool*, bao, sasa huyu ategemea atakuwa na maisha bora kwa kila Mtanzania? Mwananchi mwenyewe ndiyo anayeamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine wanapewa ruzuku ya pembejeo, anapewa *voucher* anaenda kuuza, anakunywa pombe, sasa hayo maisha bora kwa kila Mtanzania huyu

yatawezekana? Kwa hiyo, ni mwananchi mwenyewe anaye *determine* kwamba maisha bora yatawezekana vipi. Mimi nawapa mfano mmoja tu. Ulanga, mwaka 2005, nauli ya kutoka Mahenge mpaka Dar es Slaam ilikuwa shilingi 25,000 barabara zimeboreshwa sasa hivi nauli imeshuka mpaka shilingi 15,000, ina maana kwamba tukiboresha hizo huduma tumemsaidia huyo Mtanzania. Kwa hiyo, kila mtu kwenye maisha bora anaangalia mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niingie moja kwa moja kwenye hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa upande wa utawala bora. Mheshimiwa Lubeleje wa Mpwapwa, amesema kwamba Wakuu wa Mkoa wahakikishe kwamba amani na utulivu vinakuwepo nchini kwetu. Mimi nasema kwamba Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Halmashauri zetu, zimefanya kazi nzuri sana, kazi ya ulinzi na usalama katika sehemu zote nchini, ndiyo maana nchi hii kuna utulivu, isingewa wao, utulivu usingekuwepo. Kwa hiyo, wanatimiza wajibu wao vizuri ndiyo maana kuna amani na utulivu. Mheshimiwa Rais kwenye kikao cha Wakuu wa Mikoa juzi pia hilo alilisitiza sana kwamba wahakikishe kunakuwa na ulinzi na usalama wakati wa uchaguzi. Kwa hiyo, wanatimiza wajibu wao na wanatekeleza vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, suala la pili la utawala bora ni la Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, ambapo alisema hela ziwafikie walengwa, mimi nasema kwamba zinapelekwa kule lakini sisi kama Serikali lazima tuongeze juhudi za kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatumika vizuri. Huu ni wajibu wetu na tuna mikakati mingi ya kuhakikisha kwamba fedha hizi zinawafikia walengwa moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi pia walizungumzia kuhusu suala la uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwamba haukuwa wa haki na huru. Mimi nasema ule uchaguzi wa Serikali za Mitaa ulikuwa wa haki na huru na tulishirikisha Vyama vyote vya Siasa, mchakato wake ulienda vizuri. Mimi nilifanya mkutano na Vyama vyote vya Siasa 17, tulikuwa nao pale Morogoro, tukakubaliana mambo tuliyokubaliana, tukawekeana saini, baada ya hapo nikaenda kutunga kanuni na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Ibrahim Lipumba alikuwepo pale akani-*challenge* kwenye vyombo vya habari kwamba nimekiuka yale makubaliano, nilimwambia naomba lete makubaliano, lete kanuni unionyeshe wapi ambapo nimekiuka, hakuweza kufanya hivyo mpaka leo, ina maana sikukiuka kicho chochote. Ule mchakato ulienda vizuri, tatizo letu zile kanuni bahati mbaya wengi huwa hawazisomi, ndiyo tatizo letu. Kwa hiyo, nasema hizo kanuni na sheria zikitoka, ni vyema tukazisoma kwanza kabla hatujatoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la utawala bora pia lilitolewa na Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga kuhusu Jiji la Mwanza kuwatumia Walimu kuwa Watendaji wa Vijiji. Suala hili tunasema hivi, mara nyingi Watendaji wa Vijiji au Watendaji wa Mtaa, wakiondoka kwenye sehemu zao za kazi, ni kweli tunamtumia Mwalimu kukaimu, kama Mtendaji ameenda kuchukua mshahara ili ofisi isibaki tupu, angalieni kwenye vijiji vyetu, nani ana uwezo zaidi ya Mwalimu? Kwa hiyo, tunawatumia Walimu angalau kukaimu kwa siku mbili tatu ili ofisi isibaki tupu, ni suala ambalo tunasema ni kukaimu kama wanavyokaimu wengine.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la utawala bora, ofisi za Wabunge zinazojengwa ziongezewe bajeti. Ni kweli, tulivyoanza ujenzi wa ofisi za Wabunge, tulianza milioni 25 sasa hivi tumeongeza mpaka milioni 40 ili kukidhi haja. Baadhi ya sehemu, kwa kweli wamejenga ofisi nzuri sana na baadhi ya sehemu, inategemeana na mazingira ya sehemu hizo. Kwa kweli hilo tunaliangalia. Kama Waheshimiwa Wabunge mnaona kwamba hizo shilingi milioni 40 hazitoshi basi tutaliangalia ili ziweze kuongezeka ili ofisi za Wabunge ziweze kujengwa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, pia suala la utawala bora, Serikali iimarishe Mabaraza ya Ardhi, kwa kweli tunasema kwamba tutaimarisha hayo Mabaraza ya Ardhi. Suala la kwamba Mabaraza ya Ardhi yanatoza ada kubwa sana, nachosema ni kwamba Mabaraza ya Ardhi kwa mujibu wa sheria, faini yake haitakiwi kuzidi shilingi 10,000 kama imezidi hapo ujue wamevunja sheria. Lakini pamoja na hayo, ofisi yangu ili kuondoa huo mkanganyiko wa Mabaraza ya Ardhi, ofisi yangu na ofisi ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, tunapitia upya kanuni na taratibu zilizoanzisha Mabaraza hayo ili kuyaimarisha zaidi.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa mapato na matumizi, kama ilivyokuwa kwenye maelekezo ya hotuba yangu ya kiutendaji, aya ya 24 na 25, Serikali inakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba ni kweli wakati umefika wa kuhakikisha kwamba tunadhibiti usimamizi wa mapato na matumizi. Ndiyo maana ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ina kitengo maalumu cha *inspection,* kukagua miradi mbalimbali ili kuangalia *value for money*. Kwa mwaka huu, kimekagua miradi ya maendeleo katika Mikoa kumi na tano, kuimarisha shughuli za Uhasibu na Ukaguzi wa Ndani, mipango na uhandisi na upande wa manunuzi, tumetoa mafunzo katika kada mbalimbali, Kamati ya *LAAC* imenisaidia sana katika kuangalia mapato na matumizi katika Halmashauri mbalimbali ili *value for* ionekane. Aidha, zoezi endelevu katika ngazi ya Mkoa na Serikali za Mitaa la kukagua miradi ili kuangalia *value for money,* kwa kweli linaendelea na tunazidi kusisitiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, Serikali imeongeza mamlaka ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, atasimamia matumizi ya fedha za Serikali za Mitaa yaani pale kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali kutakuwa na Mhasibu Mkuu ambaye atashughulikia fedha za Serikali za Mitaa tu. Kwa hiyo, hizo ni hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali. Aidha, Waheshimiwa Wabunge, niwaombe, wote ni Wajumbe wa Kamati ya Fedha, wote ni wajumbe wa Mabaraza ya Madiwani, mnapoona tatizo lolote kwenye Mabaraza, ni vyema tukawasiliana ili tuyatatue hayo matatizo mapema kabla hayajafikia mahali pabaya.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wameliongelea, ni uboreshaji wa huduma za jamii ambalo naona limeshajibiwa na Mheshimiwa Mwanri, Naibu Waziri wangu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nilitaka kutolea ufafanuzi, ni uboreshaji wa hospitali zetu, nafikiri Mheshimiwa Mwakyusa ameliongelea vizuri, kuhusu uboreshaji wa hospitali zetu na hata kwenye hotuba yangu, nimeonyesha ni wapi ambapo tunaendelea na ukarabati wa hospitali zetu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni elimu, ameshalitolea ufafanuzi Mheshimiwa Waziri wa Elimu.

Mheshimiwa Spika, suala la nafasi ya Mbunge katika mamlaka za Serikali za Mitaa, limeongelewa na Mheshimiwa Mntangi, tunasema kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Sura ya 287 na 288, Mwenyekiti au Meya wa Halmashauri, huchaguliwa na Madiwani wote akiwemo Mheshimiwa Mbunge mwenyewe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ni Diwani kwa nafasi na ni mjumbe wa Baraza la Madiwani linaloongozwa na Mwenyekiti au Meya wa Halmashauri. Kwa kuzingatia maelekezo hayo, si kweli kuwa Mwenyekiti au Meya amepewa nafasi ya kujijengea mazingira ya kuwa na madaraka makubwa zaidi ya aliyonayo. Viongozi hawa wanafanya kazi kulingana na sheria na taratibu za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya utawala, Wizara iunde hilo, Mheshimiwa Jackson Makwetta, amesema kwamba Wizara ya Maendeleo ya Vijiji iundwe, tunasema kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, muundaji wa Wizara, ni Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, amelisikia, kama kuna haja ya kufanya hivyo, naona atafanya hivyo kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tena maeneo ya utawala, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa John Lwanji, wanasema kwamba idadi ya watu isiwe kigezo pekee cha ugawaji wa maeneo ya utawala. Kwenye jibu letu tunasema vigezo vinavyozingatiwa katika kugawa Wilaya sio idadi ya watu peke yake, vigezo vingine ni pamoja na ukubwa wa eneo, Tarafa zisizopungua tano, kata zisizopungua kumi na tano na vijiji visivyopungua 45. Aidha, jiografia ya maeneo husika inazingatiwa sana. Kwa mfano Liwale, Liwale ni kubwa sana lakini ina watu wapatao 75,000 tu, ina mbuga ya Selous, kwa hiyo, tungehesabu na wale wanyama kwa kweli wangekuwa wengi sana lakini sehemu kubwa imekaliwa na wanyamapori. Kwa hiyo, vigezo hivi vinaangaliwa lakini mgawaji wa maeneo ya utawala, sisi tumeanza na vitongoji, vijiji, mitaa, kata ndiyo tumeishia hapo, Mikoa, Wilaya, Tarafa jamani ni mamlaka ya Rais. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais akiona kwa wakati unaofaa, anaweza akatangaza Tarafa, Wilaya na Mikoa kwa wakati muafaka. Hilo tunamwachia yeye mwenyewe, anasikia.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mpaka wa Malawi na Ziwa Nyasa, naomba niliache kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa sababu yeye ndiye anayeshughulikia masuala haya.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na tatizo pia la utawala bora, hao ma-*VEO* na ma-*MEO* na hao Watendaji wa Kata kule chini, ni Miungu Watu, wavunjaji wa sheria, madikteta, na maneno mengi ambayo yameelezwa na Waheshimiwa Wabunge, mmojawapo ni Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa. Tunasema jukumu la Watendaji wa Vijiji na wa Kata, ni kuhakikisha kwamba utekelezaji wa mipango ya vijiji na maelekezo mengine ya Serikali, yanazingatiwa kwa mujibu wa sheria na sio kupiga watu wala kunyanyasa watu. Kama ikitoea hivyo, jamani toeni taarifa ili waweze kuchukuliwa hatua hata za Kimahakama, mkituletea kwetu, Halmashauri husika ziwachukulie hatua za kinidhamu. Kwa kweli sisi kwa ujumla hatupendi wananchi wetu wanyanyaswe ndiyo maana hata katika michango Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kabisa kwamba jamani michango iwe na mipaka, wakati wa kilimo acheni wananchi walime, wakati wa mavuno ndiyo mnawadai michango mbalimbali na sehemu nyingi wanazingatia hilo. Lakini wananchi wengine ni wajanja, wakati wa mavuno anakataa, ana-*delay* kwa makusudi, anangojea wakati wa masika ili apate kisingizio kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema sasa hivi tusibugudhiwe. Kwa hiyo, wanakuwa na *record* maalum kwamba ni kipindi gani na nani walimfuata, kama alikataa, kwa hiyo, anachukuliwa hatua kipindi hicho hicho cha kilimo kwa sababu alikataa wakati ule wa mavuno.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maslahi ya Waheshimiwa Madiwani, tunasema kwamba maslahi ya Madiwani yameshughulikiwa kwa kiasi kikubwa kwa sababu walikuwa na madai makubwa manne, posho ziongezwe; kupata angalu kiunua mgongo; kuwekwa kwenye Mfuko wa Bima ya Afya na kukopeshwa na kuondolewa kodi katika vyombo vya usafiri. Mambo yote haya matatu tumeyatekeleza vizuri. Waheshimiwa Wabunge, mnajua kabisa kwamba posho zimeongezeka na pili tumewaingiza kwenye Mfuko wa Bima ya Afya na tatu watalipwa *gratuity* kutokana na miaka mitano waliyotumikia Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lililobakia ni la kupata *exemption* kwenye vyombo vya usafiri. Waheshimiwa Wabunge, hili linashughulikiwa na mimi nina uhakika kwamba ufumbuzi utapatikana. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge watuamini kama hayo mengine matatu tumeyatekeleza vizuri, hilo moja haliwezi kutushinda, maslahi yao yataangaliwa muda hadi muda.

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo mapya ya utawala, kuna suala la Wilaya ya Ilemela na Nyamagana kuwa Manispaa, hilo tunalifanyia kazi. Tunataka tuwashirikishe wadau kwa karibu sana ili tuweze kupata muafaka kwa sababu suala la mipaka kwa kweli lazima uwashirikishe wananchi, huwezi tu ukahamisha kijiji kutoka hapa kwenda mahali pengine, hii kwa kweli inaleta matatizo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la mwisho ambalo nataka kuliongelea, ni suala la ugawaji wa kata. Waheshimiwa Wabunge, tumetumia demokrasia ya hali ya juu katika ugawaji wa kata. Tuliwaambia Wakurugenzi mara ya kwanza kwamba leteni maombi yenu, tukakumbusha tena mara ya pili kwamba leteni wakaleta. Tukafanya mkutano wa

Wakurugenzi wote kwamba Wakurugenzi wote jamani mje mhakikishe kata na vijiji kama vimo, wamekuja tumehakiki moja baada ya lingine, kwa Wakurugenzi waliokuwa makini, mambo yao hayakuwa na matatizo yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Waheshimiwa Wabunge, Bunge lililopita, Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliniamuru nihakikishe kila Mbunge anaangalia Kata zake. Jamani Waheshimiwa Wabunge, nimegawa hivyo vitabu, waliosahihisha, wamesahihisha na sasa hivi ndiyo tumegawa hizo kata. Baada ya kugawa hizo *GN,* imetoka mwezi wa nne, vitabu tumetoa bado watu wanaleta maombi, kwamba Kata yangu imesahaulika na mengineyo. Jamani sheria inasema hivi, Kata zitagawanywa miezi sita kabla ya uchaguzi mkuu. Mkiniambia mimi sasa hivi nigawe Kata au Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninyi hao hao mtakuja kutu-*challenge* kwamba haikuwa miezi sita kabla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaomba radhi wale wote ambao Kata zao hazikugawanywa, demokrasia tuliyoitumia ni ya hali ya juu sana, kwa kweli, watatusamehe. Kwa sasa kipindi kimepita, tumefunga. Kila kitu kina mwisho wake na sisi tunafanya kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, Kata zile ambazo zimesahaulika kwa njia moja au nyingine, tunaomba radhi hatutaweza kufanya lolote kwa wakati huu mpaka uchaguzi mkuu uwe umekwisha. Ndugu Kilavi sasa hivi yuko na Wakurugenzi wote Tanzania nzima kule Dar es Salaam, wanaona mipaka ya Kata sasa ikoje, hatuwezi tukamwigilia tena, kazi imeshakwenda kwenye Tume ya Uchaguzi ya Taifa, hatuwezi tukafanya lolote kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kweli wamenilea kiasi cha kutosha. Wamenipika nikapikika na mimi nasema kwamba nafuata nyayo zao na nafuata maelekezo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Mwanri, wenyewe mnamuita ‘Jemedali wa siasa’ kwa kweli namtumia vizuri sana, namtumia kwenye Mikoa na Wilaya mbalimbali ili aweze kunisaidia katika kazi mbalimbali na ananisaidia vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Katibu Mkuu, Katibu Mkuu, ni mama mwenzangu. Wale wanaosema kwamba akina mama hawawezi wakafanya kazi pamoja, sisi tumefanya kazi kwa miaka mitano kwa amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru Manaibu Katibu Wakuu, Ndugu Maswi na Ndugu Sagini, kwa kweli wamefanya kazi nzuri. Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ndugu yangu Lyimo, amefanya kazi nzuri ya kutusaidia. Naibu wake, Ndugu Mbonde, ametusaidia sana katika ushauri mbalimbali. Wakuu wa Mikoa, wamefanya kazi nzuri sana na ninyi wenyewe mmeona Wakuu wa Wilaya pamoja na Wakurugenzi. Upo upungufu ambao tumeubaini na tumeainisha kwenye hotuba yetu kwamba upo upungufu wa hapa na pale, tutaushughulikia hatua kwa hatua. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Marmo tumefanya kazi karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru kipekee wewe mwenyewe, kwanza, ulikuwa ni mpiga debe wangu wakati nikiwa Naibu Waziri, ulikuwa unasema kwamba, 'una uhakika huyu Naibu Waziri baada ya muda ataibuka' na kweli maneno hayakuishia kwenye maji, yamenifikisha hapo nilipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, tumeshirikiana vizuri sana, mashahidi Wabunge wa upande wa Upinzani na CCM, tumeshirikiana kwa vizuri sana na Waheshimiwa Mawaziri wenzangu.

Mheshimiwa Spika, mwisho niishukuru familia yangu, Mheshimiwa Spika, alisema nilimshukuru mume wangu Ahmed Pongolani, sikuwashukuru mawifi, mimi nasema nawashukuru. Pia nawashukuru watoto wangu na ndugu zangu. Mwisho, nawashukuru wapiga kura wa Jimbo la Ulanga Mashariki, niliyoyafanya wameyaona, upungufu upo, mimi nawaomba wazidi kuendelea kunichagua ili miaka mitano mingine tuweze kufanya kazi kwa pamoja na niweze kuingia tena hapa kwenye mjengo kuwawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa ufafanuzi mzuri kabisa. Sisi Wazee tulijua tu kwamba wewe utafika mbali na maneno ya Wazee huwa hayadondoki chini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kazi tuliyojipangia kufikia mchana huu, ndiyo tumefikia hapo. Ninalo tangazo muhimu, wajumbe wote wa Tume ya Huduma za Bunge, tukutane kesho saa tano katika ukumbi wa Spika kuzingatia mambo muhimu sana ya sisi Wabunge.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.07 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha shughuli za Bunge pale mchana ilikuwa imebaki sasa tuweze kumsikiliza Mtoa Hoja ambaye ni Mheshimiwa Waziri

Mkuu wetu. Kwa hiyo, kwa heshima na taadhima, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu sasa aje ahitimishe hoja yake, Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha na kunipa afya njema hadi jioni ya leo ninapohitimisha majadiliano ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Taasisi zilizo chini ya Waziri Mkuu pamoja na Ofisi ya Bunge, kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana wewe mwenyewe, Naibu Spika na Wenyeviti wote, kwa kusimamia kwa umakini mkubwa majadiliano ya Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake. Kwa namna ya pekee, niwashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote, kwa michango yenu ya kina ambayo imefanikisha kwa kiasi kikubwa kazi ambayo ilikusudiwa tuifanye.

Mheshimiwa Spika, katika mjadala huu, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 179 walichangia, Waheshimiwa Wabunge 70 walichangia kwa kuzungumza moja kwa moja hapa Bungeni na Wabunge 109 wamechangia kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, hoja ni nyingi, tumejitahidi kujibu baadhi na zimebaki nyingi. Wizara nazo zimejitahidi kujibu lakini na wenyewe hawakuweza kumaliza zote, matumaini yangu ni kwamba wataziendeleza wakati wakiwasilisha hotuba za bajeti zao.

Mheshimiwa Spika, hata baada ya kufanya hivyo, bado naamini hoja nyingi zitaendelea kubaki. Nataka niahidi Bunge lako Tukufu kwamba hoja zote hizi kwa ujumla wake, zitaandaliwa katika maelezo ya maandishi na zitagawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuendelea kutoa ufafanuzi katika baadhi ya maeneo, niruhusu kwanza niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale waliochangia kwa maandishi kama ifuatavyo. Waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Mheshimiwa Dr. Willibrod P. Slaa, Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Mbunge wa Karatu, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mbunge wa Same, Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, kutoka Kilombero, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Viti Maalum, Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, Viti Maalum, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Viti Maalum, Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, Kuteuliwa, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Shinyanga Mjini, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani na Mheshimiwa Gosbert B. Blandes Mbunge wa Karagwe. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa John P. Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame, Mbunge wa Mbozi Magharibi, Mheshimiwa Prof. Philemon N. Sarungi, Mbunge wa Rorya, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mbunge wa Babati, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mbunge wa Kigamboni na Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah, Mbunge wa Mafia, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mbunge wa Nzega, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Viti Maalum, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mbunge wa Temeke, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mbunge wa Misungwi na Mheshimiwa Aziza S. Ally, Mbunge Viti Maalum. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Muyuni, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mtambile, Mheshimiwa Halima O. Kimbau, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mbunge wa Longido, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini na Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mbunge Viti Maalum. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa, Mbunge wa Ulanga Magharibi, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mbunge wa Vunjo, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba na Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Bujibu P. Sakila, Mbunge wa Kwimba, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mbunge wa Kyerwa, Mheshimiwa Janet B. Kahama, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mbunge wa Kibiti, Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mbunge wa Ngorongoro, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Kusini, Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mbunge Viti Maalum na Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mbunge Viti Maalum. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, Mbunge wa Simanjiro, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mbunge wa Hai, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Mbunge wa Igalula, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Prof.

Jumanne A. Maghembe, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Dr. Shukuru J. Kawambwa, Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Phillip S. Marmo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Celina O. Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella, Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Samuel M. Chitalilo, Mbunge wa Buchosa, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mbunge wa Muheza, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Wete, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mbunge wa Chonga, Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, Mbunge wa Kilwa Kaskazini na Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mbunge wa Gairo. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mbunge wa Handeni, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Athuman Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mbunge wa Ilala, Mheshimiwa Ephrahim N. Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla, Mbunge wa Kilolo, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mbunge wa Makete, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki na Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mbunge wa Kigamboni. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mbunge wa Rombo, Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi, Mheshimiwa Eng. Fuya G. Kimbita, Mbunge wa Hai, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Omar Ally Mzee, Mbunge wa Kiwani, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Kusini, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, Mheshimiwa William H.Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Said Msabaha, Mbunge wa Kibaha Vijijini, Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhil, Mbunge Viti Maalum na Mheshimiwa James D. Lembeli, Mbunge wa Kahama. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, Mheshimiwa Rajab Ahmad Juma, Mbunge wa Tumbatu, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mbunge wa Karagwe, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Mbunge wa Nachingwea, Mheshimiwa

Jacob D. Shibiliti Mbunge wa Misungwi, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mbunge wa Iramga Mashariki, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni, Mheshimiwa Omari Shaabani Kwaangw' Mbunge wa Babati Mjini na Mheshimiwa Col. Feteh Saad Mgeni, Mbunge wa Bumbwini na Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Riziki O. Juma, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mbunge wa Ileje, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, Mheshimiwa Dr. Maua A. Daftari, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Fatma Abdalla Tamim, Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa na Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Viti Maalum. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Joyce M. Masunga, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame, Mbunge wa Mbozi Magharibi, Mheshimiwa Eng. Mohammed Habib Juma Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mbunge wa Ole, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini na Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mbunge Viti Maalum. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Felister A. Bura, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mbunge wa Nzega, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Mbunge wa Mwanga, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Mtambwe, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa Halima O. Kimbau, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mbunge Viti Maalum na Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Bujibu P. Sakila, Mbunge wa Kwimba, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, Mbunge wa Kilosa, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mbunge wa Temeke, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mbunge wa Bariadi, Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushashu, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mbunge wa Koani, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mbunge wa Kilombero na Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mbunge wa Bukombe. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu, Mbunge wa Hanang, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mbunge wa Mtoni, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mbunge wa Matemwe, Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara, Mheshimiwa Marim Salum Mfaki, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mbunge Viti Maalum na Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mbunge Viti Maalum. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Mbunge wa Igalula, Mheshimiwa Teddy Louise Kasella - Bantu, Mbunge wa Bukene, Mheshimiwa Halima M. Mamuya, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan, Mbunge wa Kinondoni, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mbunge wa Kongwa na Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, nafurahi kukufahamisha kwamba, muda wote uliotumia kuwataja majina, hautahesabiwa katika muda wako wa kujibu hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Afadhali.

**SPIKA:** Kwa hiyo, kuanzia sasa ndiyo una dakika zisizozidi sitini.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, inawezekana katika majina haya, kuna mengine tumeyasahau, kama tutakumbushwa basi tutalitambua vilevile.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba muda wa kujadili bajeti ulikuwa mfupi, idadi hii kubwa ya wachangiaji, inaonyesha jinsi ambavyo Waheshimiwa Wabunge mnavyoweka umuhimu katika majukumu yanayotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake, wote tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa jinsi mlivyochambua kwa kina utekelezaji wa shughuli za Serikali, mmefuatilia kwa karibu utekelezaji wa Serikali, mmedai taarifa mbalimbali na mmezijadili kwa lengo la kujiridhisha kuhusu ufanisi katika utendaji wake. Aidha, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kumpongeza Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali yake, kwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nawashukuru wote walioonyesha pale tulipofikia katika utekelezaji wake na pia niwashukuru wale wote walioonyesha maeneo ambayo hatukuweza kuyafikia kiutekelezaji. Kwangu mimi, michango yote inatusaidia kufungua macho na kuona zaidi kile ambacho wananchi wanategemea kutoka kwa viongozi wao na Serikali yao kwa

ujumla. Aidha, inatuonyesha kile ambacho wananchi wamefanikiwa kupata na pale ambapo bado tunahitaji kupafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii tena, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa michango yao mmoja mmoja na kwa nia nzuri ya kulisaidia Taifa letu na wananchi wake. Mimi ninaamini kwamba mijadala yote inatusaidia kujua maeneo ambayo tumefanya vizuri na yale ambayo hatukufanya vizuri tuendelee kujipanga, tuweze kufanya vizuri. Aidha, kwa wote walioipongeza Serikali, pongezi hizo tutazitumia kuimarisha utendaji wetu wa kila siku na vilevile kwa Serikali yote kwa ujumla. Kwa ufupi, nasema ahsanteni sana kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukurani hizo, naomba pia uniruhusu nitoe angalau dukuduku langu moja kwa Watanzania wenzangu. Wako baadhi yao na wengine wamo humu Bungeni ambao wamekuwa kwa muda mrefu hivi wanadiriki kubeza baadhi ya juhudi ambazo Serikali imefanya hadi hivi sasa na kuonyesha kana kwamba hapa tulipo, ni pabaya zaidi, duni zaidi, ni mahali panapotisha zaidi na panakatisha tamaa zaidi kuliko hata huko tulikotoka. Mimi binafsi siamini kuwa kauli hizi ni za dhati. Naelewa kuwa, wapo Watanzania waliozaliwa kabla ya uhuru, wako wa kipindi kati ya Uhuru na Muungano, wako pia waliozaliwa kati ya Muungano na miaka ya sabini, wako pia wa kizazi kipya. Inawezekana kabisa kwa wale wote ambao hawakuzaliwa huko walikozaliwa hawa wazee waliotutangulia isiwe rahisi sana kuona tumetoka wapi na tunakwenda wapi na kwa bahati mbaya baadhi ya kauli hizi zinatoka hapa Bungeni, kwa hiyo, ndiyo kusema wako katika makundi haya. Kwa wale waliozaliwa baadaye, ni dhahiri hawawezi kujua yaliyowasibu wa enzi hizo isipokuwa kwa kuelezwa au kusoma historia. Hali kadhalika, kwa waliozaliwa nyakati nyingine zilizofuata itakuwa hivyo hivyo. Ni dhahiri kuwa, kauli za namna hii, kwa muono wangu, wakati mwingine zinavunja moyo, zinakatisha watu tamaa na zinafanya ionekane kana kwamba hakuna matumaini ya kwenda mbele. Lakini ukweli uliopo ni kwamba Tanzania imepiga hatua kubwa ya maendeleo na ninalisema hili kwa sababu hata wadau wetu wa maendeleo wanakubali kwamba Tanzania imefanya juhudi kubwa katika kuwasaidia wananchi kujiletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nieleze basi angalau maeneo machache ambayo wote tungepaswa kuyakiri. Kwanza, ni namna ambavyo Serikali chini ya Chama cha Mapinduzi, imeweza kuiongoza nchi hii kwa kipindi chote hiki katika hali ya amani na utulivu mkubwa kabisa wa kisiasa. Leo tupo hapa tunajivuna kwa kuwa na demokrasia iliyopanuka, mfumo wa vyama vingi, uhuru mkubwa sana wa watu kwenda wanakotaka na kusema wanalotaka, umepanua sana wigo wa vyombo vya habari wakati mwingine watu wanafikiri kwamba pengine tumetoa uhuru kupita kiasi.

Mheshimiwa Spika, pili, maisha ya wananchi. Nimekuwa najiuliza sana hivi, ni kweli haya yanayosemwa? Hebu tazameni huduma za jamii nini kimefanyika? Hivi ni kweli kwamba wale waliokuwepo mwaka wa 1961 wakati wa uhuru hali ya huduma za elimu zilikuwa kama zilivyo leo? Hali ya huduma za afya, ni kweli zilikuwa kama zilivyo leo? Mimi siamini kama ni kweli.

Mheshimiwa Spika, hebu tazameni hali ya miundombinu ilivyo nchini Tanzania sasa, hivi ni kweli juhudi zote hizi ambazo zimefanyika si chochote, hazina maana na kwamba hazimsaidii Mtanzania? Mimi siamini hivyo.

Mheshimiwa Spika, hebu tazameni vilevile hatua tuliyopata katika matumizi ya TEKNOHAMA, mawasiliano yameongezeka, simu za mkononi zimeongezeka, sasa hivi mnazungumza *internet* na vitu vingine chungu nzima, hivi ni kweli hakuna kilichofanyika kwamba hali ni bora kuliko ilivyokuwa siku za nyuma kuliko leo?

Mheshimiwa Spika, hata upeo wa Bunge lako ni tofauti kabisa na siku za nyuma, mijadala ninayoisikia hapa na hoja zinazotolewa hapa, ni kielelezo tosha kwamba mliomo humu, ni watu sasa ambao mmepea na mmepea kwa sababu wengi wenu mmesoma kutoka katika shule ambazo zimejengwa chini ya Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu, nimejitahidi kujaribu kufanya mapitio ya mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya matumizi ya fedha za Ofisi yangu na ya Bunge, nimejaribu sana kutumia kipindi kirefu sana kujaribu kuonyesha ni kiasi gani nchi hii hata kwa kutumia mfano huu wa kipindi tu cha uongozi wa Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, ni mambo gani tumeyafanya na kwa kiwango gani? Nashukuru sana, kwani wako Wabunge ambao wamekiri kwamba kazi iliyofanyika ni nzuri lakini wapo bado wenzangu wanaosema yote haya ni lelemama tu. Ndiyo maana baadhi ya wachangiaji hapa wametukumbusha wimbo wa “Mtoto acha kupiga mayowe, acha watu waone wenyewe”. Wengine wakasema, “Wana macho lakini hawaoni na wana masikio lakini hawasikii”. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niseme vilevile kwa kuwambusha tu iko ile hadithi moja ambayo wengi tunaijua ya Sungura Mjanja, kashindwa kupata ndizi zilizoiva, aliposhindwa akasema aah, kwanza hazikuiva, akaondoka anasononeka, anatukana, analaani lakini ukweli ukabaki palepale kwamba, ni kwa sababu ameshindwa kuzifikia zile ndizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa Uhuru, tulikuwa na Chuo Kikuu kimoja tu, leo tuna vyuo 32, tena kana kwamba haitoshi Bunge lako hili liko pua na mdomo na Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu ambacho sasa hivi kimeshadahili wanafunzi zaidi ya 10,000, Chuo Kikuu kikubwa kuliko vyote hapa nchini. Wote wanaokwenda hawaamini kwamba, ni nchi yetu imefanya haya, hawaamini zaidi kwamba hili limefanywa na Serikali kwa kutumia vyanzo vyake. Lakini bado watu wanasema yote haya si chochote, aah, basi tutamuachia Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatoa rai hii kwa Watanzania wenzangu, nikiamini kabisa kwamba katika kuyasema haya, nimejitahidi kusema bila kujali jinsia, itikadi zetu za kisiasa na imani zetu za dini. Nimejaribu kuonesha tu kwamba, kama yapo mazuri

ambayo yamefanywa na mwenzenu mmoja ni vyema kwa uungwana tukaamua kumpongeza huyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi, naomba sasa uniruhusu nipitie baadhi ya maeneo ambayo nadhani ni vizuri nikayasema. Eneo moja lililopata michango mingi ni la kilimo. Wako waliotushauri vizuri sana na ushauri wao ninataka nikuhakikishie Mheshimiwa Spika, tutauzingatia.

Mheshimiwa Spika, wako vilevile mmoja mmoja, waliyoyasema ambayo siyo mazuri sana, mengine kwa kubeza lakini ninataka nikuhakikishie kwamba Serikali imedhamiria kwa kuleta mapinduzi ya kweli ya kilimo kwa maana ya kilimo cha mazao ya chakula na biashara, mifugo, uvuvi na raslimali zinazotokana na misitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Rais Jakaya Mrisho Kikwete, tumeona tuyape kipaumbele maeneo haya kwa kuwa Watanzania wengi ndiko wanakotegemea. Nakubali kwamba katika bajeti hii, kilimo kimepewa kipaumbele cha nne. Lakini naomba vilevile niseme kwamba, hivi ni nani asiyeona kwamba, pamoja na kufanya kilimo kuwa kipaumbele yako mambo mengi ambayo tumeyataja yatakayosaidia sana katika kuongeza ufanisi wa kilimo. Moja, ni ongezeko la bajeti, lakini pili ni juhudi ambazo tumezifanya kupunguza baadhi ya kodi pamoja na maeneo mengine ili kuvutia uwekezaji katika eneo hili. Lakini pili ni kwamba, kwa hapa tulipofika kwa nini mtu uone tatizo kuwa na bajeti ambayo kipaumbele chake ni katika elimu? Tumefanya makubwa, tunahitaji kuyaimarisha na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, asubuhi ametoa ufafanuzi mzuri sana. Lazima haya mafanikio tuliyoyapata sasa tuyaimarishe, tuhakikishe tunajenga sasa nyumba za Walimu, tuhakikishe tunajenga maabara nyingi na tuhakikishe vilevile sasa miondombinu ya msingi inakamilika na kuimarishwa vizuri. Lengo la Serikali ya Awamu ya Nne, si kukibeza kilimo, ni kutaka itambulike tu kwamba, pamoja na yote yanayosemwa dhamira ya Serikali iko palepale na tuna hakika tutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali hii, bado ninaamini kwamba wote sasa tunafahamu kwamba, Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika eneo hili la kilimo azma yake kupitia Kilimo Kwanza ni dhahiri na mimi nataka niseme uamuzi huu ni wa dhati kabisa na tumedhamiria kushirikisha sekta binafsi kwa nguvu sana pamoja na taasisi nyingine za fedha na wadau wengine ili kuweza kuongeza uwezo wa sekta hii katika kuchangia katika pato la Taifa na mimi ninaamini tutafika huko.

Mheshimiwa Spika, tangu uamuzi wa kutekeleza azma hii, yapo mambo mengi yamefanyika. Hata hivyo, ipo hoja kwamba utekelezaji wa Kilimo Kwanza haujapewa kipaumbele kwa maana ya kuwepo Mabwana Shamba, mbolea, mbegu bora za kisasa na uratibu maalum wa Mikoa yote. Aidha, tunahitaji uhakiki wa miundombinu, masoko na bei nzuri. Tunakubali na tunayafanyia kazi chini ya uongozi wa kiongozi thabiti kabisa Mzee wangu Stephen M. Wasira, haya yote ni baadhi ya maeneo ambayo tumeyapa kipaumbele kikubwa sana. Ndiyo maana tumeamua kutoa ruzuku ya mbolea, madawa na

mbegu bora, tumeamua kuongeza idadi ya wagani na bajeti ya umwagiliaji, tumeamua ununuzi wa zana za kilimo upewe kipaumbele, tumeamua kuanzisha Benki ya Kilimo kwa madhumuni hayo hayo. Vile vile Wizara, Mikoa na Wilaya zimeagizwa kuweka mipango ya utekelezaji na tayari mipango ipo kwenye mipango ya mwaka 2010/2011. Vilevile sekta binafsi kama nilivyosema sasa imehamasishwa ili ishiriki kikamilifu katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2010/2011, sekta ya kilimo imepewa kipaumbele na hivyo kupewa vivutio vifuatavyo, msamaha wa kodi katika usafirishaji wa bidhaa za kilimo, ikiwa ni pamoja na miwa, katani na chai; msamaha wa kodi kwa mashine za zana za kukusanyia mazao ya maziwa; msamaha wa kodi ya *VAT* kwenye zana za kilimo ikiwa ni pamoja na *combine harvesters*, *hay making machines* na *mores*; ushuru wa asilimia sifuri (*zero rated VAT*) kwa mafuta ya kupikia yanayozalishwa humu nchini; msamaha wa kodi kwa vifungashio vya juisi na mazao ya maziwa; kutoza ushuru wa mazao kati ya 3% -5% kwa vyakula vya mifugo na mashudu na msamaha maalum wa vifaa vya mifugo na Madaktari wa Mifugo. Yote haya ni katika kuonesha dhamira ya Serikali ya Awamu ya Nne katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, yapo malalamiko vilevile kuhusu *power tillers.* Mheshimiwa Waziri alilieleza vizuri sana asubuhi hii na mimi ninataka tu niongeze kwamba, wakati mwingine tofauti zinatokana na wapi matrekta hayo yametoka. Mengine yanatoka China, mengine yanatoka Japan, yako yanayotoka India, kwa hiyo, hii zote ni namna ambazo zinasababisha gharama hizi ziweze kubadilika. Hata hivyo, Serikali imekwishaliona hilo, tunalifanyia kazi na tunaamini kabisa, tutaweza kusimamia vizuri zaidi ili bei za vifaa hivi zisiwe kubwa kuliko matarajio ya Watanzania. Nataka niwakumbushe kwamba, Tanzania inahitaji wastani wa matrekta 18,000, sasa hivi tunayo karibuni 9,500 tu. Tunaagiza wastani wa trekta 200 mpaka 300. Hivi sasa inakadiriwa kwamba tuna majembe ya kukokotwa na wanyama ‘plau’ 820,000, mikokoteni milioni 1.3 na inakadiriwa kwamba tuna majembe ya mkono takribani milioni 14. Hii ni dalili wazi kabisa kwamba ni lazima kasi katika eneo la kilimo iongezwe na tuweze kufanya vizuri zaidi katika miaka inayokuja.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu, nimejaribu kueleza juu ya programu mpya iliyobuniwa na benki yetu ya *CRDB* kuhusu utaratibu wa kusaidia kubeba wanafunzi pale mjini Dar es Salaam. Nataka nirudie nilichosema kuipongeza sana Benki hii kwa jambo hili zuri na mimi nitalifanyia kazi kuhakikisha kwamba, suala la kodi linatizamwe ili iweze kuwa ni mchango mkubwa katika eneo hili, ili watu wengi zaidi katika sekta binafsi waone namna ya kuchangia katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo hili halina budi kwenda sambamba na jitihada nyingine za kupunguza msongamano jijini Dar es Salaam na moja ya mpango kabambe tulionao ni ule wa mabasi yaendayo kwa kasi. Sasa jambo hili limezungumzwa kwa muda mrefu lakini sasa nataka niwahakikishie Watanzania kwamba, jambo hili sasa karibu litakamilika na utaratibu wa kujenga utaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tayari tumeshapokea dola za Marekani milioni 122 baada ya kuweka saini mkataba. Lakini vilevile nataka niwaarifu Watanzania kwamba, barabara tunazotarajia kuzijenga zina urefu wa kilomita 20.9 ikiwa ni upanuzi wa barabara ya Morogoro kuanzia Kimara hadi Kivukoni na barabara ya Kawawa kuanzia Magomeni hadi Moroco katika hatua ya kwanza. Barabara nyingine zitafuata baada ya hapo.

Mheshimiwa Spika, katika hatua hii vilevile tutafanya ujenzi wa vituo vya stesheni za mabasi (*bus stations*) vitano. Vituo vikubwa 29 na vituo vidogo sita na karakana mbili za kuegesha mabasi (*depots*) na kwa sasa tayari tumeshatiliana saini mkataba kwa ajili ya kuanza kuhamisha nguzo za umeme za *TANESCO*, ambao uliwekwa tarehe 31 Mei, 2010 na mkandarasi anaendelea na hilo zoezi. Jumatatu tarehe 21, tutawekeana saini kwa ajili sasa ya kuanza ujenzi wa kituo cha Kivukoni na mkataba wa ujenzi wa vituo vingine 29. Ni matumaini yangu kwamba, mpango huu utakapokamilika, utasaidia sana kupunguza kero hii jijini Dar es Salaam na utasaidia vilevile katika ubebaji wa wanafunzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limesemwa na Wabunge wengi na kwa mkazo mkubwa ambalo na mimi nakubaliana nao, ni udhibiti wa fedha za Serikali. Nakubaliana kabisa na Wabunge wote waliosema jambo hili. Yapo mawazo kwamba Serikali ipunguze safari za nje kwa watumishi wake na kuzingatia tu zenye tija ili kupunguza gharama za uendeshaji na badala yake zielekezwe kwenye miradi ya maendeleo. Ni kweli tunahitaji kutafuta utaratibu wa kudumu katika kudhibiti matumizi. Kwa sasa Serikali inao utaratibu maalum wa kutoa vibali kwa safari za nje. Aidha, vibali maalum hutolewa kwa safari muhimu zenye manufaa kwa nchi. Serikali itaendeleza juhudi hizo na kuhakikisha tunabana zaidi ili tuweze kuokoa fedha zisizokuwa lazima kutumika huko.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna maoni kuhusu hali ya udanganyifu, ubadhirifu wa matumizi yasiyo mazuri ya rasilimali. Baadhi ya udanganyifu huu unatokana na majengo yasiyofuata ramani na ubora na mambo haya, sasa tunayafanyia kazi. Serikali muda wote imekuwa ikisimamia na kudhibiti matumizi mabaya ya rasilimali zake. Aidha, imeanzisha kitengo cha kufuatilia matumizi kwenye miradi ya Serikali ambacho kiko Hazina na pia kuna Kitengo cha Wataalam wa kukagua miradi ya ujenzi. Serikali pia kwa kushirikiana na Bodi ya Wakandarasi imeendelea kuimarisha udhibiti wa ujenzi wa majengo mbalimbali ili yazingatie viwango, ubora, ramani na mipango miji na thamani ya fedha, tutaendeleza juhudi hizi. Nataka nichukue nafasi hii, kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, viongozi na wanachi, kuendelea kuisadia Serikali kufichua matumizi mabaya ya fedha.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwa msisitizo mkubwa juu ya eneo ambalo vile vile limesemwa kwa nguvu sana ambalo linahusu kwa ujumla Serikali za Mitaa. Hili ni eneo ambalo bado tunahitaji kulifanyia kazi kwa nguvu sana. Serikali imefanya kazi kubwa kuhakikisha inapeleka fedha za kutosha katika maeneo ya Serikali za Mitaa, Vijijini, kwenye Kata na kwenye Wilaya lakini bado tunahitaji kudhibiti kikamilifu hatua

zote zinazoweza kuwa ni mianya ya kuweza kufanya fedha hizo ziibwe au zitumike isivyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejitahidi, tumeweza kuwajengea uwezo Serikali za Mitaa kwa kiasi kikubwa. Tumefanya hivyo kupitia *Capital Development Grant* pamoja na *Capacity Building Grant*. Lakini pamoja na mambo yote haya tuliyofanya, Wizara vile vile kwa namna zake zimejaribu kusaidai Halmashauri kwa kuzijengea uwezo. Mfano mzuri ni Wizara ya Kilimo kupitia *ASDP*, Wizara ya Maji kupitia *Rural Water Sewage and Sanitation Program (*mradi ule wa maji safi na maji taka), Wizara ya Afya kwa kupitia mpango wake wa utoaji wa fedha kwa ajili ya kusaidia kujenga uwezo na Wizara ya Elimu na Ufundi kupitia mpango wake wa kutoa msaada au fedha kwa ajili ya kujenga uwezo. Kiasi cha fedha ambacho mpaka sasa kimeshatolewa ni shilingi bilioni 26, kati ya hizo shilingi bilioni 18 zimeshatumika na kiasi kingine bado. Kwa hiyo, ni jitihada kubwa, kutokana na jitihada hizi tumeweza kutoa mafunzo kwa Madiwani pamoja na watumishi 77,030 ili kuwajengea uwezo ili waweze kufanya vizuri zaidi katika kusimamia fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya ukaguzi ya mwaka 2009/2010 imeonesha 80.3% ya Halmashauri zilizopimwa, zimekutwa zikiwa na watumishi wenye sifa na uwezo unaotakiwa. Tatizo hapa ni sisi, lazima sasa tujipange vizuri kuweza kusimamia mianya yote ambayo inaweza kuwa bado inavujisha mali ya umma. Nataka nitoe wito kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, timizeni wajibu wenu, jitahidini kuwa karibu sana na hizi Halmashauri. Msiogope, wakati mwingine mnaogopa kupita kiasi, mnashindwa hata kuhoji mambo ambayo ni halali kabisa. Hakuna atakayekufanyia lolote endapo katika kutekeleza majukumu yako unachotaka kufanya ni kunusuru fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziko dalili zimeanza kujitokeza za kupungua kwa Halmashauri zinazopata Hati Chafu za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG),* pamoja na hayo bado tunayo kazi kubwa ya kuwa na uhakika kama fedha hizo zilizotoa Hati Safi, ni kweli zinawiana na miradi au utekelezaji wa miradi ambayo iko katika maeneo hayo yaani thamani ya fedha zetu. Kwa hiyo, bado tuna changamoto nyingi na tutajitahidi kuendelea kufanya kila litakalowezekana kuhakikisha kwamba tunasimamia vizuri eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tayari katika kipindi cha mwaka 2005 – 2010, watumishi 1,556 katika katika Halmashauri walichukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu kutokana na kukiuka kanuni, taratibu na Sheria za Utumishi wa umma. Kati ya hawa, watumishi 1,063 katika Halmashauri hizo walifikishwa Mahakamani kwa mujibu wa Sheria, wengine baadhi yao ni Wakurugenzi wa Halmashauri zenyewe na maeneo ambayo hasa yalisababisha kufikishwa kwao Mahakamani, ni yale yale mnayosema Waheshimiwa Wabunge, matumizi mabaya ya fedha, upokeaji wa rushwa, kuhujumu uchumi, wizi wa mali ya umma na wakati mwingine kughushi. Idadi ya watumishi waliohamishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu ya kutaka kuimarisha utendaji kazi katika maeneo mbalimbali kwa kipindi hicho ni 2,858. Wote hawa lengo lake ni kuhakikisha kwamba

watu hawakai katika eneo moja kwa muda mrefu na kujenga mazoea na kufanya kazi kwa mazoea.

Mheshimiwa Spika, imetokea hoja hapa nzuri ya uvunaji haramu wa misitu katika Misitu ya Shengena. Nimeona hili nilieleze kwa sababu ni jambo kubwa na linagusa eneo muhimu sana la hifadhi ya mazingira ambalo linawiana vizuri sana na mabadiliko ya tabianchi. Taarifa ya uvunaji haramu wa misitu katika eneo la msitu wa Shengena, msitu ambao uko katika Hifadhi ya Mkomazi, ilitolewa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki. Kulingana na taarifa hiyo uvunaji huo unafanywa na majangili ambao pamoja na kutokufuata taratibu, watu hao hawana vibali vinavyowaruhusu kuvuna katika misitu katika eneo hilo. Aidha, majangili hao wamekuwa wakitumia majina ya viongozi mbalimbali kuwa wamewatuma kuja kufanya uvunaji katika eneo hilo. Uongo mtupu, kitendo ambacho si cha kweli. Pia majangili hao wamekuwa wakikata miti hovyo kwa njia batili na wakati mwingine kuchoma moto misitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uvamizi wa misitu huo ulikuwa kati ya mwaka 2005 na 2009 kwa ajili ya kuchimba dhahabu na *boxaute*. Uharibifu ulikuwa katika vyanzo vya maji, pia ukataji miti katika misitu. Taarifa zilizopo ni kwamba hali ya sasa ni sharwi zaidi kuliko ilivyokuwa mwanzoni na imedhibitiwa kwa ushirikiano kati ya Wilaya na Wizara ya Nishati na Madini. Hata hivyo, bado wapo wachimbaji wamejiingiza katika maeneo hayo na kuanza kuchimba na hivyo kusababisha makusudi mengine ya vijana kuvamia tena eneo hili. Tutaendelea kufanya juhudi zaidi ili kuhakikisha tunadhibiti uharibifu huo usiendelee.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limezungumzwa hapa na Waheshimiwa Wabunge ni namna Serikali inavyokabiliana na tatizo la rushwa nchini. Suala hili ni vizuri tukarudi nyuma na kutazama kwa lengo la kuangalia juhudi tulizofanya. Mwaka 2006 ndipo Serikali ilipounda Tume ya Mheshimiwa Jaji Joseph Warioba, ili kutazama eneo hili kwa upana na kutoa mapendekezo namna ya kuziba mianya katika maeneo mbalimbali. Tunaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Jaji Joseph Warioba, alifanya kazi nzuri ambayo imetupa namna nzuri zaidi na kubwa zaidi ya kujaribu kuendelea kupigana vita dhidi ya rushwa. Vita hii itaendelea, ni vita yetu sisi wote, nataka niwashukuru Wabunge kwa namna moja au nyingine, nanyi mmeendelea kusaidia sana katika kukemea na kukaripia sana tatizo hili la rushwa, ninawashukuruni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo zote, Serikali kwa upande wake imeweza kutunga Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 yaani *Public Procurement Act* ya mwaka 2004. Imetunga vile vile Sheria ya Kuzuia Fedha Haramu ya mwaka 2006 *(The Anti Money Laundering)* ya mwaka 2006, imeweza vile vile kutunga Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa *(The Prevention and Combating of Corruption Act),* ya mwaka 2007, imeweza vile vile kutunga Sheria ya Maadili ya Viongozi ya mwaka 1995 na kuifanyia marekebisho yaani *The Public Leadership Code of Ethics Act 1995*. Yote haya ni jitihada za Serikali kulenga kukabiliana na tatizo hili kubwa ambalo tusipoangalia linaweza lisituletee matunda mazuri sana.

Mheshimiwa Spika, muda wote tumekuwa tunaendelea kueleza kwa kiasi tunachoweza juu ya nini kilifanyika kuhusu suala zima la Akaunti ya Madeni ya Nje *(The External Payment Arreas (EPA)),* iliyotoka katika Benki Kuu ya Tanzania. Tunaendelea kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali yetu itaendelea kusimamia eneo hili na tayari watu kumi na tatu wameshafikishwa Mahakamani na kesi nyingine bado zinaendelea, tutakapokamilisha uchunguzi wake, nazo tutazifikisha kwa *DPP* kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye vyombo vya Kisheria. Ni lazima wote tutambue kwamba juhudi hizi ni zetu wote na lazima tuzivalie njuga kwa nguvu sana ili tuweze kupambana na tatizo hili kubwa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limesemwa kwa nguvu ni suala zima la uanzishaji wa maeneo mapya. Mheshimiwa Celina Kombani ametoa maelezo asubuhi kuhusiana na Vitongoji, Vijiji na Kata na baadaye akasema maeneo yaliyobaki kwa sehemu kubwa ni eneo la Mheshimiwa Rais. Sasa nimeona kuliko kuacha Bunge hili mnaendelea kuliulizia ulizia nimeona pengine ni vizuri nitoe maelezo kwa ufupi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais tarehe 14 Juni, 2010 tayari amekwisharidhia uanzishwaji wa maeneo mapya katika maeneo mbalimbali na naomba niseme alichosema. Katika mapendekezo yaliyowasilishwa kwake amekubali mapendekezo yote kuhusu kugawa Tarafa mpya ambazo nitazitaja; amekubali vile vile mapendekezo yote ya kugawa Wilaya isipokuwa eneo moja tu la Wilaya ya Bagamoyo; tatu, amekubali mapendekezo ya kuunda Mikoa mipya mitatu ambayo nayo nitaieleza na nne, kwa upande wa Mkoa wa Mpanda ambao ulikuwa umependekezwa nao kuundwa kutokana na ukubwa wake ameshauri tusubiri kwanza ili mashauriano yafanyike kati ya Mkoa wa Tabora na Rukwa. Hilo nalo tutalifanya kwa lengo la kuhakikisha kwamba jambo hili linafanyika kwa nia njema na kwa nia nzuri.

Mheshimiwa Spika, Mikoa hiyo ni ipi? Mkoa wa kwanza ni Mkoa wa Njoluma, wale wanaotoka kwenye eneo hilo wanalijua. Njoluma ni Njombe, Ludewa na Makete. Ingawa Mheshimiwa Rais amesema kwa nini usiitwe tu Mkoa wa Njombe? Mbona mnaanza majina mapya? Mkoa wa pili ni Mkoa wa Geita.

Baadaye Bungeni humu tutatoa maelezo ya kina kuonyesha Mkoa huo ulivyoundwa. Mkoa wa tatu, ni mkoa wa Simiu, nao Rais amekubali uanzishwe na baadaye tutatoa kwa maandishi kueleza kwa ufafanuzi zaidi, Shinyanga ndiyo imeanzisha Mkoa mwingine unaitwa Simiu. Geita mnaelewa kuna sehemu ya Kagera, Mwanza na Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wilaya mpya zitakazoanzisha, wale wanaotoka kwenye maeneo hayo wanajua Wilaya ya Mulele, hii ni Wilaya ya Mpanda, Wilaya ya Gairo, Wilaya ya Kalambo, Mkoani Rukwa, Wilaya ya Kakonko, Wilaya ya Uvinza, Wilaya ya Nyasa, Wilaya ya Kaliua, Wilaya ya Chemba, Wilaya ya Butiama, Wilaya ya Buhigwe, Wilaya ya Ikungi, Wilaya ya Momba, Wilaya ya Wanging'ombe, Wilaya ya Nyangw'ale, Wilaya ya Mbogwe, Wilaya ya Itilima na Wilaya ya Mkarama, Wilaya ya Ushetu. Wanaoijua ndiyo maana unasikia wanapiga makofi, maana wanajua hata Ushetu ni wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tarafa mpya alizoridhia Mheshimiwa Rais zianzishwe ni Tarafa ya Tunduma, Tarafa ya Itaka, Tarafa ya Kizengi, Tarafa ya Nyaronga, Tarafa ya Kifura, Tarafa ya Mpwayungu, Tarafa ya Mima, Tarafa ya Nkoswe, Tarafa ya Ruaha, Tarafa ya Ngohelanga, Tarafa ya Hagati, Tarafa ya Bukombe, Tarafa ya Ushirombo, Tarafa ya Kasharunga, Tarafa ya Mkwedu, Tarafa ya Mkunya, Tarafa ya Mangaka, Tarafa ya Chalinze, Tarafa ya Minsukumilo, Tarafa ya Mamba, Tarafa ya Ndurumo na Tarafa ya Kindoroko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amekubali vile vile Tarafa zitakazotokana na kupandishwa hadhi baadhi ya Kata ambazo zimeshapandishwa hadhi nazo ni Tarafa ya Kigonsera pamoja na Tarafa ya Mkumbi. Iko vile vile Tarafa itakayotokana na marekebisho ya tangazo la Serikali ambayo katika tangazo la mara ya mwisho iliachwa ni Tarafa ya Siha Kaskazini na yenyewe sasa itakuwemo katika Tarafa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumradhi kidogo bado nina eneo lingine nataka nilisemee na sijui kama nitaligundua. Ziko Halmashauri vile vile ambazo zimeridhiwa nazo zianzishwe. Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua mtaona zinaendana pamoja na Wilaya hizo mpya. Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko, Halmashauri ya Wilaya ya Gairo, Halmashauri ya Wilaya ya Mulele, Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Halmashauri ya Wilaya ya Kwela, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Halmashauri ya Wilaya ya Mkarama, Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe, Halmashauri ya Wilaya ya Momba, Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'wale, Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe, Halmashauri ya Wilaya ya Itilima.

Nyingine ni Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Halmashauri ya Mji wa Kahama, Halmashauri ya Mji wa Masasi, Halmashauri ya Mji wa Handeni, Halmashauri ya Mji wa Nzega na Halmashauri ya Mji wa Lindi imepandishwa hadhi kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi kama alivyosema Mheshimiwa Kombani asubuhi hii. Bado tutadaiwa eneo moja ambalo nalo itabidi baadaye tuje tulieleze, ni Halmashauri ya Jiji la Arusha, bado tunakamilisha taratibu zake baada ya muda mfupi na lenyewe litatangazwa kulingana na hadhi yake.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nimeona nalo niligusie kidogo kabla ya kumalizia ni lile ambalo Mheshimiwa Ngasongwa amelizungumza alipokuwa anatoa mchango wake kwamba haitoshi tu kwa Serikali kujitapa kwamba tumekuwa na wawekezaji wengi. Tuna miradi mingi hapa nchini imeanzishwa kama hatuwezi kujua ni kiasi gani cha miradi hiyo kweli imeanza kufanya kazi. Kwa hiyo, kutokana na uhakiki uliofanyika miradi ambayo inatekelezwa kwa uhakika kwa sasa ni asilimia 80 na miradi 20 imekwama kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za ukosefu wa mitaji, ucheleweshaji wa upatikanaji wa vibali kama vya ujenzi, *(building permit)* na hati za kumiliki ardhi. Zoezi hili tunaendelea nalo chini ya Mamlaka ya *TIC*.

Sambamba na hilo, kituo hiki cha *TIC* kimeanzisha Kitengo Maalum *After Care Unit* ambacho moja ya shughuli zake kubwa sasa ni kutembelea miradi iliyosajiliwa na kituo hicho na kuona ufanisi wake kulingana na makubaliano tuliyofikia.

Aidha, Serikali imejitahidi kuimarisha kituo kwa kuitengea bajeti ya kutosha. Pia Kituo cha Uwekezaji sasa kinashirikiana na Mashirika ya Kimataifa kama vile *UNIDO, UNTAD, WIPER* pamoja na programu ya *BEST* inayochangiwa na wahisani mbalimbali. Aidha, Serikali imekwishateua Bodi mpya, Bodi mahiri ambayo tunaamini kwa kushirikiana na *TIC* na Watendaji wake itaweza sasa kutuongoza vizuri na kutupeleka mahali pazuri.

Mheshimiwa Spika, liko eneo moja ambalo nilidhani vile vile ni vizuri nikalisemea kidogo nalo lilisemwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kujaribu kuonyesha kwamba mfumko wa bei unaoelezwa inawezekana sio mfumko wa kweli kweli wa dhati, inawezekana pengine ni maneno maneno tu ya Serikali.

Kwa takwimu tulizonazo mwaka 2000 mfumko wa bei ulikuwa ni asilimia sita, mwaka 2001 ulikuwa asilimia 5.1, mwaka 2002 ilikuwa asilimia 4.3, mwaka 2003 ulikuwa asilimia 5.3, mwaka 2004 ulikuwa asilimia 4.7, mwaka 2005 ulikuwa asilimia 5.0, mwaka 2006 ikapanda kuwa asilimia 7.3, mwaka 2007 ikawa asilimia 7, mwaka 2008 ikawa asilimia 10.3, mwaka 2009 ilikuwa asilimia 12.1 na hadi Aprili, 2010 ilikuwa asilimia 9.8, imeteremka kidogo kutokana na juhudi ambazo zimefanyika.

Serikali imekwishaeleza kwamba ziko sababu kubwa mbili kuu ambazo zinapelekea jambo hili kutokea. Moja ni ongezeko la bei ya mafuta ya petroli na dizeli kwa ujumla wake katika Soko la Dunia ambayo imekuwa ikipanda muda wote hata pale iliposhuka kidogo, lakini haikutupa ahueni kubwa sana. Eneo la pili ni upungufu wa chakula hapa nchini ambao umesababisha bei kuwa kubwa na kwa hiyo, kuongeza kwa kiasi kikubwa gharama hizo ambazo zinazaa mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, pengine kwa kutoa mfano tu kwa upande wa mafuta, nichukue petroli Januari, 2004 bei ya mafuta kwa *metric tone* moja ya petroli ilikuwa ni Dola 220.888. Mafuta ya taa na ndege ilikuwa ni Dola 304.64, dizeli ilikuwa ni Dola 271.35. Mafuta hayo hayo ilipofika Aprili, 2010 mwaka huu bei ya mafuta hayo kwa upande wa petroli ilikuwa ni Dola 778.62. Kwa upande wa mafuta ya ndege na taa ilikuwa ni Dola 733.62 na kwa upande wa mafuta ya dizeli ilikuwa ni Dola 695.17.

Mheshimiwa Spika, hali hii inajitokeza vile vile katika hali halisi ya bei hizo hapa nchini. Petroli Januari, 2004 hapa nchini kwa lita moja ilikuwa ni Sh. 725/=, mafuta ya taa ilikuwa Sh. 520/=, dizeli ilikuwa Sh. 660/=. Mafuta hayo hayo Mei, 2010 petroli ni Sh. 1,727.87, mafuta ya taa ni Sh. 1,225.70, mafuta ya dizeli ni Sh. 1,728.08.

Ninachotaka kusema hapa ni nini? Ni kwamba maelezo haya ya Serikali sio kwamba yanasemwa kwa kujaribu tu kudanganya jamii au kutokutaka kutoa picha ya kweli. Ni kweli kwamba uko uwiano wa karibu sana kati ya gharama za mafuta ambazo ndio tunatumia kwa kiasi kikubwa katika bei za ulimwenguni na namna zinavyoathiri bei hizo hapa nchini. Tutaendeleza juhudi kubwa katika kuhakikisha kwamba tunadhibiti hali yoyote ile ambayo inaweza ikatumika na wafanyabiashara kufanya bei hiyo iongezeke wakati sio lazima iongezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa chakula, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kipindi chote tangu mwaka 2005, Serikali imesimamia eneo la sekta hii vizuri sana na tumeweza kuzalisha chakula cha kujitosheleza kwa mwaka 2004/2005 kwa asilimia 103, mwaka 2006 kwa kiwango cha asilimia 102, mwaka 2006/2007 kwa asilimia 112, mwaka 2007/2008 kwa asilimia 106, mwaka 2008/2009 kwa asilimia 105, mwaka huu tunaamini tutakwenda zaidi ya asilimia 100. Kwa nini nalisema hilo?

Nalisema hili kwa lengo la kuonyesha kwamba ziko juhudi za kweli ambazo zikiwekwa na Serikali na Watanzania wote eneo hili ambalo linachangia vile vile katika kuongeza mfumko wa bei tunaweza kabisa tukashusha mfumko huo kwa kuwa na chakula cha kutosha ambayo bei yake ikiwa ndogo mfumko wa bei nao utashuka.

Tatizo tulilonalo ni kwamba kwa sehemu kubwa chakula hiki kinatoka katika Mikoa michache na inalazimika kulisha Mikoa mingine ambayo ina ukame mkubwa. Hata hivyo, Serikali itaendelea kufanya kila litakalowezekana ili tuweze kuhakikisha kwamba kazi hiyo inazaa matunda mazuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie basi, liko jambo moja nalo limejitokeza kwa nguvu sana linalotokana na maafa yaliyotokea hapa nchini. Niliyaeleza wakati natoa maelezo wakati fulani, lakini naomba nilirudie leo. Yako maafa ya aina nyingi, lakini kwa safari hii nimesema Serikali itaangalia kwa dhati na kwa karibu sana suala zima la yale maeneo yaliyopata ukame katika maeneo ya ufugaji.

Wilaya zote katika Mikoa ya Arusha, Simanjiro na maeneo mengine, Serikali imeshaanza kujaribu kutazama nini tufanye hata kama kitakuwa ni kidogo lakini kwa lengo la kuwaonyesha Watanzania kwamba tunatambua tatizo hili na Serikali iko tayari kujaribu kusaidia kwa kadri itakavyowezekana kuleta kitu ambacho kinaweza kikawatia moyo kidogo. Waswahili wanasema: “Kutoa ni moyo na wala sio utajiri”. Tutawaomba basi wananchi wa maeneo hayo yote washirikiane na Serikali tutakapokuwa tunaomba kupata maelezo ya ukweli na ya dhati, takwimu za kweli juu ya kiwango cha athari, idadi ya wanyama waliokufa, familia zilizoathirika kikweli kweli kwa kiwango kikubwa na hawana namna nyingine yoyote ya kuweza kujisaidia.

La pili, Serikali vile vile imekubali kwamba kwa kuwa maafa haya kwa maeneo ya wafugaji sio kwamba imewapunguzia wao wenyewe chanzo muhimu kwa mapato yao na chakula, lakini vile vile kimeathiri sana uwezo wao wa kuweza kuchangia katika huduma za msingi. Ni wachangiaji wazuri sana katika ujenzi wa Shule za Sekondari, Vituo vya Afya, Zahanati, lakini kutokana na hali hii sasa uwezo huo umepungua kwa kiasi kikubwa sana. Serikali imesema tutaliangalia angalau tuweze kuchangia katika kuwezesha hiyo miundombinu isibaki kama ilivyo ili kuwezesha watoto waweze kwenda shule na Vituo vya Afya kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziko aina nyingine za maafa ambazo nilizieleza wakati natoa maelezo yangu, lakini Prof. Sarungi naye amekuja na maafa ya aina yake. Katika mapigano yaliyotokea kule Rorya kati ya koo na makabila mbalimbali, ni kweli na yale ya mwisho kabisa ni mabaya, ni yale yaliyosababisha vifo vya watu 40 na ng’ombe

wengi kuibiwa na kuchomwa nyumba nyingi. Ametoa rai kwa Serikali, kwamba Serikali ingeangalia eneo hili waone ni namna gani tunaweza tukasaidia pengine kuona namna yoyote ile ya kuweza kuwapunguzia wale hasa ambao wameathirika kwa kiasi kikubwa. Ni wazo kubwa, ni wazo jema, ni kweli yalitokea. Serikali inakubali kwamba italiangalia hasa kwa zile familia zilizochomewa nyumba ambao sasa walipata matatizo makubwa ya namna ya kuishi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba nirejee nilichosema kwamba nimejitahidi kuyapitia maeneo yale ambayo nimeona ni makubwa, lakini ni kweli hata mimi sikuweza kuyamaliza yote. Tutajitahidi kujaribu kuyatolea maelezo ya kina kwa wakati muafaka ili kila Mbunge aweze kujua lile alilotolea mchango na lile ambalo aliweza kulisemea, basi lipate maelezo ya kina na ufafanuzi stahiki kwa lengo la kuwezesha kujua ni nini Serikali imedhamiria kufanya katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, narejea kukushukuru wewe mwenyewe, niwashukuru sana Wenyeviti wako, niwashukuru sana Wabunge wenzangu ambao tumesaidiana kwa namna nzuri sana katika kipindi chote kuhakikisha kwamba Bunge hili linafanya kazi yake vizuri na kwa viwango vinavyotakiwa na mimi nimefarijika sana.

Nataka vile vile nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Mawaziri wenzangu na hasa Mawaziri wale ambao wanasaidia moja kwa moja chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa namna ya pekee ambayo wamefanya kazi na mimi kwa karibu sana katika kipindi chote, wameshauriana nami kwa namna nzuri sana na hivyo kutuwezesha kutoa mchango wetu mdogo kwa kadri tulivyoweza.

Nawashukuru sana Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Viongozi hawa Mikoani na Wilayani ni nguzo muhimu sana katika maendeleo ya Watanzania. Nachelea na sikubaliani hata kidogo na baadhi ya Wabunge wachache ambao mara nyingine huwa wanasahau na wanafika mahali wanasema hawaoni sababu za Mkuu wa Wilaya kuwepo.

Mheshimiwa Spika, tukimwondoa leo Mkuu wa Wilaya, siku mbili mtasema mrudisheni. Sababu zake ni dhahiri, haya mapungufu yote mnayoyaona katika Halmashauri zetu, katika Serikali zetu kama kusingekuwa hata na juhudi ndogo za Wakuu wa Wilaya hali ingekuwa mbaya sana.

Nataka niwasihi sana Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kuthamini kada hii ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya pamoja na Maafisa Tarafa ambao wanaisaidia Serikali Kuu. Tuwasaidie wajenge uwezo zaidi, waweze kuwa ndio Maaskari wetu wa mbele, majemadari wa karibu kabisa katika kusimamia Serikali za Mitaa ambazo ndio vyombo vya utekelezaji ili waweze kutimiza majukumu yao vizuri zaidi.

Nataka niwashukuru Madiwani wote nchi nzima, Wakurugenzi wao chini ya uongozi wa Wenyeviti wao na Mameya wao kwa namna ambayo pamoja na mambo yote yanayosemwa bado kuna Halmashauri zimeendelea kufanya vizuri. Tunawaomba na wale wengine ambao bado hawajajipanga vizuri, waige mifano kwa wenzao wanaofanya vizuri na wahimize zaidi kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba alisema: “Tatizo tulilonalo hapa wako watu wamezoea kupokea rushwa, wako watu wamezoea kuiba, wako watu wamezoea kusema uongo na kudanganya.” Wakati mwingine kuweza kuwabaini watu wa namna hii inataka juhudi za pamoja. Serikali peke yake sio rahisi.

Kwa hiyo, tunaomba sana Watanzania wote, Waheshimiwa Wabunge, viongozi wote, wote tudhamirie kwa dhati kutambua kwamba fedha zinazokwenda katika maeneo yetu ya Vijijini ni fedha nyingi sana, zikisimamiwa vizuri zikafanya kazi iliyopangwa matokeo yake ni mazuri maradufu. Ni imani yangu kwamba katika vipindi vijavyo kuanzia mwaka huu wa fedha tunaomalizia tutaweza kufanya vizuri zaidi kwa kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, nirejee sasa kuwashukuru wapigakura kutoka Jimbo la Mpanda Mashariki wamenipa heshima kubwa, upendo mkubwa sana kwa kipindi chote. Ninawashukuru sana viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Mpanda kwa kuendelea kunisaidia kunishauri na kila walipoweza kwenda kunisemea vizuri kwa Watanzania, nawashukuru sana. Nawashukuru viongozi wa Rukwa kwa ujumla wao kwa namna ambavyo tumefanya nao kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, najua kazi hizi zinakuwa ni nzito na ngumu sana. Niendelee kumshukuru huyu mama anaitwa Mama Pinda kwa kunivumilia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nimalizie kwa kumshukuru Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Rais huyu amefanya kazi kubwa, kazi inayoonekana mbele ya macho ya Watanzania. Mimi ninayo imani kubwa sana kwamba atashinda kwa kishindo. *(Makofi)*

Lakini pengine sio vibaya nikamshukuru Mheshimiwa Shibuda ambaye baada ya jitihada zote alizofanya kama ilivyo kawaida yake, juzi alifika mahali akasema hapana, anaahirisha nia yake na dhamira yake ya kutaka kugombea nafasi hii kupitia Chama cha Mapinduzi. Hakusema ameahirisha kwa kipindi gani, lakini tunaomba tumtakie mema kwenye Jimbo lake, Mungu amjalie kufanya kazi vizuri kwa kadri atakavyoweza. *(Kisheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imani yangu ni kwamba Wabunge wengi tutarudi hapa ndani, ninawatakia kila la kherli mfanye kila litakalowezekana. Wale jamaa aliowaita Mheshimiwa Mpanda nimesahau jina, sijui *Mavuvuzela* sijui! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana ukashtukia yako Bungeni na yenyewe siku moja. Kwa hiyo, ni vizuri tukubali kwamba kwa mfumo wa demokrasia tuliojiwekea, *anything is possible.* Wanaotuchagua ni Watanzania, wenye maamuzi juu yetu ni Watanzania, *let us get prepared* kwa lolote watakalokuwa wametuamulia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nitoe hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuhitimisha hoja vizuri kama ilivyo kawaida yako.

Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kupitisha makadirio ya Ofisi yake imetolewa na imeungwa mkono, lakini tumefungwa na Kanuni ya 100 na 101 kwamba inabidi twende katika utaratibu mwingine ili kufika mwisho mzuri.

## KAMATI YA MATUMIZI

**MWENYEKITI:** Wakati tunaendelea kusubiri kuingia katika vifungu vya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa wale wanaopenda kandanda na hii imethibitishwa kabisa na huyu ni *authority* kabisa, ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, sasa hivi kwenye mechi kati ya Marekani na Slovenia. Slovenia inaongoza kwa magoli mawili kwa bila (2 - 0) na ni *half time. (Makofi)*

## FUNGU 25 – WAZIRI MKUU

## MATUMIZI YA KAWAIDA

Kif. 1001 -*Administration and General*…Sh.5,529,966,000/-

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nitumie dakika moja kusema neno la awali tu. Baada ya kumsikia Mheshimiwa Waziri nataka kusema kwamba ile kura yangu ya ndiyo, *was correct* na ilikuwa sawa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ya *Party Caucus* ni *UDP Party Caucus* na kwenye Kambi hatuna *Party Caucus*. Mengine nitayaachia huko. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hebu keti kwanza. Mheshimiwa Cheyo haya unayaleta sijui ya nini? Kwa mujibu wa Kanuni ya 15(2) mlikubaliana wenyewe muunde *Caucus* ya Vyama vya Upinzani, ndiyo hiyo inatokana na kuweza kuwa na Baraza la Mawaziri ambalo ni kivuli. Sasa mimi sitaki niuendeleze mjadala huu, nataka uende kwenye lengo tu kwa sababu ukienda huko ziko hoja nyingi sana na pengine utaonekana kama vile unapingana na maamuzi ya Spika na ingawa muda wetu unakaribia kwisha… *(Hapa kengere ililia)*

We unanigongea kengele tena? *(Kicheko)*

Kanuni mpya imenipa mamlaka fulani ya kuchukua hatua. Kwa hiyo, *ruling* ya Spika kama imekwishapita, sasa wewe nafasi yako ni kuandika hati ya rufani ambayo

itajadiliwa na Kamati ya Kanuni. Kwa sasa tuendelee na haya tu. Unapokubali Mheshimiwa Cheyo unapokubali cheo, pia ukubali kikikuponyoka. Sasa endelea na hoja ya Waziri Mkuu. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukuhakikishia sitarudia huko. Mojawapo la jukumu pia la Waziri Mkuu ni mambo ya Bunge na pia mambo ya Mahakama maana yake ni vitu vyote ndivyo vinakwenda kwenye utawala. Kumetokea mtindo kwa Bajeti ya Bunge kwa mfano hujui leo mtapata pesa, leo mtapata posho au kesho kutwa. Sasa utaratibu wa namna hii sio njia ya kuendesha Bunge lenye *standard*.

Kwenye *CAG* tumefanya jambo zuri sana. Wakati nimechangia kwa maandishi nilisema labda utaratibu ule ambapo Bajeti ya Bunge, Bajeti ya Mahakama ikishakubaliwa itengenezwe utaratibu kama ulivyofanywa kwa Mdhibiti na Mkuguzi Mkuu wa Serikali *(CAG),* basi hizo pesa kwa mihimili hii miwili ipatikane bila kusuasua kama vile ilivyo kwa hivi sasa. Ndivyo ambavyo nimemweleza Mheshimiwa Waziri Mkuu, sikusikia jibu juu ya jambo hilo, kwa hiyo, ningefurani kama Waziri Mkuu ameiona au hakuiona, basi angalau kwa kuwa ameisikia sasa atuambie: Je, atafanyaje ili kuhakikisha kwamba mihimili hii miwili ina-*guaranteed funds* za kuweza kufanya kazi za kutunga sheria na kazi ya kutoa haki kwa watu?

**MWENYEKITI:** Kabla sijamwita mwingine yoyote naungana mkono na wewe kwa sababu ndiyo maana nimeitisha Tume ya Huduma za Bunge kesho saa 5.00 asubuhi. Mambo yaliyotokea katika Bajeti ya mwaka huu hayatendi haki hata kidogo kwa Bunge. Bunge ambalo litakuwa na Wajumbe 360 sio tu limepunguziwa Bajeti, lakini mtiririko wa fedha umezidi kuwa ni wa kama kudhalilisha hovyo hovyo tu. Mara Wabunge hawana pesa, vyombo vingine hivi vina heshima yake. Sasa kuandikwa kwamba Wabunge sasa wameishiwa kabisa, wanahaha wanakwenda madukani kukopa. Lakini sisi tutazungumza kesho na tutapeleka mapendekezo yetu Serikalini.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilitaka ufafanuzi juu ya watu wawili waliopigwa risasi karibu na Mgahawa wa Mugesa kule Tunduru katika kile ambacho kinadaiwa *TRA* na Polisi kukusanya kodi na sikupata maelezo yoyote. Ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeomba Mheshimiwa Mbunge atuletee tatizo lake kwa maandishi ili Wizara ya Mambo ya Ndani ilifuatilie tukio hili kwa kina na kwa kweli kifungu ambacho tunakiongelea sasa hivi ni tofauti kabisa na kifungu cha Wizara ya Mambo ya Ndani.

**MWENYEKITI:** Nadhani Mbunge alitumia haki yake kwa sababu fungu la Mheshimiwa Waziri Mkuu wakishatoa mshahara, wanazungumzia mambo yote ya uratibu. Tena wewe uliyejibu ndiye Waziri wa Uratibu. Kwa hiyo, huo ni wajibu wako

kuwasiliana na Mambo ya Ndani ili Mheshimiwa Mbunge apate jibu. Tunaendelea na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia nilizungumzia suala la tabia ya viongozi kubambika kesi hasa Viongozi wa Chama cha Mapinduzi wakishirikiana na viongozi wa Wilaya wanabambika kesi kwa viongozi wa Vyama vya Upinzani wanaposhinda nafasi za Utendaji wa Vijiji na Vitongoji.

Alipokuwa anajibu Mheshimiwa Waziri wa masuala ya Bunge alisema kwamba *NEC* inaandaa maadili ya uchaguzi kwa kushirikiana na vyama vya siasa. Tatizo hapa sio kuandaa maadili, tatizo hapa ni kwamba tatizo hili lipo na limeanza tangu huko nyuma na wapo wengine ambao wameshaondolewa kwenye nafasi zao kwa utaratibu uliopo sasa hivi. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itoe tamko kwamba, nini kinafanywa kutokana na watendaji hawa? Kwa sababu suala la kuandaa maadili ni suala lingine na suala linaloendelea sasa ni suala lingine. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Kidogo umejichanganya. Watendaji wa CCM au Watendaji wa Serikali?

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Watendaji wa Serikali. Kwa sababu ninayo mifano hai ambapo Mkurugenzi alihusika katika kuhakikisha kwamba aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Upinzani aliondolewa kwa awamu iliyopita na hata kipindi hiki yamekuwa mambo ni hayo hayo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tuhuma kama ni ya uhakika na ina ushahidi, Mheshimiwa Mbunge atuletee tulishughulikie. Kwa sasa hatuwezi kusema lolote kwa sababu hatuna ushahidi wowote wa kesi anayoisemea.

**MWENYEKITI:** Basi hayo na mengine ambayo yako sehemu nyingine mara nyingine ni vizuri tu kuifikishia Serikali. Hatua zimekuwa zimechukuliwa kuliko kusubiri mpaka sasa tena inakuwa ngumu na ni mwisho wa kipindi cha Bunge. Niseme tu kwamba mara kwa mara nimekuwa nasikiliza baadhi ya maswali hapa nashangaa sana, kwa sababu Serikali ipo wakati wote, utaona Mbunge anaulizia tukio lililotokea katika sehemu anayoijua mwaka jana tarehe fulani, lakini anakuja Bungeni. Kwa hiyo, jibu la Serikali linakuwa hivyo, kwamba ukipata ushahidi huo tuleteee tulifanyie kazi.

Kwa hiyo, tunapoteza muda tu Wabunge kwa sababu kama mambo haya yangekuwa yanashughulikiwa na Serikali ngazi zote na Mbunge una ruhusa ya kwenda mpaka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa nadhani tuzingatie hayo, tusichukue muda wa wananchi bure. Mheshimiwa Riziki.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nikichangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu niliuliza kuhusu namna Mbunge anavyopatikana. Mbunge wa Tanzania Bara na Mbunge anayetoka katika Jimbo la

Zanzibar namna anavyopatikana kwa kutumia Sheria mbili tafauti. Ninaomba ufafanuzi zaidi.

**MWENYEKITI:** Hebu fafanua wewe swali lako. Maana yake mimi sidhani kama hilo ni kweli. Sasa msingi ukiwa sio kweli, swali linakuwa sio halali. Sheria tofuati vipi? Sheria kwa maana ya kuwapata Wabunge ni moja tu.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti. Kule Zanzibar tunatumia *ZEC* na wanaandikishwa wapigakura kwa kutumia daftari la *ZEC*. Lakini daftari hilo wanaochaguliwa ni Mheshimiwa Diwani, Mwakilishi, Mbunge na Rais wa Zanzibar. Lakini sasa hivi Tume ya Uchaguzi ya *NEC* wanaandikisha wapigakura ambao watapiga kura kwa kumchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano na Mheshimiwa Mbunge.

Lakini katika daftari hilo ambalo linaandikishwa tayari wapigakura ambao watamchagua Mheshimiwa Mbunge kwa Zanzibar wameshaandikishwa kwenye daftari la *ZEC*. Sheria ya kule na Sheria ya huku ni tofauti ambayo inampata mpigakura. Jimbo la Kojani na Jimbo la Handeni au Geita wote ni Wabunge sawa. Kwanini kule wanaandikishwa kwa kutumia daftari la *ZEC* na huku anaandikishwa kwa daftari la *NEC?*

Mkurugenzi alisema kwamba kule watakaoandikishwa sasa hivi kwenye daftari la Muungano watamchagua Rais. Je, wale ambao wamekosa nafasi ya kuandikishwa katika daftari la *ZEC* kule ambao wana haki ya kumchagua Mbunge watafanyaje na haki? Hii inakuaje? Kwa sababu Wabunge wa Bara na Zanzibar ni sawa sawa. Nadhani nimeeleweka.

**MWENYEKITI:** Nadhani umeeleweka kwa sababu *ZEC* huwa inafanya kazi kama wakala wa *NEC*. Lakini kama *ZEC* inakunja na inafanya kazi yake bila kufuata Sheria ya Muungano, hapo kuna tatizo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge alete hoja yake hii tukifikia kifungu cha 37 na hiki ni kifungu 25 ambacho sio mahala pake.

**MWENYEKITI:** Ahsante, umetusaidia. Lakini litakuja hivyo hivyo. Mheshimiwa Riziki linawekwa kiporo hilo kwa dakika chache na nadhani litasaidiana kupata ushauri wa kitaalam. Mheshimiwa Mwakyembe.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi nimeeleza mkanganyiko unaojitokeza pale ambapo katika Majimbo yetu, Kata inakufa kupisha uanzishwaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo, wakati mfumo wote wa utawala wa Kata unaondoka lakini Diwani anabaki akiwa hana Afisa Mtendaji, wala Mamlaka yoyote ndani ya Mamlaka mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipewe maelezo ni nini kinazuia Serikali au Ofisi ya Waziri Mkuu kutangaza kutokuwepo kwa nafasi hiyo hewa pale ambapo Mamlaka ya Mji Mdogo ipo ili tusiendelee kutapanya fedha ndogo tuliyonayo ambayo ingeweza kutumika kwa vitu vingine? Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anachosema Mheshimiwa Mwakyembe, Sheria hiyo haiko wazi na ina mkanganyiko. Sasa hivi tunarekebisha Sheria hiyo ili huo mkanganyiko usiwepo. Kwa kweli mimi nakiri kwamba ina mkanganyiko na unapoanzishwa Mji mdogo zile Kata sasa hazina kazi kwa sababu wanasema Wajumbe ni wale Wenyeviti wa Vitongoji.

Kwa hiyo, utakuta kwamba Diwani anakuwa hana kazi katika ile Kata. Kwa hiyo, kwa kweli hili lina mkanganyiko kama alivyosema. Naomba atuvumilie kwa sababu ni kweli linatakiwa kufanyiwa marekebisho.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa naomba kuondoa nia yangu ya kuchangia katika kifungu hiki nitakwenda kwenye kifungu cha 37.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 27- Msajili wa Vyama vya Siasa**

Kifungu cha 1001 - *Administration and General*.......sh. 19,367,967,000

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kuulizia tu kwamba fedha ambazo amepewa Msajili wa Vyama vya Siasa ni shilingi bilioni 19.3. Wakati mwaka huu wa fedha unaoisha alipata shilingi bilioni 19.9, nilitegemea kuwa kwa sababu ni mwaka wa uchaguzi angepewa pesa zaidi. Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa huu ni mwaka wa uchaguzi kifungu hiki kimepunguzwa kwa sababu ya kupunguza gharama mbalimbali kama ambavyo tumesema hapo awali. Gharama za usafiri wa ndani na wa nje ambao siyo wa lazima na matumizi mengine ambayo siyo ya lazima, lakini kwa upande wa shughuli za maendeleo baadae tutakuja kuona kwamba tumeongeza fedha kwa ajili ya elimu kwa ajili ya mpiga kura na elimu kwa ajili ya sheria mpya ya gharama za uchaguzi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kifungu 1001- *Prime Ministers Office*..........................sh.3,340,852,655

**MWENYEKITI:** Nadhani hapa ndiyo Mheshimiwa Riziki na Mheshimiwa Chrisopher Ole-Sendeka, ameongezeka Mheshimiwa Omari Kwaangw' na Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, kulikuwa na swali la Mheshimiwa Riziki labda Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge utusaidie lilikuwa *ZEC* kutofuata Sheria ya Muungano pamoja na kuwa ni wakala wa *NEC* kuandikisha watu Zanzibar.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria zetu za Uchaguzi Sura ya 343 Tume ya Taifa ya Uchaguzi huwa inatumia Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kama wakala na daftari la Tume ya Uchaguzi Zanzibar *(ZEC)* ndilo daftari ambalo linatumiwa na Tume ya Uchaguzi ya Taifa na hii ni kwa mujibu wa sheria za nchi na Katiba ya nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani ufafanue kidogo tuelewe, haitoshi kusema ni kwa mujibu wa Katiba kwa sababu swali hapo ni halali *ZEC* kutumia sheria yake tu yenyewe kama wakala badala ya kutumia sheria ya *NEC?* Ndiyo swali lenyewe.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *ZEC* haiwezi kutumia sura ya 343 kwa sababu yenyewe haijaanzishwa na sheria hiyo, yenyewe imeanzishwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi wakati Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeanzishwa na sheria ilitungwa na Bunge hili na kwa uchaguzi ambao unaendeshwa kwa upande wa Zanzibar, Tume ya Uchaguzi inakuwa na mamlaka kwanza kuwasajili wale wananchi ambao siyo Wazanzibar kwa mujibu wa sheria ya Zanzibar, lakini ni Watanzania ambao wanastahili kumpigia kura Rais wa Jamhuri ya Muungano na Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kuhakiki orodha ya wapiga kura ambao watampigia Rais na Mbunge ambayo iko katika daftari la *ZEC* na haya ndiyo masharti ya Sheria za Uchaguzi za Jamhuri ya Muungano na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Itakuwa ni vizuri litazamwe, wale watakaokuwapo walitazame katika Bunge la Kumi. Kanuni tumetengua, huwezi kusimama zaidi ya mara moja mimi nimekusemea hapa nimekusaidia tu kwamba suala hili kwa kweli halijaisha ndiyo ninachosema kwa sababu huwezi ukishatumia daftari la *ZEC* lina masharti ambayo raia mwingine anayepigia kura Wabunge, Madiwani na Rais hafungwi na masharti hayo kwa hiyo, inaleta taabu hii, lazima tukubali kuna taabu na tulifanyie kazi tu. *(Makofi)*

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi ambao nilimfikishia Mheshimiwa Waziri nilitaka maelezo kutoka kwake kwamba wakati nilipotoa mchango wangu siku ya kwanza nilipoapishwa hapa

niliuliza suala la muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na haja ya kurekebisha nikijua kwamba hilo linaratibiwa na Katiba na katika majibu yake Mheshimiwa Waziri alisema kwamba anaelewa umuhimu wake na analikubali, lakini linahitaji marekebisho ya Katiba ambayo kwa muda huu uliobakia kabla ya uchaguzi ni mfupi akaahidi kuwa litafanyiwa kazi, sasa nataka hapa atoe kauli ya Serikali kuhakikisha kuwa muda huu tunakubali kuwa ni mfupi lakini baada ya uchaguzi suala hili litashughulikiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameniambia kuwa atanijibu kwa maandishi lakini nilikuwa nataka *commitment* ili irekodiwe kuwa suala hili litafanyiwa kazi baada ya uchaguzi. Naomba maelezo ya Waziri ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu katika mchango wake wa maandishi alitukumbusha yale ambayo tulikuwa tukijadili wakati tukirekebisha sheria sura ya 343 na napenda kuchukua fursa hii kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi iko pale kwa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuna mchakato kama kuna tatizo na Tume ama muundo wake au namna inavyoendesha kazi mchakato na nikasema kwamba kwa wale raia ambao wanaona wana tatizo na Tume hii muda uliobaki hadi Uchaguzi Mkuu ni mdogo, kwa hiyo, haitawezekana kuanzisha mchakato wa kufanya jambo lolote katika Tume ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kama kuna raia bado watahitaji mchakato uanze, hakatazwi kwa sababu unaweza ukaleta badiliko katika sheria kwa kuleta Muswada binafsi au kwa kuishauri Serikali ili ianzishe mchakato wa kufanya mabadiliko iwapo itaona inafaa. Kwa hiyo, bado namshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba afuate utaratibu uliopo wa kubadilisha Katiba. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ah! Sijui mambo mengine Serikali ingekuwa inakubali kwamba yatafanyiwa kazi inatosha. Tukianza kuingia kwenye mtu kuleta Muswada binafsi ili kubadili Katiba ni haki yenu lakini hapa kuna jambo ambalo linahitaji kama lile lile lililoulizwa na Mheshimiwa Riziki kwamba Bunge la Kumi likae vizuri tu sisi ni nchi yetu tupange mambo yetu vizuri yasiwe yana mikingamo humu humu ndani halafu tunaendelea nayo tu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mawaziri wanajibu au wanachangia hoja ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu hakuweka hoja vizuri aliyotoa Mheshimiwa Pascal Degera na ambayo imegusa barabara ya kutoka Dodoma kwenda Babati. Sasa tunataka ufafanuzi tu kwa suala hili kwamba mwaka jana Bajeti ya Wizara ya Miundombinu ililala na kama majibu ni yale ambayo leo ameyatoa tena nadhani itakuwa taabu zaidi katika barabara ya Dodoma kwenda Babati, Serikali ilikubali kutoa shilingi bilioni 40 kuongezea shilingi bilioni 5.6 iliyokuwepo ambayo ilikuwa imewekwa kwenye Bajeti lakini Mheshimiwa Degera aliuliza hapa leo bilioni 40 zile mbona hazionekani tena?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujaona kazi yoyote iliyofanyika na mwaka wa fedha ndiyo huu unamalizika. Sasa tungependa kujua kwamba Waziri alisema tu kwamba ahadi ya Serikali itatekelezwa, sasa tunataka kujua hizi shilingi bilioni 40 ambazo mwaka jana Serikali ilikubali wameziweka wapi kama kazi haijafanyika na kama kazi ingefanyika bila shaka wakandarasi wangeteuliwa na wangeshaanza *mobilization* kama wangelipwa fedha kiasi tungeona kwenye hiyo barabara, sasa nilitaka ufafanuzi juu ya eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mkumbuke tu kuwa mnapochangia katika hatua hii tulivyozikarabati Kanuni zetu muda siyo dakika tano ni dakika tatu. Ndiyo maana kengele imegonga bahati mbaya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu hayupo lakini atakuwepo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Hansard* itaonekana kwamba Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu alisema kwamba kwa kipande kati ya Dodoma na Mayamaya fedha zipo na *tender* imetangazwa na hali kadhalika kati ya Babati na Bonga kilomita 16 na kile kipande cha Bicha hadi mjini Kondoa sasa tusubiri wakati wa Bajeti yake fedha ziko wapi na atazifafanua kama alivyosema pale awali.

**MWENYEKITI:** Ushauri mzuri tu, Mheshimiwa Christopher ole-Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo tu la kuomba ushauri. Pamoja na kutambua na kuthamini msimamo na nia njema ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika suala zima la kuanza mchakato wa kuona namna bora ya kuwasaidia wafugaji kutokana na athari ya ukame lakini bado nilipokuwa nikichangia niliainisha baadhi ya maeneo ambayo kwa fedha ambazo tuliweza kusaidiwa na Serikali kutokana na ukosefu wa maji kwenye jimbo la Simanjiro tuliweza kupata baadhi ya visima ambavyo vina maji na baadhi ya maeneo mengine tuliweza kuchimba maji kwa kutumia fedha za *CDG* lakini miundombinu yake bado haijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kujua kwamba Waziri Mkuu amekuwa akifuatilia jambo hili na kwa sasa kwa kuwa tunaingia katika wakati wa ukame ambapo mifugo inakosa maji na binadamu wanakosa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kuendelea kupata kauli ya Serikali itakayoweza kuwafariji wananchi wa Simanjiro kutokana na visima hivyo ambavyo maji yanapatikana ili kuona namna bora ya kuweza kukamilisha miundombinu hiyo na maji haya yaweze sasa kutumika na binadamu katika maeneo hayo ikiwemo Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro, Olkesmeti na maeneo mengine ya Kata za Emboreti na Kata ya Terati na maeneo ya Kata ya Kitwai na maeneo mengine ambayo niliweza kutaja ambayo sitaki kutumia muda huu kupoteza muda wa Bunge kwa sababu hoja yangu itakuwa imeeleweka.

**MWENYEKITI:** Ni mpango maalumu wa maji katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge sijui Waziri wa Maji hayupo. Pengine tusubiri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemshauri Mheshimiwa Mbunge asubiri siku ambapo hoja ya Waziri wa maji na Umwagiliaji itakapowasilishwa Bungeni.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 *Finance and Accounts* ………………….sh.819,265,100
Kifungu 1003 - *Policy and Planning………….........*sh.3, 146, 015,250
Kifungu 1004 - *Internal Audit*……….....................................sh. 253,718,000
Kifungu1005-*Information, Education and Com.*……sh.224,784,300
Kifungu 1006- *Procurement Management Unit*……...sh.244,526,100
Kifungu 1007 - *Legal Services Unit*………………………….sh.99,498,200
Kifungu 1008- *Management Information System Unit*..sh.131,724,595
Kifungu2001-*Civil Affairs and Contingencencies*….sh.8,873,660,900
Kifungu 2002 - *National Festivals*……....………………..sh.810,643,300
Kifungu 3001-*Parliamentary and Political Affairs*……..sh.668,993,200
Kifungu 4001- *Investment and Private*
*Sector Development's* ..................................................sh. 4,962,234,600

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001- *Coordination of Government Business*..sh. 786,262,700

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zambi *Item* ipi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *programme 50, sub vote* 5001nilitaka kujiridhisha.

**MWENYEKITI:** Hujafika popote hapo 5001 ni *sub-vote* sasa katika hizi kasma ndogo unaulizia kitu gani sasa? *Basic salaries* nasikitika hakuna kitu cha namna hiyo kwa sababu tunapozungumzia mshahara ni mshahara wa kiongozi mkuu wa *vote,* huu mshahara wa hapa ni mshahara sijui wa nani Mkurugenzi sijui hawa wauguzi?

**MHE. GODREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuhoji kwa sababu wenyewe umepungua sana ndiyo lilikuwa swali langu yaani ukilinganisha na mwaka jana, mwaka huu limepungua sana.

**MWENYEKITI:** Kama utaratibu hauruhusu huwezi kuuliza.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 7001- *Government Printer*...………………..sh.5, 439,087,100

**MHE. JUMA S. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub vote* 7001 kifungu 221300 nataka tu maelezo kwa nini kifungu hiki kimepanda sana ghafla baina ya mwaka jana na mwaka huu.

**MWENYEKITI:** Kutoka shilingi milioni 47 kuwa bilioni moja na milioni 876.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kifungu cha Mpigachapa Mkuu wa Serikali, hiki na inajulikana mwaka jana kulikuwa na kazi nyingi sana za kuchapisha nyaraka za uchaguzi wa Serikali za Mitaa na mwaka huu kuna uchaguzi mkuu. Watumishi wa Mpigachapa Mkuu wa Serikali huwa wakati mwingine wanafanya kazi saa 24 lakini pia tumeongeza mashine mpya nane kwa ajili ya shughuli hizi za uchaguzi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 42 - National Assembly Fund**

Kifungu 1001 – *Administration and General*………sh.10,487,444,000
Kifungu 2001 – *National Assembly*............................sh. 42,094,054,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 61 - *Electoral Commission***

Kifungu 1001 – *Admnistration and General* …………sh. 2,761,077,400
Kifungu 1002 – *Planning Monitoring and Ev. Division*…sh. 408,163,800
Kifungu 1003 – *Finance and Accounts Unit* ……………sh. 375,362,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit* ……………………….sh. 343,480,000
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit*……………………..sh. 310,232,300
Kifungu 1006- *Procurement MGT &Logistics Unit*…sh.7,790,750,100

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 – *Election Management Division*…sh. 48,902,325,400
Kifungu 2002–*Permanent National Voters*
*Reg. Sys. Division*.................................................................sh. 580,728,800
Kifungu 2003 – *Voters Educ. Public*
*Information Division*..........................................................sh. 620,963,200

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati yaMatumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 91 - *Anti Drug Commission***

Kifungu 1001 – *Admnistration and General* ………. sh.1,123,361,000

*(Kifingu kilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 92 - *Tanzania Commission for Aids (Tacaids)***

Kifungu 1001 – *Policy, Planning and National Response*…........................................................sh. 59,400,000
Kifungu 1002 – *Finance, Administration and Resource Mobilization*…....................................…sh. 3,433,076,000
Kifungu 1003 – *Monitoring, Evaluation, Research and Mis* ....…..sh. 0
Kifungu 1004 - *Advocacy, Information, Education and Com* ……...........................................................……..sh. 0
Kifungu 1005 – *District and Community Response*……..........…sh. 0
Kifungu 1006 – *Procurement Management* Unit……..sh. 33,436,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

***Section 111 - Regional Supply Vote***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nashauri tunapopitia Mikoa yetu hii, ingekuwa ni ufanisi zaidi tukipitia Fungu la Mkoa mzima, lakini mnaruhusiwa sasa kurejea na kuuliza sehemu ambayo unataka ufafanuzi. Vinginevyo tutarudia vifungu vidogo vidogo kila Mkoa na itachukua muda mrefu sana, kwa kuwa mmekaa kimya na wengine mmesema ni sawa sikusikia aliyesema hapana, basi tunaendelea.

**Fungu 70 - Mkoa wa Arusha**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management*...........................................................….....sh. 1,812,497,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts*..........…………sh. 170,436,000
Kifungu 1003- *Internal Audit Unit*………...........………..sh. 31,520,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit* …….sh. 66,776,000
Kifungu 1005 – *DAS - Arusha*………………………........sh. 222,056,000
Kifungu 1006 – *DAS - Ngorongoro*……………………......sh. 254,600,000
Kifungu 1007 – *DAS – Karatu*……………………….........sh. 224,525,000
Kifungu 1008 – *DAS- Meru* ……………………………….sh. 278,715,000
Kifungu 1009 – *DAS Monduli* ……………………..………sh. 226,420,000
Kifungu 1010 – *DAS - Longido*……………….........…..sh. 3,535,184,000
Kifungu 2001 – *Planning and Coordination*….....……..sh. 243,687,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productivity Sector*…sh. 150,891,000

Kifungu 2003 – *Infrustructure Sector*………......………sh.160,573,000
Kifungu 2004 - *Social Sector* ……………………….……sh. 210,237,000
Kifungu 2005 – *Local Government Management Services*……..................................................................sh. 927,101,000
Kifungu 3001 – *Regional Hospital*………………...…..sh. 3,073,330,000
Kifungu 3002 – *Preventive Services*………………….sh. 3,073,330,000
Kifungu 8091 – *Local Government*………………..sh. 80,084,439,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 71 - Mkoa wa Pwani**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resource Management*…..........................…..sh. 1,018,677,000
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* Units..…....…..sh. 160,508,000
Kifungu 1003- *Internal Audit Unit* ……………..…………sh. 37,700,000
Kifungu 1004 - *Procurement Management Unit*………sh. 98,213,000
Kifungu1005 – *DAS - Kibaha* ……………….......…………sh. 254,141,000
Kifungu 1006 – *DAS - Mafia* ……………....……………..sh. 255,285,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu1007- *DAS-Kisarawe* …………………………….sh. 254,051,000
Kifungu1008 – *DAS - Bagamoyo*…………………………sh. 316,378,000
Kifungu 1009 – *DAS – Rufiji*………………………………..sh. 314,149,000
Kifungu 2010- *DAS - Mkururanga*………………………sh. 2,963,270,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 – *Planning and Coordination* … … … ....sh. 244,672,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector* … sh.175,150,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure Sector*… … … … … ..… sh.184,550,000
Kifungu 2004 - *Social Sector*… … … … … ........… … sh. 209,598,000
Kifungu 2005 – *Local Government Management Services*......................................................................……sh. 931,718,000
Kifungu 3001 – *Regional Hospital* … … … ...........… … sh. 202,798,000
Kifungu 8091 – *Local Government*.… … … … … *Tshs*.61,631,291,000

*(Vifingu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge ya Matumizi bila mabadiliko yeyote)*

**Fungu 72 - Mkoa wa Dodoma**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management*..........................................................................sh. 962,894,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*… … …..... sh.128,809,000
Kifungu 1003- *Internal Audit Unit*… … … … … … … ... sh. 15,680,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit* … ... sh.18,458,000
Kifungu 1005 – *DAS - Kondoa* … … … … … … … .. ... ...sh. 269,629,000
Kifungu 1006 – *DAS - Mpwapwa* ... ... … … … … … … sh. 224,181,000
Kifungu 1007 – *DAS – Kongwa* … … … … … … ... … … sh.191,714,000
Kifungu 1008 – *DAS- Bahi* … … … … … … …. …. .. … sh.188,017,000
Kifungu 1009 – *DAS Chamwino* … … … … … ... … … … sh. 212,497,000
Kifungu 1010- *DAS-Dodoma* … … … … … … … … …sh. 2,410,627,000
Kifungu 2001 – *Planning and Coordination*… … … … sh. 164,034,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productivity Sector* … sh. 141,206,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure Sector*… … … … … … … sh. 86,525,000
Kifungu 2004 - *Social Sector* … … … … … … … … … sh. 330,811,000
Kifungu 2005 – *Local Government Management Services*…...........................................................................…sh. 781,578,000
Kifungu 3001 – *Regional Hospital* … … … … … … …sh. 3,032,454,000
Kifungu 3002 – *Preventive Services*… … … ... … … sh. 3,032,454,000
Kifungu 8091 – *Local Government* … … … … ... … sh. 83,296,044,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 73 - Mkoa wa Iringa**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management*..........................................................................sh. 789,058,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……....…sh.130,348,000
Kifungu 1003- *Internal Audit Unit*…………………………sh. 29,218,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit* ………sh.23,334,000
Kifungu 1005 – *DAS - Iringa* ……………………………….sh. 303,462,000
Kifungu 1006 – *DAS – Njombe*…………………………..sh. 297,051,000
Kifungu 1007 – *DAS – Mufindi* …………………………..sh. 245,276,000
Kifungu 1008 – *DAS- Ludewa*……………………………sh. 315,536,000
Kifungu 1009 – *DAS- Makete* ……………………………..sh. 291,001,000
Kifungu 1010- *DAS - Kilolo* ………………………………sh. 2,682,763,000
Kifungu 2001 – *Planning and Coordination*…………..sh. 141,071,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productivity Sector* …sh. 212,632,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure Sector*……………………sh.199,266,000
Kifungu 2004 - *Social Sector*…………………………….sh. 446,783,000
Kifungu 2005 – *Local Government Management Services* …............................................sh.1,124,726,000
Kifungu 3001 – *Regional Hospital* ……………………sh. 2,826,031,000

Kifungu 3002 – *Preventive Services*………………….sh. 2,826,031,000
Kifungu 8091 – *Local Government* ………………….sh. 97,583,958,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 74 - Mkoa wa Kagera**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management*..........................................................….sh. 1,134,483,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…………….sh. 94,819,000=
Kifungu 1003- *Internal Audit Unit*……………....................sh. 42,360,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit* ……sh. 44,307,000
Kifungu 1005 – *DAS – Kigoma* ……………….......…….sh. 232,238,000
Kifungu 1006 – *DAS - Kasulu* ……………………..…….sh. 224,299,000
Kifungu 1007 – *DAS – Kibondo* …………….………….sh. 2,016,887,000
Kifungu 2001 – *Planning and Coordination*………….sh. 258,699,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*….sh. 146,745,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure Sector*…………………….sh. 225,977,000
Kifungu 2004 - *Social Sector*……………………..…….sh. 238,201,000
Kifungu 2005 – *Local Government Management Services*…......................................................................sh. 973,842,000
Kifungu 3001 – *Regional Hospital* ….............……….sh.1,735,124,000
Kifungu 8091 – *Local Government*………………….sh. 58,336,594,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 75 - Mkoa wa Kilimanjaro**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management*……......................................................…sh. 1,007,337,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…… … … … sh. 96,320,000
Kifungu 1003 - *Internal Audit Unit*……………….....…….sh.18,171,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*…….sh. 73,717,000
Kifungu 1005 – *DAS – Moshi* ………………………..….sh. 175,593,000
Kifungu 1006 – *DAS-Hai* ……………………........…….sh.180,766,000
Kifungu 1007 – *DAS – Rombo* ………………………….sh.174,137,8000
Kifungu 1008 – *DAS- Same* ……………...……………….sh. 244,825,000
Kifungu 1009 – *DAS Mwanga*…………………………….sh. 205,926,000
Kifungu 1010 - *DAS-Siha*………….....…………………sh. 2,287,898,800
Kifungu 2001 – *Planning and Coordination*………….sh. 365,182,200
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*….sh. 427,356,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure Sector*…………………….sh. 257,208,000
Kifungu 2004 - *Social Sector*………………………….sh. 263,218,000
Kifungu 2005 – *Local Government Management*

*Services*…...................................................................sh. 1,426,835,200
Kifungu 3001 – *Regional Hospital* … … … … … … … sh. 3,261,182,000
Kifungu 3002 – *Preventive Services*…………….......……………….sh. 0
Kifungu 2003 - *Transitional personnel*………………….sh. 3,261,182,000
Kifungu 8091 – *Local Government* ……………….sh.105,284,388,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu la 76 - Mkoa wa Lindi**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management*…......................................................……sh. 2,445,692,000

**MHE. RIZIKI SAID LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia katika hoja hii ya Waziri Mkuu niliangalia vifungu na kuona baadhi ya Mikoa inapata mafungu makubwa na Mikoa mingine ambayo iko nyuma kwa muda mrefu mafungu yao ni madogo kupita kiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufafanuzi kwa nini mafungu yanazidi kuwa madogo katika Mikoa ambayo iko nyuma? Nilitegemea Mikoa hiyo ingeongezewa mafungu ili kuipa changamoto ya maendeleo. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Serikali zinagawanywa kulingana na *formula* na *formula* ya Serikali ina vigezo vingi, idadi ya watu, eneo husika, na miundombinu mbalimbali. Kwa hiyo, mgawanyo wake unatokana na vigezo ambavyo vimewekwa, baadhi ya sehemu utakuta kwamba watu wako wengi sana kwa hiyo, mgawanyo wake unatokana na watu walivyo wengi katika Mkoa husika, kwa sababu ni lazima kutakuwa na huduma kama za afya, ni lazima ziwe nyingi, huduma zingine zote zile ni lazima ziwe nyingi kulingana na idadi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hakuna upendeleo wa aina yoyote bali ni *formula* ambazo tumejiwekea, kama tumeona *formula* zetu zimepitwa na wakati ni vyema tukazifanyia kazi ili ziweze kukidhi mahitaji ya sasa.

**MWENYEKITI**: Ahsante sana, Mwenyekiti wa Mkoa wa Lindi.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli lakini tupo Mikoa yote ya Tanzania. Mimi ningefurahi kama Waziri angetueleza ni lini ataleta hiyo *formula* ili na sisi tuweze kuifahamu.

**MWENYEKITI:** Ni suala la ufahamu, nadhani linaweza kusambazwa kwa maandishi tu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*………...….sh. 86,240,000
Kifungu 1003- *Internal Audit Unit*……….....…………….sh. 30,160,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*………sh. 35,000,000
Kifungu 1005 – *DAS – Lindi*………....………….......…….sh. 149,400,000
Kifungu1006- *DAS Kilwa* ……………….........…………….sh.160,000,000
Kifungu 1007 – *DAS-Liwale*………....…………………….sh.138,160,000
Kifungu 1008 – *DAS –* …………………......…..........……….sh.164,820,000
Kifungu 1009 – *DAS- Ruangwa*…………………..…….sh. 3,321,472,000
Kifungu 2001 – *Planning and Coordination*…………….sh. 131,658,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*….sh. 235,561,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure Sector*…………………….sh.184,064,000
Kifungu 2004 - *Social Sector*…………………………….sh. 283,785,000
Kifungu 2005 – *Local Government Management Services*….....................................................................sh. 971,534,000
Kifungu 3001 – *Regional Hospital* ……….........………….sh. 867,922,000
Kifungu 3002 – *Preventive Services*…………………….sh. 867,922,000
Kifungu 8091 – *Local Government*………………….sh. 43,347,363,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 77 - Mkoa wa Mara**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management*................................................................sh. 1,003,274,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit* … … … … sh..221,067,000
Kifungu 1003- *Internal Audit Unit*…………………...…….sh. 65,712,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*…….sh. 104,336,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1005 – *DAS – Musoma*………………………….sh. 249,416,000

**MHE. PROF. PHILLEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Waziri Mkuu.

**MWENYEKITI:** Unazungumzia kifungu gani?

**MHE. PROF. PHILLEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote* 77, *sub-vote1005 DAS* Musoma.

**MWENYEKITI:** Endelea katika hizo kasma ndogo zaidi.

**MHE. PROF. PHILLEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia kwa sababu Waziri Mkuu ametaja kwamba Butiama itakuwa Wilaya na Halmashauri sasa itaanza kutekelezwa mara moja, ilikuwa chini ya Musoma, hapa sioni fungu lolote kuhusu Wilaya ya Butiama, ninataka ufafanuzi tu, itaanza lini?

**MWENYEKITI:** Hilo linahusu Mikoa yote na Wilaya zote na sijui hii itaanzaje, mimi nadhani ili tusirudie rudie kila Mkoa swali hilo hilo, hii Mikoa mipya imepangiwa fedha ili ianze kazi na hizi Wilaya mpya na Tarafa mpya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba Wilaya mpya hizi zimetangazwa sasa hivi na mchakato wake bado haujaisha, sasa hivi kinachofanyika inabidi utoe *GN*, Mheshimiwa Rais ni lazima apelekewe, anatoa *notice* kwa ajili ya mipaka na mambo mengine kama unavyojua Makao Makuu na kadhalika, kwa hiyo, mchakato huu bado haujaisha, ukiisha huo na *notice* ikitolewa wananchi hawana *objection, GN* inatolewa, baada ya *GN* kutolewa ndiyo mpango wa Bajeti ndiyo unawekwa. Lakini mpaka sasa hivi hatujakubaliana kwamba mipaka iwe ya namna gani, mpaka wananchi wote washirikishwe ili mipaka iwe mizuri zaidi.

**MWENYEKITI:** Hili ni suala la Julai 2011, nia imetangazwa ya kuunda hizi Wilaya, lakini fedha yake kwa kweli ingebidi itengwe katika mchakato wa Bajeti unaoanza Novemba kuelekea 2011. Hili linaondoa utata kwa sababu watu wakianza kunyang'anyana tena nyumba na magari. *(Kicheko)*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1006 – *DAS-Bunda* …………………...………….sh. 224,086,000
Kifungu 1007 – *DAS – Serengeti*………………………….sh. 228,138,000
Kifungu 1008 – *DAS- Tarime* …………………………….sh. 229,210,000
Kifungu 1009 – *DAS Rorya*…………………...………….sh. 2,544,600,000
Kifungu 2001 – *Planning and Coordination*…………….sh. 302,140,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*….sh. 222,304,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure Sector*……………………sh.190,979,000
Kifungu 2004 - *Social Sector*…………………………….sh. 310,702,000
Kifungu 2005 – *Local Government Management Services*….....................................................................sh. 1,146,922,000
Kifungu 3001 – *Regional Hospital* …………………….sh. 2,340,118,000
Kifungu 3002 – *Preventive Services*…………………..sh. 2,340,118,000
Kifungu 2003- *Transitional personnel*…………………..sh. 3,261,182,000
Kifungu 8091 – *Local Government* ………………….sh. 77,295,457,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 78 - Mkoa wa Mbeya**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management*.................................................................sh.1,055,705,000

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu 10, *sub-vote* 1001, inazungumzia kuhusu mishahara, nimeangalia Mikoa mingi nimeona mishahara imepungua kwa kiasi kikubwa sana, lakini nilikuwa natafuta sehemu ya kusisima nikaona nisimame Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mwaka 2008/2009 mishahara hiyo ilikuwa karibu shilingi bilioni 1.2 mwaka 2009/2010 ikawa shilingi milioni 490.8 lakini mwaka huu imekuwa milioni 337, tofauti yake ni karibu milioni 153 ikilinganishwa na mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia pia kwa mfano Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Ruvuma na Mikoa mingine sehemu nyingine mishahara imepungua kwa sehemu kubwa sana, nilikuwa najiuliza kama watu wametoka kwa kiasi kikubwa hivyo au ni namna gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asiwe na wasiwasi kwamba wafanyakazi wamekuwa *distributed* katika *sub-vote* mbalimbali ndiyo maana unakuta kuna *sub-vote* nyingi kulingana na sekta husika, hilo siyo kwamba wamepunguzwa ila wameingizwa katika *sub-vote* zinazohusika.

**MWENYEKITI:** Ni utaratibu umefanyika wa kimahesabu badala ya wote kuwekwa *kwenye basic salaries* kama ilivyokuwa mwaka 2008/2009 mtaona sasa *basic salaries* zitakuwa *reflected* kila mahali. Kwa hiyo, siyo upungufu.

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*………….sh. 102,677,000
Kifungu 1003- *Internal Audit Unit*……………......……….sh. 34,983,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*…….sh. 35,982,000
Kifungu 1005 – *DAS – Mbeya* ……………................…….sh. 236,096,000
Kifungu 1006 – *DAS-Ileje* ………………........…………….sh. 198,346,000
Kifungu 1007 – *DAS – Kyela*……………....……………….sh. 198,566,000
Kifungu 1008 – *DAS- Chunya* …………..……………………sh. 213,952,000
Kifungu 1009 – *DAS Mbozi*…………………........………….sh. 253,966,000
Kifungu 1010 - *DAS - Rungwe*……………….…………….sh. 210,773,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1011 – *DAS-Mbarali*…………………………….sh. 2,745,044,000
Kifungu 2001 – *Planning and Coordination*…………….sh. 183,076,000

Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*….sh. 190,813,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure Sector*…………………….sh. 146,621,000
Kifungu 2004 - *Social Sector* ……………………………sh. 359,493,000
Kifungu 2005 – *Local GVT. Management Services*….sh. 986,120,000
Kifungu 3001 – *Regional Hospital* …………………….sh. 1,266,786,000
Kifungu 3002 – *Preventive Services*………………….sh. 1,266,786,000
Kifungu 8091 – *Local Government*……………….sh. 111,414,270,000

*(Vifingu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 79 - Mkoa wa Morogoro**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management*…..................................................................sh. 855,500,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…………….sh. 135,848,000
Kifungu 1003- *Internal Audit Unit*………………......……sh. 31,882,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*…….sh. 45,191,000
Kifungu 1005 – *DAS – Morogoro* ………………....…….sh. 270,257,000
Kifungu 1006 – *DAS - Kilosa* …………………….............sh. 264,322,000
Kifungu 1007 – *DAS – Kilombero* ………………….....….sh. 244,735,000
Kifungu 1008 – *DAS- Ulanga*…………………….........….sh. 260,139,000
Kifungu 1009 – *DAS Mvomero*……………………….....sh. 2,327,821,000
Kifungu 2001 – *Planning and Coordination*…………….sh. 191,297,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*…….sh. 230,909,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure Sector*…………………….sh. 153,592,000
Kifungu 2004 - *Social Sector*………………..………….sh. 315,805,000
Kifungu 2005 – *Local Government Management Services*......................................................................….sh. 956,352,000
Kifungu 3001 – *Regional Hospital* …………………….sh. 3,966,273,000
Kifungu 3002 – *Preventive Services*………………….sh. 3,966,273,000
Kifungu 8091 – *Local Government* ………………….sh. 96,148,691,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 80 - Mkoa wa Mtwara**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management*…...........................................................…sh. 1,432,516,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……………….sh. 42,088,000
Kifungu 1003- *Internal Audit Unit*……………........……sh. 27,088,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*……….sh. 39,425,000
Kifungu 1005 – *DAS – Mtwara* …………………………….sh. 137,724,000
Kifungu 1006 – *DAS-Newala* …………………………….sh. 163,641,000

Kifungu 1007 – *DAS – Masasi* …………………………….sh. 179,826,000
Kifungu 1008 – *DAS- Tandahimba* …..………………….sh. 193,084,000
Kifungu 1009 – *DAS Nanyumbu* ……………………….sh. 2,395,718,000
Kifungu 2001 – *Planning and Coordination*…………….sh. 208,428,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*…….sh. 189,051,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure Sector*…………………….sh. 198,510,000
Kifungu 2004 - *Social Sector*…………………………….sh. 251,936,000
Kifungu 2005 – *Local Government Management Services*….....................................................................sh. 925,453,000
Kifungu 3001 – *Regional Hospital* ……………………….sh. 1,873,457,000
Kifungu 3002 – *Preventive Services*…………………….sh. 1,884,950,000
Kifungu 8091 – *Local Government* ………………….sh. 57,331,466,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 81 - Mkoa wa Mwanza**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management*……......................................................….sh. 1,459,977,000

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu 10 *sub vote* 1001, *item* 220100 *General Office and General Supply and Services*, Bajeti hii ya *General Office na General Supply and Offices* imepungua kwa nusu, kutoka shilingi milioni 45 kwenda 21. Lakini mwaka uliotangulia 2008/2009 ilikuwa shilingi milioni 113.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani hili ni punguzo kali sana ambalo litaathiri sana shughuli za ofisi ya Mkuu wa Mkoa?

**MWENYEKITI:** Nadhani mtajirudia bure, maelezo ni yale yale, nikitazama huku kila Idara imepewa kifungu chake peke yake kinasomeka hivyo hivyo, *Office and General Supply and Services*, ukivijumlisha hivyo sasa ndiyo utavilinganisha na utaratibu wa mwaka 2008/2009 ambapo *Office and General Supply and Services* iliwekwa kwenye kifungu kimoja, naomba hili msiulize tena kwa kifungu chochote, kwa sababu haitakuwa na maana, kwa sababu sasa mtasema na *fuel, oil and lubricants*, wamezigawa hivi, huu ni utaratibu mzuri zaidi kwa sababu zinalengwa sasa kumpa kila Mkuu wa Idara awajibike kwa matumizi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*………….sh. 127,708,000
Kifungu 1003- *Internal Audit Unit*……………......……….sh. 51,652,000

Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*…….sh. 56,518,000
Kifungu 1005 – *DAS – Nyamagana* …………………….sh. 174,360,000
Kifungu 1006 – *DAS-Sengerema* ……………………….sh. 232,178,000
Kifungu 1007 – *DAS – Geita* ……………………..…….sh. 301,220,000
Kifungu 1008 – *DAS- Kwimba* ……………………………sh. 234,070,000
Kifungu 1009 – *DAS- Magu*……………...……………….sh. 244,954,000
Kifungu 1010 – *DAS Misungwi*……………………………sh. 230,581,000
Kifungu 1011 – *DAS-Ilemela* ……………………………sh. 177,310,000
Kifungu 1012 – *DAS- Ukerewe* ……………………….sh. 3,514,528,000
Kifungu 2001 – *Planning and Coordination*…………….sh. 233,393,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*……sh. 163,492,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure Sector*…………………….sh. 186,391,000
Kifungu 2004 - *Social Sector* ……………………………sh. 424,712,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2005 – *Local GVT. Management Services*.....sh. 1,124,137,000
Kifungu 3001 – *Regional Hospital*……………………….sh. 2,170,218,000
Kifungu 3002 – *Preventive Services* ……….....…………………….sh. 0
Kifungu 2003- *Transitional personnel*………………….sh. 2,170,218,000
Kifungu 8091 – *Local Government*………………….sh. 135,724,847,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 82 - Mkoa wa Ruvuma**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management*...sh. 907,669,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…………….sh. 112,173,000
Kifungu 1003- *Internal Audit Unit*…………………..…….sh. 42,091,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*……….sh. 35,854,000

*(Vifingu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1005 – *DAS – Songea* ……………………………sh. 290,913,000
Kifungu 1006 – *DAS-Tunduru*……………………………sh. 350,053,000
Kifungu 1007 – *DAS – Mbinga* ……………………………sh. 290,590,000
Kifungu 1008 – *DAS - Namtumbo*…………………….sh. 2,282,060,000
Kifungu 2001 – *Planning and Coordination*…………….sh. 219,855,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*…….sh. 165,314,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure Sector*…………………….sh. 154,570,000
Kifungu 2004 - *Social Sector* ……………………………sh. 313,264,000
Kifungu 2005 – *Local Government Management*

*Services*....................................................................…sh. 939,662,000
Kifungu 3001 – *Regional Hospital*…………………….sh. 3,113,522,000
Kifungu 3002 – *Preventive Services*…………………….sh. 2,340,118,000
Kifungu 2003 - *Transitional personnel*………………….sh. 3,261,182,000
Kifungu 8091 – *Local Government* ………………….sh. 64,939,597,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 83 - Mkoa wa Shinyanga**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management*..................................................................sh. 1,125,398,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…………….sh. 109,668,000
Kifungu 1003- *Internal Audit Unit*……………...……….sh. 31,481,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*…….sh. 43,159,000
Kifungu 1005 – *DAS – Shinyanga* …………………….....sh. 251,107,000
Kifungu 1006 – *DAS-Maswa* …………………………….sh. 219,277,000
Kifungu 1007 – *DAS – Bariadi* …………………………….sh. 236,248,000
Kifungu 1008 – *DAS - Kahama*……………......………….sh. 238,655,000
Kifungu 1009 – *DAS - Meatu*…………………….…….sh. 223,320,000
Kifungu 1010 –*DAS - Bukombe* ………………………….sh. 258,844,000
Kifungu 1011- *DAS - Kishapu*…………………………….sh. 2,944,651,000
Kifungu 2001 – *Planning and Coordination*…………….sh. 143,795,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*….sh. 143,668,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure Sector*…………..…….sh. 132,619,000
Kifungu 2004 - *Social Sector* …………………………….sh. 299,433,000
Kifungu 2005 – *Local Government Management Services*…...................................................................…sh. 844,612,000
Kifungu 3001 – *Regional Hospital* …………………….sh. 2,016,868,000
Kifungu 3002 – *Preventive Services*………………….sh. 2,340,118,000
Kifungu 8091 – *Local Government* ………………….sh. 77,295,457,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 84 - Mkoa wa Singida**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management*……......................................................…sh. 1,286,470,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…………….sh. 76,000,000
Kifungu 1003- *Internal Audit Unit*………………….sh. 38,000,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*…….sh. 59,000,000
Kifungu 1005 – *DAS – Singida*…………………………….sh. 208,000,000
Kifungu 1006 – *DAS - Manyoni*…………………………….sh. 175,000,000
Kifungu 1007 – *DAS – Iramba*………………………….sh. 2,017,470,000

Kifungu 2001 – *Planning and Coordination*…………….sh. 282,692,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*….sh. 213,641,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure Sector*…………………….sh. 180,706,000
Kifungu 2004 - *Social Sector* ……………………………sh. 272,300,000
Kifungu 2005 – *Local Government Management Services*…..................................................................sh. 1,022,339,000
Kifungu 3001 – *Regional Hospital*…………………….sh. 2,340,118,000
Kifungu 3002 – *Preventive Services*…………………….sh. 1,922,938,000
Kifungu 8091 – *Local Government* ………………….sh. 50,920,102,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 85 - Mkoa wa Tabora**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management*…...........................................................sh. 1,001,031,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…………….sh. 87,121,000
Kifungu 1003- *Internal Audit Unit*………………..……….sh. 59,556,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*…….sh. 61,715,000
Kifungu 1005 – *DAS – Tabora*……………………………sh. 209,294,000
Kifungu 1006 – *DAS-Nzega*………………...…………….sh. 267,579,000
Kifungu 1007 – *DAS – Sikonge* ………………………….sh. 214,814,000
Kifungu 1008 – *DAS- Igunga* ……………………………sh. 276,509,000
Kifungu 1009 – *DAS -Urambo* ……………………………sh. 262,032,000
Kifungu 1010- *DAS –Uyui* ………………………...….sh. 2,672,900,000
Kifungu 2001 – *Planning and Coordination*…………….sh. 181,000,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*…….sh. 123,230,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure Sector*…………………….sh. 123,881,000
Kifungu 2004 - *Social Sector*……………………………sh. 228,765,000
Kifungu 2005 – *Local Government Management Services*…...................................................................sh. 721,829,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 – *Regional Hospital* …………………….sh. 1,986,986,000

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu 30, *sub vote* 3001, kifungu kidogo cha 220400, kinachohusu *Medical Supplies and Service*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kinahusu Hospitali ya Mkoa, hospitali hii ina matatizo mengi lakini naenda kwenye hili moja ambalo fungu limepungua sana tofauti na miaka iliyopita, mwaka jana imepata shilingi milioni 91.7 sasa imezidi kupunguza kwenda chini wakati *population* inaongezeka kwa hiyo, matatizo yanaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi hapo.
**MWENYEKITI:** Hebu rudia tafadhali hatujaiona hii.

**MHE MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni programu 30 *Operational Personnel sub-vote* 3001, *Regional Hospital,* Kifungu kidogo cha 220400 kinachohusu *Medical Supplies and Services,* nilikuwa nasema kwamba hapa Serikali wamepunguza sana wakati tunafahamu kwamba hii hospitali ni kubwa na inahudumia watu wengi sana, kwa hiyo, hata mapungufu yaliyopo sasa hivi ina maana itashindwa kuhudumia wagonjwa kwa sababu fungu limepunguzwa zaidi pamoja na kuwa watu wanaongezeka kila siku na kila mwaka.

**MWENYEKITI:** Hospitali ya Mkoa. Mheshimiwa Mbunge programu 30 halafu 21.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** *Program 30, sub vote 3001 Regional Hospital* kifungu kidogo cha 224, *Medical Supplies and Services*.

**MWENYEKITI:** Si ndiyo hiyo hiyo nilisema. Kutoka shilingi milioni 91 kuwa shilingi milioni 67.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu wakati wa mchakato wa Bajeti, Wizara pamoja na Mikoa mpaka Halmashauri Bajeti zilipungua kwa Wizara asilimia 16, Mikoa asilimia mbili na kwa Halmashauri asilimia mbili. Sasa hiyo ndiyo imefanya hata kule kwingine ambako wanasema kwamba kwa nini imepungua, ni kwa sababu ya hiyo asilimia mbili ambayo tumeipunguza ili kukidhi mahitaji mengine.

**MWENYEKITI:** Kwa maana ya ukomo wa Bajeti? Basi tuchangamke mwaka ujao kazi kwa bidii ili Bajeti isiwe inakuwa finyu namna hii.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru mimi niko ukurasa 162 *sub-vote 3002 Preventive Services.* Pamoja na majibu ya Waziri aliyojibu sasa hivi ya kupungua kwa Bajeti lakini ukiona kifungu hiki hata kwenye Mikoa mingine chenyewe kimefutiliwa mbali kabisa, hakuna fedha yoyote ambayo imetengewa kwenye kifungu hiki. Hata kwenye Mikoa mingine ukiacha Tabora hata Mwanza ambako kuna Hospitali ya Rufaa na mahali pengine pia. Mimi ningedhani *preventive service* ingekuwa ya kwanza kuongezewa fungu kuliko kuondolewa kabisa. Naomba maelezo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *preventive services* zinaingia kwenye *medical general*. Kwa hiyo, zitaonekana kwenye vitabu vya Halmashauri mbalimbali yaani zinakwenda moja kwa moja kwenye Halmashauri husika.

**MWENYEKITI:** Nadhani haya marekebisho ya uhasibu na uandishi yanaleta shida kidogo. Pengine vizuri tuwe tunapata maelezo mapema ili tusihangaike wakati wa Kamati ya Matumizi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3002 – *Preventive Services*………………….sh. 1,986,986,000
Kifungu 8091 – *Local Government* ………………….sh. 67,805,286,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 86 – Mkoa wa Tanga**

Kifungu 1001 – *Administration and H/R Management*…............................................................sh. 1,837,402,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit* …………….sh. 70,320,000
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit* ……………………….sh. 31,664,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*……….sh. 31,644,000
Kifungu 1005 – *DAS – Tanga* …………………………...….sh. 82,626,000
Kifungu 1006 – *DAS – Kilindi* …………………..……….sh. 141,866,000
Kifungu 1007 – *DAS - Korogwe* …………………………….sh. 103,703,000
Kifungu 1008 - *DAS – Lushoto* …………………………….sh. 125,258,000
Kifungu 1009 - *DAS – Mkinga* …………………………….sh. 237,347,000
Kifungu 1010 - *DAS – Muheza* …………………………….sh. 99,767,000
Kifungu 1011 - *DAS – Pangani* …………………………….sh. 98,448,000
Kifungu 1012 - *DAS – Handeni*………………………….sh. 2,983,105,000
Kifungu 2001 - *Planning And Coordination*…………….sh. 151,389,000
Kifungu 2002 – *Economic and Productive Sector*….sh. 222,105,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure sector* …………………….sh. 180,739,000
Kifungu 2004 – *Social Sector* …………………………….sh. 340,028,000
Kifungu 2005 – *Local Government Management Services*….....................................................................sh. 1,023,916,000
Kifungu 3001 – *Regional Hospital*…………………….sh. 3,056,094,000
Kifungu 3002 – *Preventive Services* …………………….sh. 33,502,000
Kifungu 8091 – *Local Government* ……………….sh. 99,184,631,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 87 – Mkoa wa Kagera**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management*………........................................................sh. 1,036,397,000

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……………sh. 113,621,000
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit* …………………………sh. 37,973,000
Kifungu 1004 - *Procurement Management Unit* …….sh. 70,378,000
Kifungu 1005 - *DAS - Bukoba…* ……………………………sh. 243,126,000
Kifungu 1006 – *DAS – Biharamulo* ………………………sh. 198,141,000
Kifungu 1007 – *DAS – Chato …* ……………………………sh. 206,947,000
Kifungu 1008 – *DAS – Karagwe …* ………………………sh. 243,371,000
Kifungu 1009 - *DAS – Misenyi …* …………………………sh. 185,739,000
Kifungu 1010 – *DAS – Muleba* ……………………………sh. 220,057,000
Kifungu 1011 - *DAS – Ngara …* ……………………………sh. 222,040,000
Kifungu 2001 - *Planning and Coordination* …………sh. 197,241,000
Kifungu 2002 – *Economic and Productive Sector*….sh. 210,925,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure*……………………………sh. 190,552,000
Kifungu 2004 – *Social Sector*……………………………sh. 279,720,000
Kifungu 2005 – *Local Government Management Services*…......................................................................sh. 155,685,000
Kifungu 3001 – *Regional Hospital* ……………………sh. 2,288,825,000
Kifungu 3002 – *Preventive Services …* …………………sh. 41,698,000
Kifungu 8091 – *Local Government* …………………sh. 88,323,626,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 88 - Mkoa wa Dar es Salaam**

Kifungu 1001 - *Administrative and HR Management*……........................................................…sh. 1,595,077,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*………………sh. 91,105,000
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit …* ………………………sh. 25,098,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*……….sh. 46,680,000
Kifungu 1005 – *DAS – Ilala*…………………………....….sh. 150,000,000
Kifungu 1006 - *DAS – Kinondoni*…………………………sh. 150,000,000
Kifungu 1007 - *DAS – Temeke* ……………………………sh. 150,000,000
Kifungu 2001 – *Planning and Coordination*…….……sh. 184,390,000
Kifungu 2002 – *Economic and Productive Sector*…….sh. 195,875,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure Sector* ……………………sh. 175,491,000
Kifungu 2004 – *Social Sector* ……………………………sh. 304,054,000
Kifungu 2005 – *Local Government Management Services*......................................................................……sh. 93,440,000
Kifungu 8091 – *Local Government* …………………sh. 160,608,812,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 89 – Mkoa wa Rukwa**

Kifungu 1001 – *Administrative and HR Management*……...................................................……sh. 1,251,409,800
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…………….sh. 164,825,000
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit* ……………………….sh. 39,550,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit* ……….sh. 44,704,000
Kifungu 1005 – *DAS – Sumbawanga* …………………….sh. 356,869,000
Kifungu 1006 -*DAS – Nkasa*……………………...…….sh. 287,249,000
Kifungu 1007 – *DAS – Mpanda* …………………………….sh. 351,381,000
Kifungu 2001 - *Planning and Coordination* …………….sh. 185,610,000
Kifungu 2002 – *Economic and Productive Sector*…….sh. 228,744,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure* …………………………….sh. 179,034,000
Kifungu 2004 – *Social Sector*…………………………….sh. 331,189,000
Kifungu 2005 - *Local Government Management Service*….......................................................................sh. 126,538,400
Kifungu 3001 – *Regional Hospital* …………………….sh. 1,613,565,800
Kifungu 3002 – *Preventive Services* …………………........……….sh. 0
Kifungu 8091 – *Local Government*………………….sh. 50,807,021,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 95 - Mkoa wa Manyara**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management* ……...................................................……sh. 919,040,000
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*…………….sh. 224,658,000
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit* ………………………….sh. 45,665,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*……….sh. 45,665,000
Kifungu 1005 – *DAS - Babati*……………………....….sh. 204,978,000
Kifungu 1006 – *DAS Hanang* ...…………………………sh. 242,044,000
Kifungu 1007 – *DAS – Kiteto* …………………………….sh. 233,676,000
Kifungu 1008 – *DAS – Mbulu* ……………………….……sh. 236,909,000
Kifungu 1009 – *DAS – Simanjiro* ………………………….sh. 278,353,000
Kifungu 2001 – *Planning and Coordination*……….sh. 320,549,000,000
Kifungu 2002 – *Economic and Productive Sector*….sh. 233,058,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure Sector* …………………….sh. 152,118,000Kifungu 2004 – *Social Sector* ….
*Services*….....................................................................sh. 157,905,000
Kifungu 3001 – *Regional Hospital* ……………………….sh. 231,938,000
Kifungu 8091 – *Local Government* ………………….sh. 56,694,421,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 27 - Msajili wa Vyama vya Siasa**

Kifungu 1001 - *Administration and General* …………….sh. 20,181,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kifungu 1001 – *Administrative and General* ……….sh. 4,792,570,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning* ………………….sh. 1,855,850,000
Kifungu 1005 – *Information,*
*Education and Communication*……..........................................…sh. 0
Kifungu 1008 – *Management Information*
*System Unit* …………………...........................................................……sh. 0
Kifungu 2001 – *Civil Affairs and Contingencies*……….sh. 378,000,000
Kifungu 2002 – *National Festivals* ………………………….sh. 81,230,000
Kifungu 3001 – *Parliamentary and Political Affairs* ………………….sh.0
Kifungu 4001 – *Investment and Private*
*Sector Development.…………….*…………………sh. 29,946,482,000
Kifungu 5001 – *Coordination of Government*
*Business*...............................................................……sh. 1,440,251,000
Kifungu 7001 – *Government Printer* ………………….sh. 812,300,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 42 - Mfuko wa Ofisi ya Bunge**

Kifungu 1001 – *Administration and General*………….sh. 500,000,000
Kifungu 2001 – *National Assembly* …………….…….sh. 3,814,400,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 61 – Tume Ya Uchaguzi**

Kifungu 1001 – *Administration and General* ……….....………….sh. 0
Kifungu 2002 – *Permanent National Voters*
*Registration System Division*.........................................sh. 5,65,550,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 91 – Tume ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya**

Kifungu 1001 – *Administration and General* …………sh.146,700,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti Ukimwi**

Kifungu 1001 – *Policy, Planning and National Response*……....................................................................sh. 3,353,656,000
Kifungu 1002 – *Finance, Administration Resource Mobilization*…....................................................................sh. 2,888,262,900
Kifungu 1003 – *Monitoring, Evaluation, Research and Management Information System*….........................sh. 2,741,674,000
Kifungu 1004 -*Advocacy, Information, Education and Communication*…………………….sh. 3,189,931,300
Kifungu 1005 - *District and Community Response*…sh. 3,817,047,000

**MWENYEKITI:** Subiri kidogo kifungu kilirukwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwenye *Volume II.*

Waheshimiwa Wabunge, turekebishe kidogo katika *Volume II Estimate* TAMISEMI, Fungu la 56 inaelekea lilirukwa kwa bahati mbaya. Sasa kwa usahihi wa kupitisha makadirio hatuna budi kulirejea hilo.

**Fungu 56 – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)**

Kifungu 1001 – *Administration and General* ………sh. 4,361,141,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts*………………….sh. 541,857,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning* ………………….sh. 2,207,889,000
Kifungu 1004 – *Management Information System Division*……........................................................................sh. 461,844,000
Kifungu 1005 – *Legal Services Division* ………………….sh. 460,914,000
Kifungu 1006 - *Internal Audit Unit* …..………………….sh. 314,411,000
Kifungu 1007 - *Information, Education and Communication Unit*.................................................….sh. 424,559,000
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*…….sh. 330,353,000
Kifungu 2001 – *Regional Administration Division*…….sh. 745,911,000
Kifungu 2002 – *Local Government Coordination Division*…........................................................................sh. 22,052,919,000
Kifungu 2003 – *Sector Coordination Division*……….sh. 14,065,814,000
Kifungu 3001 – *Organization Development Division*……...............................................................……sh. 9,015,187,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Unajua vifungu hivi viko vingi sana kwa hiyo, si vigumu kukuta mmeviruka. Basi tunarejea tena kitabu cha nne. Katibu alikuwa amefikia Fungu la 37, sasa tuendelea. Turudi Fungu 56, ukurasa wa 127.

**Fungu 56 – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)**

Kifungu 1001 – *Administration and General*………….sh. 300,000,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning*…………………….sh. 4,640,000,000Kifungu 1004 – *Management Infor*
*Division*…...........................................................................….sh. 603,052,760
Kifungu 1005 – *Legal Services Division* …………………..………….sh. 0
Kifungu 2001 – *Regional Administration Division*……sh. 337,028,970

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwana Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 – *Local Government Coordination*
*Division*..........................................................................….sh. 26,249,043,000

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika fungu hili *subvote 2002, item 6360, Consumption of MPs Offices*.

Kama unavyojua kwamba Wabunge wanatumia nyumba kama ofisi. Katika mchango wangu nilionyesha wasiwasi na matatizo kuhusu ujenzi wa hizi ofisi. Ile Ofisi ya Bunge ya Zanzibar namna gani ambavyo bado haijatumiwa ipasavyo na Wabunge wote wa Zanzibar tunapata taabu sana na Ujenzi wa Ofisi za Wabunge. Fedha katika miaka mitatu iliyopita kila mwaka shilingi bilioni moja inatengwa lakini namna inavyopelekwa kama ni Tawala za Mikoa kule vikosi vya *SMZ* au watu hatuelewi na Mbunge si rahisi kufuatilia.

Katika mwaka wa fedha uliopita *DC* wa Wilaya yangu Mkoani katika mashauriano ilikuwa katika Jimbo la Mkanyageni lijengewa ofisi. Mwaka umepita sijui fedha kiasi gani iliyopelekwa hatujui chochote hata *DC* mwenyewe hana taarifa yoyote, Mbunge anatoa hela mfukoni. *DC* baada ya kutoa barua ya kuwa kipimwe kiwanja kikawa *allocated,* Mbunge anatoa fedha mfukoni ili kiwanja kipimwe halafu hakijulikani chochote.

Sasa Mbunge hajui afuatilie nini, nilitaka ufafanuzi kwa nini Ofisi ya Bunge iliyoko Zanzibar isitumiwe ipasavyo ikawa Mbunge ana uwezo wa kufuatilia na kwa nini pasiwepo na ratiba tukajua mwaka huu fedha iliyokuwa *allocated* ni kiasi gani, zitajengwa ofisi fulani Zanzibar, Mwanza, ili tuweze kufuatilia. Naomba ufafanuzi na

hasa matumizi ya Ofisi yetu ya Bunge katika mambo kama haya ya Ofisi ya Mbunge, ili aweze kufuatilia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa ujenzi wa Ofisi za Wabunge kwa upande wa Bara hatuna matatizo yoyote. Kwa sababu zinapitia kwenye Halmashauri za Wilaya. Lakini kwa upande wa Zanzibar kule tunapeleka Ofisi ya *DC* na ndivyo tulivyokubaliana. Tunawasiliana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ ndivyo tulivyokubaliana. *(Makofi)*

Baadhi ya Wabunge wamewasiliana na Ma-*DC* wao vizuri wameshirikiana nao na Ofisi zimejengwa, ushahidi Mheshimiwa Shoka amejenga ofisi nzuri sana, akatae pale. Lakini baadhi kuna matatizo mimi nasema kama walivyofanya kwenye fedha za Mfuko wa Jimbo kwenye sheria, sisi tulisema kwamba tutazipeleka kwa Ma-*DC* wakasema hapana hatutaki kupeleka kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano tumefanya hivyo kwa makubaliano.

Kwa hiyo, kama wanaona ni kikwazo waje tu tujadiliane kwamba hiyo njia mnayoitumia sio nzuri lakini tunafanya kwa uwazi kabisa, Bungeni natangaza kila siku kwamba mwaka huu tutajenga ofisi kiasi fulani Bara, kiasi fulani Visiwani na baadhi ya ofisi tumeenda kuzikagua zimekwenda vizuri. Sasa kama kuna matatizo ya hapa na pale mimi naomba tu Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar tukae pamoja tuone ni namna gani bora ya kupeleka hizo fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mimi kwa ushauri wangu tu, hili la kujenga ofisi za Wabunge ni ndogo lakini Serikali mmeling'ang'ania kabisa lazima mjenge ofisi za Wabunge. Kama ilivyo Idara nyingine kama Mahakama wanajenga Mahakama, wanajenga nyumba mbalimbali, lingekuwa na mtiririko wa uwajibikaji mzuri, kama lingesimamiwa na Katibu wa Bunge basi. Lakini ninyi mna Waziri Mkuu, mna maabo makubwa, miprogramu mikubwa mikubwa ya mabilioni sasa hili nalo kwa kuwa yule *DC* hawajibiki kwa Mbunge na baya zaidi ni kwamba hata fedha zile za ofisi, hakuna Mbunge yeyote anaziona hata ukishajengewa ofisi hakuna na ukiwauliza wanasema tutaonana wewe, tutakuona basi.

Ah! Sasa kama yalivyo Mabunge mengine, fungu hili lingekabidhiwa kwenye mfuko maalum wa Bunge na kazi ingekwenda vizuri na lisingeulizwa tena humu ndani ya Bunge. Lakini hayo nadhani ni ya Bunge la Kumi. Mkipata Spika goigoi shauri yenu. Tunaendelea.*(Kicheko na Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2003 - *Sector Coordination Division*……….sh. 6,712,671,270
Kifungu 3001 -*Organisation Development Division*…......................................................................….sh. 1,500,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti Ukimwi**

Kifungu 1001 – *Policy Planning and National Response*…..........................................................................sh. 3,353,656,000
Kifungu 1002 - *Finance, Administration and Resource Mobilization*….......................................…sh. 2,888,262,900
Kifungu 1003 - *Monitoring, Evaluation, Research and MIS*......................................................................…sh. 2,741,674,000
Kifungu 1004 - *Advocacy, Information, Education and Com*…..................................................sh. 3,189,931,300
Kifungu 1005 - *District and Community Response*…sh. 3,817,047,000
Kifungu 1007 - *Legal unit*…………………........…………sh. 203,844,000
Kifungu 1008 - *Management Information Systems*...sh. 1,479,243,000
Kifungu 1009 - *Internal Audit Unit* ……………..………sh. 288,546,900
Kifungu 1010 - *Special Programs*……………………sh. 1,125,303,900

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1011 – *Information, Education and Com. Unit*…....................................................................sh. 20,648,509,000

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina moja la jumla katika *vote* zote hizi tulizopitia lakini nitatumia hiki kifungu cha mwisho ili kutoa hoja yangu kuomba ufafanuzi. Ni kwamba Bajeti yote hii ya *TACAIDS* ni *foreign funded,* sasa maana yake nini, hawa wasipotupa hizi pesa tunafunga kazi? Nataka ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli shughuli nyingi za Tume ya Kudhibiti UKIMWI zinafadhiliwa kutokana na fedha kutoka nje, tumeliona hilo na ndio maana kuanzia mwaka huu kwa kutumia masharti ya sheria iliyounda Tume hii, tumeanzisha *Trust Fund* ambapo pesa itawekwa kutoka Hazina na pia wafadhili hao wamekubali ili itakapotokea kwamba kutakuwa na upungufu wa fedha kutoka nje basi fedha hizo ambazo zitakuwa kwenye *Trust Fund* ziweze zikafanya shughuli hizi ambazo zinafanyika sasa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 70 – Mkoa wa Arusha**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management*……...........................................................….sh. 1,146,958,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*……………….sh.   10,000,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*…….sh. 87,797,000
Kifungu 2003 - *Infrastructure Sector* ……………………….sh. 30,000,000
Kifungu 2004 - *Social Sector*…………...…………………sh. 30,000,000
Kifungu 3001 - *Regional Hospital*…………………….sh. 1,194,294,000
Kifungu 8091- *Local Government* ………………….sh. 32,139,816,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 71- Mkoa wa Pwani**

Kifungu 1001- *Administration and HR Management*….sh. 50,000,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*…………….sh. 143,616,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*…….sh. 92,041,000
Kifungu 2003 - *Infrastructure Sector* ………………….sh. 1,264,000,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital*……………..………….sh. 211,364,000
Kifungu 8091- *Local Government*…………………….sh. 22,379,990,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 72 - Mkoa wa Dodoma**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management*………......................................................sh. 4,195,778,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*…….sh. 98,710,000
Kifungu 2004 - *Social Sector* ………………...………….sh. 367,967,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital* ……………………….sh. 800,000,000
Kifungu 3002 - *Preventive Services* …………......………………….sh. 0
Kifungu 8091- *Local Government*………………….sh. 34,818,509,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 73 - Mkoa wa Iringa**

Kifungu 1001- *Administration and HR Management*..............................................................….sh. 453,946,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*…………….sh.  893,000,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*….sh. 137,740,000
Kifungu 2003 - *Infrastructure Sector*…………………….sh. 35,000,000
Kifungu 2004 - *Social Sector*………….....……………….sh. 227,273,000
Kifungu 8091- *Local Government*………………….sh. 35,569,795,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 74 - Mkoa wa Kigoma**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management*……........................................................…sh. 1,675,436,000
Kifungu 2001 - *Planning and Coordination*…..……….sh. 225,400,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector*……….sh. 6,000,000
Kifungu 2004 - *Social Sector*……………...……………….sh. 30,000,000
Kifungu 3001 - *Regional Hospital*……………………….sh. 322,898,000
Kifungu 3002 - *Preventive Services* ………………........…………….sh. 0
Kifungu 8091- *Local Government*………………….sh. 38,721,493,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 75 - Mkoa wa Kilimanjaro**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management*…..................................................................sh. 734,900,000
Kifungu 2001 - *Planning and Coordination*…………….sh. 78,000,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*…….sh. 87,928,000
Kifungu 2003 - *Infrastructure Sector*…………………….sh. 30,400,000
Kifungu 2004 - *Social Sector*…………………...……….sh. 30,000,000
Kifungu 3001 - *Regional Hospital* …………………….sh. 1,761,362,000
Kifungu 8091- *Local Government* ………………….sh. 29,159,571,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 76 - Mkoa wa Lindi**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management*..............................................................…sh. 254,800,000
Kifungu 2001 - *Planning and Coordination*…………….sh. 162,322,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*….sh. 101,938,000
Kifungu 2003 - *Infrastructure Sector* …………………….sh. 390,958,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital* ……………………….sh. 845,455,000
Kifungu 3002 - *Preventive Services*……………………….sh. 30,000,000
Kifungu 8091 - *Local Government* ………………….sh. 20,528,020,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 77 - Mkoa wa Mara**

Kifungu 1001- *Administration and HR Management*……..........................................................……….sh. 20,000,000
Kifungu 1005 – *DAS - Musoma* ……………………….……sh. 5,000,000
Kifungu 1006 – *DAS - Bunda* ……………….....……………….sh. 5,000,000
Kifungu 1007 – *DAS- Serengeti* ……………..……………….sh. 5,000,000
Kifungu 1008- *DAS- Tarime* …………………......………….sh. 5,000,000
Kifungu 1009- *DAS- Rorya* ………………….........……….sh. 5,000,000
Kifungu 2001 - *Planning and Coordination*…………….sh. 60,000,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*….sh. 111,844,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector*………………….sh. 1,514,979,000
Kifungu 2004 - *Social Sector*……………………...…….sh. 30,400,000
Kifungu 3001 - *Regional Hospital* ……………………….sh. 615,454,000
Kifungu 8091- *Local Government*…………………sh. 28,893,990,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 78 - Mkoa wa Mbeya**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management*…….............................................................sh. 614,070,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*……………….sh. 43,990,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*….sh. 139,341,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector*……………………….sh. 35,000,000
Kifungu 2004 - *Social Sector*…………………..……….sh. 307,273,000
Kifungu 3001 - *Regional Hospital* ……………………….sh. 709,759,000
Kifungu 8091- *Local Government* ………………….sh. 47,743,815,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 79 - Mkoa wa Morogoro**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management*………........................................................sh. 1,804,774,000
Kifungu 1005- *DAS- Morogoro* …………………………….sh. 10,000,000
Kifungu 1006- *DAS- Kilosa* ……………………..........……sh. 5,000,000
Kifungu 1007- *DAS- Kilombero*…………………..……….sh. 5,000,000
Kifungu 1008- *DAS- Ulanga* …………………......……….sh. 5,000,000
Kifungu 1009- *DAS- Mvomero* ……………………..…….sh. 5,000,000
Kifungu 2001 - *Planning and Coordination*…………….sh. 20,000,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*….sh. 100,000,000

Kifungu 2003 - *Infrastructure Sector* …………………….sh. 35,000,000
Kifungu 2004 - *Social Sector* ……………………………sh. 195,455,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital* ……………………….sh. 730,000,000
Kifungu 8091 - *Local Government*………………….sh. 38,880,931,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 80 - Mkoa wa Mtwara**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management*……......................................................…sh. 1,002,900,000
Kifungu 2001 - *Planning and Coordination*…………….sh. 25,000,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector* …….sh. 96,228,000
Kifungu 2003 - *Infrastructure Sector* …………………….sh. 30,400,000
Kifungu 2004 - *Social Sector* ……………………...…….sh. 30,000,000
Kifungu 3001 - *Regional Hospital* …………...………….sh. 975,455,000
Kifungu 8091 - *Local Government*………………….sh. 29,709,490,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 81 - Mkoa wa Mwanza**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management*….................................................................sh. 60,000,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination* …………….sh. 150,393,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*…….sh. 90,071,000
Kifungu 2003 - *Infrastructure Sector* ………………….sh. 1,348,000,000
Kifungu 2004 - *Social Sector*……………………………sh. 211,364,000
Kifungu 3001 - *Regional Hospital* ……………………….sh. 400,000,000
Kifungu 8091- *Local Government*………………….sh. 53,871,597,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 82 - Mkoa wa Ruvuma**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management*…....................................................……sh. 1,249,865,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*………………………….sh. 0
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector*…….sh. 106,763,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector*……………………….sh. 20,000,000
Kifungu 2004 - *Social Sector* ……………………………sh. 382,327,000
Kifungu 3001 - *Regional Hospital* ……………………….sh. 250,000,000
Kifungu 8091 - *Local Government*………………….sh. 26,987,224,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 83 - Mkoa wa Shinyanga**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management* …..........................................................……….sh. 186,000,000
Kifungu 2001 - *Planning and Coordination*…………….sh. 82,247,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*….sh. 124,426,000
Kifungu 2003 - *Infrastructure Sector*………………….sh. 1,233,100,000
Kifungu 2004 - *Social Sector* ……………......…………….sh. 88, 847,000
Kifungu 3001 - *Regional Hospital*……………………….sh. 130,000,000
Kifungu 8091- *Local Government*………………….sh. 48,486,733,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 84 - Mkoa wa Singida**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management* ............................................................……sh. 235,000,000
Kifungu 2001 - *Planning and Coordination*……………sh. 40,000,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*…….sh. 86,547,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector*……………………….sh. 30,400,000
Kifungu 3001 - *Regional Hospital* …………………….sh. 2,293,285,000
Kifungu3002 - *Preventive Services*…………………...........……….sh. 0
Kifungu 8091 - *Local Government* ………………….sh. 21,227,130,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 85 - Mkoa wa Tabora**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management*………......................................................sh. 1,342,665,000
Kifungu 2001 - *Planning and Coordination*…....………….sh. 4,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*…….sh. 91,520,000

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub- vote 2002* kifungu kidogo cha 45(53), *Livestock Development Fund.* Kumekuwa na mpango maalum mzuri sana ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu ameuanzisha kuhakikisha kwamba Mikoa yote yenye mifugo inaweza kufugwa kisasa na hivyo tuweze kuwa na pato kubwa

tukanalo na mifugo, mojawapo ikiwa ni Mkoa wa Tabora. Shilingi milioni tatu zilizotengwa hapa nashindwa kuelewa kwa namna gani ambapo tutaweza kuboresha mifugo ikiwa ni pamoja kutenga na maeneo ya mifugo, kuwa na wataalamu wa kutosha wa mifugo na kuhakikisha kwamba tunakuwa na pamoja na viwanda kwa ajili ya maziwa, nyama ili mifugo iweze kuleta tija kwa Mkoa wa Tabora, naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Kabla sijamuita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kujibu, labda Mheshimiwa Sakaya unaweza kusema Jimbo unalokusudia kugombea hasa ni lipi? Maana yake... *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Sakaya kama ifuatavyo, Fedha hizi ni fedha za *supervision,* kusimamia Halmashauri wakati wanapoenda safari mbalimbali na sio fedha za kuimarisha ufugaji. Fedha husika za kuimarisha mifugo za *DADPS* na nini ziko kwenye mafungu ya Halmashauri mbalimbali.

Kifungu 2003 - *Infrastructure Sector* ……………………….sh. 35,000,000
Kifungu 2004 - *Social Sector*……………………...…….sh. 30,000,000
Kifungu 3001 - *Regional Hospital* ……………………….sh. 486,288,000
Kifungu 8091 - *Local Government*………………….sh. 31,362,705,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 86 - Mkoa wa Tanga**

Kifungu 1001- *Administration and HR Management*………...................................................…sh. 1,209,679,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*……………….sh. 75,000,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*….sh. 129,443,000
Kifungu 2004 - *Social Sector* ……………………...…….sh. 35,000,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital* ……………………….sh. 498,951,000
Kifungu 3002- *Preventive Services* ……...........…………....…….sh. 0
Kifungu 8091- *Local Government* ………………….sh. 39,995,945,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 87 - Mkoa wa Kagera**

Kifungu 1001 - *Administration and HR*

*Management* …….......................................................….sh. 1,516,852,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination* …………….sh. 263,292,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector* …….sh. 95,476,000
Kifungu 2003 - *Infrastructure Sector* ………………….sh. 1,035,000,000
Kifungu 2004 - *Social Sector* …………………………….sh. 222,273,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital* ……………………….sh. 100,000,000
Kifungu 3002 - *Preventive Services* ……………………….sh. 50,000,000
Kifungu 8091 - *Local Government* ………………….sh. 37,312,988,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 88 - Mkoa wa Dar es Salaam**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management* ....................................................…......sh. 852,251,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*…………….sh. 470,643,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*…….sh. 79,576,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector* …………………….sh. 25,000,000
Kifungu 8091- *Local Government*………………….sh. 31,120,039,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 89 - Mkoa wa Rukwa**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management*…..................................................……sh. 1,609,060,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*……..……….sh. 30,000,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector*…….sh. 12,000,000
Kifungu 2003 - *Infrastructure Sector* …………………….sh. 30,400,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital* ……………………….sh. 307,999,000
Kifungu 3002 - *Preventive Services* ……………......……………….sh. 0
Kifungu 8091- *Local Government* ………………….sh. 31,246,335,000

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 95 - Mkoa wa Manyara**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management* …….................................................……sh. 281,791,000
Kifungu 1005 - *DAS – Babati* …………......………………….sh. 5,000,000
Kifungu 1006 - *DAS – Hanang*……………..……………….sh. 25,000,000
Kif 1007- *DAS – Kiteto*…………………..............………….sh. 30,000,000

Kif 1008- *DAS –Mbulu* ……………….........…….......……….sh. 5,000,000
Kif 1009- *DAS – Simanjiro* ……………………......……….sh. 25, 000,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*…….sh. 89,007,000
Kifungu 2003 - *Infrastructure Sector*……………………sh. 30,400,000
Kifungu 2004 - *Social Sector* ……...……………………sh. 225,455,000

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 - *Regional Hospital*……………………sh. 2,000,000,000

**MHE. OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Fungu hilo hilo 95, ukurasa ule 328, sub-vote 3001 Regional Hospital. Wakati nachangia niliipongeza Serikali kwa kutenga shilingi bilioni 2 kwa ujenzi wa hospitali ya Mkoa wa Manyara pale Babati, lakini nilitoa changamoto kwamba tukiendelea kuziambia Mikoa inayo jenga hospitali ambapo baadae zitakuwa za Rufaa, kwamba watenge fedha za ujenzi kwa kutumia bajeti zao ni kama wanasimamisha miradi mingine yote.

Kwa hiyo, ile ceiling ya Mkoa ni kama inamalizika kwa kutoa kipaombele kwa ujenzi wa majengo kama hayo, makubwa kama hospitali. Kwa hiyo, hawatafanya jambo lingine lolote maana hii ni kama asilimia 85 inakuwenda tu kwenye hospitali kwa bajeti ya Mkoa wa Manyara na Mikoa mingine inayojenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema kwa miradi hii Serikali inapashwa ukaangalia ijengwe kupitia mifuko maalum kwa utaratibu maalum, hospitali za Mikoa ambazo baadae zitakuwa za Rufaa, badala ya kutumia ceiling ya bajeti ya Mkoa. Sasa je, maelezo yanasema nini, Serikali inakubali changamoto?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nikubaliane tu na ushauri wake tuufanyiakazi, tuonane namna bora ya kuweza kujenga mapema hospitali.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 8091- *Local Government* …………………sh. 25,095,280,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge Lilirudia)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi baada ya kujadili taarifa ya mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali imeyapitia matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na asasi zilizo chini yake na yale ya Ofisi ya

Bunge kwa mwaka 2010/2011, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi naomba sasa Bunge lako liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja tuliyokuwa tukiishughulikia kwa siku tatu, hapa tunafika tamati, hoja iliyo mbele yetu ni ya kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Waziri Mkuu ambayo yanajumuisha pia Taasisi mbalimbali zinazoshughulikiwa Kibajeti na Ofisi ya Waziri Mkuu. Hoja ilitolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na ikaungwa mkono, sasa wajibu wangu tu ni kuwahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yalipitishw ana Bunge)*

**SPIKA:** Nafurahi sasa kutangaza kwamba Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 yamepitishwa rasmi na Bunge la Jamuhuri ya Muungano na namtakia yeye mwenyewe afya njema aendelee kutuongoza vizuri na taasisi zote zilizoko chini ya ofisi hiyo, ziweze kufanya kazi zake kama ilivyotazamiwa na ule mwenendo mzuri tunaoanza kuuona sasa katika matumizi ya fedha za Serikali uendelee ili liwe ni jambo la kawaida tu kuweza kukagua na kuona kwamba matumizi yamekuwa mazuri na yamekubalika katika kutupa mafanikio mazuri.

Waheshimiwa Wabunge, lililobaki mimi ni kukumbusha tu kwamba kesho saa tano asubuhi Tume ya Huduma za Bunge itakutana kwenye ukumbi wa Spika na mnajua Tume haikamiliki bila kuwapo upande wa Upinzani na pia viongozi wa Serikali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, pamoja na Mwanasheria Mkuu ndio tunaunda Tume, hata tukiwepo sote lakini mmoja kati ya makundi hayo wasipokuwepo tutakuwa tunapoteza muda kwa sababu akidi inahitaji makundi hayo yawepo. Kwa hiyo, nawasihi sana ni kikao kifupi sana, jambo ni muhimu lakini kikao kifupi saa tano ukumbi wa Spika. Ahsanteni sana Wabunge wote mjadala ulikuwa mzuri sasa nahairisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.42 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumamosi, Tarehe 19 Juni, 2010 saa tatu asubuhi)*